# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Saba– Tarehe 25 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU WA MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimazi wa Udhibiti wa Nishati na Maji kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2017 *[The Annual Report of Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) for the Year Ended 30th June, 2017].*

**MWENYEKITI:** ahsante, Katibu.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali yetu ya kawaida, tunaanza Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza Mbunge wa Chumbuni, kwa niaba ya Mheshimiwa Machano.

Na. 135

### Kuwakamata Wafanyabiashara Wakubwa wa Dawa za Kulevya

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID (K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua dhidi ya wauzaji wakubwa wa dawa za kulevya wanaoingiza na kuuza badala ya kuakamata waathirika ambao wanahitaji misaada na ushauri nasaha wa kuachana na matumizi ya dawa hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga na inaendelea kukabiliana na wafanyabiashara wakubwa na wadogo wa dawa za kulevya ambao wote wanasababisha madhara kwa jamii kwa kufanya biashara hiyo. Hadi kufikia Februari, 2018 jumla ya wanyabiashara 3,486 wa dawa za kulevya walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Kati ya hao zaidi ya asilimia 30 ni wafanyabiashara wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wamekimbia nchini kutokana na ukali wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba

Tano ya mwaka 2015 na marekebisho yake ya mwaka 2017 pamoja na udhibiti unaofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola. Aidha, Serikali imeendelea kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya kwa kutoa elimu ya madhara ya dawa za kulevya kwa watumiaji na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wale walioathirika kwa kutumia dawa za kulevya, wanapopatikana Serikalini imekuwa ikijikita zaidi kutoa ushauri nasaha, tiba na kuwahamasisha kupata tiba hiyo kwani hutolewa bure. Hadi kufikia mwezi Februari, 2018 zaidi ya warahibu 5,560 wamendelea kupata tiba katika vituo vya Serikali, mpango wa Serikali ni kusambaza huduma hii nchi nzima ili kuwafikia waathirika wengi wenye uhitaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machano.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake. Lakini pamoja na jibu hilo naomba kuuliza maswala mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii ya dawa za kulevya ina mtandao mrefu, na katika mtandao huo wapo baadhi ya raia ya wa kigeni ambao wanaishi Tanzania wanajishirikisha na dawa hizi. Miaka miwili, mitatu, minne nyuma kuna mwanamke mmoja kutoka nchi jirani alikamatwa maeneo ya *Mbezi beach* na alikuwa akitumia *passport* nyingi na majina tofauti.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na wageni ambao wanaitumia Tanzania kwa uuzaji wa madawa ya kulevya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, miongoni mwa waathirika wakubwa watumiaji wa dawa za kulevya ni wasanii wetu. Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wasanii

hawa kuondokana na tatizo hili la utumiaji wa dawa za kulevya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwanza, sheria yetu haibagui wenyeji na ugeni. Inapotokea mtu yeyote anajihusisha na dawa za kulevya sheria yetu imekuwa ikitumika kwa kuhakikisha kwamba hatua stahiki zinachukuliwa na kufanya kitu ambacho kinaitwa *deterrence* ili kuwazuia watu wengine wasifanye biashara hii ya dawa za kulevya. Adhabu kali kali hutolewa na hatua stahiki huchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusu kuwasaidia wasanii; katika mpango tulionao wa kuhakikisha kwamba tunatatua changamo hii ya dawa za kulevya ambayo inawaathiri vijana wengi ikiwemo nguvu kazi ya taifa hili, moja kati ya kazi kubwa tunayofanya ni kuendelea kutoa elimu juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile katika mpango mmoja wapo ni kuhakikisha kwamba tunafanya kitu kinaitwa *supply reduction* kuhakikisha kwamba madawa hawa hayapatikani na hivyo kutokuwalazimu vijana wengi zaidi kuweza kuyatumia. Tume imefanya kazi kubwa mpaka hivi sasa na wameendelea kukamata na kuteketeza dawa nyingi na hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana wa dawa za kulevya katika viunga vya miji yetu mingi ya Tanzania kutokana na kazi kubwa ambayo inafanywa na tume.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bulembo Halima.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuku kwa kuniona. Kumekuwa na malalamiko mengi ya waathirika wa dawa za kulevya wanapokuwa *rehab (rehabilitation)* wanakaribia kupona wahusika wanawachoma tena dawa ya kulevya ili wasiweze kutoka na lengo limekuwa ili waendelee kujipatia fedha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha *rehab* zao wenyewe ili kuweza kuwasaidia waathirka hawa dawa za kulevya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya *sober house* zinamilikiwa na watu binafsi na hilo lililolalamikiwa na Mheshimiwa Mbunge hatujapata malalamiko rasmi. Hata hivyo niseme tu kwamba kwa kuzingati hizi *sober house* nyingi ziko chini ya watu binafsi tumeamua sasa kutengeneza miongozo ambayo itasaidia namna bora ya *management* ya hizi *sober house* ili inapotokea mazingira ya namna hiyo tuwe tuna sehemu ya kuweza kukabiliana nao, kwa sababu miongozo ile itakuwa inaeleza mtu ambaye ni muathirika wa madawa ya kulevya awe *treated* vipi. Mpango wa Serikali, katika swali lake, ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *sober house* nyingi za Serikali ili kuondokana na changamo hii ambayo wananchi wengi wanaipata hasa kutokana na gharama kubwa ya kulipia katika hiyo *sober house*.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa suala la madawa ya kulevya ni suala ambalo walinzi wake ni wananchi wote, hatuwezi kuiachia Mamlaka na Serikali peke yake. Mbunge, mwananchi unapouona kuna athari kama hiyo unatakiwa useme, utoe taarifa kwa mamlaka zinazohusika, Mheshimiwa Waziri Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Tumepokea hii taarifa sasa mara kadhaa na hata wakati wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wametuarifu kwamba uko mchezo mbaya unaoendelea kwenye *sober house;* badala kuwasaidia vijana wetu wapone na waondoke ndani ya *sober house*, lakini taarifa ambazo tumekuwa tukizipokea ni kwamba wamiliki

wa *sober house* wanataka kuendelea kuwaweka vijana wetu pale kwa faida binafsi. Naomba sasa nitoe tena agizo kwa wamiliki wa *sober house* wote ambao wana mchezo huo ambao umekuwa ukisemekana wauache haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninatumia muda huu pia kuiagiza mamlaka sasa kuanza kufanya uchunguzi wa kina na atakaye bainika ana tabia hiyo aweze kuchukuliwa hatua haraka sana na hiyo itatusai kuwaokoa vijana wetu kutokuendea kutumia dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha.

Na. 136

**Mafanikio ya Mradi wa MIVARF**

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA** aliuliza:-

Mradi wa Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi Vijijini *(MIVARF)* katika Mkoa wetu wa Kusini Unguja umeweza kuwakomboa wananchi kwa kuongeza uzalishaji wa mazao na kuboresha mawasiliano ya barabara na kuweza kusafirisha mazao yao kwa urahisi. Kwa kuwa mradi huu umeonesha mafanikio na wananchi wamehamasika.

Je, Serikali ipo tayari kuwaongezea mitaji na mafunzo wananchi hao ili waweze kufikia malengo yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha inaunga mkono juhudi za wananchi kushiriki katika uchumi wa kilimo kwa kusaidia upatikanaji wa mitaji na kuwapatia mafunzo stahiki. Hatua za kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kimtaji zilianza kwa kuvijengea uwezo wa kiutawala na kiutendaji Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na vikundi vingine vya uzalishaji ili viweze kuratibu na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya mitaji itakayopatikana kupitia mikopo inayotolewa na taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matayarisho yanaendelea ili kuvipatia vikundi vya wazalishaji ambavyo tayari vimehakikiwa na uwezo wao baada ya ziara ya uongozi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* kutembelea Zanzibar mwezi Mei, 2017. Benki hii ni mshiriki mkubwa wa *MIVARF,* ambayo huendesha mfuko wa dahamana (*Guarantee Fund*) wa mikopo utakaofanya benki kuwakopesha wakulima kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekit, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango na Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* wamesaini makubaliano ya uendeshaji wa mfuko wa dhamana tarehe 3 Novemba, mwaka 2017. Kwa kupitia makubaliano hayo, Serikali tayari imetoa shilingi bilioni 22 kwa *TADB* ili kuanza utekelezaji kwa kushirikisha benki za biashara kufikisha huduma ya mikopo kwa makundi mbalimbali. *TADB* walishaanza utaratibu huu kwa kutangaza kwenye magazeti ili kupata benki zitakazoshiriki. Nawashauri wananchi wote watumie fursa hii adhimu kujipatia mikopo ili kupanua shughuli zao za maendeleo na kujiongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa kitoa mafunzo mbalimbali kwa wananchi kupitia mradi wa *MIVARF* ili waweze kuyafikia masoko yenye tija. Mafunzo hayo ni pamoja mbinu bora za kilimo (*good agricultural practice),* uongezaji thamani mazao na jinsi ya kuyafikisha masoko yenye tija na kukuza na uimarishaji Vikundi vya Akiba na Mikopo *(SACCOS).* Programu kupitia kwa watoa huduma *(Business Coaches)* inaendelea kutoa mafunzo haya kwa

wananchi hasa katika Nyanja za kuongeza thamani mazao na kuyafikisha masoko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza niipongeze kupitia mradi huu, kwa kweli imejitahidi sana kwa haya waliyoyasema na wanachi tayari wameonesha matunda na uzalishaji umekuwa. Mheshimiwa Jenista ni shahidi alikuja kutembelea maeneo ya Kongoroni na akajionea jinsi gani wananchi walivyoimarika katika uzalishaji wa kilimo cha ndimu. Kwa taarifa niliyonayo sasa hivi kwamba mitambo ya kiwanda cha ndimu tayari imefika na tayari imejaribiwa bado ufungaji tu naamini kazi hiyo itafanyika. Kwa kuwa mradi huu umeonesha maendeleo makubwa na bado kuna maeneo mengine yanahitaji mradi kama huu.

Je, Serikali kupitia mradi iko tayari kuendelea kwa yale maeneo mengine ambayo hayajafikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swala langu la pili elimu haina mwisho; kwa kuwa vikundi hivi vineonesha mwelekeo mzuri na bado vingali na changamoto ya kuyafikia masoko lakini hata kuongeza ujuzi wao.

Je, mradi huu uko tayari kuendelea na vikundi hivi ili kufikia lile lengo la kuondokana na uchumi mdogo na kuingia uchumi wa kati katika ulimwengu huu wa sasa hivi wa viwnda? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, tayari Serikali inafanya vizuri, kwa hiyo majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kama

Serikali kupitia mradi huu utaendelea kuyafikia maeneo ambayo hayafikiwa. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba mradi huu ambao una lengo la kwenda kurekebisha miundombinu ya barabara na masoko maeneo ya vijijini na kuongea tija katika mazao unaendelea kuwanufaisha Watanzania, na kadri ambavyo miradi inazidi kuibuliwa basi tutayafikia pia na yale maeneo ambayo bado hayaguswa kutokana na maelekezo na mwongozo wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Mheshimiwa Mbunge amezungumza kuhusu suala la mafunzo na kuviendeleza vikundi ambavyo vimeshapatiwa fedha kupitia mradi huu. Kwa mujibu wa utaratibu wa mradi huu wa *MIVARF* miradi hii ikisha ibuliwa katika halmashauri kazi sisi tunayoyanya ni kuwezesha na baadaye kazi ya kuendelea kuvilea vikundi hivi inabaki katika halmashauri husika. Kwa hiyo niendelee tu kumuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sababu tayari mradi huu umeshafanya kazi yake eneo la uendelezaji wa vikundi hivyo pia na wenyewe kwa nafasi yao waweze kushiriki kuhakikisha kwamba vikundi hivi vinakuwa endelevu na viweze kuleta tija kwa Mtanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, swali namba 138 Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga. Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha tayari, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Ofisi ya Rais.

Na. 137

**Kuzifungua Zahanati za Solowu na Makoja**

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifungua Zahanati za Solowu na Makoja ambazo zimekamilika ili kuwapunguzia adha ya kufuata huduma ya afya vijiji vya mbali akina mama, watoto, wazee na wananchi wa vijiji hivyo kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati za Solowu na Makoja zimejengwa na Halmashauri kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Ujenzi wa Zahanati ya Solowu imegharimu shilingi milioni 79.605 ambapo wananchi wamechangia shilingi milioni 10.6 na Halmashauri imechangia shilingi milioni 69; na ujenzi wa Zahanati ya Makoja imegharimu shilingi milioni 137.26 ambapo wananchi wamechangia shilingi 640,000.00 na Halmashauri imechangia milioni 136.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Zahanati za Solowu na Makoja zimetengewa fedha *MSD* kiasi cha shilingi 640,800.00 kila moja kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa katika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha, na tayari Halmashauri imepeleka *order* kwa ajili kupatiwa dawa kwa matumizi ya zahanati hizo. Dawa na vifaa hivi vitachukuliwa kutoka Bohari ya Dawa ya Serikali Dodoma mara taratibu zitakapokuwa zimekamilika. Aidha, baadhi ya vifaa na vifaa tiba mbalimbali kwa ajili ya zahanati hizi vilishanunuliwa na vimehifadhiwa katika Kituo cha Afya cha Chamwino na vitapelekwa kwenye zahanati hizo kabla ya mwisho wa mwezi huu Aprili, 2018. Vifaa na vifaatiba hivyo ni pamoja na vitanda vya kuzalishia, vifaa vya kutakasia, magodoro, seti za kuzalishia, vitanda vya hospitali, mizani ya kupimia uzito kwa watoto na watu wazima, vifaa tiba, vitanda vya kupimia wagonjwa, mashine za kupimia shinikizo la damu, samani kwa maana ya meza, viti na makabati pamoja na ma-*shelves* ya kuhifadhia dawa. Wakati huo hu halmashauri imepanga watumishi wawili wa kada ya uuguzi kwa kila zahanati ambao wataanza kutoa huduma ndani ya mwezi ujao wa mwezi Mei, 2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makanyaga.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yanayotia moyo wananchi wa Jimbo la Chilonwa. Lakini pamoja na majibu mazuri sana naomba niwe na swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya sababu zinazofanya badhi ya watumishi kukwepa kwenda kufanya vijiji vya ndani ndani ni ukosefu wa nyumba za kuishi.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kusaidia upatikanaji wa nyumba katika zahati zilizo vijiji vya ndani ndani sana? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaka, Mbunge wa Ikulu kuwa kwanza naomba niipongeze Halmashauri ya Chilonwa kwa jinsi ambavyo wameweza kukamilisha zahanati nne. Yeye katika swali lake anauliza namna Serikali kuwezesha kupatikana nyumba za watumishi. Kama ambavyo amefanya kazi nzuri kwa kushirikiana na Halmashauri yao kuhakikisha wanakamilisha zahanati hizo ni vizuri jitihada hizo ambazo zimefanyika wakaanzisha uanzishaji na ukamilishaji wa nyumba za watumishi kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba ukiwa na zahanati nzuri bila watumishi kuwa na sehemu iliyo salama ya kwenda kufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba na mimi nimuulize Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli katika Kata ya Makuyuni, Lemowoti na Halaramii

wameonesha juhudi kubwa katika ujenzi wa vituo vya afya; na kwa kuwa Waziri wa TAMISEMI alivyokuja Monduli mwaka 2016 akiwa Naibu Waziri aliahidi kutoa michango kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za wananchi wale. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya kuwasiadia wananchi wale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri na kwamba na yeye mwenyewe atakiri na kuungana na jitihada za Serikali na hivi karibuni tumepeleka pesa katika vituo 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba safari ni hatua, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinajengwa katika kila kata. Kama tumefanya katika kata nyingine, naamini kabisa na kwake itakuwa katika safari ijayo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu ni mdogo. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

Na.138

**Kushuka kwa Kiwango cha Elimu Mkoani Tabora**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Kiwango cha elimu katika Mkoa wa Tabora kimeshuka sana, Mkoa umefanya vibaya katika mtihani wa darasa la saba, kidato cha nne na cha sita. Kufanya vibaya kunatokana na changamoto mbalimbali kama walimu, upungufu wa madawati na idadi kubwa ya wanafunzi katika madarasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kero hizi zinatatuliwa ili kurejesha hadhi ya elimu Mkoa wa Tabora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, ambaye ni mtoto wa shangazi yangu na Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zilizotajwa katika swali, si kweli kwamba kiwango cha elimu kimeshuka sana Mkoani Tabora kwa kufanya vibaya kwenye mitihani. Takwimu zinathibitisha hali tofauti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika mitihani ya darasa la saba ya mwaa 2016 kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 71.35 ambapo Mkoa wa Tabora ulishika nafasi ya 10 kitaifa, lakini mwaka 2017 ufaulu ulipanda hadi asilimia 73.61 na Mkoa ukaendelea kushika nafasi ya 10 kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2016 kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 71 ambapo Mkoa wa Tabora ulishika nafasi ya 10 kitaifa, lakini mwaka 2017 ufaulu ulipanda hadi asilimia 84 na Mkoa kushika nafasi ya 3 Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa upande wa kidato cha sita, ufaulu mwaka 2016 ulikuwa asilimia 97.8 na Mkoa wa Tabora ulishika nafasi ya 11 kitaifa. Kwa mwaka 2017 pamoja na takwimu kuonesha kuwa ufaulu ulikuwa asilimia 87, nafasi ya mkoa kitaifa ilipanda hadi nafasi ya 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka yote miwili mfululizo, Mkoa wa Tabora umekuwa juu ya wastani wa ufaulu kitaifa, hilo ni jambo la kujivunia. Kwa hali hiyo hatuwezei kusema kiwango cha elimu katika Mkoa wa Tabora kimeshuka bali kimepanda. Serikali ina kila sababu ya kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na viongozi wote wa Mkoa wa Tabora wakiwemo viongozi wa wilaya zote na hamashauri zote kwa juhudi zao zilizowezesha matokeo hayo mazuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambaye na yeye pia ni mkazi wa Mkoa wa Tabora katika Jimbo la Sikonge anafahamu hali halisi ya elimu za watoto wetu na ndugu zetu katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea hapa na takwimu zinazooneshwa ni shule chache ambazo zimefaulu kwa kiwango kikubwa zinatengenezewa takwimu na zinaonekana kwamba ndiyo takwimu halisi; lakini uhalisia uliopo katika Mkoa wa Tabora, elimu yetu imeshuka kutokana na miundombinu hakuna walimu. ...

**MWENYEKITI:** Swali, uliza swali, uliza swali.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** ... je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha wa kuboresha miundombinu ya elimu katika Mkoa wa Tabora ili watoto wetu waweze kufanya vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika shule za sekondari ambazo ni shule zilizokuwa zinafaulisha vizuri miaka ya nyuma ambapo watu wengi humu ndani wamesoma katika shule hizo leo shule hizo zimekuwa na changamoto za vitanda, changamoto za viti na changamoto za miundombinu mbalimbali. Serikali ina mpango gani pia wa kuweza kuhakikisha maeneo yale yanaboreshwa ili shule zile ziweze kufanyavizuri kama ilivyokuwa hapo awali?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimsifu san binamu yangu kwa kufuatailia sana sekta ya elimu. Nakubaliana nae kwamba kuna baadhi ya shule hususani za pembezoni kabisa hazifanyi

vizuri lakini mara nyingi tunapozungumzia mkoa huwa tunajumlisha kupata matokeo ya kimkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, Serikali ina mpango gani kuboresha miundombinu? Kama tulivyowasilisha bajeti yetu vizuri ya juzi, tumejidhatiti kweli kweli. Mwaka huu tumepeleka walimu 112 katika shule za msingi, walimu wa sayansi tumepeleka walimu 20 katika Mkoa wa Tabora lakini kwa mwakani 2018/2019 tutajenga vyumba vya madarasa 207, matundu ya vyoo 689, nyumba za walimu 123 na kwa upande wa sekondari tutajenga nyumba za walimu 179, vyumba vya madarasa 159, matundu ya vyoo 166 na kukamilisha maabara 163 kwa ajili ya masomo ya sayansi. Tunaamini kuwa mchango huu utasaidia kuboresha sana hali ya ufaulu wa vijana wetu katika shule mbalimbali za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili; shule maalum ambazo zilikuwa zinafaulisha sana zamani. Kwanza naendelea kuzipongeza shule hizo ikiwemo *Tabora Boys* ambayo imekuwa ikichangia sana kuinua ufaulu wa Mkoa wa Tabora na ni kweli kwamba baadi ya miundombinu yake iko katika hali ambayo inahitaji sana msaada na naomba niungane nae katika kuzifuatilia shule hizo ili tusaidiane katika kuzitendea haki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo yanayowakabili wananchi wa Mkoa wa Tabora yanafanana kabisa na wananchi wa Mkoa wa Morogoro hususani katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki hasa katika shule ya Mkuyuni ambayo upungufu wa madarasa yanayohitajika ni zaidi ya 18, shule ya msingi Ngerengere Njia Nne madarasa 21 yanahitajika na shule ya msingi Mikese Fulwe madarasa zaidi ya 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa uwezo wa halmashauri yetu ni mdogo na uwezo wa wananchi kujenga madarasa haya yote ni mdogo sana. Je, Serikali kuu ina mpango gani wa kutusaidia kumaliza tatizo hili la vyumba vya madarasa ili kuinua ubora katika shule zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimwa Omari Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki nikutane naye baada tu ya Bunge mchana saa saba na nusu ili tuweze kupanga mikakati pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Udhaifu katika sekta ya elimu ni mkubwa kwa nchi nzima na hiyo imekuwa ni mjadala kwa muda mrefu na Wabunge hapa wanaulizia miundombinu na mambo mengine kama walimu, mishahara, yapo ni mambo mtambuka. Sasa Serikali haioni umuhimu, ili elimu yetu iweze ikawa sawa, bora na shirikishi kwa wote, tukawa na mjadala wa Kitaifa namna ya kuboresha elimu kwa kuwa ndio tunda la mfumo wa maendeleo yote Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sanaMheshimiwa James Mbatia kwa kurejea kauli ambayo aliitoa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wetu mstaafu kuhusu mjadala wa kitaifa ambao sasa hivi tunafikiria namna ya kuuandaa. Kwahiyo naomba ashiriki na sisi katika kuandaa mjadala huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu ni mdogo, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kaboyoka.

Na.139

**Uharibifu wa Mazingira Mto Yongoma na Saseni-Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza:-

Uharibifu wa mazingira kwenye Msitu wa Chome (Shengena) umeleta athari kubwa ya uchafuzi wa maji hasa katika Mito mikubwa ya Yongoma na Saseni; mito hiyo kuanzia kwenye vyanzo vya maji imebadilika rangi na kuonesha rangi yenye matope. Kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilikanusha kwamba hakuna ushahidi unaoonesha kwamba athari za mazingira katika msitu huo zinatokana na uchimbaji wa madini ya *bauxite.*

(a) Je, Serikali ipo tayari kuunda Kamati ya kuchunguza chanzo cha uharibifu huo katika Msitu wa Shengena?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwapatia wananchi miti ya asili inayoongeza maji ili kudhibiti upungufu wa maji katika vyanzo vya maji mito hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira kwenye msitu wa Chome - Shengena unachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo shughuli za kilimo katika maeneo jirani yanayozunguka mlima Shengena na wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu waliovamia msitu huo miaka ya nyuma kati ya mwaka 2008 na 2010. Katika kutatua changamoto hii Serikali iliunda timu ya watalaam kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa

la Hifadhi ya Mazingira yaani *NEMC,* Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS),* Ofisi ya Madini Mkoa wa Kilimanjaro na Bodi ya Mto Pangani ambayo ilitembelea eneo hilo kwa nyakato tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hiyo ya wataalam ilibaini changamoto za uharibifu wa mazingira katika eneo hilo na kupendekeza hatua za kuzuia uharibifu huo ambazo zimetekelezwa ikiwa ni pamoja na kuzuia shughuli za uchimbaji wa madini ndani ya msitu kwa kuweka ulinzi ambao unafanywa na Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).

Hivyo, Serikali itapitia upya mapendekezo ya timu ya wataalam na kuhakikisha kuwa ina...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hebu vuta hiyo *microphone* karibu kwako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): ...**hivyo, Serikali itapitia upya mapendekezo ya timu ya wataalam na kuhakikisha kuwa yanatekelezwa kikamilifu na iwapo itaonekana ni lazima kuunda Kamati, Serikali haitasita kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* imeanza kuchukua hatua za kuwapatia wananchi miti ya asili na rafiki kwa mazingira kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji katika Mito ya Yongoma na Saseni. Aidha, katika jitihada za kutunza vyanzo vya maji katika eneo hili, Serikali kupitia *TFS* imepanda miti ya asili takribani 2500 kati ya mwaka 2012 mpaka 2017 ndani ya eneo la Msitu wa Chome lililoharibiwa na shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kuwasihi viongozi na watendaji wa Serikali katika ngazi zote kuchukua hatua kadri itakavyowezekana kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili kudhibiti uharibifu wa mazingira nchini.

**MWENYEKITI:** Mhesimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kama Mheshimiwa Waziri atafuatilia na naamini ataunda hiyo Kamati maana najua bado mazingira ni machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni kwamba; kwa kuwa hii mito mikubwa minne ya Yongoma, Saseni, Hingilini na Nakombo imejaa magogo ambayo yameletwa kutoka misituni na hivyo kufanya maji yatuame na yasiwafikie watu walioko mabondeni.

Je, Waziri atatusaidiaje au Serikali itatusaiaje kufundisha wananchi na kuwapa vifaa ili waweze kufanya usafi wa ile mito yaani Kiingereza wanaita *dredging* ili watoe yale magogo ili maji yaweze kufikia wananchi walioko bondeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana. Jiandae Mheshimiwa Mlata.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Mito ile ya Hingilini, Saseni, Yongoma pamoja na Nakombo ni kweli imeathiriwa na shughuli za kibinadamu yakiwemo hayo mdgogo aliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kifupi tutauma tena timu ya wataalam ili waende waone ukubwa wa lile tatizo na baada ya kuona ukubwa wa lile tatizo watatupa taarifa ambayo tutawashirikisha wananchi wenyewe katika maeneo yale ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha juu ya matatizo haya ambayo yanafanyika katika vyanzo vya maji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kaboyoka usiwe na wasiwasi na kama utakuwa tayari kuambatana na mimi nitakapokuja kule, mimi nitakuwa tayari pia kuambata na wewe, ahsante sana.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Nitakuwa tayari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Iramba, Tarafa ya Ndago, Kata ya Ndago kwenye Magereza ya Ushora ambayo yana "A" na "B", Ushora pamoja na Mirungu kulikuwa na msitu mkubwa na miti mikubwa ambayo ilikuwa ni chakula cha tembo lakini wafungwa wale wamemaliza ile miti hadi wale wanyama wamehama kule. Waziri ananiambia nini kuwapelekea miti wale wafungwa wakapande waturudishie msitu wetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni lini, hana mazungumzo mengi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Martha Mlata, alipokuwa kwenye Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira alikuwa anazungumzia sana juu ya ukataji wa miti hovyo kwenye Gereza la Ushora. Mimi niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote na niwakumbushe kwamba suala kulinda, kutunza na kuhifadhi mazingira kwa mujibu wa kifungu namba sita cha Sheria Namba 20 ya mwaka 2004 sote tunawajibika kufanya hivyo. Tuendelee kuhakikisha kwamba zile taasisi ambazo ziko kwenye maeneo yetu yakiwemo magereza, shule, hospitali wahakikishe kwamba wanatumia nishati mbadala kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyoelekeza.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Martha Mlata kupitia swali lako hili, naendelea kuzitaka taasisi zote ambazo tulishazielekeza wasiendelee kukata miti kwa ajili ya nishati, waendelee kutumia nishati mbadala na katika siku ya Mazingira Duniani ambayo tunaanza tarehe 30 Mei mpaka tarehe 5 Juni, 2018 kutakuwa na maonesho ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kwa kifupi sana majibu yako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** ...watu mbalimbali katika kutumia nishati mbadala. Mheshimiwa Martha Mlata nitakuwa tayari kuambatana na wewe kwenda Gereza la Ushora, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hilo ndiyo jibu sahihi. Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Waswahili wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta. Imekuwa ni tatizo linaloendelea na ni maneno kila siku yanazungumzwa kuhusiana na uharibifu wa vyanzo vya maji na hususani Chemchemi.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha inatoa elimu kwa wananchi wote wanaozunguka maeneo ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha kwamba wao ndio walinzi lakini hao hao wawe ndiyo watunzanji wa mazingira wa maeneo yale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sera yetu hii ya Taifa ya Hifadhi ya Mazingira pamoja na Sheria ya Mazingira tayari Mheshimiwa Waziri alishatoa miongozo na maelekezo kwa Halmashauri zote 185 Tanzania watuletee orodha ya vyanzo vyote vya maji ikiwa ni pamoja na changamoto. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuko katika harakati za kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati ya utoaji wa elimu kwa wananchi ambao wako kwenye vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwenye Magazeti ya Serikali. Ahsante sana.

**MWENYEKIT:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

Na.140

## Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Mabonde ya mpunga katika Vijiji vya Masela, Bukangilija na Mwatigi katika Wilaya ya Maswa yanaweza kuzalisha mpunga mwingi kuliko ilivyo hivi sasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa na mifereji ya umwagiliaji katika maeneo hayo ili kuwawezesha wakulima kuongeza tija katika uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina mikakati ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchi nzima ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imekuwa ikiendekeza *scheme* za umwagiliaji zinazotumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua kwa kujenga mabanio ya kuchepusha maji na mfumo wa mifereji ya umwagiliaji katika mashamba. Kwa maeneo ambayo yemeonekana yanafaa usanifu wa kina hufanyika na kisha ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Maswa ipo miradi mbalimbali ya umwagiliai inayotumia mifumo mbalimbali ikiwemo miradi ya umwagiliaji ya Masela, Bukangilija na Mwatigi. Kwa mradi wa Masela wenye eno la hekta 450 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ulifanywa usanifu wa mwanzo wa ujenzi wa mabwawa na mifereji. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina ili ujenzi wa bwawa na mifereji ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umwagiliaji wa Bukangilija wenye hekta 307 ulijengwa mwaka 2004 kupitia Mpango wa Kuendeleza Kilimo Wilayani *(DADPS)* hivyo miundombinu yake imechaka na inahitaji ukarabati mkubwa. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ukaratabati wa mradi huo kwa upande wa bonde la Mwatigi lenye ukubwa wa hekari 100. Mwaka 2013 chini ya ufadhili wa *World Food Program* ulichimbwa mfereji mkuu lakini miundombinu mingine haikujengwa hivyo fedha zitahitajika kukamilisha ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kufanya usanifu wa awali ili kuangalia uwezekano wa ujenzi wa mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo yaliyotajwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka jana niliuliza swali kuhusiana na bwawa la Mwamihanza nikaambiwa Serikali inatafuta fedha; mwaka huu pia nimeuliza juu ya miradi hii ya umwagiliaji kwenye vijiji hivi vitatu majibu ya Serikali ni kwamba bado Serikali inatafuta fedha. Sasa nataka kuiuliza Serikali, pesa itapatikana lini? Kwa sababu kwenye Bwawa la Masela usanifu ulishafanyika na watu walishaondolewa kwenye eneo ambalo bwawa litachimbwa. Sasa Serikali inapata pesa lini ili kuanza ujenzi wa Bwawa la Masela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inapata pesa kidogo sana, ndiyo maana miradi mingi ya umwagiliaji inakwama. Mradi wangu wa Bukangilija umekwama wa Mwatigi umekwama wa Kulimi umekwama sasa ni lini Serikali itatenga kiasi cha fedha cha kutosha ili kushughulikia miradi ya umwagiliaji hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze kwanza Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofanya kazi. Pili, amezungumzia kuhusu suala la uchache wa fedha na lini Serikali itatoa fedha. Pamoja na Serikali kutoa fedha lakini kupitia ziara tulizokuwa tumezifanya tumeona katika miradi mingi ya umwagiliaji kumekuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tuna miradi ya zaidi ya 889 ambayo imejengwa lakini miundombinu yake haijakamilika, lakini la pili ipo miradi 54 ambayo imejengwa lakini haifanyi kazi kabisa. Kutokana na changamoto hiyo Waziri wangu akaona haja ya kupitia mpango kabambe wa mwaka 2002 wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili kuangalia namna gani tutaweza kutumia fedha ingawa kwa uchache lakini miradi iwe yenye tija. Nataka nimhakikishie kupititа mapitio haya tuliyoyafanya miradi ile ambao tumeiorodhesha na tumeibainisha ipo haja ya kutengeneza maaboreshe na ili hata kama miradi inatekelezawa lazima iwe miradi ambayo imekamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu miradi yake ambayo ameelekeza, katika miradi ambayo tumeanisha na yeye tutamuweka katika utekelezaji ili miradi iende kwa wananchi kama zamani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na swali moja la nyongeza. Mji wa Kibondo unakaabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa maji, na mji huo uko kilimani. Pampu zinazosukuma maji kusambaza ndani ya mji wa Kibondo zimechakaa, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya mradi wa maji Wilayani Kibondo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni lini? Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa

Mbunge Genzabuke kuhusiana na matatizo ya maji ya Kibondo, kwanza Mheshimiwa Genzabuke pamoja na wananchi wa Jimbo la Kibondo nikufahamishe tu kwamba tayari tunasaini mkataba wa mkopo wa fedha nafuu kutoka Serikali ya India na katika ya fedha hizo sehemu ya fedha itashughulikia utoaji wa maji, huduma ya maji katika mji wa Kibondo, kwa hiyo sasa hivi vuta subira mambo baada ya muda mfupi yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine halafu Mheshimiwa Murad.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Maji mengi sana ya mvua yanapotea katika nchi hii kiasi kwamba tungekuwa na utaratibu wa kuyavuna yangeweza kusaidia katika shughuli za umwagiliaji na shughuli za wanyama. Kwa mfano katika Jimbo langu la Rombo kuna mito ya msimu kama Ungwasi, Marwe, Tarakea, Uashi pamoja na Nana ambapo maji ya mvua ambayo yanakwenda nchini Kenya wale wameyazuia wanafanya nayo umwagiliaji halafu wanatuletea tena bidhaa huku kwetu.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari utakapopata nafasi twende wote Rombo ukayaone haya mabonde ya mito hii ya msimu ili tuweze kuangalia uwezekano wa kuyazuia ili tuweze baadae kuyatumia kwa ajili ya umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Selasini Mzee wangu, mimi kama Naibu wa Waziri wa maji nipo tayari baada ya Bunge twende pamoja Rombo ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Catherine halafu Mheshimiwa Murad.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la

nyongeza; katika Wilaya ya Karatu mkoa wa Arusha kijiji cha Mang'ola kuna biashara kubwa ya kimataifa ya vitunguu ambapo robo ya mapato ya Halmashauri ya Karatu yanatokana na kilimo hiki cha vitunguu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea mabwawa na mifereji ya umwagiliaji wananchi hawa wa Mang'ola ili kuongeza tija kuwainua kimaisha wananchi wa Karatu hasa akina mama waliowekeza katika kilimo hiki cha vitunguu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Murad.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu asilimia kubwa zaidi ya 70 wanaishi vijijini na wanategemea kilimo cha kudra za Mwenyezi Mungu kwa maana ya mvua. Kwa hiyo sisi kama Wizara ya Maji tukaona haja sasa ya kuwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika kuhakikisha kilimo chetu kinakuwa bora na tija katika suala zima la uzalishaji, kwa maana ya kupata malighafi za viwandani na hata katika suala zima la biashara. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo katika kuhakikisha tunatengeneza miundombinu ya umwagiliaji eneo hilo ili wananchi wale waweze kunufaika na kilimo cha kisasa.

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa Murad, ajiandae Mheshimiwa *Bulembo Senior*.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo lililopo Maswa Magharibi linafanana na la Mvomero, na kwa kuwa Mvomero kuna maji mengi, kuna mabonde mazuri sana na kwa kuwa wananchi wa Mvomero wamejipanga katika kilimo cha umwagiliaji, na kwa kuwa kuna ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Maji injinia Isack kwa kusaidia

mabonde mawili, Bonde la Kigugu na Bonde la Mbogo, je, ni lini fedha zile zitatoka ili kuleta tija kwa wananchi wa Mvomero na Taifa kwa ujumla? (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri majibu; Mheshimiwa Waziri muhusika.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika bajeti ya mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa miradi ya Kigugu na usanifu umekamilika, wakati wowote Mheshimiwa Murad nikuhakikishie hatutaingia kwenye kutangaza *tender* kuhakikisha kwamba hiyo miradi imetekelezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Dar es Salaam pale kwenye kulaza bomba la kutoka Bagamoyo kuja Chuo Kikuu kuna watu walivunjiwa na watu wengine wakakataa wakapelekwa mahakamani, walipopelekwa mahakani wameshindwa mpaka leo wanasema wanalindwa na wakubwa hawataki kuvunja nataka Wizara iniambie wanavunjiwa lini ili Dar es Salaam tupatae maji Chuo Kikuu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanayo taarifa kwa sababu wameshapewa *notice* kwamba wanavunjiwa, kwa hiyo ni wakati wowote hatua za kuvunja zile nyumba zitafanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea swali namba 141 Mheshimiwa Dkt. Mponda.

Na. 141

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Katika Vijiji vya Mkoa wa Morogoro**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Mkoa wa Morogoro umechaguliwa kuwa ni Ghala la Chakula la Taifa hususani katika mazao ya mpunga na miwa. Katika kutaekeleza hili Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ujenzi wa skimu za umwagiliaji katika Vijiji/Kata za Usangule – Mto Lwasesa, Igawa – Mto Furua, Lupunga – Mto Mwalisi na Kilosa – Mto Mwalisi.

(a) Je, ni lini kazi hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itakamilika?

(b) Katika kipindi hiki cha maandalizi ya ujenzi wa mabanio haya ya kilimo cha umwagiliaji, je, Serikali ina utaratibu gani wa usimamizi wa ardhi husika ili kuepuka migogoro ya watumiaji wa mabanio hayo siku za usoni?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa maji na umwagiliaji naomba kijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya kuongeza wigo wa kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mengi hapa nchini yakiwemo maeneo yaliyotajwa. Utekelezaji wa shughuli hizo unategemea upatikanaji wa fedha. Katika mwaka huu wa fedha 2017 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Vijiji/Kata za Usengule Mto Lwasesa, Igawa Mto Puma, Lupunga Mto Mwalisi na Kilosa Mto Mwalisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kuepuka migogoro ya watumiaji wa mabanio ya maji kwa siku za usoni, Halmashauri ya Malinyi inashauriwa kuandaamipango ya matumizi bora ya ardhi ambapo ardhi inayofaha kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji itabainishwa na kutengwa rasmi kwa matumizi hayo. Mipango hii itawezesha usimamizi wa kisheria wa ardhi inayofaa kwa umwagiliaji katika maeneo ya vijiji hivyo. Aidha, wakati wa kuanza ujenzi wa mabanio hayo kutaundwa vyama vya umwagiliaji kulingana na sheria ya umwagiliaji ya mwaka 2013. Vyama hivyo vitakuwa na jukumu la kusimamia maeneo hayo na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Dkt. Mponda.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pia ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri hao wote wawili wa Wizara hii; Waziri na Naibu wake wamefika eneo hilo. Mara ya mwisho mwezi wa pili Mheshimiwa Naibu Waziri amefika na wana Malinyi tumempa jina la Dogo Janja. Ameona hali halisi pale katika Skimu ya Itete, kwa kuwa imetokana na usanifu wa kina ambao haukuwa mzuri na hata ujenzi ule uliofanyika haukuwa mzuri imesababisha skimu ile inashindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu ile haina barabara za kuingia kwenye mashamba, skimu ile wakati wa kiangazi haina maji ya kutosha kumwagilia mashamba yale na Serikali wameadhidi kwamba watafanya marekebisho swali langu la kwanza, ni lini mtafanya marekebisho ambayo mmehaidi kwenye Skimu ya Itete?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, menejimenti ya skimu ile inasimamiwa na injinia ambaye anakaa Malinyi kilometa 50 kutoka pale kwenye skimu mpaka anapoishi yule injinia; tuliomba ombi maalum apatiwe usafiri injinia yule, ni lini sasa ombi hili litatekelezwa? Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muhusika.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimefika pale Itete na Mheshimiwa Naibu Waziri amefika. Tatizo moja kubwa la Itete ni kwamba skimu ipo haijakamilishwa ujenzi lakini inafanya kazi. Tatizo lililo kubwa ni kwamba sasa hivi baada ya kumaliza huu mpango kabambe tunataka kujenga bwawa kubwa ambalo litatunza maji ili wananchi waendelee kulima wakati wote. Tatizo lingine lililokuwepo ni kwamba ile Kamati iliyokuwa imeundwa ambayo inasimamia kilimo kile cha mpunga ilikuwa na makosa kidogo, tukaivunja na sasa hivi tumeweka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi lake la kwamba injinia sasa awe sehemu ya karibu kwa ajili ya kusimamia ile skimu tutalitekeleza tuwasiliane Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kumpatia huyo injinia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikipanga miradi mingi ya umwagiliaji katika mkoa wa Morogoro ambayo haitekelezeki, je, Serikali sasa haioni kuna haja ya kwuaatumia wataalam ambao wanatoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA)* waweze kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Morogoro kuendeleza kilimo cha umwagiliaji?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizarani pamoja na changamoto ambazo tumeziona tukaona haja sasa ya kupitia ule mpango kabambe, na tumejipanga katika kuhakikisha tunakuwa na miradi michache lakini yenye tija ya uzalishaji katika nchi yetu. Kwa hiyo, wazo lako na ushauri wako tumeupokea katika kuhakikisha tunaboresha

miundombinu ya umwagiliaji ili iweze kuwa na tija katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea swali namba 142 Wizara hiyo Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

Na. 142

**Mradi wa Umwagiliaji Katika Kijiji cha Nundwe Mufindi**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Mheshimiwa Mizengo Pinda akiwa Waziri Mkuu mwaka 2013 aliahidi kuchangia shilingi 295,000,000 katika mradi wa umwagiliaji uliopo kijiji cha Nundwe, kata ya Ihalimba.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo ili wananchi wa eneo hilo waweze kujikwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2013 alitoa ahadi ya kuchangia kiasi cha shilingi 295,000,000 katika ujenzi wa mradi wa umwagiliaji wa kijiji cha Nundwe kata ya Ihalimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari serikali ilishaanza utekelezaji wa mradi huo kwa kuwezesha upimaji wa ulalo wa ardhi, usanifu wa banio, ujenzi wa banio, ujenzi wa mfereji mkuu wenye urefu wa mita 2000 na ujenzi wa maumbo ya mashambani. Kazi zote hizo zilikamilika mwaka 2015 na kugharimu kiasi cha shilingi 101,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa mradi huo kwa wananchi wa Kijiji cha Nundwe na Taifa kwa ujumla Serikali itaendelea kutafuta na kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji iliyobaki kwa lengo la kuongeza uhakika wa usalama wa chakula na kipato na hivyo kujikwamua kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Ahante Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu mstaafu alipotembelea kwenye kijiji hiki alikuta tayari Serikali imeshaanza kutekeleza, lakini yalijitokeza mapungufu ambayo yalikuwa yanagharimu milioni 295,000,000 kwa ajili ya kujenga mifereji *(main canal),* kwa ajili ya kujenga vivuko vya watu na wanyama na kwa ajili ya kujenga vigawa maji kuelekea mashambani. Pia kumalizia na kuongeza eneo la mfereji lifike kilometa 2.2 na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya kuona hilo akaahidi kwa wale wananchi wa Nundwe kwamba niko tayari kutoa shilingi 295,000,000 mradi huu uweze kukamilika. Mradi huu ukikamilika utaajiri vijana...

**MWENYEKITI:** Swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye swali, utaajiri vijana walio wengi. Sasa swali langu hapa linasema lini hiyo shilingi 295,000,000 itatoka kusudi haya mambo ambayo tunayazungumza yaweze kutekelezwa Mheshimiwa Waziri? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri aje kwenye *site* aone hili jambo ambalo tunalizungumzia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge mzee wangu Mgimwa, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Kwa hiyo kama Mwenyekiti wangu ahadi ni deni na sisi kama viongozi wa Wizara hii hatutokuwa kikwazo katika kuhakikisha tunakamilisha ahadi ile ambayo imetolewa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Pinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu ahadi ya mimi kwenda kule katika jimbo lake, nipo tayari Mheshimiwa Mbunge na Mwenyekiti wangu kuongozana pamoja katika kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa mradi ule ili hatimaye tuongeze jitihada kwa haraka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ungando, atafuatiwa na Mheshimiwa Massare na Mheshimiwa Bobali ajiandae.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyogeza. Kwanza sina budi kuwashukuru vyombo vyote vya ulinzi na usalama, Kibiti hali shwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, wananchi wa maeneo ya Delta, Mbwela, Msala, Salale, Mapaloni, Kiongoloni wana shida kubwa ya maji ambayo sasa inapelekea hata ndoa kulegalega kwenye nyumba. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji safi na sala katika maeneo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Delta tayari tumelifanyia utafiti na tumechimba visima kiasi. Ukienda zaidi ya mita tano unapata maji ya chumvi, kwa hiyo, sasa tunajaribu kuangalia mfumo mzuri ambao utahakikisha kwamba wananchi wa Delta

wanapata maji bila shida, lakini ukienda mita nne tayari tumechimba visima wanapata maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Massare ajiandae Mheshimiwa Bobali na Balozi Mwamoto.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyopo huko kwenye jimbo Mheshimiwa Mgimwa yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika jimbo langu ambapo Serikali imeonesha nia njema ya kujenga skimu ya umwagiliaji katika Bwawa la Itagata. Sasa kwa kuwa bwawa hili lilikuwa lilishaanza kuvuja na ile pesa ya kujenga skimu Serikali; maana ya Wizara ilituambia tutoe ili tuwape wale wakandarasi wa umwagiliaji kutoka Wizarani wa kuziba mabwawa; sisi pesa tumeshalipa.

Je, Serikali sasa iko tayari kurudisha ile pesa haraka ili na sisi *certificate* iliyioko kwenye halmashauri tuweze kumlipa mkandarasi katika Skimu ya Umwagiliaji ya Itagata? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri muhusika majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kwanza nimpongeze kwa jinsi anavyofuatilia shughuli za ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji na kweli Bwawa la Itagata limekamilika. Naomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki leo tukutane ili tuweze kuangalia jinsi ya kukupa hiyo fedha muende mkakamilishe miradi mingine inayoendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Balozi Mwamoto ajiandae Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Mheshimiwa Waziri amekuwa akija Mkoani Lindi mara kwa mara, zaidi ya mara

mbili au tatu nimekutana naye kwa ajili ya mradi ule wa maji pale Napa. Lakini tuna Skimu ya Umwagiliaji iliyopo kwenye Jimbo la Mchinga, ya Kinyope na skimu nyingine iko Jimbo la Mtama kwa Mheshimiwa Nape, ya Kiwalala. Skimu hizi zilijengwa chini ya kiwango na hivi sasa hazifanyi kazi vizuri ingawa zilitumie pesa nyingi ya Serikali. Je, Waziri uko tayari kutuma wawakilishi wako au wewe mwenyewe kwenda kujionea kinachoendelea katika skimu hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli skimu hizo zilitekelezwa, zilikumbwa na matatizo ya mafuriko lakini kwa sasa tayari tunazifanyia kazi ili ziweze kujengwa na kutimiza matakwa ambayo yalikuwa yanatakiwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi huduma nzuri ya maji ili waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji. Niko tayari kwenda kutembelea eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Balozi Mwamoto, ajiandae Mheshimiwa Bashe.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi lilikuwa linauliza habari ya ahadi za viongozi. Mheshimiwa Rais aliahidi pale Ilula, Kilolo kwamba suala la maji litakuwa ni historia. Nataka nijue Mheshimiwa Waziri ni lini mkataba ule utasainiwa ili wananchi wa Kilolo, Ilula tatizo la maji liwe historia kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ujenzi wa mfumo wa maji Kilolo. Tulikuwa tunatarajia kwamba fedha ambazo zingetumika ilikuwa ni fedha kutoka Austria, lakini baada ya kuona kwamba fedha za Austria zinachelewa Serikali kwa kutumia makusanyo ya ndani imefanya mchakato imekamilisha na tarehe 30 Aprili, Jumatatu ijayo

tunakwenda kutia saini mkataba ili sasa utekelezaji uanze wananchi wa Kilolo wapate maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashe ajiandae Mheshimiwa Paresso.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nimshukuru Waziri kwa utekelezaji wa mradi wa visima katika Jimbo la Nzega. Naomba kujua mwaka 2015 moja ya hadi kubwa ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kufufua skimu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Idudumo katika Halmashauri ya Mji wa Nzega. Je, ni lini ahadi hii Serikali itaanza utekelezaji wake kwa ajili ya kulipitia na kulirekebisha bwawa hilo na kutekeleza ahadi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Anataka kujua ni lini tu, sasa usianze kuzunguka zunguka.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na napenda nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge juu ni lini utekelezaji. Miradi ya utekelezaji wa umwagiliaji inategemeana na fedha. Fedha zitakapopatikana ka wakati na sisi tutatekeleza kwa wakati katika kuhakikisha mradi huu unakamilika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa vitunguu katika Tarafa ya Eyasi wanayo miundombinu ya umwagiliaji ambayo imejengwa na *World Vision* na fedha za *DADPs* na Shirika na Maendeleo la Jimbo Katoliki la Mbulu na Waziri Mkuu alikuja kuzindua. Tatizo kubwa si miundombinu kama ambavyo imeelezwa na Mbunge mmoja hapa, suala ni uhifadhi wa chanzo ambao wakulima wale wanatumia kumwagilia vitunguu vyao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhifadhi chanzo kile ili wananchi waweze kulima zao hilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Waziri mhusika.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Eyasi linatumia chanzo cha maji ya mbubujiko kutoka chini ya ardhi eneo la Mang'ola. Nilikwenda kule na tayari tumeshaweka mipaka ili kuzuia wananchi wasifanye shughuli za kibinadamu karibu na vile vyanzo. Mipaka hiyo inaendelea kuwekwa na Mheshimwa Mbunge tuendelee kushirikiana, na kama utaona kwamba kuna kitu ambacho hakiendi vizuri, tuwasiliane. Lengo ni kuboresha ili yale maji yaendelee kutoka kila wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis

Na. 143

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mkokotoni**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Mkokotoni kiliungua mnamo tarehe 27/12/2010 na ujenzi wake ulianza mara moja.

Je, ni lini ujenzi huu utakamilika na kituo hicho kuendelea na shughuli zake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kituo cha polisi cha Mkokotoni kilipata ajali ya moto mwaka 2010. Baada ya kuungua kwa kituo hichi, wananchi wa eneo husika waliendelea kupata huduma za kipolisi kupitia jengo

lililokuwa pembeni na kituo kilichoungua moto. Serikali kupitia Jeshi la Polisi ilitafuta mkandarasi ambaye alianza kujenga upya kituo hicho na kwa sasa ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 80. Aidha, shughuli za Kituo cha Polisi cha Mkokotoni zitaanza katika jengo jipya baada ya kukamilika kwa ujenzi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri tuliyoyazoea, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban tangu kuungua kwa kitu hiki ni miaka tisa na kipindi hicho chote askari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kiasi wanahatarisha afya zao. Kwa kuwa Serikali imeshindwa kukamilisha kituo hiki katia muda mwafaka, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kukifunga kituo hiki mpaka ujenzi wake ukamilike kwa usalama wa skari wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kupunguza madeni ya wakandarasi. Kituo cha Mkokotoni kimetengewa shilingi milioni 200 kwa ajili ya mkandarasi aliyejenga kituo kile, nataka kujua, je, mkandarasi huyo ameshalipwa pesa zake? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hatuna mpango wa kukifunga hiki kituo kwa sababu mipangilio ya kukiendeleza, kukikamilisha iko mbioni na ndiyo maana naomba nichukue fursa hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshafanya uhakiki na kuwasilisha Hazina ili mkandarasi aweze kulipwa na ujenzi uweze kukamilika. Kitakapokamilika kituo hiki kitatumika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha bajeti maswali mwisho ni saa nne. Najua Wabunge mna mambo mengi lakini na mimi nafuata Kanuni na Mwongozo ambao ninapewa na wakubwa.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliopo Jukwaa la Spika, mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Adelardius Kilangi, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ni Mheshimiwa Said Ally Said, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Katibu wa Bunge ambao ni madaktari kutoka Hospitali ya Saratani ya *Ocean Road,* Taasisi za Moyo ya Jakaya Kikwente na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili walioletwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* waliokuja Bungeni kwa ajili ya uchunguzi wa afya za Waheshimiwa Wabunge. Ahsante, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mbunge na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wapiga kura wake kutoka Ushetu Mkoa wa Shinyanga. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 130 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana na Ajira ambao ni wanachama wa umoja wa mafundi cherehani Mkoani Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa umaa Aweso, Mbunge na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye ni mpiga kura wake kutoka Pangani Mkoa wa Tanga, Ndugu Omary Kibwanga, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Khadija Nassir Ali ambaye ni baba yake mzazi kutoka Zanzibar, *Engineer* Nassir Ali Juma. Karibu Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Allan Kiula, (Mbunge) ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa - CCM kutoka

Mkalama Mkoani Singida wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Jackson Masaka. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, (Mbunge) ambao ni viongozi wa CCM Jimbo la Amani na wapiga kura wake kutoka Zanzibar, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Maria Kangoye (Mbunge) ambao ni wadogo zake pamoja na wafanyabiashara kutoka Arusha.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Josepher Komba, (Mbunge) ambao ni ndugu zake kutoka Musoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni rafiki zake kutoka Lushoto Mkoani Tanga, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Nassor Omar (Mbunge) ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha (Mbunge) kutoka Sumbawanga Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Ally Ungando (Mbunge) kutoka Jimboni kwake Kibiti Mkoa wa Pwani, ambao ni Ndugu Yusuph Momboka mwenyekiti wa Kijiji cha Nyamisati, Ndugu Abdallah Mapande Mwenyekiti wa Kijiji cha Mfisini na Ndugu Hamada Ngokoro, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mchinga, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Machano Said (Mbunge) ambaye ni ndugu yake kutoka Mjini Magharibu Ndugu Juma Ahmed. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 48 na walimu watano kutoka shule ya awali na msingi ya El Shaadai ya Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Washiriki 100 wa shindano la tunzo za vipaji vya kazi mbalimbali za wanafunzi kutoka Vyuo Vikuu vyote vya hapa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Frank Peter. Karibuni. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 15 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kilichopo Mkoani Dodoma.

Tangazo la mechi za kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi kwa ujumla kuwa kesho tarehe 26 Aprili, 2018 katika Uwanja wa Jamhuri kutakuwa na mechi za kirafiki za mpira wa miguu na *netball* kati ya *Bunge Sports Club* na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki – *EALA.* Mechi hizo zinatarajiwa kuchezwa jioni baada ya kumalizika sherehe za maadhimisho ya Muungano. Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi mnaalikwa kuhudhuria mechi hiyo.

Ofisi ya Waziri Mkuu kwa pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais inawaalika Waheshimiwa Wabunge wote kwenye sherehe ya Muungano kwenye viwanja vya Jamhuri kesho kuanzia sa amoja asubuhi. Kadi za mialiko zitasambazwa na Ofisi ya Katibu wa Bunge. Ratiba na utaratibu wote umetolewa na Bunge. hili tangazo limetolewa na Mheshimiwa Jenista, *Chief Whip.*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamuita Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea na shughuli za Bunge.

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia kiti*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jana baada ya kipindi cha maswali Mheshimiwa Spika alitueleza utaratibu wa namna ya kupata zile *e-passports.* Alieleza mahitaji ya aina tatu ili kupata hizi *passport* mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Amina Mollel aliomba pia Mwongozo akionesha jinsi wenzetu walemavu watakavyopata shida kwenda kwenye lile Jengo la *Immigration* hapa Mkoani. *Immigration* wana *files* za Wabunge wote, wana picha za Wabunge wote, wana *fingerprints* za Wabunge wote na isitoshe sisi Wabunge tulipopata *passport* tulizonazo walikuja kwenye majengo ya Bunge ambapo ilikuwa ni rahisi sana na tulipata *passport* tukiendelea na shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako, ni kwa nini wasiagizwe wakafanya kama walivyofanya tulivyopewa hizi *passport* tulizonazo wakaja hapa, tukapata hizo *passport* wakaendelea na shughuli zao, na kwa njia hiyo walemavu watapata kwa urahisi hapa Bungeni, wale ambao ni Wabunge wenzetu wakati huo huo mambo mengine yakiwa yanaendelea huko katika Jengo lao la *Immigration* kuhusu namna watu wengine watakavyopata hizi *passport. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. ABDALLAH S. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa kazi zilizopo mezani leo ni pamoja na Wizara yetu ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; na kwa kuwa Wizara hii inahusisha taasisi nyingi, mojawapo taasisi yetu ya *SUMATRA* inayosimamia suala la usafirishaji na kwa kuwa kwa muda wa siku tatu sasa Jiji la

Dar es Salaam wananchi wetu wanautumia usafiri wa *UDA,* mabasi yaendayo kasi wamepata tatizo kubwa la upataji wa tiketi na malipo kuhusu usafirishaji. Kwa kuwa jambo hili limetokana na mgogoro uliopo kati ya *UDART* na *MaxMalipo* ambao walikuwa wakisimamia mfumo wa ukusanyaji malipo, na kwa kuwa mgogoro huu unasababisha wananchi ndio wanaathirika na ndani yake inaonekana kuna upotevu wa fedha na malalamiko mengi kwamba kuna ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi naomba Mwongozo wako, Serikali inasaidiaje wananchi wa Dar es Salaam, hasa wanaotumia mfumo hu wa usafiri ili kuhakikisha tatizo hili linaondoka na kuhakikisha sintofahamu hii iliyopo kati ya *UDART* na *MaxMalipo* inaondoka? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi nilikuwa na hoja hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitoa ya kuhusiana na mgogoro wa usafiri katika Jiji la Dar es Salaam na nilikuwa naomba nitumie Kanuni ya 47(1), (2) na (3) ya kuomba Bunge lako tukufu lisitishe shughuli zilizopo kwa sasa ili mjadala uwepo wa kuhusiana na suala zima la usafiri wa Jiji la Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kwa idhini yako tutumie Kanuni ya 47(1), (2) na (3) ili uwepo mjadala mzima kuhusiana na suala la usafiri wa Dar es Salaam. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kuna taarifa zilizunguka kwenye mitandao kauli ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa John Heche na taarifa hizo leo zimesambaa kwenye mitandao na kwenye magazeti ya

leo kwamba maisha yake yako hatarini, lakini pia imeunganishwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu aliwahi kusema kwamba na yeye anafuatiliwa na watu wasiojulikana, akataja na magari, hata hivyojambo hilo halikupewa uzito sana na matokeo yake Mheshimiwa Lissu alipigwa risasi nyingi na mpaka tunavyozungumza sasa tuko Bungeni mwenzetu yuko kitandani anaendelea na matibabu na maumivu makali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba Mwongozo wako kwa sababu kama mwenzetu amepata taarifa hizo na ameongea na vyombo vya habari na taarifa zimesambaa mtaani kwamba maisha yake yako hatarini. Jambo hili tungeomba Mwongozo wako kwa sababu Mheshimiwa Spika alizungumza siku za karibuni kwamba sisi wabunge tuko salama sana sasa tungetaka kujua kwamba mwenzetu uhatarishi wa maisha yake unasababishwa na nini na nini hatua za dharura za kuchukua ili na sisi wengine tujue kama tupo salama tufanye kazi za Kibunge bila kuwa na hofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ili jambo hili tupate majibu ya Serikali na mwenzetu asikilizwe hoja zake, wanaomtishia maisha ni akina nani, wametumia mbinu zipi, wanataka kumfanyaje ili kuanzia yeye mwenyewe, familia yake, chama chake, ndugu zake wa Tarime, Mkoa wa Mara na Watanzania wengine tufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzetu anasema maisha yake yako hatarini, jambo hili halikubaliki tunaomba mwongozo wako ili tuweze kujua kinachoendelea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Wabunge kadhaa hapa nitaanza na mwongozo wa Mheshimiwa Selasini ambaye yeye ametoa maelezo kwamba jambo hili lilitokea jana na akatoa maelezo hapo kwamba Mheshimiwa Spika alieleza kuhusu

utaratibu wa kupata *passport* na ametoa maelezo marefu Mheshimiwa Selasini na sina haja ya kuyarudia.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka jambo hili kama limetokea jana mwongozo wake ulipaswa kuwa jana na si leo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Selasini kama yanahitajika maelezo ya ziada kuhusu jambo hili utafute tu utaratibu mwingine Kiti hakina mwongozo juu ya jambo lililotokea jana.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Mtulia ambaye yeye anatoa maelezo kwa kuihusisha hoja ambayo iko mbele yetu leo, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu mgogoro ambao upo kati ya *UDART* na *MaxMalipo* na kwamba mgogoro huu unaleta tabu kwa wananchi na Serikali inaweza kusema nini. Yeye amehusisha na hii hoja iliyopo mbele yetu leo na kwa kuwa siku ya leo tutapata majibu ya Serikali wakati wa kufunga hoja, Mheshimiwa Waziri amelisikia hilo, nadhani atalitolea maelezo wakati akifunga hoja yake.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kubenea yeye hajaomba mwongozo lakini ameomba matumizi ya Kanuni ya 47 ili hoja ambayo ameshaisema Mheshimiwa Mtulia ya *UDART* iweze kujadiliwa na Bunge hili kama jambo la dharura. Kanuni ya 47 inahusu jambo la dharura lile ambalo haliwezi kutumia utaratibu wa kawaida. Kwa kuwa Mheshimiwa Mtulia ameshaomba mwongozo wa Kiti na Kiti kimeagiza Serikali itoe maelezo kuhusu jambo hili watakapohitimisha hoja yao jambo hili haliwezi kujadiliwa na Bunge sasa kwa sababu halina udharura huo.

Mheshimiwa Salome Makamba nazungumza na wewe unazungumza, ni tabia mbaya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Waitara na yeye ametoa maelezo kwamba siku ya jana yalitoka maelezo kuhusu maisha ya Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Zitto kwamba yako hatarini. Pia ametoa maelezo kwamba leo mjadala umeendelea kwenye

mitandao na magazeti na ametoa mambo haya akiyahusisha na jambo ambalo lilimpata Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye mpaka sasa yuko kwenye matibabu na akalihusisha pia na maelezo ambayo yameshawahi kutolewa na Mheshimiwa Spika kuhusu usalama wa Wabunge na kwamba Mheshimiwa Spika aliwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba wako salama.

Sasa yanapotokea mambo kama haya yaliyojadiliwa jana lakini pia leo yanaendelea kujadiliwa kwenye mitandao ya kijamii na magazeti, Mheshimiwa Waitara anaomba mwongozo wa Kiti kuhusu jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, mimi niwaombe Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Zitto mambo haya wakayaripoti polisi na Waziri yuko hapa kwa sababu jambo hili limezungumzwa na Mheshimiwa Mbunge na ni kuhusu usalama wa Wabunge lifuatilie kwa karibu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio maelezo ya Kiti, tutaendelea, Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nimeletewa majina hapa ya wachangiaji tulionao kwa siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Lucy Owenya ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya awali ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba Wizara hii ukiangalia kwenye fedha za maendeleo ndiyo Wizara ambayo inapata fedha nyingi kuliko Wizara zote. Kwa sababu katika shilingi trilioni 12 za maendeleo Wizara hii ambayo najua ni Wizara kama tatu zina takribani shilingi trilioni 4.1 sawa na asilimia 33. Pamoja na kupata fedha nyingi kiasi hiki tunaona ni jinsi gani barabara zetu zinavyojengwa chini ya viwango na fedha zinaibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitajikita zaidi kwenye suala ambalo lililetwa na Mheshimiwa Kiwanga akisema kwamba Mkoa wa Morogoro hawakuwa na *Road Board* wala *RCC* na Mheshimiwa Zitto alitaka kusimama kuomba Mwongozo, lakini haikuwezekana. Huu ni mwendelezo wa jinsi gani Serikali inayosema ni Serikali ya wanyonge lakini kama kilometa nne zinaweza kujengwa kwa shilingi bilioni 13 wakati katika hali ya kawaida kilometa moja ni kuanzia shilingi milioni 700 mpaka shilingi bilioni moja leo tunazungumzia shilingi bilioni 13 na zaidi kwa kilometa nne, hii inamaanisha kwamba kilometa moja imejengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Jambo hili tunaliona ni wizi mkubwa na najua Mheshimiwa Magufuli amekuwa akisema anapambana na rushwa.

Sasa tunaitaka Serikali na Waziri atakapokuja kutoa majumuisho jioni atuambie fedha hizi zimekwenda wapi na wahusika wamechukuliwa hatua gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni upanuzi wa barabara ya Morogoro. Haya masuala ya ubaguzi yakiendelea katika nchi hii tunaenda pabaya. Haiwezekani katika eneo moja la barabara, mimi ninavyojua barabara inapaswa iwe imenyooka na iwe na upana wa kufanana. Barabara ya Morogoro inapoanzia kule bandarini upana wake ni kama mita 35 mpaka 40; lakini inapofika Ubungo hasa maeneo ya Kimara barabara ile upana kwa pande zote

mbili ni mita 121. Kwa hiyo, naomba kufahamu hivi barabara siku hizi inakuwa sawa na chatu aliyemeza mtu au barabara inapaswa iwe imenyooka? Tunaomba maelezo najua Mheshimiwa Naibu Spika na wewe unakaa kule na umeona ni jinsi gani watu wamebomolewa halafu zinapokuja kauli kwamba hawa wabomelewe au hawa wasibomelewe kwa sababu wamenipa kura, haya mambo hatuwezi kuyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nije kwenye suala zima la hapa Dodoma. Inajulikana kwamba Wabunge wengi, Mawaziri pamoja na wewe mwenyewe tunakaa maeneo ya *Area D.* Ilikuwa kuja Bungeni tunatumia takribani dakika tatu au nne, ilikuwa ni kama kilometa moja na nusu lakini sasa hivi tunakwenda mwendo wa kilometa sita na tunazunguka kwenye maeneo hatarishi sana. Wengine ukifika kwenye ile shule na tunashukuru Mungu kwamba kuna ile shule pale ambayo tunaweza kupita kwenye miti mvua zikinyesha tunahamia pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najua kuna teknolojia ya kila aina, hivi ni kwa nini Mheshimiwa Waziri na niliongea naye wasichimbe barabara ya chini hapa *airport* ili magari yaweze kupita chini? Najua Mheshimiwa Waziri umetembea nchi nyingi haya tunayajua. Jana kuna mmoja alisema kwamba magari ya Wabunge yawe yanapita, lakini tujue kuna *emergency landing* ya ndege jambo ambalo ni hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hapo ni nusu kilometa tu kujenga barabara ya chini ili magari yaweze kupita na hasa ukizingatia kwamba hata yale maeneo pale biashara zimekufa kabisa. Kwa hiyo, naomba sana jambo hilo lifanyike kwa sababu tunaona barabara nyingine ya kwenda kwa Waziri Mkuu kule inajengwa tulidhani hii ya hapa ambayo inapitisha watu wengi ingekuwa rahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nyumba za *TBA,* nimesoma kwenye kitabu hiki, mimi nimekaa kwenye nyumba ya *TBA* huu ni mwaka wangu wa 11, haijawahi kukarabatiwa

wala kufanywa chochote hasa ukizingatia miundombinu ya maji ni ile ya zamani sana na kwa maana hiyo tunahitaji wabadilishe miundombinu hiyo ili iwe ya plastiki. Mimi nashangaa kama wameshindwa kuzi-*maintain* hizi nyumba ni bora wawauzie Wabunge au watu wanaozihitaji waweze kuzi-*maintain. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa kwamba *TBA* wanapewa vibali vya kujenga nyumba mbalimbali *including* zile hosteli za Magufuli ambazo zimekuwa na *expansion joint* ni kwamba hawana uwezo, lakini huku wanaendelea kupewa matumizi makubwa ya kwenda kujenga nyumba mbalimbali. Kwa hiyo, mimi niseme kwa kweli haya mambo haya tukiendelea kunyamaza kama wenyewe wanashindwa ku-*maintain* za kwao wanawezaje kwenda kujenga na huko kwenye kujenga tayari wameharibu. Kwa hiyo, nadhani *TBA* kuna tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie barabara ya kutoka Bahama Mama kwenda Chuo Kikuu. Barabara ile kwa kweli imesaidia sana lakini bado haijakamilika. Kwa hiyo, tunaomba kujua hii barabara ya Goba - Makongo mpaka Chuo cha Ardhi inaisha lini? Vilevile ile ya Msewe ambayo kwa kiasi kikubwa imeharibu sana mazingira ya Chuo Kikuu. Barabara za chuo kikuu zimekufa kabisa kwani zimekuwa na mashimo makubwa, tunaomba sana mmalize ili watu waweze kupita kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ili kusiwe na malalamiko CHADEMA leo wana nafasi mbili, CCM wana nafasi saba na CUF nafasi moja. CHADEMA yameletwa majina matano, Mheshimiwa Susan ameshachangia na nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Owenya. Kwa hiyo, isije ikaonekana kwamba meza ndiyo ambayo haijachukua muda, kwa hiyo, mna majina mawili.

**WABUNGE FULANI:** Ni dakika tano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan hajachangia dakika tano.

**MBUNGE FULANI:** Dakika tano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna utaratibu kama tuna nafasi ndogo za kuchangia, tunagawana dakika tano. Kumekuwa na tabia ya upande wa Wabunge wa Upinzani kupunjwa dakika na meza ya Makatibu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Halima Mdee alikuwa achangie dakika 10 kachangia dakika sita na sisi tuna saa tunaangalia. Mheshimiwa Susan Lyimo amechangia dakika tano. Kwa muktadha huo, kama CHADEMA tuna nafasi mbili kwa dakika kumi na tena siyo mbili hapa tumeambiwa nafasi tatu, tunapaswa kuchangia watu sita. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya nimesema hivi CHADEMA nafasi mbili, CUF nafasi moja na CCM nafasi saba. Hapa mezani naambiwa Mheshimiwa Susan amechangia dakika saba tutazifanya tano ili turahisishe uchangiaji. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Owenya atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri mara nyingi nimekuwa nikizungumza naye kuhusu kilio changu cha barabara ya Old Moshi - Kiboroloni - Kikarara - Tsuduni. Mheshimiwa Waziri anafahamu kabisa umuhimu wa barabara ile, ni barabara

ambayo *KINAPA* ime-*identify* kama njia ya kupanda mlima kwa ajili ya watu mashuhuri, lakini kwa sasa hivi barabara ile haipitiki, ni mbaya, lakini mmekuwa mkitupa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016/2017 kwenye kitabu cha Waziri alitenga shilingi bilioni 2.583; kwa mwaka 2017/2018 mkatenga shilingi milioni 811 na mwaka 2018/2019 ukurasa wa 198 mmetenga shilingi bilioni moja. Naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, *TANROADS* Makao Makuu wamesema wameshauza *tender* na upembuzi yakinifu unaendelea, ni lini sasa barabara ile itaanza kutengenezwa badala ya kutuwekea tu fedha kwenye makabrasha lakini hamtengi fedha hizi. Naomba atueleze ni lini sasa barabara ile itaanza ili wananchi wa kule Old Moshi waweze kufaidika ili na Serikali iweze kupata mapato kutokana na ile njia ya kupanda Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu lakini *Moshi Airport* imesahaulika kabisa. Mlisema mnatenga fedha kwa ajili ya *Moshi Airport*, uwanja huu ni *very strategic.* Wageni wakija kupanda Mlima Kilimanjaro wanaweza wakatumia *Moshi Airport* wakaruka wakaenda Seronera ambayo ina-*save time* na wakaweza kwenda mpaka Zanzibar, lakini uwanja ule sasa hivi umekuwa ni wa kulima maharage na karanga. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri ana mpango gani maana tayari *airport* iko inaweza ikatumika pia kwa *emergency landing.* Atakapokuja ku-*windup* atatueleza wana mikakati gani kwa ajili ya *Moshi Airport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kuhusu reli ya Dar es Salaam mpaka Arusha; sijaona katika mkakati wana mpango gani na reli ile. Tumekuwa tunalalamika barabara zetu zinaharabika, malori yanabeba mizigo mizito sana inaharibu barabara, lakini ile reli ingeweza kutumika ikabeba mizigo ikapeleka Arusha, mizigo ingetoka Tanga ambako kuna bandari ikaletwa Dar es Salaam au Moshi kwa njia ya reli. Sasa hivi tunatumia malori halafu barabara zinaharibika na tunalalamika malori yana-*overload* lazima ya-*overload* kwa sababu wanahitaji fedha, lakini tungetumia treni na

kukawa na treni ya wageni pia wageni wangeweza kutumia kama *scenery* kwa ajili ya kuangalia nchi yetu na vivutio vyetu kupitia reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAMESA* ilijengwa mikoa yote ili kuokoa fedha za Serikali za kutengenezea magari ya Serikali. Tayari *TAMESA* kuna mashine na vipuri kwa ajili ya kutengeneza magari, lakini vimepitwa na wakati, miundombinu iko pale lakini kwa nini hawatengi fedha ili waweze kununua miundombinu ya kisasa ili gari za Serikali ziweze kwenda kufanyiwa *service* kule *TAMESA* ili kuokoa fedha za Serikali? Sasa hivi *TAMESA* wamekuwa ni wakala wa *private sector* badala ya *TAMESA* kutengeneza magari wamekuwa wakitoa barua wanawapa Serikali, Serikali inaenda kupeleka kwa Mchina wanaenda kutengeneza gari hizo, sasa huu siyo ufisadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa jinsi gani wamejiandaa kuirudisha *TAMESA* iweze kufanya kazi ili tuweze kuokoa fedha nyingi ambazo zinapotea kwenye *private sector.* Maana yake hamuwalipi kwa wakati wanaongeza 10% au pengine hawa watu wa Serikali ndiyo wanaoongeza 10% unakuta matumizi ya Serikali yanakuwa makubwa sana. Hamuwalipi wakati na wao wenyewe wamekopa benki mwisho wa siku unakuta fedha zinakuwa ni nyingi sana kwa wale ambao wanatengeneza magari *TAMESA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba niungane na wenzangu kuzungumzia *TBA*. Nyumba za *TBA* ni mbaya na mbovu. Sasa hivi *TBA* wamepewa zile nyumba za Uhindini, zilizokuwa za *CDA,* huwezi kuamini mtu anaweza kuishi pale. Mmewahamisha wafanyakazi kutoka Dar es Salaam mnakuja kuwaweka kwenye yale magofu, hivi huu ni utu? Mtu kaacha nyumba yake Dar es Salaam, familia yake, watoto wake mnakuja kuwaweka kwenye haya magofu?

Mimi nataka kujua Serikali mtaiwezeshaje *TBA* ili waweze kutengeneza zile nyumba watu waweze kuingia ndani waishi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kiisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Sebastian Kapufi ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mara nyingi nimekuwa nikieleza hapa kwamba huduma ya simu katika Wilaya ya Rombo hasa maeneo ya Useri, Tarakea, Ukanda wa Chini na Mkuu kuna muingiliano mkubwa sana kati ya mitandao yetu na mitandao ya Kenya hususan *Safaricom.* Ukiwa Tarakea pale lazima uwe na laini ya huku kwetu Vodacom na uwe na *Safaricom.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikijibiwa kwamba hii inatokana na mitandao yetu kuwa dhaifu. Sasa ni kwa nini Serikali isifanye mkakati wa makusudi wa kutatua tatizo hili kwa sababu wananchi wanajikuta wameingia kwenye utaratibu wa *roaming* bila wao kukusudia na matokeo yake wanatumia pesa nyingi sana. Naomba hili sasa lishughulikiwe nipate majibu kwamba tatizo hili litaisha lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuna barabara kutoka Mamsera - Mahida – *KNCU* - Abiola ambayo ilichukuliwa na *TANROADS,* ilifanyiwa kazi kwa miaka kama miwili, mitatu hivi, lakini tangu mwaka wa fedha 2014/2015 barabara ile imetelekezwa mpaka sasa haijafanyiwa kazi yoyote. Tunataka kujua *TANROADS* imeamua kuiachia halmashauri barabara ile au bado iko chini ya *TANROADS?* Kama bado iko chini ya *TANROADS* basi ile barabara ishughulikiwe kwa sababu sasa haipitiki hata kwa tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, mimi nilipongeza uanzishwaji wa *TARURA* kwa sababu nilisema zile barabara za Halmashauri wakati mwingine zilikuwa zinatengenezwa kisiasa kwa Madiwani kila mmoja kuvutia upande wake, lakini fedha zinazotengwa kwa ajili ya *TARURA* ni ndogo. Jana nilikuwa naongea na *Engineer* wa *TARURA*

kule kwangu anasema pesa walizonazo wana mkakati wa kutengeneza barabara mbili tu. Sasa nashangaa barabara nyingine za Wilaya nzima zitajengwa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kusema, sisi Wabunge kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Nimekuwa nikisikia malumbano mengi kuhusu Taarifa ya *CAG,* shilingi trilioni 1.5 na kadhalika. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nawashauri Wabunge wenzangu tuwe tunasoma hivi vitabu. Mwaka wa fedha wa 2015/2016 *CAG* alikuja pia na vitabu hapa na akasema mapato ya Serikali yalikuwa ni shilingi trilioni 21.9, matumizi shilingi trilioni 20.2 na akaonesha kwamba kulikuwa na shilingi trilioni 1.088 ambazo zilikuwa zinahitaji maelezo, hayakutoka. Sasa hiki kinachoulizwa sasa hivi tunakijadili kisiasa wakati ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba fedha hizi zinaonekana ili hii miradi ya maendeleo ambayo tunapigia kelele hapa iweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, hizi sio fedha zetu ni fedha za wananchi. Mimi nawaomba Wabunge wenzangu, tunapojaribu mambo ya kitaifa tuyajadili tukijua kwamba tunajadili kwa niaba ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kusema hakuna Mbunge yeyote wa upinzani ambaye anakataa ufufuaji wa *ATCL,* ambaye anakataa miradi inayojengwa ya reli, barabara na kadhalika kwa sababu ziko kwenye Ilani. Tunachokisema hapa ni kwamba tunashauri ufufuaji huu uende kwa namna ambayo baadae Taifa halitapata hasara. Kama ni ununuaji wa ndege basi taratibu zifuatwe, kama ni *management, management* ziangaliwe, kama ni utengenezaji wa *route, route* ziangaliwe, hicho ndicho tunachoshauri, lakini hakuna Mbunge yeyote wa upinzani ambaye anasema shirika lile lisifufuliwe au tusitengeneze reli au mradi mwingine wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *infact* sisi tunataka maendeleo na hii miradi ikifanikiwa ni kwa faida ya Taifa hili. Moja tu tunalosema, tunatahadharisha miradi hii wataalam wasikilizwe, wataalam washauriwe, ushauri wa kitaalam ukubalike ili Taifa lisipoteze pesa kidogo za wananchi bila sababu yoyote ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mimi namshauri Rais na namshauri tena kwamba Mheshimiwa Rais cha kufanya aagize wataalam wapeleke *documents* zote zitakazoonesha kwamba shilingi trilioni 1.5 zimetumika na siyo vinginevyo. Hapa hatusemi kwamba kuna mtu kaiba, tunachosema Afisa Masuuli abebe makabrasha yake aende nayo kwa *CAG* aseme kwamba fedha nimezitumia hivi, *CAG* afunge hoja, kama Afisa Masuuli atashindwa fukuza kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Daniel Mtuka ajiandae.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza, nataka nijiridhishe, nina dakika kumi eeh?

**NAIBU SPIKA:** Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, majina yaliyoletwa hapa yanaashiria kwamba kila mtu anachangia dakika tano ili yaishe. Kwa hiyo, kila mtu ni dakika tano.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimeomba dakika kumi.

**NAIBU SPIKA:** Sasa hilo linakuwa siyo la kwangu mimi tena, wao waniambie ni yupi atolewe ili wewe upewe dakika kumi.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri zaidi inayofanywa. Pia nimpongeze Mheshimiwa Profesa Mbarawa, ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa na mwenzangu Mheshimiwa Nditiye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu madogo. La kwanza katika kuunga mkono jitihada za kuhamia makao makuu na kuchochea maendeleo ya maeneo ya makao makuu tumeona hapa kwenye *CDD,* mji wa makao makuu tunajenga *ring roads* lakini pia tunahitaji kujenga *ring roads* kwenye wilaya za pembezoni mfano unazungumzia Katesh - Kondoa, Babati - Kiteto ili na haya maeneo mengine ya pembezoni yaweze kuchochewa maendeleo kwa kupitia miundombinu ya barabara kama za lami. *Ring roads* zitengenezwe sio tu kwa makao makuu lakini nje ya mji wa makao makuu kwa kiwango cha lami. Hii itatusaidia sana katika kuchochea maendeleo ya maeneo yale ya pembezoni. Hilo ni moja ambalo ningeshauri lifanyiwe mchakato na lenyewe liweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la *TARURA.* Hawa watu wa *TARURA* na wenyewe ni wataalam kama ambavyo *TANROADS* walivyo lakini barabara zinazotengenezwa na *TARURA* zinaonekana kama ziko chini sana ya viwango. Unatengeneza barabara hakuna mitaro wala matoleo matokeo yake mahitaji ya matengenezo yanakuwa ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri tutengeneze vigezo vya viwango kwamba kila barabara inayotengenezwa iwe na viwango kama ambavyo kwenye *TANROADS* wanatengeneza ili barabara hizi ziweze kudumu na kukaa muda mrefu *whether* ni ya *light grading* au iwe *heavy grading* lakini vigezo vya mitaro kwa maana ya mifereji na matoleo viweze kuwepo maji yapite barabara zidumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine hapohapo kwenye *TARURA,* nadhani ni muhimu kidogo kuongeza bajeti. Ule mgawanyo wa 30 kwa 70 sasa tuufikirie hata kama sio 50 walau 40. Najua kiwango cha barabara zinazotengenezwa na *TARURA* haziwezi kuhitaji gharama kubwa kama hizi barabara kuu za lami, lakini mtandao wake ni mkubwa sana. Tunahitaji tuwaongezee bajeti na wao waweze kufanya kazi ambayo itakidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo kwenye *TARURA,* wazingatie vipindi vya kutengeneza barabara. Tunapoteza hela kwa kutengeneza barabara wakati wa mvua, muda mfupi tu baadae inabidi turudie. Kwa hiyo, labda kile kipindi cha mvua ni kuangalia upungufu uko wapi halafu baada ya mvua ndiyo barabara zinatengenezwa, hasa zile za udongo na za viwango vya changarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nataka kuongelea kuhusu alama za barabarani kwenye hii barabara yetu ambayo Mheshimiwa Rais anakwenda kuifungua rasmi kesho kutwa tarehe 27 Aprili. Barabara imejengwa vizuri, tunawapongeza sana lakini kuna maeneo mawili ya hatari sana, pale kwenye Daraja la Ausia na kwenye Milima ya Kolo, ni maeneo hatari kwelikweli yanahitaji kuwekwa alama za aina yake, alama kubwa kama kule kwenye madaraja mengine kama Wami ili kupunguza ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yale yamekuwa wakisababisha ajali nyingi sana na kupoteza maisha ya Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, tunasisitiza na kusihi, tumeshaongea kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa lakini si vibaya kuliweka tena hapa, ili mradi suala hili lipewe uzito unaostahili na hatimaye alama hizo kubwa kabisa ziwekwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine na dogo la mwisho, nataka kuzungumzia habari ya mawasiliano kwenye Jimbo la Kondoa Mjini. Mawasiliano yapo karibu maeneo yote lakini yapo maeneo yenye changamoto mawasiliano hayapatikani vizuri hasa katika Kata za Kondoa Mjini, Seria

pamoja na Kingale usikivu unakuwa siyo mzuri na *drop calls* mara nyingi zinatokea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yake hebu naomba watuangalizie kule Kondoa nini tatizo hasa ili tuweze kulipatia ufumbuzi tatizo la mawasiliano yasiyosikika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa najua sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Ntuka na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuanzia naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa kwa kazi wanazoendelea kuzifanya na kwa ujumla wake chanda chema hivikwa pete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mpanda – Koga – Tabora kwa maana ya kilometa 373 inayoendelea kutengenezwa, naendelea kuieleza Wizara, tunalo eneo korofi la Mto Koga. Eneo lile ni korofi muda wote, kwa mfano sasa hivi barabara ile haipitiki kutokana na ukorofi wa ule Mto Koga. Naomba hata haya matengenezo yanayoendelea tuzingatie maeneo yale ya daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana wakati tukiitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kukomboa maeneo yote ya Mkoa wa Katavi na Tabora kwa ujumla wake, tusisahau barabara ya Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyankulu - Kahama kwa maana ya kilometa 457.

Barabara hii hata kama ikitokea imepata tatizo tunakuwa na *escaping route,* hii barabara nyingine inatukomboa wakati ambapo barabara moja inakuwa na matatizo. Kwa hiyo, naomba barabara zote hizi ziende sambamba, lakini napongeza jitihada ya kutengeneza barabara ya Mpanda – Koga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Kiwanja cha Ndege cha Mpanda. Mara ya mwisho niliuliza swali hapa, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye alinihakikishia kupatikana kwa gari la zimamoto katika uwanja ule. Pamoja na kupatiwa gari la zimamoto na huduma nyingine tunaomba tupatiwe *route* sasa ya ndege kuja eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala la *route* za ndege, vigezo vya kusema, je, tutapata wasafiri, hebu leteni ndege halafu muone kama mtapata wasafiri. Kuna maeneo mwanzoni walikuwa wanaona kama hawana wasafiri, nitatoa mfano wa Bukoba, leo hii wanatamani kuongeza *route* au Tabora, tunaomba mtuletee ndege halafu muone. Hii habari ya kusema tutapelekaje magari hakuna abiria lakii mkipeleka barabara mnashangaa magari yamejaa. Sasa hivi Sumbawanga kwenda Mbeya magari ni mengi lakini mwanzo walikuwa wanasema *route* ile haina magari. Kwa hiyo, naomba upande wa uwanja wa ndege tuleteeni *route* halafu muone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo naomba nizungumzie suala la reli. Kipindi hiki naomba ziendelee kutengwa fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa reli kutoka Tabora - Mpanda, maeneo ni korofi. Sambamba na utengenezaji naomba kitu kingine, tuna mabehewa machache na nashangaa reli ile kwa muda mrefu hatujabahatika kupata behewa la daraja la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, najiuliza wananachi wako kule na si kwamba wanapanda bure, wanalipia, vipi tunashindwa kupatiwa behewa la daraja la kwanza? Naomba ufafanuzi wa suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niwasemee pia wananchi wa maeneo ya Msasani - Tambukareli. Kulikuwa na bomoabomoa, wataalam njooni muendelee kutusaidia, je, ni umbali upi hasa ambao watu wanatakiwa kupewa fidia? Njooni mtusaidie kuangalia kama wananchi wale wako katika maeneo husika na kama kweli wako katika maeneo husika wale ambao wamebomolewa suala la fidia lichukue mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme jambo moja lenye sura ya kitaifa. Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam ni jicho la nchi hii, ni kioo cha nchi hii na ni ubalozi unafanyika pale, wanapokuja watu kutoka nchi za nje inatia aibu. Naomba kasi ya ujenzi wa *Terminal III* iongezwe maana nimejaribu kuangalia hapa kwa kipindi hiki wametengewa shilingi milioni 179.82 kwa ajili ya ujenzi wake, tuujenge uwanja huo. Watalii wanapokuja, watu mbalimbali wanapokuja tunapata aibu na jambo dogo kama suala la *air condition* katika uwanja ule linatutia aibu. Naomba tulifanye hilo kwa sababu mtu anapokuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, lakini kwa mujibu wa Katibu wangu nimepewa dakika kumi, naomba niendelee.

**NAIBU SPIKA:** Katibu gani huyo, anayeleta majina hapa au Katibu wako yupi?

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Anayeleta majina hapo.

**NAIBU SPIKA:** Ni dakika tano Mheshimiwa.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa nafasi hii fupi, lakini nitajitahidi kujikita kwa harakaharaka kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, Watanzania wote wanaona. Pia niwapongeze Mawaziri wanaohusika na Wizara hii, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa, tunaona juhudi zao na wanavyochapa kazi kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani zangu baada ya kutizama kitabu hiki cha bajeti, Jimbo langu la Manyoni tumetengewa fedha katika barabara za Ikungi – Londoni – Kilimatinde; Manyoni – Heka – Ikasi; Heka – Iluma na pia Daraja kubwa la Sanza nalo limetengewa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niombe ufafanuzi tu kidogo hapo kwenye barabara ya Ikungi – Londoni – Kilimatinde. Katika ukurasa wa 221, nimeona kuna barabara kama mbili tofauti, kuna moja imeandikwa Ikungi – Londoni – Kilimatinde na nyingine imeandikwa Ikungi – Kilimatinde. Mimi naona hicho ni kitu kimoja, lakini naona wametenganisha na fedha zimetengwa kwa kila kipande shilingi milioni 60. Kama ni kitu kimoja basi ile pesa msiitoe, iunganisheni tu basi nipate shilingi milioni 120. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mawasiliano ya simu. Wilaya ya Manyoni imekuwa na tatizo kubwa sana la mtandao wa simu, lakini naishukuru Serikali kwa kiasi imejitahidi sana kutujengea mitandao. Niombe kasi ya Kampuni ya *Halotel* ambao wamepewa *tender* hii hebu wafanye haraka, ni mwaka mzima sasa kwa mfano sehemu za Asasilo, Mpapa, Sanza na Nkonko minara wameweka tu misingi, hawaja-*erect* ile minara na kuwasha simu kwa

mwaka mzima sasa. Naomba wahimizwe basi wajenge ile minara na kuwasha ili tuweze kuanza kuwasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia maeneo ambayo hayasikiki kabisa katika jimbo langu ni vijiji vya Hika, Igwamadete, Mangoli, Mafurungu, Simbangulu, Imalampaka, havina kabisa mawasiliano. Ukifika katika eneo hili unakuwa kama uko katika kisiwa. Kampuni ya *Halotel* tunaomba sana Mheshimiwa Waziri awahimize kwa sababu ndiyo waliopata *tender* na wamezuia wengine, wafanye haraka basi sisi tunahitaji mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa reli, nizungumzie kidogo suala la reli ya Singida – Manyoni. Reli hii ilifunguliwa tarehe 24 Oktoba, 1985, ilikuwa kwa ajili ya kusafirisha mazao ya pamba na ngano kule Basuto pamoja na kuwasafirisha abiria na ilianza ku-*operate* vizuri sana ilikuwa na mabehewa matatu, mabehewa ya abiria mawili na la mizigo moja, ilitusaidia sana kipindi kile. Cha ajabu nilishuhudia tarehe 9 Septemba, 2009 ndiyo ilikuwa safari ya mwisho kusafiri lakini tarehe 12 Septemba, 2009 safari hizi zilisitishwa rasmi tukawa hatuna treni tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anayehusika tunaiomba treni yetu ya Singida kwa sababu mlisema kwamba tumesitisha safari eti kwa sababu ya ujio wa lami na pamba hailimwi tena. Sasa hivi sababu hizo hazina msingi wowote kwa sababu mtu anaposafiri analinganisha gharama za usafirishaji. Sasa hivi tunajenga Daraja la Sibiti, tutapata mizigo kutoka Simiyu na maeneo mengi ya Singida pale, tunalima vitunguu, tunao kuku, tunayo miwa, tuna viazi, tunaomba sana mturudishie treni ile, Mwalimu Nyerere hakukosea kutuletea treni ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika ujenzi wa *standard gauge,* msiisahau hii reli. Ifungueni ianze ku-*operate* sasa hivi, lakini *standard gauge* itakapoanza kujengwa reli hii pia ikumbukwe, mtujengee *standard gauge,* tunahitaji sana hii treni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ajali zinazotokea sana kwenye mteremko wa Mbwasa pale Chikuyu. Kumekuwa na ajali nyingi sana pale Mbwasa na pale Sekenke. Mimi kama mtaalam wa mambo haya ya ujenzi wa barabara nilipoangalia pale kuna makosa ya *design*.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri atume wataalam pale waende Mbwasa na Sekenke waka-*design* upya, wanyooshe zile kona maana kuna mteremko halafu kuna kona ghafla. Lori linapo-*fail* pale huwezi kukata kona ukikata kona ghafla unalipiga ngwala lile lori lazima litaanguka tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waka-*design* upya ili wanyooshe zile barabara ziteremke pale chini halafu kona isiwe kali sana. Hili linawezekana mimi kama mtaalam nimepita, nimeona kuna uwezekano kabisa wa kufanya marekebisho kuepusha ajali hizi, tunapoteza maisha ya watu wengi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nianze kwa kuwapongeza viongozi wa Wizara hii, ndugu yangu Profesa na wasaidizi wake Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye kwa namna ambavyo mnatekeleza majukumu yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala zima la *TARURA*. Tumeanza na *TARURA* inafanya kazi lakini bado ina changamoto na kule kwetu Kilwa *TARURA* hawana vifaa vya

usafiri, hawana gari kwa hiyo utendaji wao wa kazi unakuwa ni shida. Kwa hiyo, niombe Wizara iwaone hawa ili waweze kufanya kazi yao vizuri zao sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna hoja ya upembuzi yakinifu katika barabara ya Nangurukuru - Liwale. Imeelezwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu lakini mpaka sasa hakuna chochote kimefanyika. Niiombe Wizara ituangalie watu wa Kilwa, Liwale kufanya upembuzi yakinifu tayari kwa kuijenga barabara ile kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la barabara zinazounganisha mikoa hasa barabara inayounganisha Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro. Mheshimiwa Waziri naomba aliangalie hilo, sisi watu wa Lindi tuna haja ya kuunganishwa na wenzetu wa Morogoro ili tuweze kuwasiliana kijamii na kiuchumi ili mambo yetu yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara ya Kipatimu - Njia Nne ambayo iko chini ya *TANROADS* inahudumiwa na hata sasa hivi wakandarasi wako *site* lakini tuna changamoto kubwa ya miinuko na milima. Kwa hiyo, tuombe Wizara katika milima mikali watuwekee hata vipande vya lami ili ile barabara iweze kupitika wakati wote. Kwa mfano, kuna Mlima wa Ndundu ni mkali sana, Mlima wa Ngoge na Mlima Kinywanyu Wizara ituangalie hivyo vipande viweze kuwekewa lami ili barabara hiyo ipitike wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa suala la mawasiliano ya simu. Katika Jimbo langu kuna Kata ya Chumo, mawasiliano ya simu yapo lakini mnara wa Vodacom uliofungwa pale una matatizo. Unafanya kazi kwa muda wa saa saba hadi nane tu kwa siku, wananchi wangu wanapata hasara kubwa. Ukianza saa tatu mwisho saa mbili usiku baada ya hapo mnara ule haufanyi kazi tena na ni kwa sababu ya chanzo cha umeme pale, wanatumia *solar power* ambayo nafikiri ina matatizo. Nimeshafikisha tatizo hilo Wizarani naomba mlishughulikie kwa sababu mawasiliano pale ni kama yapo nusu nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuna Kata ya Kandawale hawana mawasiliano kabisa, kuna Vijiji vya Mkarango, Dandete, Kinjumbi hivi vyote havina mawasiliano ya simu. Naomba basi ndugu yangu Mheshimiwa Nditiye utuangalie na sisi tuweze kupata mawasiliano hayo ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee suala la mgawanyo wa bajeti ya barabara kwa mikoa. Nimejaribu kufuatilia bajeti za kila mwaka za mikoa inaonekana mgawanyo ni kama haulingani, kuna mikoa ambayo bajeti inakuwa kubwa sana na mingine kila mwaka bajeti inakuwa hafifu sana. Angalau mngejitahidi tuwe tunalinganalingana kwa sababu mikoa mingine kila mwaka bajeti iko juu sana lakini mikoa mingine kama Lindi kila mwaka bajeti iko chini sana. Mheshimiwa Profesa angaliaangalia, hatuwezi kufanana kwa asilimia lakini angalau tulinganelingane kwa sababu hatuelewi mnatumia vigezo gani ya kwamba mikoa mingine bajeti juu na mikoa mingine bajeti inakuwa chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la mawasiliano ya redio. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 walisema wangejenga mnara pale Nangurukuru ili na sisi watu wa Kilwa tupate mawasiliano ya Redio Tanzania, lakini mpaka sasa hakuna chochote ambacho kimefanyika. Tunakosa mawasiliano ya redio hasa redio yetu ya Taifa, Redio Tanzania. Tunaomba sasa mnara ule ujengwe, wananchi wanashindwa kuelewa nini kinachoendelea hasa kupitia mawasiliano ya redio. Ni muhimu sana mnara ule ukajengwa ili wananchi wapate mawasiliano ya redio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la upanuzi wa Bandari ya Kilwa Masoko. Kama ambavyo mnafahamu tunayo bandari yetu pale, lakini mpaka sasa hivi bado haijaonwa. Wizara iione Bandari ya Kilwa Masoko iifanyie upanuzi. Bandari ile ni kama imesahaulika, mtukumbuke na sisi watu wa Kilwa, Bandari ya Kilwa Masoko ipanuliwe kwani itatusaidia sana katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la upanuzi wa Uwanja wa Ndege Kilwa Masoko. Katika miaka miwili, mitatu iliyopita kulikuwa kuna mpango wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege Kilwa Masoko na kuna tathmini ilikuja kufanyika pale ili wale wananchi wanaozunguka uwanja ule waweze kupata fidia lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea, wananchi wale wamebaki pale hakuna uendelezaji wowote unaofanyika na hakuna dalili kwamba ni lini wananchi wale watafidiwa. Kwa hiyo, niiombe Serikali na Wizara iwaangalie wananchi wa Kilwa Masoko ili basi na wao waweze kupata stahiki zao, wafanye mambo mengine kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho na mimi niungane na Wabunge wengine ambao wamejaribu kuelezea shida Waheshimiwa Wabunge wanayoipata ya kusafiri kutoka hapa tulipo kuelekea *Area D.* Mimi nafikiri Serikali itafute suluhu ya haraka sana kwa sababu haieleweki sehemu ambako Waheshimiwa Wabunge wanakaa namna ya kusafiri inakuwa shida yaani ni kana kwamba Wizara imelala au haioni. Waheshimiwa Wabunge wanapitapita vichochoroni wanaweza wakaibiwa, lakini mazingira yale siyo rafiki. Kwa hiyo, hilo liangaliwe ili Waheshimiwa Wabunge waweze kusafiri *comfortable* kwenda katika zile nyumba ambazo wanaishi na kufika hapa Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Ally Ungando ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nitachangia dakika hizi tano *specifically* katika Mkoa wangu wa Singida, sitazungumzia masuala ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kwa masikitiko makubwa sana, inaaminika na kwa uzoefu kwamba maeneo ambayo yanakuwa karibu na miji mikuu katika nchi mara nyingi huwa yananufaika kwa kiwango

kikubwa sana na fursa ambazo zinakuwepo katika mji mkuu. Singida ni eneo ambalo liko pua na mdogo na mji mkuu wa Tanzania, lakini kuna mambo ambayo yanaonesha dhahiri shahiri kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inashindwa kuwatendea haki wananchi wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, treni ya kutoka Dodoma kwenda Singida imeshakufa toka mwaka 2009. Uchumi wa wananchi wa Singida kwa sehemu kubwa ni wafugaji, inaonesha kwamba kuna mifugo milioni moja na laki nne. Hawa wafugaji wanapotaka kutafuta masoko usafiri ambao ni bora na wa uhakika walikuwa wanatumia treni kwa ajili ya kusafirisha mifugo yao. Wakulima wa Singida walikuwa wanatumia usafiri wa treni kwa ajili ya kusafirisha mazao yao. Gharama za bidhaa kutoka maeneo mengine kuja Singida na kutoka Singida kwenda maeneo mengine zilikuwa za kiwango cha chini kwa sababu gharama za usafirishaji zilikuwa za kiwango cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna ajira nyingi zimepotea kutokana na treni hii kutoonekana tena Singida pamoja na mama ntilie ambao walikuwa wanapika pale *station,* kulikuwa na vijana waliokuwa wanafanya biashara ndogo ndogo pale mpaka sasa hivi watu wale hawana uhakika wa maisha yao yanakwendaje. Nataka Waziri husika ajue kwamba wananchi wa Singida wanataka treni yao. Wananchi wa Singida tunataka treni yetu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *airport* ya Singida; huu ni mwaka wa 30 toka eneo kutengwa. Baada ya eneo kutengwa Naibu Spika nikikupeleka Singida sasa hivi huwezi kujua kama uko *airport* kwa sababu hata *fence* hakuna ni pori tupu liko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, najiuliza *and I want government* kunijibu hapa, hivi mnapata hisia gani ambapo mnaona kwamba eneo ambalo mwaka 2010, mwaka 2015 wamekuwa *champion* kuwaweka kwenye viti hapa mnazunguka halafu leo ni mkoa ambao hata uki-*google*

kwenye *Wikipedia* wanasema ni mkoa wa kimaskini Tanzania. Wananchi wa Singida siyo wajinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *this is not fair.* Wanakwenda kujenga *International Airport Chato* kwenye watu 365,000 mnaacha Singida ambako kuna watu 1,300,000. *This is not fair at all*, tumewakosea nini ninyi. Linapokuja suala la sikukuu ya Chama cha Mapinduzi miaka 30 ndio mnakuja mnatuletea ubwabwa, hatutaki ubwabwa tunataka maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *this is not fair,* hii haikubaliki. Inaumiza sana karne hii eneo lenye hadhi ya mkoa ambalo lipo karibu na makao makuu ya nchi halina *airport?* Mambo mengine yote yamewashinda, hakuna hata chuo kikuu kimoja, hakuna treni, umeme wa upepo umewashinda, kila kitu kimewashinda Singida tumewakosea nini sisi? *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Namheshimu sana dada yangu anayechangia, lakini alipozungumza kwamba Chato kuna watu 300,000 nadhani alikuwa ametazama vibaya. Chato ni Wilaya ya Geita na Mkoa ni Geita kama ilivyo *Singida airport* ya Mkoa na kw amujibu wa sensa una watu 2,000,000 hatuna watu 300,000. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni shemeji yetu huyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri niendelee tu na kuchangia kwa sababu

nilipokuwa nazungumzia Chato sikusema Geita nimesema Chato kuna wananchi 365,000 asome ataona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Iramba mpaka sasa hivi kwa muda...

**MBUNGE FULANI:** Shemeji.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri muda wake umekwisha, nimemuongezea dakika kwa sababu ya ile taarifa aliyokuwa amepewa pale.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, sekunde moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sekunde moja naomba nimpe taarifa kwamba ...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Uwanja wa ndege wa Chato pamoja na kwamba upo kimkoa lakini upo kimkakati kwa maana ya kiutalii kwa sababu kuna mapori makubwa matano katika ukanda ule na uwanja wa ule utatumika kwa shughuli za utalii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu hata Singida kuna utalii vilevile.

**T A A R I F A**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bwege, taarifa haiwezi kuwa taarifa mbili Wabunge mkaongea kwa wakati mmoja. Ndiyo maana ulipozungumza kwa sababu wewe ni Mbunge mzoefu nikakuacha amalize aliyekuwa anatoa taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ahsante, basi nipe sasa hivi.

**NAIBU SPIKA:** Sasa hivi mzungumzaji hajaanza hata kuzungumza. Kwa hiyo, subiri aanze kuzungumza ndiyo umpe taarifa kwa sababu ukimpa wakati anapokea hiyo taarifa nyingine unakuwa unavunja kanuni.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Nimekuelewa.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Bwege. Mheshimiwa Jesca Kishoa, endelea.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Iramba kwa muda mrefu...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Iramba kwa muda mrefu sana...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa. *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara, muda wake umekwisha. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atakuwa na dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Ungando atakuwa na dakika nane.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili mimi niweze kuchangia Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu wa Wizara na wataalam wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye Mkoa wangu wa Tabora, nianze kuongelea suala zima la fidia. Kule Tabora tumepata pesa ya kujenga barabara ya Chaya - Nyahua ambayo ni barabara yetu kubwa tunayoitegemea kututoa Tabora mpaka Dar es Salaam na sehemu zingine lakini tunasumbuliwa sana na suala zima la fidia. Mkandarasi anapata shida sasa, anafanya kazi kipande hiki anaruka anaenda kufanya kazi kipande kingine anaruka. Uthamini ulishafanyika lakini bado fidia haijalipwa. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri sana anapokuja hapa kujibu atupe *commitment* ya fidia hii italipwa lini. Vilevile kuna fidia ya Urambo - Kaliua bado haijalipwa, matokeo yake mkandarasi pia anasuasua lakini fedha zimeshapatikana bado fidia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara ya Kaliua – Kazilambwa - Chagu ambayo ina kilometa 41 tu ili tutoke na lami kutoka Tabora mpaka Kigoma. Mheshimiwa Waziri, tunaomba mtupe pesa ya kilometa 41 ili tuweze kutoa hiki kipande kidogo sana kinachotuwekea doa. Kwa mfano, sasa hivi hii kilometa 41 haipitiki, kwa hiyo, lami yote mliyotuwekea inakosa maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora kuna barabara zimejengwa na *TANROADS* vizuri, lakini kuna tatizo la taa eneo la Isevya Tabora, usalama ni mdogo sana. Namuomba

Mheshimiwa Waziri amuagize Meneja wa *TANROADS* wa Tabora atuwekee taa eneo lile kwa ajili ya usalama. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Kubenea, jana alisema kwamba hela zote zinakwenda kwenye Kanda ya Ziwa kwa ajili ya upendeleo, tumepeleka pesa Tabora kwa ajili ya upendeleo. Hakusoma amesema tu, ukiangalia ukurasa wa 20 unasema hivi, ujenzi wa barabara ya Nzega - Tabora kilometa 145 kwa kiwango cha lami umekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri. Haya ni madai ya nyuma, tusipoleta Bungeni kupitisha mnasema Serikali imeiba, tukileta Bungeni hamsomi mnaropoka, acheni kuropoka. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee barabara ya Ndala – Ziba, hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, tunaomba Mheshimiwa Waziri aiwekee lami.

Naomba niongelee reli ya kati ambayo sasa hivi inajengwa *standard gauge,* kule ambako *standard gauge* bado haijafika hali ni mbaya. Tunaomba itengenezwe wananchi wanakaa mpaka saa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuongea sasa maajabu ya miaka miwili na nusu ya Rais John Pombe Magufuli. Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli amejenga reli ya *standard gauge* kwa muda wa miaka miwili na nusu kitu ambacho huwezi ukakiamini. Ameanza Dar es Salaam-Morogoro na sasa hivi ameanza Morogoro-Makutopora, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amenunua ndege ambazo zinawatoa sana mapovu upande wa pili. Haya ni maajabu ya Rais John Pombe Magufuli ndani ya miaka miwili na nusu ameweza kutuletea ndege tatu na kwa taarifa yao kuna *Boeing* zingine ziko njiani zinakuja. Naonge haraka haraka siingii ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maajabu ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, *flyover* tumefika asilimia 72. Waambie waangalie ukurasa wa 22 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maajabu ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli, barabara *line* sita *Morogoro Road,* haijawahi kutokea Tanzania tukawa na *highway* ...

**T A A R I FA**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde, naomba ukae kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bungara.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa muda wangu.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tupate maajabu ya shilingi trilioni 1.5 yamefikia wapi mpaka sasa hivi? *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah endelea.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kujibishana na bwege, mimi siyo bwege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kutaja maajabu ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika Wizara ya Ujenzi. Amenunua vivuko vinne: MV Kazi, MV Magogoni na MV Kivukoni kwa muda wa miaka miwili na nusu. Mimi najiuliza amewezaje ndani ya miaka miwili na nusu? Mbona sisi Wabunge kwenye majimbo yetu hatujaweza kufanya haya mengi kwa miaka miwili na nusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea na maajabu ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli; nawapongeza *TCAA*

na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya ununuzi wa rada. Nawapongeza *TPA,* Mkurugenzi Kakoko anafanya kazi kubwa sana waongezewe tu kina cha bahari pamoja na pesa za ujenzi wa Gati Namba 7 mpaka 13 ili waweze kufanya mambo yao vizuri. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde, kuna taarifa, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naendelea kutafakari na kujiuliza, najua dada yangu Mheshimiwa Munde anasafiri sana. Wakati anataja maajabu yaliyofanywa kipindi hiki cha miaka miwili ametuambia kwamba kuna *flyovers* zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninavyojua kile kilichojengwa pale Dar es Salaam ni *intersections* pale ambapo kuna muunganiko wa magari yanapita njia. Mfano wa *flyover* anaweza kwenda tu Nairobi, *Thika road* akaona *flyover,* acha mbali aende tu hapo Nairobi. Nilipenda kumpa tu hiyo taarifa na unavyoshauri...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umeshampa taarifa, sasa unaanza tena anaposhauri, naomba ukae. Mheshimiwa Munde unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Esther narudia kusema nakuheshimu halafu nakupenda, nakuomba sana usinichokoze Esther na unajua. *(Makofi/Kicheko)*

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilindie muda wangu.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Nilikuwa nimefikia *TPA*, naomba Serikali iwape pesa kwa ajili ya kujenga gati...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde naomba ukae, kanuni.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Hizo sindano zimewaingia wanyamaze bwana.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 68, iliyovunjwa ni Kanuni ipi?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji ambaye anachangia sasa hivi...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa Kubenea, Kanuni ya 68(1) inataka ukishasema utaratibu nikikupa fursa ya kuzungumza unanitajia Kanuni iliyovunjwa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1).

**NAIBU SPIKA:** Inasemaje?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64, inasema kwamba Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala wa hoja kwamba nilisema ndani ya Bunge hili kwamba fedha zimepelekwa Mkoa mmoja wa Kanda ya Ziwa, Kiti kiliamua matamshi hayo niyafute na nikayafuta kwa idhini ya Kiti. Sasa Mbunge anayechangia amerejesha tena na amenituhumu. Anaonesha aheshimu Kiti na aheshimu Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba maneno hayo ambayo yananidhalilisha mimi ayaondoe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea sijasikia ukitajwa pale.

**WABUNGE FULANI:** Kasema.

**MBUNGE FULANI:** Kasema anaropoka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo. Mheshimiwa Kubenea, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa mimi sijamsikia akizungumza, tusikilizane msiwe mnakuwa na haraka sana, Mheshimiwa Rhoda muwe mnasikiliza kidogo kama ninyi mnavyosikilizwa.

Kwa kuwa mimi sijamsikia Mheshimiwa Munde akimtuhumu Mheshimiwa Kubenea kwamba anaropoka nitaagiza hapa Taarifa Rasmi za Bunge zije nitatoa uamuzi kuhusu jambo hilo lililoombewa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Munde, endelea.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa pia napenda kuiambia Serikali iwasaidie *TTCL* ili waweze kuendana na ushindani kwa kuhakikisha wanalipwa madeni wanayodai kwenye taasisi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maajabu mengine ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ndani ya miaka

miwili amepanua viwanja kadhaa vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Tabora. Sisi tulikuwa tumekata tamaa, tulikuwa hatuna barabara ya lami tunayo, tulikuwa hatuna uwanja wa ndege upo, tulikuwa hatuna *standard gauge* inakuja, Mungu atupe nini, mambo ni *fire*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaambie tu ndugu zangu hawa wanaopenda kulalamika kila siku tusilalamike, tufanye kazi. Kila siku Serikali inaiba, inaiba haya mambo mazuri yamefanyikaje? Kama huu wizi unaotendeka kila siku na mambo haya mazuri yanafanyikaje? Wao ruzuku wanaiba hatusemi mpaka michango ya wagonjwa wameiba hatusemi. Wameenda kuomba msaada Ubalozi wa Ujerumani mgonjwa atibiwe wakati wametuchangisha humu mapesa, wamechangisha kwa mitandao, wamechangisha watu chungu mzima hela zote wameiba, sisi mbona hatusemi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tu kuwaambia waache kusemasema sana, wafanye kazi ili Taifa liwe na maendeleo. Mbona Rais kila siku anaongea yeye ni Rais wa CHADEMA, wa CCM na wa Watanzania wote na analeta maendeleo ya Watanzania wote. Sijawahi kuona tukaambiwa madarasa yanajengwa kwenye majimbo ya CCM, majimbo ya upinzani hayajengewi madarasa, mimi sijawahi kuona lakini nashangaa ni kila siku shutumu Serikali inaiba, kushutumu Chato imejengewa kiwanja cha ndege. Jamani yule ni Rais wa nchi hii muwe mnaelewa, yule ni mamlaka hata vitabu vya dini vinatamka kutakuwa na mamlaka na ile ni mamlaka. Mkitaka msitake Mwenyezi Mungu ameiweka pale na itaendelea kuwepo pale mpaka muda wake utakapokwisha. Rudisheni hela za mgonjwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde. Mheshimiwa Ally Ungando atachangia dakika nane na Mheshimiwa Anastazia Wambura ajiandae.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa leo salama salmini nachangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na barabara ya Bungu – Nyamisati. Waziri barabara hii ni muhimu sana na ukiangalia ni ahadi takribani ya Marais awamu mbili zilizopita walisema kwamba barabara hii tutajengewa kwa kiwango cha lami. Barabara hii ikijengwa itafaidisha Wilaya mbili, Wilaya ya Kibiti na Mafia. Mimi kila siku napokwenda kwenye mikutano yangu ya hadhara nashindwa kutoa jibu kuhusu barabara hii ya Nyamisati kwamba Serikali ina mpango gani kuhakikisha inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara ya kutoka Kibiti kwenda Mloka; barabara hii nayo ni muhimu sana ukizingatia sasa hivi kuna mkakati wa kufua umeme wa maji kule Mloka. Ningeomba sasa Serikali basi iangalie kwa jicho la huruma barabara hii ya Bungu - Nyamisati na Kibiti - Mloka na ukiangalia hivi karibuni Wilaya ya Kibiti tumekumbwa na janga la watu wasiojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ziko barabara zetu za mitaa ambazo ni barabara za Kibiti, Bungu na Jaribu, *TARURA* haina kipato kikubwa cha kuweza kujenga barabara hizi kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ujenzi wa Gati Nyamisati ambapo tunaambiwa mkandarasi yuko *site* lakini leo asubuhi nimeongea na wananchi wangu wa Nyamisati bado kazi haijaanza ya ujenzi wa Gati Nyamisati. Tukijenga Gati Nyamisati watafaidika wananchi wa Kibiti, lakini hata wananchi wa Mafia watafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la wananchi wanaokwenda Mafia kutoka Nyamisati hawana usafiri wa uhakika. Tunaiomba Serikali waangalie jinsi gani ya kutununulia meli ili tupeleke kule Nyamisati itoke Nyamisati na kwenda Mafia. Usafiri ambao unatumika sasa hivi ni usafiri

ambao siyo salama, siku yoyote Mwenyezi Mungu akileta mtihani wake linaweza likatokea la kutokea. Kwa hiyo, tunaomba Kibiti na Mafia muiangalie kwa jicho la huruma, sababu tunajua ndiyo kasungura kenyewe ni kadogo lakini hiki hiki tugawane na siye wananchi wa Kibiti tufaidike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda katika mawasiliano, Kibiti kwenye baadhi ya maeneo yetu hatuna mawasiliano kwa maana ya minara ya simu. Iko minara miwili ambayo imejengwa maeneo ya Delta, kule Mbwera lakini mpaka leo haijafunguliwa. Uko mnara umejengwa Mbuchi lakini mpaka leo bado haujafunguliwa lakini viko karibu vijiji 20 hatuna mawasiliano ndiyo maana hata kule Delta tukivua samaki wetu tunashindwa kupiga simu sokoni kujua leo soko bei yake ikoje. Kama kungekuwa na mawasiliano tungepiga simu tukajua sokoni leo *prawns* bei imekuwa juu na sisi tupeleke samaki wetu ili tupate faida yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa ndugu zetu hawa wa *SUMATRA*. *SUMATRA* wanafanya kazi lakini ninachoomba watoe ushirikiano na wadau. Hivi leo Kibiti wamezuia Noah zisipakie abiria kwenda kwenye barabara kuu, lakini wametoa zuio lile hawakuwashirikisha wadau. Kumekuwa na manung'uniko mengi inaonekana Serikali hii ya Awamu ya Tano siyo ya wanyonge kwa sababu wamefanya maamuzi pasipo kuwashirikisha wadau. Wangewashirikisha wadau wangejua mbadala wake ni nini kusingekuwa na manung'uniko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Wizara hii ya Ujenzi kwamba barabara nyingi zinazokwenda mikoani ziimarishwe na washirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu nguvukazi nyingi zinatembea barabarani kwa muda mrefu mchana. Kwa mfano, mtu anapanda basi saa 12.00 Dar es Salaam anakuja Dodoma anafika saa 12.00 jioni, muda ule ukiuangalia ni kwamba watu hawakuweza kuzalisha mchana kutwa walikuwa wanatembea tu barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika takwimu takribani wananchi 12,000 kwa siku wanatembea barabarani kwa muda mfupi. Ningeomba sasa waangalie utaratibu kama nchi jirani ya Kenya wananchi wengi wanasafiri usiku ili mchana waweze kufanya kazi na shughuli za uzalishaji mali. Kwa hiyo, hili liangaliwe kwamba jinsi gani wataboresha ulinzi na usafiri wananchi wasafiri usiku ili mchana waweze kuzalisha mali na kuiletea tija Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niipongeze sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi. Ndugu zanguni kila zama ina wakati wake. Tulianza na Mzee wetu hapa Baba wa Taifa (ujamaa na kujitegemea), akaja Mzee Mwinyi (ruksa), kweli tukaona ruksa, akaja Mzee Mkapa (utandawazi) kweli tukaona utandawazi, akaja Mzee Jakaya (maisha bora kwa kila Mtanzania) lakini sasa tumekuja Hapa Kazi Tu. Sasa nashangaa kazi inafanyika bado watu wana maneno maneno. Jamani tubadilike, sasa hivi hakuna maisha ya ujanja ujanja, sasa hivi ni maisha ya Hapa Kazi Tu. Pia inasemwa asiyefanya kazi asile, hata kwenye vitabu vya dini ipo. Kwa hiyo, ndugu zangu kama mlikuwa ni watu wenye ujanja msubiri mwaka 2025 muendelee na ujanja wenu, lakini awamu hii ni awamu ya Hapa Kazi Tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nipo katika Jimbo langu la Kibiti tunashukuru tumepata pesa ya kujenga daraja katika Daraja la Mbuchi, lakini barabara ya kutoka Muhoro kwenda Mbwera naomba nayo hii muiangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anastazia Wambura atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze

kuchangia katika bajeti hii muhimu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema zote katika maisha yangu. Vilevile nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Mbarawa pamoja na Naibu Mawaziri wake, Makatibu Wakuu pamoja na timu yote ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika Wizara hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuvunja rekodi ya bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi kwa sababu imetenga shilingi trilioni 4.2, ni kitu ambacho hakijawahi kutokea, hongera sana Serikali. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ajili ya kuruhusu kazi ifanyike katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. Naunga mkono hoja ili fedha hii ambayo imetengwa iweze kutoka kazi iende kufanyika katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa Mkoa wetu wa Mtwara katika fedha hizi ambazo zimetengwa imepata zaidi ya shilingi bilioni 42. Nichukue nafasi hii kwa niaba ya wana Mtwara kushukuru sana Serikali kwa sababu fedha hizi zinakwenda kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Mtwara takribani shilingi bilioni 12.8 na shilingi bilioni 10 kwenye ujenzi wa barabara yetu ya uchumi ya Mtwara – Tandahimba - Newala - Masasi na nyingine zilizobaki zinakwenda kufanya matengenezo ya barabara za mkoa na barabara kuu za lami pamoja na zile za changarawe. Pamoja na hayo pia fedha hii inakwenda kutengeneza madaraja, kutengeneza maeneo korofi na kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia faraja kwamba fedha hizi siyo kwamba zinakwenda Mtwara tu, kuna fedha kiasi tofauti kinakwenda katika mikoa mingine. Kwa mfano, nichukulie katika utengenezaji wa viwanja vya ndege utaona

kuna fedha zinakwenda kutengeneza Kiwanja cha Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mwanza, Arusha, Mtwara ipo pia, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Geita, Iringa, Musoma, Songea, Dodoma, Tanga, Manyara, Lindi, Simiyu, ni maeneo mengi tu fedha inakwenda kutengeneza viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, naomba ninukuu maneno ya wanafalsafa ambao wanasema kwamba, *everything will be okay in the end. If it's not okay, it's not the end.* Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbarawa asonge mbele, kwa sababu huu siyo mwisho wa kazi mwaka ujao naamini kabisa wataendelea katika maeneo mengine.

Pamoja na hayo niombe kutoa kilio cha wana Mtwara katika eneo la barabara ya Mtwara – Tandahimba - Newala - Masasi. Mwaka uliopita tuliambiwa kwamba kiasi ambacho kimetengenezwa pale ni asilimia 16 ya kilometa 50 ambalo ni eneo la Mtwara Mnivata. Sasa asilimia 16 ukiangalia itakuwa ni kama kilometa 8 lakini mwaka huu tuna shilingi bilioni 10 za matengenezo ya kipande hicho hicho. Kwa hiyo, ukichukua zile kilometa 200 kuna maeneo mengine tunaambiwa ni kilometa 209 lakini *document* zingine tunaambiwa ni 221 ni kwamba tunaweza tukachukua miaka mingi sana kumaliza eneo hili. Kwa hiyo, niombe mwaka ujao Wizara iangalie uwezekano wa kuongeza kasi ya matengenezo ya barabara hii kwa sababu ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu lakini kwa wakulima wa Mtwara kwa sababu mara nyingi unapopita...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado eeh?

**NAIBU SPIKA:** Tayari Mheshimiwa, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nadhani ninazo dakika kumi hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa pamoja na wasaidizi wake *Engineer* Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tuombe Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na jukumu letu sisi ni kuwatia nguvu na kuishauri Serikali katika yale ambayo wanayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la gati katika eneo la Mkinga ambalo tumepata mwekezaji wa kiwanda kikubwa sana cha saruji. Niombe sana Wizara hii ihakikishe kwamba jambo hili linakwenda kutokea. Tunazungumza mara kwa mara humu ndani ya Bunge kwamba tunahitaji kuwa na miradi ya *PPP.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii japo sio *PPP* lakini *private sector* moja kwa moja ameamua kuwekeza kujenga gati katika eneo hili la Mkinga ili aweze kurahisisha shughuli zake katika kiwanda cha saruji ambacho kitakuwa kikubwa zaidi kuliko viwanda vyote vilivyopo nchini na kitakuwa kinazalisha sana. Kwa hiyo, niombe sana wizara hii iharakishe kutoa vibali vyote vinavyohusika ili jambo hili litokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua uwepo wa reli ya Tanga - Arusha kwenda mpaka Musoma, reli hii ilikuwa inazungumzwa mara kwa mara lakini sasa tunaomba pamoja na jitihada ambazo zimeanza kufufua reli ya zamani na nimpongeze sana Mkurugenzi wa Shirika la Reli, Ndugu Masanja Kadogosa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya lakini tunaomba sasa kwenye huu mpango wa *standard gauge* uchukue hatua za haraka na sisi tuweze kuwa na reli hiyo ya kiwango cha kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni miongoni mwa mashahidi ambao wamepita barabara ya kutoka Mlalo kwenda Lushoto kilometa 45. Barabara hii tumekuwa

tukiiombea fedha mara kwa mara katika mfuko wa barabara wa mkoa lakini mara nyingi tunakwamishwa na wenzetu wa Wakala wa Barabara Taifa *(TANROADS). Engineer* Mfugale ninafahamu kwamba upo katika majengo haya na unasikia, barabara hii ya Lushoto – Mlalo ni muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli kubwa ya uchumi ya wananchi wa Lushoto ni kilimo cha mboga mboga na matunda. Kwa hiyo, utagundua kwamba bidhaa hizi zinatakiwa zifike sokoni kwa wakati. Sasa kama hatuna barabara madhubuti maana yake ni kwamba wananchi wanapata hasara kwa sababu kwa kuwepo kwa barabara ambazo sio rafiki mazao yanaharibika yakiwa njiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana tumeshaomba mara mbili kufanyiwa upembuzi yakinifu pamoja na *detailed designing* ya barabara hii na kila mara tukiomba wenyewe hawaleti mrejesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana safari hii barabara hii iingizwe katika mpango, najua mwaka huu tumeshachelewa lakini katika mwaka wa fedha unaokuja tafadhali sana kilometa hizi 45 tupate barabara ya kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mawasiliano ya simu, katika Halmashauri ya Lushoto maeneo mengi tunashukuru kwamba simu zinapatikana. Changamoto ipo kwa sababu jiografia yetu ni milima baadhi ya maeneo ya mabondeni hakuna mawasiliano mazuri. Kwa hiyo, niwaombe tu wizara pamoja na wadau wote wanaohusika katika eneo hili waweze kuona kwamba namna gani tutaboresha mawasiliano ili wale ambao wapo katika maeneo ambayo yamefunikwa na vilima waweze kupata mawasiliano ambayo yataweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tanga – Pangani mpaka Bagamoyo ni barabara ya siku nyingi sana

na ni barabara ya kimkakati kwa maana ipo katika ramani ile ya Afrika Mashariki. Tumeanzia kutoka Horohoro kuja mpaka Tanga sasa tunataka kilometa 45 zile za Tanga – Pangani, lakini pamoja na kuunganisha na kipande cha Mwela – Sakula – Madanga – Saadan mpaka Bagamoyo ili tuweze kusaidia pia kuimarisha shughuli za kiuchumi pamoja na kutangaza mbuga zetu za Saadan kwa upande wa Bagamoyo na Tanga, lakini pia Mbuga ya Mkomazi ambayo ipo katika Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *ATCL* hasa suala la ndege kwamba watu wengi wanazungumzia ndege kama biashara ya chai kwamba asubuhi anapika maandazi na chai, jioni atapata faida, hili ni suala ambalo lina *multiplier effect.* Yapo mambo mbalimbali ambayo uwepo wa *ATCL* umesababisha hata bei ya ndege kushuka, tulikuwa tunaona hapa *FastJet* na ndege nyingine binafsi zilikua zinatoza gharama kubwa sana kutoka eneo moja kwenda lingine, lakini uwepo wa *ATCL* na *bombardier* hizi umesaidia hata ku-*regulate* bei kiasi kwamba sasa hivi wananchi wanatoka maeneo mbalimbali kwa gharama nafuu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inasaidia kuondoa... kuna rasilimali moja ambayo Watanzania wanaisahau, rasilimali muda. Sisi shughuli zetu zinapoteza muda mwingi sana kwa sababu ya kutumia muda mrefu kusafiri, lakini uwepo wa usafiri wa anga unarahisisha mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ndugu zangu Wangoni hawa walizoea kushinda barabarani kutoka Dar es salaam kwenda mpaka Peramiho, lakini sasa hivi kwa uwepo wa *bombardier* ni saa moja anaruka kutoka Dar es Salaam kwenda Songea. Kwa hiyo, ninaomba sana tuimarishe shirika letu la ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi adimu. Nianze kwa kuipongeza Wizara inafanya vizuri sana hasa kwa kuboresha bandari nafikiri kwa kiasi kikubwa hii itapunguza gharama ya malighafi zinazokuja kutoka nje zikiwemo mbolea, lakini vilevile itapunguza gharama za bidhaa zetu ambazo tunasafirisha kwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuboresha hii bandari yetu lakini inakabiliwa na ushindani mkubwa sana hasa na bandari za jirani. Ninapendekeza Serikali iangalie namna gani iboreshe *TAZARA, TAZARA* kwa kiasi kikubwa ni *standard gauge; speed* ya treni pale ni kilometa 110 kwa saa. Tukiboresha hii ambayo maboresho yake sidhani kama yanahitaji hela nyingi, labda Serikali ijaribu kutuambia ni kiasi gani itaboresha Menejimenti ya *TAZARA* na vilevile namna gani itaondoa ukiritimba ili *TAZARA* iendeshwe kibiashara, kwa sasa hivi *TAZARA* haiendeshwi kibiashara na nina wasiwasi mpaka leo wafanyakazi wa *TAZARA* wanalipwa na hela kutoka Serikalini, wanalipwa na walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiboresha *TAZARA* tutakuwa tumejiweka katika *position* nzuri sana ya kiushindani lakini vilevile tukijenga bandari kavu Mbeya ili mizigo ambayo ni zaidi ya asilimia 70 inayokwenda nchi za nje inapitia barabara hiyo, iondokane na kuharibu barabara zetu. Tukishajenga bandari kavu pale, mbolea zote kwa ajili ya nyanda za juu kusini na mizigo yote ya kutoka Congo, Malawi na Zambia yote isipitie barabara hizo, itue pale ili ipunguze gharama na vilevile itaongeza ushindani. Vilevile ningependekeza tujenge reli ya kuanzia Mbeya kwenda Ziwa Nyasa ili tuwe na ushindani mzuri na Bandari za Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye barabara nilikuwa ninaomba sana Serikali iangalie namna ya

kuboresha barabara zetu ambazo zilikuwa ni ahadi za Mheshimiwa Rais, barabara ya Mbalizi – Makongolosi, Mbalizi – Shigamba – Isongole na barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete mpaka Njombe vilevile barabara ya *bypass* ili iweze kuondoa msongamano wa magari pale Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye Kiwanja cha Ndege cha Songwe; hiki kiwanja kimetengewa hela nyingi lakini mpaka leo hatuna taa pale za kuongozea ndege na hakuna uzio. Naiomba sana Serikali iangalie ni namna gani itaboresha Uwanja wa Ndege wa Songwe kwa kuwekea taa za kuongozea ndege vilevile na uzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna bidhaa nyingi ambazo zinahitajika kwenda nchi za nje kutoka nchi jirani, lakini vilevile kutoka Mbeya yakiwemo maparachichi na matunda mengine lakini yanasafirishwa mpaka Dar es Salaam na haya yana masoko nje. Ukienda kwenye *supermarket* za Uingereza leo hii utapata bidhaa kutoka Mbeya, lakini zinakwenda kwa gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la fidia, suala la fidia waliopisha ujenzi Uwanja wa Ndege wa Mbeya mpaka leo halijashughulikiwa. Wananchi wale wanalalamika miaka mingi na Mheshimiwa Waziri tumeongea naye mara nyingi na imo kwenye ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Miundombinu ambayo nao walipendekeza hawa wananchi walipwe. Ni shilingi milioni 800 tu lakini usumbufu uliopo ni mkubwa na ninashangaa kwa nini wananchi wale mpaka leo wanadhulumiwa pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi ambao katika ripoti yao walipewa fidia ya shilingi 2000 au shilingi 5000 kwa maheka na maheka. Sasa hili wizara ingeangalia hawa *TAA* wahakikishe wanawalipa wale wananchi hizo shilingi milioni 800 ambazo wanadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *TARURA, TARURA* zinaendana na *TANROADS,* lakini mgao wa pesa

zinazoenda *TARURA* ni ndogo mno. Kwenye Jimbo langu tuna kilometa zaidi ya 1,000 mtandao wa barabara lakini bajeti yake ni kama shilingi milioni 1.6. *TARURA* wakiongezewa pesa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Justin Monko ajiandae.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kabla ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anafanya maamuzi yaliyo mengi mazuri katika sekta hii ya uchukuzi na mawasiliano. Lakini pia niipongeze Wizara hii pamoja na Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa katika Jimbo la Busokelo ni barabara ambayo imeahidiwa kwa miaka mingi na Marais wote waliopita ukiachana na Baba wa Taifa ambayo ni Katumba – Lwangwa – Mbambo – Tukuyu yenye kilometa 85. Bahati nzuri sana nimeenda mara nyingi kwa Katibu Mkuu na amekuwa akiniahidi mara kwa mara lakini mara nyingi pia nimewasiliana na Waziri, nimepeleka mpaka maandiko lakini hadi hivi leo ninavyozungumza katika bajeti yake hakuna jambo ambalo limefanyika ambalo lilitakiwa lifanyike mwaka jana kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wetu wa Busokelo na Rungwe kwa sababu kwanza gesi asilia aina ya *carbon dioxide* inapatikana kule lakini pia kuna aina mbalimbali ya mazao kama ndizi,

viazi na maziwa kwa ajili ya ufugaji lakini barabara hii hata hivi ninavyozungumza wiki iliyopita tulikuwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati, tulikwama kwa zaidi ya dakika kadhaa kwa sababu ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali na Wizara hii ichukulie umuhimu mkubwa barabara hii kwa sababu hata Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli tarehe 28 Agosti, 2015 saa 6.30 pale viwanja vya Tukuyu Mjini aliahidi barabara hii kwamba ataitengeneza kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujibu useme kwamba barabara hii itaanza lini kutengenezwa kwa sababu mwaka huu wa fedha unakwisha na bajeti ilishatengwa hakuna lolote ambalo limefanyika, sielewi ni nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni barabara ya kutoka Luteba (Mbeya) – Makete – Njombe, ni barabara mpya ambayo inaunganisha mikoa yote miwili. Nikiwa Mbunge nimekuwa mbele pamoja na wananchi wangu kulima kwa jembe la mkono. Je, Serikali inatusaidiaje katika barabara hii kuhakikisha kwamba tunaunganisha mikoa yote miwili ya Njombe pamoja Mkoa wa Mbeya kupitia Luteba mpaka Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali haitakuwa na fedha basi nikuombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako na Katibu Mkuu twende wote tukalime kwa kushika jembe la mkono kwa sababu ninaona kila mara nikiandika hata maandiko tangu mwaka 2016 bado haya mambo hayaendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna barabara pia ya mchepuo wa kutoka Uyole kwenda Mbalizi barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Mbeya Jiji. Kwa sababu mahali pale katikati ya Jiji kumekuwa na foleni kubwa ukizingatia kwamba ule mji unakua kwa kasi. Kwa hiyo, tunaomba mchepuo wa barabara itakayoanzia Uyole

kwenda Mbalizi na *Songwe airport* iweze kukamilika ili magari makubwa yawe yanapita ile *diversion. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna jambo kubwa hili la Uwanja wa Ndege wa Songwe. Bahati nzuri sana Kamati yetu ya *PIC* tulikwenda kutembelea ule uwanja na kila mara nimemsikia Mheshimiwa Waziri hapa akijibu kwamba tunatengeneza taa za kuongozea ndege. Kwa bahati mbaya sana anasema ni shilingi bilioni nne lakini kwenye bajeti hapa ipo shilingi bilioni 3.7 na hizi fedha hazitatosha kutengeneza taa za kuongozea ndege pamoja na kujenga ukuta na *runway,* haitawezekana kwa fedha ambazo zipo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuiombe Serikali kwamba iweze kutenga fedha za kutosha katika uwanja huu wa kimataifa na ikizingatiwa kuwa katika nchi yetu ya Tanzania kuna viwanja vikubwa vinne ambavyo vinaweza kusaidia viwanja vingine. Zaidi ya viwanja 54 vinahitaji kupata mapato kutoka viwanja vya Julius Kambarage Nyerere, Songwe, *KIA* na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo, ningeishauri Serikali kwamba laiti kama tungeweza kuviwezesha hivi viwanja na vikaweza kukamilika ili fedha zile sasa ziweze kusaidia viwanja vingine ambavyo vipo kwenye mpango wa kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu ni suala la mawasiliano, katika sekta ya mawasiliano inachangia asilimia 13.1 ya pato la Taifa na kwa msingi huo tumeona mara nyingi *database* zetu ama *software* ambazo zinatumika katika mawasiliano zinatumia *commercial software*. Nikiwa mdau wa mawasiliano (TEHAMA) ningeshauri kwamba ianze kutumia *open source* kama vile *Firefox, Fidora, Tomcat, http server* na nyinginezo nyingi ili kuipunguzia gharama Serikali wakati wa kuendesha hii mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu *open source* ni mifumo ambayo inakuwa ni wazi kwa maana kwamba *own source code* anaweza aka-*edit* mtu yeyote yule, lakini

ukitumia *commercial software* maana yake unahitaji kununua *license* na zinakuwa na *expiring date* na *running cost* yake inakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niweze kuzungumzia suala zima katika suala hilo hilo la mawasiliano tumeona pia katika hii *issue* ya *commercial software* kuna baadhi ya *pirates software* ambazo zinatumika kwenye taasisi za Serikali ambazo hazijalipiwa *license* na gharama yake ni kubwa sana. Ni kubwa kwa maana kwamba wale ambao wanatengeneza *software incase* wakijua kwamba taasisi za Serikali zinatumia *software* ambazo hazina *license*, Serikali lazima itakuja kulipa fedha nyingi. Kwa hiyo, nitoe tahadhari hiyo kwamba haitakiwi tuingie kulipa huko wakati tungeweza kutumia hizi *open source software*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda kuunga mkono hoja, lakini nimuombe mheshimiwa Waziri aje na majibu yaliyo sahihi sana juu ya barabara ya kutoka Katumba – Luangwa – Mbambo – Tukuyu na ikibidi barabara ya kwenda Makete kutoka Busokelo twende wote tukalime kwa jembe la mkono kama fedha hazitapatikana hapa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa usiwe na wasiwasi, Mheshimiwa Waziri alikuwa naandika sana hapa wakati unazungumzia hiyo barabara.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Monko, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ambayo ipo mezani. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yako yote, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wote; Wizara yenu kubwa sana lakini mnachapa kazi kweli kweli. Nimewahi kukuona Profesa Mbarawa unasafiri kutoka Mbeya kwenda mpaka Itigi kwa barabara ambayo ni mbaya sana

ili uione barabara ile ilivyo, uje utujengee, hongereni sana na endeleeni kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wahenga wanasema mfinyanzi huulia gaeni, lakini kwa hapa Dodoma *Area D Site II TBA* angalieni pale maana yake barabara ya kuingia pale ni mahandaki, gari limezima, naomba *TBA* mtengeneze barabara ile ya kwenda *Site II. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kujenga barabara ya lami kutoka Mbeya kwenda Chunya kuelekea Makongorosi, barabara imekamilika nauli zimeshuka na usafiri upo siku nzima kati ya Mbeya na Chunya, nawashukuru sana kilometa 72 zimekamilika*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali imetenga fedha za kuanza ujenzi kutoka Mbeya kwenda Makongorosi kilometa 43, asanteni sana. Pia mmetenga fedha za kuanza ujenzi kutoka Mkiwa kwenda Itigi ili baadaye Chunya mtapopanda na Itigi wanashuka tukutane katikati, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lipo moja, hii barabara ya Mbeya – Chunya kwetu sisi ni tunu *(master piece)* imeturahisishia maisha mno, lakini sasa bahati mbaya Chunya kuna mazao mawili ambayo yanaharibu barabara; kuna mazao ya miti (mbao) na kuna tumbaku. Wachukuzi wanaochukua mizigo hiyo wanabeba malori ya lumbesa ili wakifika Mbeya ndio wagawe yawe magari mawili, wanaharibu barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri utuwekee *weight bridge* hata kama ni *mobile weigh bridge* tuweze kuyadhibiti magari hayo maana yanasafiri usiku, ahsante sana najua utatufanyia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaipongeza Serikali kwa kuiboresha *Tanzania – Zambia highway,* mmejenga vizuri sana kuanzia Makuyuni mmekwenda mpaka Igawa sasa hivi ni barabara nzuri sana. sasa hivi kutoka Igawa kwenda Mbeya

iko kwenye usanifu na kutoka Mbeya kwenda Tunduma ipo kwenye usanifu. Kama alivyosema Mheshimiwa Mwakibete, ninaomba mtakapokuwa mnajenga sasa kutoka Igawa kwenda Mbeya mkifika Mlima Nyoka mfanye *bypass* ya kwenda kutokea Mbalizi tujaribu kupunguza *congestion* katika Jiji la Mbeya. Tuiboreshe hiyo barabara ya katikati ya Mbeya lakini hiyo ya Mlima Nyoka kwenda Mbalizi iwe *bypass,* naomba muifikirie hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka niongelee kama walivyoongea wenzangu Mheshimiwa Njeza na Mheshimiwa Mwakibete, Uwanja wa Songwe. Kwanza ninaiomba Serikali Mkoani ianze mchakato wa kubadilisha jina kwamba isiitwe Uwanja wa Songwe, tutafute jina lingine maana yake Songwe ni Mkoa mwingine, kwa hiyo, tutakuwa tunatangaza mkoa mwingine. Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Michezo sikubagui, lakini ni mkoa mwingine, tuite jina lingine lakini uwanja huo umekamilka upo vizuri. Sasa hivi ndege wakati wa mvua zinakwenda pale wakati mwingine zinashindwa kutua pale zinarudi kwa sababu hakuna taa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hela imetengwa humu, ninaomba taa za kuongoza ndege na ukuta ujengwe naomba jengo la abiria likamilike. Ninajua Serikali imevunja mkataba na mkandarasi aliyekuwepo kwa sababu za kiufundi, ninaomba mteue mkandarasi mwingine haraka ili tukamilishe uwanja huo uanze kusaidia wana Mbeya kwa kiuchumi, tuna mazao mengi, parachichi, ndizi, viazi, mpunga na kila kitu, tuutumie uwanja huo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mashirika mengi ya nje kama Emirates yapo tayari kwenda kuchukua mizigo Uwanja wa Songwe, lakini mpaka taa ziwepo na uzio wa uwanja uwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali katika bajeti hii ya mwaka huu ikamilishe vitu hivyo vitatu; taa za kuongoza ndege, jengo la abiria na uzio katika uwanja huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambalaswa. Mimi ninaamini Mheshimiwa Waziri amelisikia hasa hilo la jina naona Mheshimiwa Shonza anaiangalia pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Justin Monko atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Nianze kwa kuipongeza sana Serikali, hasa Wizara hii, kwa fedha ambayo imeshatutengea sisi Mkoa wa Singida katika kuboresha miundombinu ya barabara tuliyonayo. Tumeona wameanza kutenga fedha kwa ajili ya *feasibility study* ya barabara ya kutoka Singida kuelekea Katesh na Singida kuelekea Shelui, sisi wa Mkoa wa Singida tunafurahi sana katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunalo tatizo la reli yetu ambayo imeunganisha kutoka Manyoni kuja Singida Mjini. Reli hii haijafanya kazi tangu mwaka 2009 na kumekuwepo na dhana potofu kwamba baada ya kuwa sasa tumepata barabara za lami basi pengine reli hiyo ilikuwa haiwezi kuzalisha na haiwezi kupata mizigo. Tukumbuke Singida ni katikati ya nchi na sisi pale Singida kwa reli hii kufika pale maana yake tunaweza tukahudumia mizigo inayotoka Simiyu, Shinyanga na Mwanza ili kuweza kuendelea kuokoa barabara hizi ambazo zimekuwa zikiharibika kwa wakati mwingi ambao tumetumia malori kwenye barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Singida Kaskazini pia tunazo barabara zenye shida. Ipo barabara ya kutoka Singida – Ilongero – Mtinko – Mudida inaelekea Haydom, ukiangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri barabara hii sasa naona imetengewa fedha ya kuanzia Karatu – Mbulu, ikishafika pale Haydom inakwenda Sibiti. Sasa

barabara hii iko katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ilikuwa ni ahadi pia ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara iangalie namna ya kufanya *feasibility study* katika barabara hii ili kuja kuunganisha na Mji wetu wa Singida ili barabara itakapofunguliwa basi wananchi hawa waweze kupata huduma kwa sababu ni barabara muhimu sana inayounganisha miji mingi sana, lakini inaunganisha huduma za muhimu sana, hasa huduma za hospitali kikiwemo Kituo cha Afya cha Ilongero, Hospitali yetu ya Mtinko, lakini tunakwenda Nkungi, lakini kuna Hospitali ya Rufaa ya Haydom.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko barabara muhimu sana katika Jimbo la Singida Kaskazini, barabara hii ni ya kimkakati hasa upande wa uchumi na barabara hii inatokea Singida Mjini, inapita katika Kata ya Kinyeto – Kinyagigi – Meria – Magojoa – Msange na inakwenda kuunganisha katika Kata ya Itaja katika Kijiji cha Sagara kwenye Barabara Kuu iendayo Katesh, Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kiuchumi, sisi ni wazalishaji wakubwa sana wa vitunguu na ni wazalishaji wakubwa sana wa alizeti, tunahitaji kuileta alizeti hii katika kiwanda kilichopo Singida Mjini, lakini pia tunahitaji kusafirisha vitunguu vyetu. Mpaka sasa wanunuzi walio wengi wanashindwa kufika katika maeneo yetu, tunashindwa kuwa na masoko ndani ya Halmashauri yetu kwa sababu barabara zetu ni mbovu na watu wanalazimika kutumia usafiri wa magari madogo madogo na hivyo badala ya wanunuzi kufika kwenye maeneo wanakuja tu wale wafanyabiashara wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii pia tuliiombea kwa Mheshimiwa Rais, ina urefu wa kilometa 42 tu na Mheshimiwa Rais alionesha utayari wa kuijenga katika kiwango cha lami. Kwa hiyo, niiombe sana Wizara iiweke

katika mpango wa kufanyiwa *feasibility study* katika kipindi cha mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunayo barabara moja ndogo, ina kilometa tano, sita, ambayo inatoka katika Kijiji cha Sagara inakwenda katika Kijiji cha Gairo na inakwenda kuunganisha katika Kijiji cha Pohama na kutoka hapo inakwenda tena kuunganisha katika Mji wa Katesh. Barabara hii ina matatizo na wananchi wanaoishi katika Vijiji vya Gairo wametengwa na eneo kwa sababu ukitokea Pohama kuna madimbwi na wakati huu wa mvua haipitiki kabisa. Lakini ukitoka Gairo kupanda hapa Sagara kuna mlima mkubwa ukiwa unapanda katika hilo Bonde la Ufa na barabara hii haipitiki kwa kweli kwa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anaozifanya pamoja na Mawaziri wote; Waziri Mkuu, Waziri mwenye dhamana na Naibu Mawaziri wa Wizara hii ambayo tunachangia pamoja na Makatibu wake na wote wanaomsaidia katika Wizara hii. Kazi zinazofanyika tunaziona, ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye Jimbo langu la Halmashauri ya Mji wa Makambako. Pale Makambako kuna eneo fulani panaitwa Idofi ambapo Wizara walikuwa wamesema tuandae kwa ajili ya kujenga *One Stop Centre* na eneo hili kazi iliyofanyika kuwaomba wananchi wale ni kazi kubwa, ngumu na ambayo mpaka sasa hatuelewi nini kinachoendelea na kwa sababu bado

hawajalipwa fidia na kwenye kitabu nilikuwa naangalia sioni mahali ambapo panaonyesha utayari wa kujenga *one stop center* kwa ajili ya manufaa ya watu wa Makambako, ombi langu niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapo atueleze *One Stop Center* ipo au haipo. Na kwa sababu pana msongamano sana wa magari na nini pale, wenyewe mnaona mnapokwenda Songea, Mbeya, pana msongamano mkubwa sana wa *jam* ya magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; niishukuru tena Serikali kwa namna ambavyo imetenga bajeti kwa ajili ya kutengeneza kilometa sita za Mji wa Makambako ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi na sasa naziona hapa, nawapongeza sana na shughuli hiyo nimeiona pale sasa imeshaanza kwa mita 150, najua kwamba sasa wakati mkandarasi anaendelea na bajeti hii itakuwa imeshafika muda wake mtaendelea kuikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara ambayo ni ya *TANROADS,* unapokwenda *Songea road* pana Kijiji kinaitwa Ilunda, kutoka Ilunda kwenda Igongolo pana kilometa tisa ambazo ni za *TANROADS,* ukiendelea mbele barabara hii mbele inaendelea inakwenda Ilengititu, inakwenda Kifumbe, Mahongole inakuja kutokea Makambako na utaona sasa barabara hii kwa kilometa tisa ambazo zimetengenezwa pale barabara mbele inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba barabara hii sasa iingizwe kwa *TANROADS* ili kusudi kwa mzunguko huu pale ni kilometa 19, ili mzunguko wa barabara kwenda kutokea Makambako uweze kuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima niipongeze tena Serikali kwa barabara ya kutoka Nyigu kwenda Igawa ambayo inapita pale kwangu Makambako, kazi inayofanyika ni nzuri sana. Ombi langu ni kwamba zile barabara za pembeni na zenyewe, naona wanaendelea, basi nina imani kwamba mtakamilisha vizuri kama ambavyo iko ile waliyokamilisha pale Mafinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze tena barabara ya kutoka Makambako kwenda Songea ambayo nimeiona iko kwenye bajeti. Ombi langu kwa Wizara, barabara hii kwenda Songea ukitoka Makambako kwenda Njombe vichepu vya basi kipo kimoja tu kiko pale Mtwango, utaona hakuna mahali ambako mabasi yanaweza kusimama na nyumba zimejaa kutoka Makambako mpaka Njombe. Ombi, muone namna ya kupanua mabega ili kuwe na vituo vya basi kwa ajili ya barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mawasiliano, katika mawasiliano kutoka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu, kuna jambo muhimu. Nije kwenye suala ambalo Rais analifanya, Mheshimiwa Rais wetu amekaa hapa ndani kwa miaka 20 akisikiliza hoja mbalimbali ambazo zilikuwa zinasemwa pande zote mbili. Hoja hizo sasa ndiyo zinatekelezwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga, shukrani. Mheshimiwa Goodluck Mlinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niweke rekodi sawa, jana katika Uwanja wetu wa Ndege wa Dar es Salaam ilitua ndege ambayo imeaminishwa kuwa ndiyo ndege kubwa kuliko zote kuwahi kutua. Nasema hapana, kwa sisi ambao tulikuwa wa kwanza kwenda Dar es Salaam, tarehe 06 Novemba, 2009 ilitua ndege aina ya *Antonov An 225* ambayo ilileta mitambo ya Richmond, ndege hiyo ilikuwa na uzito wa tani 285 wakati iliyotua jana ina tani 276, hiyo

ndege ilikuwa na urefu wa mita 84, ile iliyotua jana ilikuwa na mita 73; hiyo ndege ilikuwa na bawa lenye ukubwa wa mita 88, ile ina mita 80; hiyo ndege ilikuwa na injini sita, ile ya jana ina ijini nne; kwa hiyo tupo vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili, kusifia sio unafiki, hata dini zetu zinatuambia unapotaka kuomba lazima usifie. Kwa sisi Wakristo unapotaka kumuomba Mungu unaanza Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako ufike, utakalo lifanyike, sasa hapo swala ikishakolea unachomeka matatizo yako. Ndugu zangu Waislam tunasema *Bismillah Rahman Raheem,* Ewe Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, mwenye kurehemu, mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na neema ndogo ndogo; ukimaliza hapo unachomeka matatizo yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu, ninyi mkisimama mnaanza kukejeli Serikali, mnaitukana Serikali, mambo ya wapi hayo? Mimi sijawahi kumuona mtu anasema Mwenyezi Mungu ile mvua ya jana iliyonyesha ni mbaya imetuletea mafuriko, leo naomba hiki, mbona sijawahi kuona mkimwambia Mungu, kwa nini mnaikejeli Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Lakini nimhakikishie sio kila neema anayoileta kwa Watanzania kuna watu wote wataifurahia, hata Mwenyezi Mungu neema anayotuletea sio wote wanaifurahia. Kwa mfano mvua inaponyesha ni neema kwa wakulima, lakini wauza mitumba, wamachinga wanachukia. Kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Rais hao wanaochukia neema anayoileta awachukulie sawasawa na wale wamachinga ambao wanaichukia mvua, aichukulie sawasawa na wauza mitumba ambao wanaichukia mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hawana jema. Katika miradi yote ambayo imefanywa sijawahi kuona hata mradi mmoja ambao wanausifia, imeletwa reli wanalalamika, leo tunaanzisha mradi wa *Stiegler's Gorge* wanalalamika, elimu bure mnalalamika, ununuzi wa ndege

mnalalamika. Hebu waambieni Watanzania ni kitu gani chema kwenu ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa maana yangu. Hiki kitabu mnachokiona cha hotuba ya Waziri, hii picha ya mbele sio Daraja la Ulaya wala sio Daraja la Kigamboni, ni daraja ambalo limejengwa katika Jimbo langu la Ulanga, daraja la kimataifa. Kwa hiyo, mnapoona ninyi mmepata ndege, mimi napata vitu kaa hivi, nimshukuru Mheshimiwa Rais, na tunalifungua wiki ijayo kwa hiyo vitu vinafanyika, tafuteni utaratibu mzuri wa kushauri na kuomba, mtavipata. Lakini tangu bajeti imeanza mnatukana matusi, sijaona mpinzani ameomba hata bomba la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishukuru Serikali...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Kwa kutupa pesa kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 68 za lami kutoka...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga usubiri kidogo, Mheshimiwa Frank muda wetu umetutupa kidogo kwa hiyo, taarifa sitaziruhusu sasa hivi mpaka wamalize wachangiaji. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Nimkumbushe kitabu cha Mungu hiki anachosema.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, acha niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niishukuru Serikali kwa kutupa pesa kwa kujenga barabara ya lami kilometa 68 toka Kidatu mpaka Ifakara. Lakini ninachoomba watumalizie na kile kipande kingine toka Ifakara mpaka Mahenge.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja, *a luta continua. (Makofi)*

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa na mimi kupata kuchangia kwenye hoja iliyopo Mezani. Nitakuwa sijafanya sawa kama nisipomshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima. Lakini si mimi peke yangu na Wabunge wenzangu tukakaa hapa tukajadili haya mambo ambayo ni mazuri kabisa kwa mustakabali wa maendeleo yetu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, Manaibu wake, kwa kazi kubwa, nzuri wanayofanya. Niwashukuru kwamba na sisi Dar es Salaam maeneo mengi tunaona kuna fedha zimetengwa, tunaamini zitaenda kuleta maendeleo kwa watu wetu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mchache na kama unavyojua watu wa Jimbo la Kinondoni wana mategemeo makubwa sana na bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo na kuwaletea ili Kinondoni mpya tuliyokuwa tukiinadi kwenye kampeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na ujenzi wa nyumba kongwe za Magomeni. Nyumba hizi Mheshimiwa Rais alifanya uzinduzi pale akawaaminisha wananchi wangu wa Jimbo la Kinondoni, hasa wale waliokuwa wanakaa Magomeni, lakini vilevile na mimi nilitumia fursa ile kumuomba Mheshimiwa Rais nyumba hizi zikiisha watu wetu waliovunjiwa nyumba zao na wao wapate nafasi za kusihi, lakini nimeangalia kwenye kitabu cha bajeti hapa ukurasa

wa 160 imeoneshwa kwamba kuna ujenzi unaendelea lakini nimeenda kutafuta pesa kule nimeona kuna shilingi milioni 200 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba Wizara walitazame hili kwa jicho la rehema kwa sababu watu hawa wana matumaini makubwa sana na ujenzi wa hizi nyumba na kwa sababu Mheshimiwa Rais alishatoa *offer* kwamba watu watakaa miaka mitano bila kulipa kodi, sasa tusipojenga kwa haraka inaweza ikafika hiyo miaka mitano hata Rais mwenyewe asiwawahi watu wake wakati wanakaa. Kwa hiyo, naiomba Wizara ituongezee fedha pale na ujenzi uishe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Dar es Salaam na hasa Kinondoni ambako mji ulikuwepo zamani tulikuwa na barabara nyingi nzuri za lami, hivi sana tuna barabara zetu zimechafuka sana, zina mashimo mengi. Lakini unaona kwamba tunatengewa mpaka barabara za changarawe na vumbi, pale Kinondoni utaweka wapi barabara ya vumbi? Ni barabara ambazo nyumba zimesongamana, unapoweka vumbi maana yake vumbi unawapelekea wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sasa Waziri aangalie namna gani atazipandisha daraja barabara zetu za Manispaa ya Kinondoni. Mfano, tuna barabara muhimu sana, hii hapa ya Ndugumbi inakwenda pale Mwananyamala ya zamani sasa hivi inaitwa Makumbusho, Daraja la Harubu limevunjika, ile barabara tukiijenga tutasaidia watu kutoka katika njia kuu. Michepuko kwenye barabara inakubalika, labda kwenye mambo mengine huko ndiyo sina uhakika, lakini michepuko kwenye barabara ni jambo ambalo linasaidia sana kuondoa foleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa najikita, tuna barabara zetu za Tandale, kwa Bi. Mtumwa pale, tunahitaji ile barabara ipandishwe daraja ili ijengwe kwa kiwango kizuri. Tuna barabara zetu pale kwa Dunga, hii barabara ya Biafra ni barabara inatoka Biafra inakwenda kule Mwananyamala, ni barabara inayotumika sana. Lakini tuna barabara yetu

nyingine inaitwa ya Biafra inayotoka pale kwenye mataa inakwenda mpaka *Best Bite.* Tuna barabara zetu za Kijitonyama - Akachube ni barabara ambayo Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka bahati nzuri ni kwamba katika Jimbo langu la Kinondoni Wabunge wengi ni wakazi lakini vilevile hata wanaokaa nje wanapita pale. Kwa hiyo, barabara ile ya Akachube, barabara ya Mabatini ni barabara muhimu sana. Lakini Magomeni kuna matoleo, watu wa mwendo kasi pale Morocco pale karibu na Kanisa Katoliki ukitaka kuzunguka uje Manispaa au uende Chalinze...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakaa chini, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mhesimiwa Hussein Mohamed Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. Lakini nina mambo machache ya kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nilitaka nimuombe Mheshimiwa Waziri mwaka 2017 Septemba walitupatia fedha kwa ajili kufanya usanifu wa kilometa 149 barabara ya kutoka Tabora - Mambali - Bukene - Itobo kwenda Kahama. Lakini safari hii na mradi huu unaisha Desemba, 2018 huu nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye *financial* hiyo inayokuja kwa kuwa mtakuwa mmesha jua gharama mtutengee bajeti kwa ajili ya ujenzi ya ile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka niombe *rehabilitation* mmetenga fedha kwa ajili ya Mambali - Tabora na mmetenga fedha tena Mambali - Bukene hamjatenga fedha Itobo - Nzega kilometa 25 ninakuomba Mheshimiwa Waziri muiangalie hii kwa jicho la

huruma sana ni muhimu sana msipofanya *rehabilitation* ile barabara itakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo nataka niseme Mheshimiwa Waziri sekta ya ujenzi inachangia *almost* asilimia kumi ya pato la Taifa la nchi yetu, na *focus* ya Serikali ni kufungua miundombinu. Nataka nikuombe Mheshimiwa Waziri leta mabadiliko ya sheria ya *TANROADS* ili tu-*establish* kitu kinaitwa *preferential treatment* kwa *local contractors* miradi mnayotenga fedha kwa ajili ya aidha, tumekopa ama fedha zetu za ndani angalau *local contractors* wapewe *preference* ili ile fedha iweze kubaki ndani ya uchumi wetu kwa kiwango kikubwa. Kwa sheria iliyoko sasa hivi inatoa *preference only* kama ni fedha za ndani, lakini hata fedha mnazokopa ni fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niongee ni ukisoma hotuba ya Waziri ukurasa wa 170 mimi naunga mkono ujenzi wa *standard gauge.* Lakini Mheshimiwa Waziri ninachosikitika ni mabadiliko ya mwelekeo, ahadi yetu ya uchaguzi ilikuwa ni kujenga reli kutoka Dar es Salam na naomba ninukuu kidogo tu au kwa sababu ya muda niache ni kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora, kwenda Mwanza; kutoka Tabora kwenda Kigoma, kutoka Uvinza kwenda Msongati; kutoka Kaliua kwenda Mpanda Kalemii. Kwenye kitabu chako cha bajeti mwaka huu tunakupitishia *one point five trillion* unatenga *one point four* kwa ajili ya *phase one* na *two* shilingi bilioni 100 unatenga kwa ajili ya kwenda Isaka kinachonishangaza hii *decision basis* ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya uchumi ya mwaka 2015/2016 mizigo kwenye bandari ilikuwa tani milioni tano asilimia 34 ni Zambia, asilimia 34 ni DRC, asilimia 12 ni Rwanda, asilimia sita ni Burundi *our cash cow* ni ku-*save Eastern and Western* Congo na Burundi kwa nini mnataka kumfanya Mnyarwanda kuwa *hub* wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *Northen route* inajengwa kwenda Rwanda na sisi tunampeleka *line* ya Isaka kwenda Kigali, kitakachotokea ataunganisha kwenda Msongati yeye ataihudumia Congo, ataihudumia Burundi na mkumbuke tuna *East African Protocols* ambazo zitamfanya yeye achague kutumia *route* anayotaka niwaombe kwa heshima tujenge reli yetu kutoka Makutupora Tabora, Tabora - Isaka, Isaka - Mwanza, Tabora - Kigoma, Uvinza - Msongati Kaliwa kwenda Kalemii, baada ya hapo tujenge kipande cha Isaka kwenda Rwanda tutakuwa tuna *age over the others*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tunajenga na reli *bottom* laini yake ni mzigo. Nataka nikuombe Mheshimwa Waziri tuanze *preparation* sisi bandari yetu ki-*location* na masoko tunayoyahudumiwa tuna-*complete* na Durban na Beira, nataka niwaombe naombeni mkaritafakari hili Mheshimiwa Waziri tuanzisheni, sasa hivi kwa *regulation* zetu za *TRA* mafuta ya *transit* yanakaa kwa siku 30, ni ya kwanza….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda tayari Mheshimiwa.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nafasi ya upendeleo atapewa Mheshimiwa Selemani Kakoso Mwenyekiti wa Kamati ya hoja hii, dakika tano Mheshimiwa Seleman Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ya miradi mingi inayotekelezwa hapa nchini ikiwemo ya barabara, viwanja vya ndege, ununuzi wa meli, ununuzi wa ndege na ununuzi wa rada pamoja na miradi mingi ambayo ipo chini ya

Wizara hii. Niwapongeze sana wafanyakazi wa Taasisi zote kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na Waziri na wasaidizi wake. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mfupi nilikuwa naomba nizungumzie maeneo ya msingi ambayo tunahitaji tuishauri Serikali; la kwanza tunahitaji suala la kurudishwa maduhuli ya fedha za taasisi zinazokusanya fedha kwenye maeneo hasa ya Bandari, *TAA, TCRA,* waweze kuwezeshwa. Maeneo haya ni ya msingi ili tuweze kuyawezesha yaweze kufanya kazi vizuri, tunapokusanya fedha na tukachukua zote zikaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali tunazinyima hizi Taasisi ziweze kushindwa kufanya kazi.

Naomba sana Serikali iangalie umuhimu wa kuwawezesha bandari tunapoiwezesha bandari kuwarudishia fedha ziweze kufanya kazi wanaweza wakatengeneza mazingira ya kukuza bandari zingine nchini kwa maana Bandaria ya Mtwara, bandari ya Tanga na bandari za maziwa makuu kwa maana ya Mwanza na Kigoma. Tunaomba hili mliangalie kwa ukubwa wa aina yake ili muweze kuzisaidia taasisi hizi. Sambamba na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, sambamba na Mamlaka ya Anga ili waweze kuwezeshwa fedha hizi ziweze kufanya kazi za kuendeleza miundombinu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilikuwa naiomba Serikali iangalie tena ni jitihada ambazo zimefanywa kwa ajili ya kuliwezesha Shirika la *MSL. MSL* mmetoa fedha nyingi Serikali. Lakini tunaomba sana Serikali muwalipe mishahara wale wafanyakazi bila kuwawezesha au kuwalipa mishahara hamna kitu tutakachokuwa tumekifanya. Serikali inakarabati meli 14 lakini mpaka leo tunavyozungumza wafanyakazi hawajapata fedha na watakao *operate* hizo meli ni hawa hawa wafanyakazi. Tunaomba muwawezeshe ili waweze kufanya kazi na kulinda miundombinu ambayo tutakuwa tumewekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mfupi naomba nijikite kwenye eneo la jimbo langu. Serikali

imefanya kazi kubwa eneo la jimbo langu tuna ujenzi wa barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma eneo hili halijatengewa fedha nilikuwa naomba Serikali iangalie umuhimu wa kuweka fedha kiasi kwa ajili ya kuendeleza ile barabara. Tunashukuru Serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora naamni Serikali itafanya kazi kubwa kwa ajili yakuziunganisha hizi barabara, tunaomba eneo hili muliwezeshe na liweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la reli; tunaomba reli ambayo imewekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ifanyiwe kazi kama ilivyotengewa. Kamati yetu imeshauri Serikali tunaunga mkono jitihada za Serikali na kazi kubwa ambazo wamezifanya. Reli ya kutoka Dar es Salaam - Morogoro, reli ya kutoka Morogoro kwenda Dodoma, reli ya kutoka Makutupora kwenda Tabora na Mwanza tunaunga mkono na tunaomba reli ya kutoka Tabora kwenda Kigoma muiwekee umuhimu wa aina yake sambamba na matawi ya kwake ya kutoka Uvinza kwenda Msongati sambamba na matawi ya kutoka Kaliua - Mpanda - Karema, tunaomba maeneo haya myafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la mwisho kwa shirika *TRC* tunaomba eneo la Mkoa wa Katavi mlipelekee mabehewa ya kutosha kwa sababu barabara ya Mpanda - Tabora imefungwa tunaomba muwasaidie wananchi mpeleke behewa ili ziweze kuwasaidia kupata usafiri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mfupi naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga - Naibu Waziri wa Maliasili dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya na kuingoza nchi yetu ili tuweze kufikia katika uchumi wa kati. Pia naomba nichukue nafsi hii kumpongeza Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Naibu Mawaziri na Viongozi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitazungumza kwa kifupi nitazungumza hoja chache. Waheshimiwa Wabunge katika kutoa michango yao wamechangia katika maeneo mengi, lakini moja ya maeneo ambayo wameyazungumzia kwa kiwango kikubwa ni pamoja na miundombinu ambayo inaenda katika hifadhi zetu, inayokwenda katika vivutia mbalimbali vya utalii nchini kwetu, wengi wametoa malalamiko na wamezungumzia. Naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba nchi yetu ukiangalia maliasili tulizonazo, ukiangalia malikale tulizonazo, ukiangalia hifadhi tulizo nazo milima, maziwa na mambo mengine yote lazima kama Serikali tuwekeze vibaya sana katika maeneo haya ili tuweze kuvutia utalii na tuweze kupata mapato ya kutosha yanatokana na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuona kwamba hii ni sehemu pekee tunayoweza kupata mapato makubwa tumeamua kuweka nguvu kabisa katika kuimarisha miundombinu ambayo inaunganisha vivutio vyetu vya utalii katika maeneo mengi. Ndiyo maana utaona tunajenga viwanja vya ndege tumezungumzia Uwanja wa Ndege wa Iringa, Uwanja wa Ndege wa Chato ambao utafufua utalii katika maeneo yote yale na katika hifadhi zote zinazoonekana Selous na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima Serikali iwekeze katika miundombinu ya barabara tunataka watalii wa nchi hii wanaokuja katika maeneo yetu wawe na uwezo wa kwenda kwa barabara, wawe na uwezo kwenda kwa ndege, wawe na uwezo wa kwenda kwa kutumia reli, wawe na uwezo wa kwenda kwa kutumia boti na vitu vingine vyote kila mtu atajipima uwezo wake yeye mwenyewe. Ndiyo

maana Serikali inawekeza katika maeneo haya, uwekezaji wa namna hii tutapata mavuno makubwa sana baada ya miaka miwili/mitatu inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo ndiyo maana Serikali sasa tumeamua kununua ndege za kutosha, ndege hizi zitafanya kazi kubwa katika kuvutia utalii na kuimarisha utalii wa nchi yetu. Wapo watu wataongea maneno mengi, ndugu zangu utajiri huu tulio nalo mimi naamini kwanza hizi ndege tunazonunua ni chache ukiangalia hali tuliyonayo bado ni chache, tunahitaji nyingi zaidi. Mimi nadhani tungehitaji tuwe na *Dream Liner* angalau nne kwa pamoja; mbili ziwe zinaenda Marekani zinapishana kuleta watalii moja kwa moja kuja hapa, mbili ziwe zinaenda bara la Asia kuleta watalii moja kwa moja sasa hivi tunayo moja bado hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanazungumzia hii moja/mbili sijui taratibu, taratibu zipi unachozungumzia hapa ni kuwekeza ili tupate mapato ya kutosha yanayotokana na sekta ya utalii na mambo mengine katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Watanzania, naomba Wabunge wenzangu tuyaangalie mambo haya kwa mtazamo mpana ili nchi yetu iweze kusonga mbele tuweze kupata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia watalii sasahivi walioko kwenye nchi yetu ambao wamekuja kwa mwaka 2016 tulipata watalii 1,284,279 ambao walituletea bilioni 2.1 dola za Marekani, mwaka 2017 tumepata watalii 1,324,143 wametuletea bilioni 2.3 dola za Marekani; bado ukiangalia vivutio tulivyonavyo watalii hawatoshi. Nchi ya Italia peke yake ukichukua lile Jimbo la Platino peke yake lenyewe lina watu laki sita, lakini linapata watalii milioni sita kwa mwaka sisi ukichukua vyote bado hatuna. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema lazima tuwekeze, hii reli ya kati *standard gauge* kwetu sisi ni fursa ya utalii, italeta watalii wengi itatusaidia sana. Kwa hiyo, naomba wale

wanaozungumzia sijui *ATC* imepata hasara, siyo wakati huu sasa hivi ndo tunawekeza hatuwezi kuzungumzia hasara leo, baada ya muda tutapata muda wa kutosha wa kuweza kutathaimini na kuona kwamba hasara ipo au haipo sasa hivi ni wakati wa uwekezaj. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja naipongeza sana Serikali. (*Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote kwa juhudi wanayoifanya katika kuitendea mema nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijikite katika ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani - Saadani - Bagamoyo. Najua katika bajeti hii ya 2018/2019 barabara hii imo kwenye mipango ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Naiomba Serikali ihakikishe barabara hii inajengwa kama ilivyopangwa katika bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo inapitia Pangani - Saadani -Bagamoyo ina umuhimu sana. Kuna mbuga ya wanyama ya Saadani ambapo simba na tembo wanacheza pamoja katika ufukwe wa bahari wa maeneo ya Saadani yaliyopo karibu na Pangani. Barabara hii itasaidia kuleta watalii na kuweza kuliingizia Taifa fedha. Mbuga hii ni nzuri kwa hiyo ujenzi wa barabara utasaidia kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kununua ndege ambazo ni hatua kubwa ya maendeleo. Katika Kata ya Bweni, Wilaya ya Pangani kuna hoteli inaitwa Mashadu. Hoteli hii ina kiwanja kizuri cha ndege ambapo ndege ndogo hutua kushusha na kupandisha abiria. Naiomba Serikali ifanye utafiti ili kama kuna uwezekano

ndege ndogo za kwetu zitue katika kiwanja hicho kilichopo Mashadu, Wilaya ya Pangani.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukumbushia ahadi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa alipokuja Mkoa wa Songwe mwaka 2017 ambapo aliahidi mbele ya Wanambozi kwamba bararaba ya kutoka Mlowo - Kamsamba - Kilyamatundu (Rukwa) itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Ukisoma ukurasa wa 222 wa hotuba ya Waziri barabara ya Mlowo – Kamsamba yenye urefu wa kilometa 130 imetengewa shilingi milioni 120 tu, je, fedha hizi zitatengeneza lami ya kilometa 200 kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naiomba Serikali itekeleze ahadi yake ya kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidi kwa wananchi. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Songwe na Rukwa na ni suala la kisera kuunganisha barabara zote ambazo zinaunganisha mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara inayounganisha Wilaya ya Mbozi na Songwe kupitia Kata ya Magamba (Songwe) na Kata ya Mgamba (Mbozi) haijatengenezwa hata kwa kiwango cha changarawe jambo ambalo linawanyima fursa wananchi wa Wilaya ya Songwe kufika Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe ambayo yapo Wilaya ya Mbozi. Wananchi wa Wilaya ya Songwe hulazimika kupitia Mbalizi, Mkoa wa Mbeya ili kufika Makao Makuu ya Mkoa. Naishauri Serikali itengeneze barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote. Aidha, nakupongeza wewe binafsi kwa kuongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tena kwa mara nyingine napenda kuzungumzia mwenendo mzima wa safari za ndege nchini hususan ndege ndogo ndogo. Namuomba

Mheshimiwa Waziri ikimpendeza atoe maelezo kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani ndege ndogo ndogo za karibu mashirika yote yanayotoa huduma kwa safari za ndani zinaendeshwa na rubani mmoja. Nakusudia kwamba nyingi ya ndege hizi zinaendeshwa na rubani mmoja tu bila ya rubani wa akiba. Ndege hizi pamoja na udogo wake zimewekewa viti vya rubani wa akiba lakini cha kushangaza hakuna siku utakuta kuna rubani wa akiba katika kiti kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, viti hivi huwa vinatumika kupewa abiria jambo ambalo sio sahihi. Rubani ni binadamu kama binadamu mwingine anaweza kupata matatizo wakati wowote na mahali popote na mifano imeshatokea. Hivi karibuni tulisikia kwenye vyombo vya habari nadhani ilikuwa Marekani bwana mmoja alikuwa akitokea kiwanja kimoja kwenda kingine kwa safari za kawaida yeye na mkewe tu. Katika safari yao walipokuwa angani yule bwana ulimpata ubinadamu kulekule angani akaumwa na kufariki kulekule angani. Kilichomsaidia yule mama kwa bahati na yeye alipitia mafunzo ya urubani na aliweza kuiongoza ndege na kutua salama na kutoa mwili/maiti kwenda kuzikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba naishauri Serikali itilie maanani juu ya kuwepo marubani wa akiba katika ndege za mashirika yote yanayomiliki ndege ndogo ndogo zinazotoa huduma ndani ya nchi na wasiachiwe vile viti vya rubani wa akiba kuviuza kwa abiria. Sina uhakika juu ya sheria zetu za anga hapa Tanzania juu ya marubani wa akiba, namuomba Waziri atufahamishe tupate uelewa mpana pengine ninavyodhani ni kinyume.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani na pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayofanyika. Nampongeza Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu; Waziri Mkuu na Baraza lote la Mawaziri, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo ninayojivunia anayoyafanya Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni pamoja na kujenga uchumi wa viwanda; kujenga nidhamu ya watumishi; kukemea uzembe; kuendesha vita dhidi ya ufisadi na dawa za kulevya; kufufua Shirika la Ndege Tanzania; kujenga reli ya kisasa *(SGR)* na barabara; kuongeza vyanzo vya umeme ikiwemo miradi ya gesi ya *Stiegler's Gorge Hydro Elecricity Power* na kusambaza umeme hadi vijijini; kujenga bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) – Tanga (Tanzania); kuimarisha huduma za afya; kutoa elimu ya msingi hadi kidato cha nne bila malipo; kujenga miradi ya maji; kuandaa mifuko ya maendeleo ya vijana, akina mama na walemavu; na kuhamishia makao makuu ya nchi Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naishukuru Serikali kwa kuipatia Wilaya ya Longido miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa maji safi na salama kutoka Mto Simba Mlimani Kilimanjaro hadi Longido Mjini wenye jumla ya shilingi bilioni 16;

(ii) Ujenzi wa vituo vitatu vya afya katika Kata za Longido, Engarenaibor na Kimokoukwa/Namanga zinazogharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.5;

(iii) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo imetengewa fedha za kujengwa katika mwaka huu wa fedha wa 2018/2019;

(iv) Umeme wa *REA* Awamu ya Kwanza na Pili ambayo ulifikia vijiji 19 kati ya vijiji 49 vya Wilaya ya Longido; na

(v) Barabara inayosimamiwa na *TANROADS* kutoka Sanya Juu hadi *juction* ya barabara ya Mto wa Mbu Ngaresero yenye zaidi ya kilometa 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika kuiomba Wizara iangalie orodha ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Sanya Juu, Wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro hadi Mjini Longido, Mkoa wa Arusha (kilometa 64). Barabara hii ilibainishwa kwenye Ilani ya CCM ya 2015-2020;

(ii) Kuendeleza mradi wa *REA* ili umeme ufike katika vijiji 30 vilivyosalia ndani ya Wilaya ya Longido. Kati ya kata 18 za Wilaya ya Longido ni kata 10 tu ndizo ambazo zimeshafikiwa na umeme wa *REA*. Kati ya vitongoji 176 za Wilaya ya Longido ni 36 tu ndizo vimefikiwa na umeme.

(iii) Katika Wilaya ya Longido bado tuna vijiji vingi ambavyo bado havina mitandao ya mawasiliano ya simu. Mbaya zaidi baadhi ya vijiji hasa kama Kata nzima ya Matale, Gelai - Wosiwosi na Kamwanga zinalazimika kutafuta mawasiliano ya simu kwa kutumia mitandao ya nchi jirani ya Kenya. Maeneo mahsusi ambayo bado hayana mawasiliano ya simu ni pamoja na Kata ya Matale, Gelai, Meirugoi, eneo la Wosiwosi, Kata ya Lumbwa, Elang'ata Dapash, Noondoto, Engikaret eneo la Kiserian na Kata ya Kamwanga.

(iv) Kutokana na kupanuka kwa eneo la jiografia na la kiutawala hasa kwa kuongezwa vijiji, kata na tarafa mpya Wilayani Longido, kuna vijiji kadhaa ambavyo bado vina changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara. Naziomba *TARURA* na *TANROADS* zitusaidie kufikisha huduma ya barabara katika vijiji vya Meirugoi – Magadini (kilometa 34); Gelai Lumbwa – Wosiwosi (kilometa 54); Ketumbeine – Elang'ata Dapash (kilometa 18); barabara ya Ketumbeine hadi Iloirienito (kilometa 24); Meirugoi – Nadaare (kilometa 14); Engarenaibor – Matale C (kilometa 15); Namanga – Sinonik na Kimwati (kilometa 40); Sinya – Namanga (kilometa 30) na Engikaret – Kiserian (kilometa 14).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna barabara nyingi za kuunga vijiji na vitongoji vyake zinazoendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi Wilayani Longido, naiomba *TARURA* itenge fedha za kuwaunga mkono wananchi kwa kupitisha greda katika barabara hizo ili zipitike kirahisi. Miongoni mwa barabara zinazojengwa kwa sasa kwa nguvu za wanachi ni pamoja na barabara ya Mundarara – Orpukel – Gelai (kilometa 20); barabara ya Mundarara – Ingokiin – Engarenaibor (kilometa 15); barabara ya Mundarara – Injalai (kilometa 8); barabara ya Mairowa – Ing'ong'wen (kilometa 12); na barabara ya Matale A – Emurutoto – Mesera (kilometa 16).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba niishauri Serikali kuhusu kuboresha huduma za usafiri wa anga na barabara kuja mji mkuu wa makao makuu ya nchi, Dodoma. Nashauri *ATCL* waanzishe safari za kutwa asubuhi na jioni kutoka Dar es Salaam – Dodoma; Dodoma – Arusha/ Kilimanjaro; Mwanza – Dodoma na Dodoma – Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri vilevile barabara za Mji wa Dodoma ziboreshwe, vibao viwekwe na kuwe na *parking* ya uhakika nje ya eneo la Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kazi nzuri. Vilevile pongezi ziwaendee Naibu Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimefurahi sana kwa maelezo yaliyopo katika ukurasa wa 11, aya ya 23, kipengele cha (iii) kwamba barabara ya Geita – *Bulyanhulu Junction* - Kahama *(Lot 1 anda Lot 2)* kuwa usanifu wa kina wa sehemu ya Geita – *Bulyanhulu Junction* (kilometa 58.3) na *Bulyanhulu Junction* – Kahama maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Kwa kuwa barabara hii ni kiunganishi kikubwa sana na muhimu kiuchumi

kati ya Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga, naomba Serikali ianze ujenzi wa barabara hii maana ni ahadi ya muda mrefu sana kwa ajili ya kuimarisha uchumi katika mikoa husika. Vilevile ndiyo barabara muhimu inayotumika kusafirisha bidhaa na malighafi muhimu zinazotumika katika shughuli za uchimbaji wa madini. Ikikamilika barabara hii itasaidia kuinua uchumi utokanao na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande na barabara za mkoa, kwanza nimpongeze sana Meneja wa *TANROADS*, Mkoa wa Geita kwa kazi nzuri sana inayofanyika ndani ya Mkoa wetu wa Geita. Kwenye bajeti ipo barabara ya Geita – Bukombe ambapo Serikali imepanga kujenga kilometa moja ya lami, mimi nashukuru sana kwa mpango huu. Niombe kwamba baada ya kupitisha bajeti hii utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii uanze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo zipo ahadi za kilometa tano za lami katika Mamlaka ya Mji Mdogo Katoro ambazo ziliahidiwa na Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wa kampeni mwaka 2015. Naomba pia ahadi hizi ziangaliwe na utekelezaji ufanyike. Tangu mwaka 2015 hadi leo ni miaka mitatu sasa sijaona utekelezaji wa ahadi hii. Naomba Wizara mlichukulie suala hili na mlifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwa mpango wa Serikali uliopo ukurasa wa 162 juu ya upanuzi wa vivuko mbalimbali ikiwemo ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Charo – Nkome. Kwa ujenzi wa maegesho ya Bukondo itarahisisha kwa kiasi kikubwa usafiri kwa wananchi wa Mkoa wa Geita kwani ilikuwa ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa maeneo ya Geita na Chato. Niombe sana ujenzi wa maegesho katika maeneo haya uanze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba barabara ya Katoro – Busanda – Nyakanga - Nyabulolo – Kamena – Nyamalimbe – Mwingiro ipandishwe hadhi kuwa barabara ya mkoa ili kurahishisha mawasiliano kati ya Wilaya ya Geita na Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina la ziada, naunga mkono hoja.

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Itoni Njombe – Ludewa -Manda imeanza kujengwa tayari kilometa 50 lakini ujenzi wake unaenda taratibu mno. Ikumbukwe barabara hii inaenda kwenye miradi kielelezi ya Mchuchuma na Liganga. Barabara hii ina vipande vinne vya ujenzi *(lots)*, tunaiomba Serikali kwa umuhimu wa miradi hii tuongezewe kipande kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kandokando ya Ziwa Nyasa - Lupingu- Matema (kilometa 139). Eneo hili ambalo linapakana na nchi ya Malawi halina barabara kabisa na hivyo kufanya vijiji 15 kutokuwa na mawasiliano ya barabara. Hata hivyo, wananchi wameanza jitihada za kulima kwa kutumia zana duni za majembe, nyundo, mitalimbo, mapanga na kadhalika. Hivyo, tunaiomba Serikali kuchangia jitihada za wananchi kwa kutoa fedha kwa mfumo wa *Force Account*. Eneo hili lina tija kwa nchi, kwani lipo mpakani mwa nchi kwa hiyo lina umuhimu kiutalii, kiulinzi na kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ndiyo pekee katika mpaka wa nchi ambalo halina barabara. Mbamba Bay - Lituli (kilometa 112) barabara ipo, Matema - Ikombe (kilometa 10) barabara ipo lakini eneo hili ambalo ndiyo katikati halina huduma ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione sasa umuhimu wa kuunda Bodi ya TEHAMA nchini kutokana na kukua kwa teknolojia ya TEHAMA ili kudhibiti mfumuko wa watu wasiozingatia taratibu na kanuni za uendeshaji wa TEHAMA. Imefikia wakati sasa wa kuwa na Bodi ya Wanataaluma ili kutengeneza udhibiti na uendeshaji mzuri. Pia viwango vya elimu katika kada hiyo vizingatiwe ili kuepuka muingiliano na pia vifaa vilivyoisha muda wake viharibiwe ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) umeanza ujenzi wa minara katika Kata za Lupingu, Makonde, Kilondo na Lumbila. Tunaipongeza Serikali kwa zoezi hilo lakini imenza kazi hiyo katika Kata ya Lupingu, Vijiji vya Nindi na Ntumbati. Zoezi hilo ambalo limeanza katika vijiji hivyo linaenda taratibu mno. Tunaiomba Serikali iongeze msukumo katika ujenzi wa minara hiyo ya mawasiliano ya simu. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Nditiye kufuatia ziara yake aliyoifanya Jimboni Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe Serikali sasa kutupatia vituo vya kupakia na kushusha mizigo katika vijiji vya Nkwimbili (Yigha), Makonde, Nsele, Chanjale na Nkanda vilivyopo kando kando ya Ziwa Nyasa. Hii ni kutokana na umbali kati ya kijiji na kijiji na pia ndiyo njia pekee ya usafirishaji kwa maeneo hayo na usafirishaji wa mizigo hasa ya kibiashara umekuwa mgumu sana, imefikia wakati sasa wananchi kupitia Serikali kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la wananchi walioachia maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa bandari kwa vijiji vya Manda na Lupingu katika Wilaya ya Ludewa. Ni lini fidia italipwa na ujenzi wa bandari hizo utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, Serikali imekuwa ikilipa shirika hili mzigo wa kuwalipa pensheni wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupelekea shirika kuyumba katika uendeshaji. Mpaka sasa Serikali inadaiwa shilingi bilioni 4.7. Hali hii inaliyumbisha shirika kwa kiasi kikubwa. Je, Serikali haioni umefika wakati sasa wa kuondoa kero hii kwani inafifisha uendeshaji wa shirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TTCL,* natoa wito kwa Serikali kulipa uwezeshaji shirika ili liweze kutengeneza mtandao mpana wa kimawasiliano nchini. Aidha, shirika hili lipewe nguvu za ushindani katika soko.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na ukarimu aliyetuwezesha kuwa na afya na uzima siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kuipongeza na kuishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya Ujenzi kwa kusikiliza ombi langu na kujibu shida za barabara yetu ya Ubena Zomozi – Ngerengere – Tununguo – Mvuha - Kisaki mpaka Selous kwa kuipandisha daraja kuwa ya mkoa na kutengewa fedha katika bajeti hii shilingi bilioni tano kwa ajili ya kutengeneza barabara hii na kuiboresha ili iweze kupitika mwaka mzima na kutumika pia kupeleka vifaa vya ujenzi katika mradi Mto Rufiji. Vilevile nashukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa matengenezo mbalimbali katika barabara ya Bigwa – Kisaki, Madamu – Kinole - Msomvinzi – Mikese na madaraja na sehemu korofi katika Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matengenezo hayo ya barabara ya Bigwa - Kisaki lakini barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi na wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki, Morogoro Vijijini, Morogoro na Taifa kwa ujumla. Nasema ni muhimu kwa sababu ni barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya Mvuha. Pia ni barabara inayokwenda katika Mbuga yetu ya Selous kwa lango la Kisaki. Ni barabara inayounganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani kupitia Kisaki - Stiegler's Gorge na kufika Kibiti, Rufiji na kurahisisha mawasiliano na muingiliano wa watu wetu kati ya Morogoro na Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ipo katika Ilani ya CCM kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa umbali wa kilometa 78 toka Morogoro - Bigwa – Mvuha. Pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wa wakati huo ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwa barabara hii itatengenezwa kwa

kiwango cha lami. Naiomba sana Serikali yangu ya CCM kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuinua uchumi wa watu wa Mororgoro Vijijini na Taifa kwa ujumla na kutusaidia watu wa Morogoro Vijijini kufikisha bidhaa zetu za mazao ya kilimo kwenye masoko kwa urahisi na kuinua utalii katika pori na Mbuga yetu ya Selous.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imebeba imani ya wananchi wangu kama Mbunge, Chama cha Mapinduzi, Serikali yangu na Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwa tukiahidi tutatekeleza na kuzingatia Ilani na sera zetu za kuunganishwa kwa kiwango cha lami. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshamalizika muda mrefu na wananchi walishapisha na kuondoka katika maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa sijaona dalili za kuanza ujenzi huo wa kiwango cha lami na tumebakiwa na miaka miwili kufika mwaka 2020 kipindi cha mwisho kutekeleza Ilani ya Chama chetu CCM ikiwamo hii barabara ya Bigwa – Kisaki kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sijaona katika bajeti hii barabara za mkoa kwa mkoa kutengenezwa kwa kiwango cha lami kati ya Mkoa wa Mororgoro na Pwani. Pia barabara hii inakwenda kwenye mradi mkubwa wa umeme wa Stiegler's ambao una manufaa makubwa kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka kuiomba Serikali kupandisha hadhi barabara ya Ngerengere – Diguzi-Matuli – Kwaba - Mkulazi mpaka Kidunda ili iwe katika ngazi ya mkoa kwa sababu pamoja na uwepo wa *TARURA,* lakini ni changa na barabara hii ni ndefu ina urefu wa kilometa 75 na ina miradi mikubwa miwili ya kitaifa ya Bwawa la Kidunda na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi. Barabara hii haipo kwenye mipango ya bajeti hii wakati miradi ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi inatelekezwa mwaka huu. Naiomba Serikali kutenga

fedha za matengenezo ya barabara hii ili kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa uwekezaji wa viwanda katika Kata ya Mkulazi na Matuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la mawasiliano; hatuna mawasiliano ya simu katika Kata ya Mkulazi, Matuli, Tununguo, Seregete A&B pamoja na Kata za Kibuko, Tomondo, Tegetelo na Ludewa. Naomba sana mawasiliano kwenye kata hizi na mkazo zaidi katika Kata ya Matuli na Mkulazi sababu ni kata zenye miradi mikubwa ya kielelezo ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda na Kiwanda cha Sukari Mkulazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo nina ushauri kwa Wizara kwa mambo yafuatayo:-

(i) Barabara ya Kidahwe – Kasulu (kilometa 63); barabara hii imeanza yapata sasa miaka 13 haijakamilika na ujenzi wake ni takribani asilimia 30 tu. Tatizo kubwa ni kwa sababu barabara hii pamoja na kipande cha Kabingo/ Nyakanazi (kilometa 50) hazipewi kipaumbele kabisa. Tafadhali namwomba Waziri a-*fast track process* ya kujenga barabara hizi kama sehemu ya barabara kubwa ya Kidahwe – Nyakanazi. Sisi wananchi wa Kigoma sasa tumechoka kusubiri barabara hii. Kwa maoni yangu juhudi zinazoendelea ni njema lakini muda ni jambo la msingi sana. Haiwezekani tusubiri zaidi ya miaka 26 barabara hii.

(ii) Barabara za *Lake Tanganyika* chini ya *Lake Tanganyika Transport Programme* (*LTTP/FS&DD*), hizi ni barabara zipi na zina urefu gani?

(iii) Barabara ya Kasulu – Manyovu, chini ya mpango wa barabara za Afrika ya Mashariki inaanza kujengwa lini? *Timeline* yake ikoje? Tusubiri tena miaka mingapi?

(iv) Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*; juhudi zinazofanyika kujenga reli hii ni za msingi sana, Dar es Salaam - Morogoro na Morogoro - Makutupora kazi inaendelea vyema. Ajabu ni shilingi bilioni 100 kutengwa kwa ajili ya Isaka – Rusumo - Kigali. Mantiki ya kibiashara na kiuchumi ya kuanza kujenga kipande hiki ni nini hasa? Je, ni kuisaidia nchi ya Rwanda kupata reli au ni kuifanya Kigali iwe *business hub* ya nchi za Maziwa Makubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi siungi mkono kabisa ujenzi wa kipande hiki kwa sasa kabla ya kujenga kipande cha Dodoma - Tabora. Pesa hiyo shilingi bilioni 100 ihamishwe na ipangwe kujenga kipande cha Dodoma - Tabora. *We have to be strategic and forward looking*. Tukifanya makosa shida na adhabu yake ni kubwa sana. Reli ni uchumi mpana.

(v) Mawasiliano vijijini na mijini; minara ya simu sehemu mbalimbali za nchi yetu ipo vizuri. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya Kata ya Muhunga, Kijiji cha Marumba mawasiliano ni taabu sana. Ili upate *network* yakubidi upande mti au usimame juu ya kichuguu. Aidha, katika Kijiji cha Karunga, Kata ya Heru Juu mtandao unasumbua sana.

| KIJIJI | KATA | JIMBO | WILAYA |
|---|---|---|---|
| Karunga | Heru Juu | Kasulu Mjini | Kasulu |
| Marumba | Muhunga | Kasulu Mjini | Kasulu |
| Mwanga | Mganza | Kasulu Mjini | Kasulu |

Tafadhali sana wenzetu wa Mawasiliano kwa Wote wafanye juhudi ili kuondokana na usumbufu huu kwa wananchi wetu.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri ya barabara iliyofanyika Singida Mjini. Naipongeza *TANROADS* kwa usimamizi mzuri wa barabara hizi hususani Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetazama bajeti ya Wizara hii sijaona utekelezaji ama mkakati wa utekelezaji

wa ahadi ya *bypass* kilometa 84 kwa kuanzia tungeanza na kilometa 46 hali itakayotusaidia kupunguza msongamano wa magari makubwa kupita katikati ya mji. Naomba Serikali kuzingatia maombi haya.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Naomba kujua ahadi ya Rais ya barabara ya Kwa Mkocho – Hospitali ya Wilaya ya Kilwa na ahadi ya Rais ya kujengwa kiwango cha lami kilometa nane katika Mji Mdogo wa Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua malipo ya wananchi waliothaminiwa katika maeneo ya mradi wa Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko. Naomba kwa heshima na taadhima wananchi hao walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua Bandari ya Kilwa Masoko upo mpango upi wa kuiendeleza kwa kuwa ni bandari muhimu hasa kwa kuwa upo mpango wa kujengwa kiwanda kikubwa cha mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa kihistoria wa Kivinje miundombinu ya barabara ni mibaya. Mifereji, barabara na madaraja ya Mji Mdogo wa Kivinje, hakuna bajeti wanayopanga. Naomba Mji Mdogo wa Kivinje utengewe fedha za kujenga miundombinu ya barabara, mifereji na madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Masoko tuna kiwanja cha ndege. Kutokana na Mji wa Kilwa Masoko na Kilwa kwa ujumla kukua ni muhimu kuimarishwa na kupanuliwa kwa uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie maombi na ushauri wangu. Natanguliza shukrani, ahsante.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa miradi mbalimbali ya

maendeleo inayoendelea katika nchi hii. Licha ya pongezi hizo, kumekuwa na changamoto nyingi mno zinazoikabili Wizara hii nazo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bandari hususani Bandari ya Dar es Salaam ina changamoto kubwa ya ujenzi wa magati na kina kirefu cha maji. Yapata miaka kumi na zaidi Serikali inahangaikia changamoto ya upanuzi wa gati hizo (gati namba 7 hadi 13). Licha ya changamoto ya gati na changamoto zote zinazoikabili Bandari yetu ya Dar es Salaam kushindwa kushindana na bandari jirani, ni vema Serikali ikajitathmini upya miaka 10 au 20 baadae hii bandari itaelemewa kupita kiasi hivyo muda umefika sasa kuigeukia Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Bagamoyo ni bandari ya kimkakati, ni mbadala mzuri kabisa wa Bandari ya Dar es Salaam. Mchakato wa bandari hii ulianza muda mrefu sana tangu mwaka 2012 - 2018 haujakamilishwa hususani wa fidia kwa wananchi wa Kata ya Zinga. Mwekezaji yupo tayari kuanza kulipa fidia wananchi wa kata hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna minong'ono kwamba mwekezaji atakuwa tayari kuchukua na kufidia ndani ya hekta 3,000 ila Serikali inahitaji mwekezaji achukue hekta 9,000. Yeye ameshajipambanua atakuwa na uwezo wa hekta 3,000 sasa hekta 9,000 hazihitaji hizo zote ni nyingi mno yeye anahitaji hekta 3,000 aendelee na kazi hii habari ya hekta 9,000 tunaweka mkwamo usiokuwa na msingi. Mnakwamisha zoezi kwa kung'ang'ania hekta 9,000 badala ya hekta 3,000 alizozihitaji mwekezaji. Serikali ifike mahali imruhusu mwekezaji a-*develop* hekta 3,000 kama alivyoomba ili kurahisisha eneo la bandari kuwa wazi na wananchi kuanza kulipwa fidia zao haraka na miundombinu ya kijamii ihamishwe haraka kama shule na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kutoa masikitiko yangu kwa Serikali. Inasikitisha sana watu hawajaondoka, hawajafidiwa, bado wanaishi pale lakini Serikali inaondoa wahudumu kwenye shule na zahanati ikiwa ni njia ya

kushinikiza wananchi wapishe eneo la bandari. Watapisha vipi ilhali bado hawajafidiwa?Kibaya zaidi hiyo shule na zahanati zimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Mawasiliano ya Simu *(TTCL)* ni Shirika la Umma ambalo linaushindani na mashirika ya simu ya binafsi (Tigo, Voda, Halotel na kadhalika). Shirika letu la umma lina madeni makubwa linadai taasisi na mashirika ya umma kitu kinachopelekea kushindwa kujiendesha na kushindana na mashirika binafsi. Hivyo ni vema wakalipwa madeni hayo ili wafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa *TAZARA* wana madai ya muda mrefu ya malimbikizo ya mishahara, *overtime* na marupurupu yao. Ni vema Serikali izingatie suala la ulipaji madeni ya watumishi ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hilo deni la mishahara ya watumishi, pia *TAZARA* imekuwa inakabiliwa na changamoto ya sheria yake kupitwa na wakati na kutoenda na wakati ulipo. Suala la *CEO* wa *TAZARA* kwa sheria ya sasa ni lazima atoke Zambia jambo ambalo sio sawa kwa maendeleo ya reli yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa mapungufu makubwa ya sheria hiyo hiyo kumekuwa hakuna *condition* juu ya masuala ya fedha, kitu ambacho mwaka huu wa fedha unaisha Serikali zote mbili Tanzania na Zambia tumetenga fedha za maendeleo shilingi bilioni 26; shilingi bilioni 16 toka vyanzo vya ndani vya *TAZARA* na shilingi bilioni 10 kutoka Serikali Kuu. Kwa upande wa Tanzania fedha hizo shilingi bilioni 10 tayari zimeshatolewa ila kwa wenzetu wa Zambia hadi hivi tunavyozungumza bado hazijatolewa. Sasa hapa tunaongelea maendeleo ya reli ya *TAZARA,* je, yanaafikiwaje kama upande wa Muungano mwingine wa reli hawatengi fedha hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali ilete mabadiliko ya sheria, sheria hiyo ya *TAZARA* ifanyiwe marekebisho na viwekwe vifungu vinavyoweza kuweka

masharti juu ya masuala ya fedha kwa maendeleo ya reli yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali kwa kazi wanayoifanya. Nilichangia kwa kuongea, sasa nataka kuongeza mchango wangu kwa maandishi. Niendelee kumpongeza Mkurugenzi wa *TTCL*, Mwenyekiti wa Bodi na watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Serikali ilipe madeni ya *TTCL* kwa sababu kuna Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali ambazo zina madeni makubwa na ya muda mrefu sana ili kampuni iweze kujiendesha kiushindani na Vodacom, Tigo, Airtel na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuja na mpango mkakati wa kuboresha Shirika la Posta. Je, mkakati huo umeishia wapi? Majengo yao yanahitaji ukarabati, vifaa vya kisasa vya kazi, pamoja na maslahi ya wafanyakazi. Nina imani kama Serikali itafanya maboresho, shirika hili litajiendesha kwa faida kwa sababu lilikuwa na mali za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Posta Kodi na Anwani za Makazi ni muhimu sana kwa Taifa letu, utasaidia uchumi wa nchi, utarahisisha kupeleka mizigo na utasaidia hata *TRA* kukusanya kodi za majengo. Mbaya zaidi mwaka 2016/2017 Serikali ilitenga shilingi bilioni tatu; zilizotolewa ni shilingi milioni 95 tu sawa na asilimia tatu; mwaka 2017/2018 zilitengwa shilingi bilioni tatu lakini Serikali haikutoa pesa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali italeta sheria, kwani miundombinu katika vyombo vya usafiri inakuwa siyo rafiki kabisa na watu wenye ulemavu hawawezi kutoka *point A* kwenda *point B*, kwa sababu baiskeli yake haiwezi kupakia katika chombo cha usafiri. Bado hata baadhi ya majengo

siyo rafiki kabisa kwa watu wenye ulemavu. Mfano, majengo ya huduma ya hospitali, vituo vya afya, mashule hata hili Jengo tu la Bunge pamoja na kufanyiwa ukarabati bado Wabunge wenye ulemavu hawawezi kuyafikia majengo yaliyopo katika maghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali yetu, lakini ni vema sasa deni la makandarasi na wahandisi washauri wa miradi ya barabara wakalipwa pesa yao ya shilingi bilioni 711.13.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha *TEMESA* ni muhimu sana hasa Kitengo cha Ufundi (karakana). Ni kwa nini Serikali isiweke mkakati wa kuwa na vitendea kazi na ukarabati katika karakana za mikoa ili kitengo hiki kiweze kusaidia matengenezo ya magari yote ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali na iweke bei ambazo zingeweza kuvutia hata taasisi za watu binafsi ili waweze kutumia karakana hizo na kuweza kujiendesha kifaida kuliko ilivyo sasa kwamba karakana hizi huduma zake zimekuwa na bei kubwa sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuwashirikisha wanawake katika kazi za barabara kwa makandarasi wanawake. Ushauri wangu ni kwamba ni vema ushirikishwaji huo ungewekewa utaratibu wa kila Ofisi za *TANROADS* Mkoa kuendesha hayo mafunzo ya kuwajenga uwezo wanawake ili wanawake wote wapate fursa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kazi zinazofanywa na Wizara hii katika sekta zote za ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Kazi nzuri zimefanyika katika sekta ya ujenzi, barabara nyingi zimejengwa kwa kiwango cha lami na kiwango cha changarawe pamoja na madaraja makubwa ya nchi hii. Sasa kuna maandalizi kati ya Kigongo - Busisi kwa kuwa daraja hili linachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika Mashariki na kati za Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, DRC na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa daraja la Kigongo - Busisi kutaleta mapinduzi katika sekta ya uchukuzi kwani kwa sasa usafiri wa vivuko vya MV Sengerema na MV Misungwi vinazidiwa na wingi wa magari ya mizigo na magari ya abiria na kwa hakika ujenzi wa daraja hili litaleta tija. Pamoja na mgawanyo wa mamlaka za Wakala wa Ujenzi wa Barabara wa *TANROADS* na *TARURA,* bado naiomba *TANROADS* waendelee na utaratibu wa kuunganisha Mkoa wa Tabora kupitia Wilaya ya Urambo, Kaliua, Mkoani Tabora na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Mkoani Shinyanga Wilaya ya Mbogwe hadi Mjini Geita, Makao Makuu ya Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *TANROADS* Mkoa wa Geita chini ya uongozi wa Meneja, Haroun Senkunku na msaidizi wake Ndugu Maribe pamoja na watumishi wote wa *TANROADS* Mkoa wa Geita wanafanya kazi nzuri ya kupigiwa mfano. Ujenzi wa barabara zote zinazojengwa na kusimamiwa na *TANROADS* Mkoa wa Geita zina kiwango cha kuridhisha. Ninachoomba na kushauri ni *TANROADS* kukichukua kipande cha Iboya – Bwendamwizo – Nyikundu - Ivumwa hadi Migo Wilayani Geita inaendana na barabara ya lami inayotokea Mjini Kahama kwenda Geita Mjini ambako ni Makao Makuu ya Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ione umuhimu wa kuimalizia barabara hii kwa kuwa kupitia Kikao cha Bodi ya Ushauri cha Mkoa wa Geita tuliomba barabara kutoka mji wa Ushirombo hadi Mbogwe kwenda Geita Mkoani, kilichotokea kipande ni sehemu hii ya maombi yetu ilichukuliwa na kipande cha Iboya - Bwendamwizo - Nyitundu - Ivumwa hadi Wigo kuelekea Mkoani Geita kiliachwa. Hivyo, naiomba Wizara isikie kilio chetu ikipandisha hadhi kwenda *TANROADS* ili Wilaya ya Mbogwe ipate barabara ya kuunganishwa na Mji Mkuu wa Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa za ujenzi wa bandari, reli, viwanja vya ndege, madaraja makubwa na meli za vivuko katika maeneo mbalimbali nchini. Hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na leo niweze kuchangia hotuba hii. Mchango wangu kwa leo naomba nianze na sera ya kuunganisha mikoa kwa barabara za lami. Ni wakati muafaka sasa sera hii iwekewe lengo, kwa maana haijulikani ni kwa muda gani sera hii itakamilika kwani hadi leo utekelezaji wake haueleweki. Mikoa mingine tumeanza kuunganisha Wilaya wakati mikoa mingine bado. Mfano, Mkoa wa Lindi na Ruvuma na Lindi na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano kwa karne hii ni jambo muhimu sana, lakini kutokupewa fedha za maendeleo ni kurudisha nyuma sekta hii, kwani sehemu kubwa ya nchi yetu mawasiliano ya simu ni duni sana. Pamoja na kuwepo kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(USCAF),* ni jambo la kusikitisha sana kuona fedha za mfuko huu nazo hazipatikani kwa wakati jambo linaloondoa dhana ya kuundwa kwa mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *USCAF* wanashindwa kutekeleza miradi yao kwa kutopewa fedha zao toka Hazina. Mfano katika Jimbo la Liwale lenye kata 20 ni sehemu chache sana kuna mawasiliano ya simu kwenye baadhi ya kata. Hali ni mbaya sana katika Kata za Mpigamiti, Lilombe, Miru, Ndapata, Mlembwe, Mkutano na Ngongowele. Kata hizi hali ya mawasiliano ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nangurukuru, Liwale ni barabara iliyotajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Hata hivyo, barabara hii ni kiungo muhimu sana kwa uchumi wa Kanda ya Kusini kwa ujumla. Pamoja na barabara ya Nangurukuru - Liwale lipo pia daraja la Mbwemkuru linalounganisha Wilaya ya Nachingwea na Liwale. Vilevile nashukuru barabara ya Liwale - Nachingwea angalau imetengewa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Ni ombi langu, fedha hizo zifike kwa wakati. Pia kuna daraja

linaunganisha Kilwa - Liwale katika Kijiji cha Nanjilinji. Naomba ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii ni bora zikapewa fedha zake kwa wakati ili ziweze kufanya vizuri. Taasisi hizi ni kama *USCAF*, *TTCL*, Bandari, *MSCL* na *TAZARA.* Taasisi hizi zinakwama sana kwa sababu ya upungufu wa mitaji na fedha za kutekeleza miradi yake ya maendeleo mfano *USCAF,* wana sababu gani ya kushindwa kutekeleza miradi yao kwa ukosefu wa fedha wakati fedha toka kwenye vyanzo vyao zinapatikana? Vilevile Serikali ilipe malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi wa *MSCL* ili wafanyakazi wawe na moto wa kufufua shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya viwanja vya mikoa ina makundi mawili; kuna vilivyotajwa kimoja kimoja na vingine vimewekwa kwa pamoja. Ninachotaka kujua, ni kwa nini iko hivi? Vile vilivyo pamoja tutajuaje vimejirudia pia kwenye madaraja ya mikoa na barabara za baadhi ya mikoa? Naomba kupata ufafanuzi juu ya jambo hili. Katika bajeti hii Mkoa wa Lindi miradi yake yote iko kwenye makundi hayo hapo juu, yaani yale ya jumla, fedha za Mkoa wa Lindi ni kidogo sana. Barabara ya Masasi – Nachingwea - Nanganga, upembuzi yakinifu umekamilika, lakini ni bajeti ya pili sasa barabara haitengewi fedha wakati huo huo ziko barabara zimekuja nyuma lakini zimepewa fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naliomba Shirika la Reli kuwalipa askari polisi waliowatumia kusindikiza treni kati ya mwaka 2016/2017 ambao bado wanadai. Askari hawa walifanya kazi kwa uaminifu, lakini malipo yao yamekuwa kitendawili. Gharama za ujenzi wa barabara zimekuwa kubwa kwa sababu ya sheria zetu ambazo kwa kiwango kikubwa hazina faida yoyote. Mfano, Sheria ya Madini, Sheria ya Maji, Sheria ya Mazingira na kadhalika. Mkandarasi hulazimika kuweka gharama za ununuzi wa madini kwa maana ya kifusi na Halmashauri kudai ushuru wa kifusi hicho. Kama vile haitoshi, watu wa mazingira nao wanadai fidia ya uharibifu wa mazingira unaotokana na ujenzi huo kwa kuacha au kufukia mashimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ingeondoa tozo hizi ili kupunguza gharama za ujenzi wa barabara hizo, kwani hayo maduhuli yote ni ya Serikali moja. Hivyo Serikali ifanye marekebisho ya sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa, naungana na ushauri wa Kamati kuwa Serikali ingeangalia sasa kushirikisha watu binafsi au kuomba wahisani kwani kutegemea fedha za ndani pekee kutaifanya Serikali kushindwa kuhudumia sekta nyingine au Wizara nyingine. Hivyo ujenzi unaoendelea sasa kwenye sehemu zilizobaki, jambo hili lingefikiriwa kwa manufaa ya Taifa kwa jumla ikiwezekana hata kukopa mkopo wa masharti nafuu. Kwa sababu ya kiuchumi, kipande cha Isaka na kile cha Kigoma Serikali ingeanza na kuacha Kigoma badala ya Isaka kwani *route* ya Kigoma ina vivutio vingi vya kiuchumi kuliko Isaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa wakandarasi ni bora yakafanywa kwa wakati kwani kulipa madeni haya kwa riba ni kupoteza fedha za walipa kodi. Wakandarasi wa kigeni wanafaidika sana na riba kuliko hata faida wanayoipata kwenye mkataba husika. Hakuna sababu ya kuingia mkataba na mkandarasi wakati hakuna fedha za kutekeleza mkataba husika.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kilometa sita zilizobakia kuwekwa lami kati ya Mbande – Kongwa, mwaka huu zifanyiwe kazi. Miaka 20 sasa tunaongelea jambo hili hili kila mwaka, haipendezi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Shirika la Posta takribani miaka 10 sasa hawafungui masanduku mapya? Imeleta matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia ya *bypass* ya barabara ya Hangoni - Sigino kwa barabara ya Babati - Singida na Babati - Dodoma italipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *TARURA* wapewe *50% not 30%.*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege Mkoa wa Manyara unajengwa lini? Eneo lipo Mamire Ngungu, Jimbo la Babati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halotel waliahidi kuweka mnara wa mawasiliano katika Vijiji vya Himit, Imbilili na Chemchem Jimboni kwangu. Jamani, hadi lini ahadi hii itatimia?

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatakie kila la heri.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa, Naibu wake Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017/2018 tulipitisha shilingi bilioni 12 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kahama – Bulyanhulu – Geita kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, hadi leo Aprili, 2018 taratibu za kupata mkandarasi hazijakamilika na kazi hazijaanza. Mwaka huu 2018/2019 Serikali imependekeza bajeti ya shilingi bilioni 18 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu lini hasa mkandarasi atapatikana na kazi kuanza? Shilingi bilioni 12 za mwaka 2017/2018, kiasi gani kimetolewa na kimefanya kazi gani? Lini hasa mradi huu utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta limekuwa likiwalipa *pension* waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Posta ya Afrika Mashariki kwa kipindi kirefu kwa niaba ya Serikali na Serikali inachelewa kurudisha shilingi bilioni nne ili Shirika la Posta liwalipe wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwalipe pesa hizo ili Shirika la Posta liweze kuendelea kwa mafanikio.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu *TEMESA;* yapo malalamiko ya wafanyakazi kwenye kivuko kwamba hawana mikataba ya ajira na hivyo kukosa fursa za kujiendeleza na hata hawawezi kukopa katika vyombo au taasisi za fedha kama wafanyakazi wengine walioajiriwa Serikalini. Naomba Serikali ifuatilie jambo hili ili wafanyakazi hawa ambao wengine wamefanya kazi kwa muda mrefu wapate haki wanazopaswa kupata kutokana na kazi wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya MV Victoria ni muhimu kwa usafiri kati ya Mkoa wa Kagera hasa Wilaya za Muleba, Bukoba, Misenyi, Karagwe na Kyerwa. Wananchi wote hawa wanategemea meli hasa kibiashara. Mkoa wa Kagera umegeuka dampo ya magari ya abiria yanayosafirisha abiria kutoka Bukoba – Mwanza kwa njia ya barabara. Biashara zote kutoka Mwanza kwenda Bukoba na Bukoba – Mwanza zinapita barabarani. Wananchi wanapata hasara kubwa. Malori yanapoharibika yakiwa yamebeba ndizi, huiva na kuharibika na hivyo kuwasababishia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya meli hii ya MV Victoria yatakamilika lini na kiwango gani cha matengenezo kimefikiwa? Wananchi wa Kagera ambao maisha yamekuwa duni kwa kupambana na ughali wa maisha kwa bidhaa kupanda bei kutokana na kusafirisha kwa njia ya barabara.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani kwako wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu wa maandishi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa umahiri wao wa kuongoza Wizara hii. Katika kuchangia Wizara hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yetu kwa namna inavyowekeza miradi mbalimbali katika nchi yetu. Miongoni mwa uwekezaji unaofanyika ni uwekezaji wa simu za mkononi. Hivi sasa simu za mkononi siyo kitu cha fahari *(luxury),* hata wananchi wa vijijini wanatumia kwa shughuli zao. Imekuwa simu ni kitendea kazi kwa watu wote lakini bado bei za simu hizo ni kubwa sana kiasi ambacho wananchi hasa wa vijijini wanashindwa kumudu gharama hizo. Ushauri wangu kwa Wizara hii ni kwamba waendelee kusimamia bei hizi na kuzifanya ziwe rafiki kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Wakurugenzi katika mashirika yetu, ni sehemu muhimu sana katika kusimamia na kuendesha mashirika hayo. Ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba ni vyema Wakurugenzi wanaochaguliwa wawe na ujuzi wa taasisi husika. Siyo vizuri Mkurugenzi wa Bodi ya *TTCL* awe ana ujuzi wa kilimo au daktari, hii haitaleta ufanisi mzuri. Ni vyema Mkurugenzi wa Bodi ya *TTCL* awe na ujuzi wa taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara tajwa hapo juu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Kanda ya Kusini ulikuwa na taa kabla ya uhuru. Baada ya uhuru taa ziliondolewa na kupelekwa Arusha. Kutokana na mahitaji, sasa hivi Uwanja wa Mtwara ni uwanja wa Kanda lakini hauna taa. Ni lini kwenye bajeti hii taa zitawekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisema akiwa Bukoba kuwa zimetengwa pesa shilingi bilioni 41 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mtwara. Mheshimiwa Waziri anasema shilingi bilioni 54 zimetengwa. Ni lini ukarabati utaanza? Kila mwaka yamekuwa yakisemwa haya na hamna utekelezaji, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa za chini chini kuwa *ATC Bombardier* wanataka kusitisha safari za Mtwara kwa kigezo kuwa abiria hawatoshi. Yapo mashirika binafsi mengi kwa mfano *Precision Air* wanaenda Mtwara kila siku asubuhi na wanapata abiria, iweje Shirika la umma lenye bei nafuu likose abiria?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kusini tunahitaji fursa ya *Bombardier (ATC)* tufaidi kama maeneo mengine. Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwa nini *Bombardier* inataka kuacha kuja Mtwara?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara hii iweke minara ya simu kwenye maeneo ambayo haipatikani mitandao hasa maeneo ya mjini pembezoni mwa Mtwara na mtandao hakuna kabisa; maeneo hayo ni Mbawala Chini, Mkangala, Mkunjanguo, Naulongo na Dimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ni lini maeneo haya ya Mtwara Mjini mtaweka minara ili mawasiliano yanapatikane?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Rukwa tunategemea Uwanja wa Sumbawanga Mjini kwa ajili ya usafiri wa anga ambao umefanyiwa uthamini lakini mpaka sasa hatujui kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Nkasi, Makao Makuu ya Wilaya ambayo yako Namanyere, tunaomba maboresho makubwa ili wananchi wake wanufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara ya Ntendo – Muze ni barabara muhimu sana kwani ikiboreshwa itawasaidia wananchi wa maeneo hayo wanaojishughulisha na biashara ndogo ndogo na kuwainua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomoa bomoa inawaacha wananchi wengi wanaathirika na sheria iliyopo ambayo inazungumzia mita 15 kwa mjini na mita 30 kwa vijijini. Tunaomba sheria hii iletwe ndani ya Bunge ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kala haina mawasiliano kabisa pamoja na Kata ya Ninde bado mawasiliano yake siyo ya uhakika. Naomba Serikali ipeleke mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *TARURA* wapewe fedha za kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa haraka na uhakika. Pesa zikipelekwa kwa muda muafaka itaepusha madhara ambayo yanajitokeza kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zinazounganisha mikoa zipewe kipaumbele ili kuleta baraka kwa wananchi kwa kuwainua kiuchumi, lakini kuepusha vifo vya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya Ziwa Tanganyika (MV Liemba) imekuwa ya muda mrefu ambayo hata ikifanyiwa matengenezo bado imechakaa. Naishauri Serikali kutafuta meli nyingine mpya ambayo itawasaidia Watanzania.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natoa pongezi nyingi kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa mengi ambayo yametekelezwa katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wake akisaidiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Naibu Mawaziri

wake wawili pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi wanavyojitoa kuhakikisha sekta inafanya vizuri na kuleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mapendekezo/maombi yafuatayo sambamba na mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vingi kama siyo vyote vya usafiri *(public transport)* havina miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu hali inayopelekea wengi wao kushindwa kusafiri toka sehemu moja mpaka nyingine au kutumia gharama kubwa kwa kutumia usafiri wa kikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri/mapendekezo/ maombi kwa changamoto hii, kuwe na ukaguzi wa miudnombinu itayowezesha mtu mwenye ulemavu kupanda pasipo shida yoyote ama kuwe na ukaguzi maalum wakati wa uagizaji wa vyombo hivi nchini/miundombinu (uwepo wa miundombinu hii) iwe ni kigezo kimojawapo cha mtu anayetaka kufanya biashara ya usafirishaji kukidhi kabla ya kupewa leseni ya usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii pia ipo kwenye usafiri wa treni zinazosafirisha abiria ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam. Watu wenye ulemavu wanashindwa kutumia usafiri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba zinaweza kutengenezwa ngazi ambazo zitasaidia watu wenye ulemavu kuitumia anapohitaji kupanda. Vilevile nashauri kuwe na msisitizo wa sheria kwenye majengo mapya pamoja na miundombinu ya barabara mpya zinapojengwa vikidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zinapotokea fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika Wizara hii, ni ombi langu kwamba kundi hili lifikiriwe. Fursa hizo ni pamoja na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba upatikanaji wa habari na mawasiliano uwe rafiki kwa watu wenye ulemavu hasa wasioona na viziwi kwa kuzingatia matumizi ya lugha ya alama na maandishi ya nukta nundu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hongera *for a good and comprehensive speech.* Nina *issue* mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya Wizara hii, barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Mataka - Mang'ola - *Old Junction* haikutajwa katika *body* ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imefichwa kwenye kiambatisho Na. 3. Nilitegemea vipande vya barabara hiyo ambavyo *FS/DD* ulikamilika zamani (Kolandoto hadi Mwanhuzi na Sibiti) vingeanza kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi. Ikumbukwe kuwa barabara hii imekuwepo kwenye mipango ya Serikali tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu - Bariadi haujaunganishwa kwa barabara ya lami kati yake na Mkoa wa Singida na Arusha. Sehemu ya kutoka Kolandoto – Mwanhuzi - Sibiti) *FS/DD* umekamilika. Ni vema sasa *FS/DD* ikaanza katika ya Ng'oboka –Mwandoya – Kisesa - Bariadi. Sehemu ya kipande hiki kipo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 - 2020. Naomba kuwasilisha.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kwa Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Same Mashariki lina tatizo kubwa sana la usafirishwaji wa mazao pamoja na abiria. Jimbo la Same Mashariki limebarikiwa sana kuwa na mito mingi pamoja na mvua za kutosha. Kwa hiyo, wananchi wanalima sana mpunga, tangawizi, mahindi na

ndizi. Pato kubwa la Halmashauri ya Same yanatoka Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Same - Kisiwani - Mkomazi ndiyo ilikuwa barabara kuu kutoka Nairobi – Arusha - Dar es Salaam, yaani ilikuwa *The great North Road.* Kutokana na siasa za wakati wa miaka ya *1970's* zilizokuwa zinaendeshwa Wilayani Same (wakati huo ikiwa ni Wilaya moja na Wilaya ya Mwanga) ilisababishwa kuanzishwa barabara ya lami ya sasa kutoka Dar es Salaam kupitia Mkomazi – Bwiko – Hedaru – Makanya – Same – Moshi – Arusha, matokeo yake wananchi wa Same, Kisiwani, Maore, Ndungu, Kihurio, Bendera, Mkomazi wakawa-*cut off,* maana usafiri wa mabasi uligeuza njia na kupitia njia mpya. Hili lilisababisha umaskini mkubwa kwa wananchi wa sehemu hii ya Same Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna miradi mikubwa ya Kitaifa inayoanzishwa Jimboni Same Mashariki. Miradi hii inaitikia wito wa Serikali wa kuanzisha viwanda. Miradi hiyo ni pamoja na *LAPF,* tayari wameagiza mashine ya kisasa ya kuchakata tangawizi. Tangawizi hii ina soko kubwa nchi za Uarabuni pamoja na Ulaya hasa Holland na Ufaransa. Wananchi kutoka Majimbo yanayopakana na Jimbo la Same Mashariki ambao pia wanatumia barabara hii ya Same Mashariki - Mkomazi yaani Majimbo ya Korogwe Vijijini, Mkinga, Mlalo na Same Magharibi ni kati ya wakulima wa Tangawizi ambao watafaidika na kiwanda hiki cha *LAPF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Umoja wa Mataifa *(United Nations Capital Development Fund-UNCDF)* wamemaliza mchakato wa uanzishwaji wa mabwawa ya kisasa ya uzalishaji wa samaki ambao watatosheleza mahitaji ya ndani ya nchi na pia kusafirisha nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mkubwa wa umwagiliaji katika Kata ya Ndungu ambao uligharamiwa na Serikali ya Japan. Mradi huu unazalisha mpunga mwingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimeleta hiyo *background* ili niiombe Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ifikirie upya kutenga fedha za kutosha ili hii barabara ya Same –Kisiwani - Mkomazi itengenezwe yote kwa kiwango cha lami. Kiuchumi itaongeza pato la Taifa na kuhakikisha *sustainability* ya viwanda vinavyoanzishwa. Fedha iliyotengwa kwa barabara hii ni kidogo sana kiasi *impact* yake haitaonekana kimaendeleo. Zaidi ya hivyo, ijulikane kwamba Jimbo hili la Same Mashariki limekuwa *marginalized* kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu iangaliwe fedha iliyotengwa kwa Mkoa wa Kilimanjaro na kiasi kinachopelekwa Jimbo la Same Mashariki utaona Jimbo hili halitengewi haki. Kibaya zaidi, kiwango cha kutengeneza barabara hizi mbili yaani Same – Kisiwani - Mkomazi ina kilometa 96.46 na Mwembe – Myamba - Ndungu kilometa 90 kimekuwa cha chini sana. Wamekuwa wakirudia rudia maeneo yale yale siku zote na kukwepa kutengeneza maeneo korofi. Sehemu kubwa haijengwi mifereji na hata Makaravati huwa yanakuwa yakifukiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hisia kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Same Mashariki kwamba kuna mchezo mchafu pamoja na ufisadi unaoendelea katika utengenezaji wa barabara hizi, ndiyo maana naona hata fedha nyingi zinatengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wakati hakuna mpango wa kutengeneza barabara hii ya Same - Kisiwani - Mkomazi kwa kiwango cha lami. Inawezekana fedha hizi zinatumika kwa manufaa ya watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sababu ya kupoteza fedha nyingi kwenye usanifu wakati hakuna nia ya kuiweka lami barabara hii ya Same – Kisiwani - Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *TARURA* kwa kushirikiana na Halmashauri zetu

wanunuliwe mitambo ya utengenezaji na kukarabati barabara zetu za vumbi. Mambo haya yamefanywa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Ushetu kwa udhamini wa Benki ya *CRDB*. Kama Wizara haina pesa, basi Wakurugenzi waruhusiwe kukopa Benki kwa masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *data* nilizonazo seti nzima ya vyombo hivi ikiwa ni pamoja na malori, *bulldozer*, kijiko haizidi shilingi bilioni moja. Kwa kufanya hivi tutapunguza gharama za *TARURA* kwani hata hivyo haina pesa. Kwa asilimia 30 hii, haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2014/2015 *ATCL* ilipata hasara ya shilingi bilioni 943 na mwaka 2015/2016 ilipata hasara ya shilingi bilioni 109.2 na mwaka 2016/2017 ilipata hasara ya shilingi bilioni 113.7

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi majuzi tumepokea ndege nyingine ya tatu. Naomba kuishauri Serikali iongeze bajeti kwa *ATCL* kwani kila mwaka hasara yake inaongezeka kwa asilimia 4.4. Hii shilingi bilioni 3.9 haitatosha kulipia gharama ya hasara ya mwaka wa fedha 2018/2019.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wizara ya Uchukuzi kwa mafanikio makubwa katika sekta za ujenzi wa barabara ya *Mtwara Corridor* kutoka Mtwara – Mbinga; ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania; ufufuaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL);* ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *SGR*; na utendaji mzuri wa bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hiyo nzuri, naomba kuchukua fursa hii kueleza changamoto zinazolikabili Jimbo la Songea Mjini ambazo zinafanya utekelezaji wa Ilani ya CCM kuwa ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya mchepuko wa *Mtwara Corridor* -Songea Mjini (kilometa 11); ili *Mtwara Corridor* ikamilike ni lazima kipande cha mchepuko cha kilometa 11 kilichopo Songea Mjini katika Kata za *Seedfarm,* Msamala na Ruhumiko. Kutokukamilika kwa kipande hiki ambacho ni sehemu ya mradi namba 4197 ni kikwazo kikubwa sana katika mradi mzima wa *Mtwara Corridor.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Songea Mjini hakuna hata barabara moja iliyotengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2018/2019. Naomba sana barabara hii ya kilometa 11 ya mchepuko ya *Mtwara Corridor* - Songea Mjini ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Songea Mjini hakuna barabara hata moja katika bajeti nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana sana Mheshimiwa waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano barabara ya *Mtwara Corridor* - Songea *bypass* kilometa 11 iingizwe.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa, Naibu Mawaziri wote na timu nzima ya utendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanayotekeleza katika kutimiza majukumu ya Wizara. Pongezi pia kwa *TANROADS Manager* wa Morogoro, *Engineer* Doroth Mtenga na timu yake kutekeleza majukumu yao katika mazingira magumu na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya barabara ni kuunganisha barabara za kuunganisha Mikoa ziwe za lami. Ni lini barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi - Kilosa Mpepo – Londo – Lumecha – Songea itaanza ujenzi wa lami? Barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli na muda umebakia kidogo na utekelezaji wa ahadi ya Rais mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Barabara inaelekeza kujenga barabara za Makao Makuu kwa kiwango cha lami. Wilaya ya Malinyi tunapendekeza/kuomba kuanza ujenzi wa barabara ya lami kwa kilomita mbili katika Mji wa malinyi. Ombi letu halitekelezwi. Tunaomba kauli ya Waziri, atueleze ni lini ataanza kutenga bajeti ya kuanza kujenga barabara ya lami katika Mji wa Malinyi (Makao Makuu ya Wilaya)?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu uharibifu wa barabara katika Mkoa wa Katavi hususani katika Jimbo la Kavuu. Kwa kuwa barabara ya Tabora - Mpanda imeharibika sana na imefungwa kwa muda; je, Serikali haiwezi kuongeza mabehewa kwa njia ya reli kutoka Tabora - Mpanda ili kuweza kuwapunguzia adha wananchi wa Katavi kwani mabehewa ni machache? Kwa hiyo, ni vyema yaongezwe kwa madaraja yote, yaani kwa maana ya mabehewa ya daraja la kwanza, la pili na la tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa na Naibu Mawaziri wake wote, Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa *Engineer* Nditiye. Nampongeza sana Katibu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nampongeza *Engineer* Mfugale na Mkurugenzi wa *SUMATRA* kwa msaada mkubwa wa Jimbo langu la Nyasa, pia wa Bandari na Mfuko wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa jitihada kubwa iliyofanyika ya kuwezesha kuanza ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbambabay kwa kiwango cha lami na mkandarasi yupo *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kukubali ombi letu la dharura la ujenzi wa Daraja la Mitomoni katika barabara ya Nyoni Liparambe – Mkende. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mto umekula watu wengi sana huu kutokana na watu kuzama kwa vivuko hafifu. Tutaomba ujenzi huo upewe kipaumbele na hata katika utoaji wa fedha uwe *first charge*, bora tuchelewe kidogo maeneo mengine japo nayo ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mahitaji ni mengi lakini kwa kuwa sungura ni mdogo itoshe kushukuru, bila kusahau mawasiliano katika Kijiji cha Kihurunga na Liparambe Ndondo na kuboresha maeneo ya Ng'ambo na Chiwande. Karibuni Nyasa!

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya barabara Mkoani Iringa yamekithiri. Ninaomba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilichukue jambo hili kwa umakini ukizingatia mkoa huu unachangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Waziri wakati wa matengenezo ya barabara hasa kwa kutumia kifusi, kitumike kifusi ambacho hakina mawe yenye ncha kali, kama kifusi kilichowekwa barabara kutoka Tagamenda - Kitayawa - Ndiwili pamoja na Kidabaga; kifusi hicho kinasababisha uharibifu wa tairi za magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wakati wa ujenzi wa barabara za lami kushirikisha Serikali za Vijiji kuwa walinzi wa alama za barabarani kwa kuwa wakati wa ziara iliyofanywa na Kamati ya Miundombinu tumekuta baadhi ya wananchi wanazitoa alama hizo na kusababisha ajali na upotevu wa hela za Serikali.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja na jitihada za Serikali juu ya ujenzi wa barabara nyingi na kwa kiwango cha lami nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu ni barabara ya *NARCO* (Hogoro) – Kibaya – Orkestmet Orjoro (Arusha); tunaomba ijengwe kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni *shortcut road* ya kwenda Tanga; mbili, kwa sababu Kiteto ni eneo linalozalisha mahindi mengi sana kwa Kanda ya Kati na kulisha Jiji la Dar es Salaam; tatu, maombi yangu tunaomba hizi kilometa 91 *NARCO* – Kibaya zijengwe kiwango cha lami maana ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipofanya ziara mwaka 2014 alipokuwa ziara Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara iokoe mazao ya wakulima kuepusha gharama kubwa za usafirishaji wakati wa msimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mawasiliano kwenye Kata za Raiseri, Loovera pamoja na Kata ya Sunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa kuikumbusha, kuisisitiza Serikali kuhusu ujenzi wa barabara ya Ifakara – Mlimba – Taweta hadi Madeke Njombe. Barabara hii imeshafanyiwa upembuzi wa kina kuanzia Ifakara hadi Kihansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina umuhimu mkubwa kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Njombe. Vilevile Jimbo la Mlimba lina uzalishaji mkubwa wa mpunga, mahindi, ufuta, ndizi, cocoa na miti ya mbao (mitiki) ambapo yanapita magari makubwa ya tani 15 hadi 30 na kuifanya barabara hiyo ambayo ni ya vumbi na udongo chepechepe na ina mito mingi ambayo hutiririka mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inapita kwenye shamba kubwa la *KPL* la mwekezaji wa Kimarekani anayelima

mpunga na mahindi kwa njia ya umwagiliaji na kufanya usafirishaji mazao kuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa barabara hii ni kuokoa maisha ya wanawake wajawazito na watoto ambapo wanaposhindwa kujifungua huhitaji kukimbizwa Hospitali ya Rufaa St. Francis iliyopo Ifakara kwa sababu Wilaya au Jimbo la Mlimba hakuna hospitali ya uhakika na kwa hiyo husababisha vifo vingi vya wazazi. Hivyo tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa daraja la Kilombero limeshaanza kutumiwa na kwa kuwa kivuko kilichokuwa kinavusha abiria hakina kazi tena hapo darajani, hivyo basi Wilaya ya Kilombero tunaomba na tulikwisha omba kivuko hicho tukabidhiwe ili kikatumike kuvusha wananchi kwenye Jimbo la Mlimba eneo la Kikoi, Kata ya Utengule, Kijiji cha Ngalimala ambako Mto Kilombero unatenganisha Wilaya ya Kilombero na Wilaya ya Malinyi. Hii ni kwa sababu miaka yote wananchi wanatumia mitumbwi ambayo ni hatari na si salama kwa usalama wa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano katika baadhi ya kata na vijiji vya Jimbo la Mlimba yanapatikana kwa shida sana. Hivyo ni muhimu kusambaza huduma hiyo hasa kwa kuliwezesha Shirika la *TTCL* kwa kutumia Mkonga wa Taifa ili kuimarisha mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* ni muhimu ikawezeshwa ili itengeneze madaraja na barabara zinazounganisha kata na kata, kata na vijiji hata vitongoji ambazo zimeanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mlimba lina mito mikubwa inayotenganisha kata na vijiji na kusababisha wananchi wengi kukosa huduma. Pia Kata ya Uchindile imetenganishwa kabisa na Makao Makuu ya Jimbo. Hivyo naomba muone umuhimu wa Jimbo la Mlimba kutengewa pesa za kutosha.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na *TARURA,* kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya *TARURA* ni ndogo na barabara za vijijini na mitaa ni nyingi na zinahitaji matengenezo makubwa, naomba Serikali itafute vyanzo vingine vya mapato kwa ajili ya *TARURA* kwa ajili ya kuboresha barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za vijiji na mitaa katika Mkoa wa Njombe ni mbaya, hazipitiki. Naiomba Serikali kuhakikisha fedha hizo za *TARURA* zinatengeneze barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara za Itoni - Ludewa, Njombe – Makete na Kibena – Lupembe – Madeke ni ndogo. Naiomba Serikali iongeze fedha hizo lakini pia fedha hizo zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Njombe ni kibovu. Kiwanja ni pori ambalo linasababisha vibaka na majambazi katika viwanja hivyo. Pia wafanyakazi wa viwanja vya ndege wanapokea rushwa kwa wananchi ili kuweza kukatisha kwenye viwanja hivyo ambapo bado uhalifu ni mkubwa. Naiomba Serikali itengeneze kiwanja hicho haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji maji, mwaka huu kuna mvua kubwa zinanyesha nchi nzima, lakini hakuna juhudi zozote za Serikali kuandaa mabwawa ya kutunza maji haya kwa ajili ya kutumia wakati wa kiangazi. Naiomba Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kutengeneza mabwawa makubwa yatakayotumika kwa ajili ya kuhifadhi maji hayo ambayo yatatusaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na uwanja wa ndege Songwe. Nimetembelea uwanja wa ndege wa Songwe na kuona jinsi ambavyo hauna taa za usiku kwa ajili ya kufanya ndege zitue vizuri na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wa Mwanza, nashauri kwamba Serikali iboreshe uwanja huo kwani unahitajika sana. Pia nishauri jengo la kuongozea ndege ambalo limesuasua kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za mwendokasi, ni wazi wananchi walifurahia ujio wa mwendo kasi, lakini Serikali imeshindwa kusimamia vizuri ili kuondoa kero zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii iliamini kuwa mwendokasi itakuwa suluhisho, lakini kero zake ni kubwa, magari ni machache hivyo watu hukata tiketi na kukaa muda mrefu pia kujazana kama njiti za viberiti. Hali hii inaondoa dhana ya usafiri salama Dar es Salaam. Niishauri Serikali mwekezaji kuongeza magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishauri Serikali kuangalia jinsi gani inaweza kwenda na mwendokasi wa ujenzi wa reli hiyo hiyo ya Kenya ambayo inatoka Mombasa na inakaribia Nairobi na wote tunawahi soko la mizigo ya Congo. Iwapo sisi tutatumia umeme kwenye reli yetu wakati Kenya wanatumia mafuta, je, gharama zitalingana za kuchukua mzigo huo Congo? Kama sivyo Serikali itaenda kupata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mlandizi Chalinze, nashauri kwamba barabara hii Serikali iamue kufanya matengenezo ya kudumu badala ya jinsi ilivyo sasa ambapo inatengenezwa na kuweka matuta muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Mlandizi ni bonde la mpunga hivyo ni bora kuinyanyua ili kuzuia ile hali ya sasa ambayo kila inapotengenezwa inatitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii iwe na vipaumbele kwani imebeba miradi mingi kwa wakati mmoja kiasi imepelekea kushindwa kutekeleza mipango yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari, niishauri Serikali kuwa kazi ya kuanzisha bandari kila kona wakati kuna Bandari ya Dar es Salaam ambayo ina miundombinu mingi iboreshwe ili kuweza kukidhi matarajio ya uendelezaji wa bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha bandari nyingine Bagamoyo tukijua kabisa bandari nyingine na zenye tija mfano Mtwara kubaki ikifanya kazi chini ya kiwango kitu ambacho si sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali juu ya ufungaji *flow meter* bandarini kuokoa ufisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanja vya ndege, nashauri viwanja vya Taifa letu kumilikishwa. Nimesema hivyo kwani mashirika ya mafuta yanayoendesha biashara ndani ya viwanja hivyo yanamilikiwa wakati viwanja vyenyewe havina hatimiliki.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri sana zinazofanyika katika nchi hii ya Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli pamoja na Waziri na Naibu Waziri na watendaji wa Wizara. Ombi, pamoja na bajeti nzuri ikiwemo barabara za Mji wa Makambako kilometa sita za lami; naomba kujua mradi wa kujenga *One Stop Center* lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaanza pale Idofi maana watu hawa wamekuwa wakisubiri muda barabara kutoka Ilunda – Igongolo urefu wa kilometa tisa ni ya *TANROADS* mbele inaendelea Kifumbe - Mahongole mpaka Makambako urefu wa kilometa 19. Ombi, iunganishwe iwe kuanzia Igongolo kuwa *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano Lyemukena – Majengo - Kifumbe, Kitandilo-Mahongole hakuna mawasiliano, tunaomba mawasiliano.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema, ni kazi kubwa inayofanywa na Rais wetu ambaye ni mzalendo namba *one* katika kuvifufua vyombo vyetu vya usafiri kama ndege, meli na ujenzi wa reli *(SGR)*. Niliwahi kusema na kuomba kuhusu *TRL* mara itakapokamilika naomba treni hiyo katika safari zake isimame katika kituo *(station)* ya Bukwimba, kwa kuwa jiografia ya Bukwimba ni eneo linalofaa kuwa na bandari kavu. Hii itasaidia kwa *station* ya Fela na *Mwanza South* kupumua. Stesheni ya Mwanza pamejaa, ukiweka bandari kavu Bukwimba itasaidia kwa wafanyabiashara wenye mizigo yao kuichukulia Bukwimba badala ya Fela au Malampaka. Miundombinu ya Bukwimba inajitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri naomba nipate majibu hii *railway levy* ambayo ni tozo ya 1.5% kwa mizigo inayopitia bandarini (magari, *container* na kadhalika) kutozwa hiyo asilimia, mfuko huu ulianza mwaka 2015/2016 na mara ya mwisho Serikali ililipa shilingi bilioni 38.41 kama *advance* kwa mkandarasi Dar es Salaam – Morogoro na hizo pesa tulikubaliana ziwe *refenced* kwa matumizi yaliyokusudiwa. Naomba kujua mambo mawili; je, hadi sasa ni kiasi gani cha pesa kimeshakusanywa kufuatia tozo hiyo? Ni kwa nini kiasi hicho hakipelekwi moja kwa moja kunakokusudiwa kama Bunge lilivyopitisha mwaka 2015/ 2016? Naomba kupata majibu kutoka Serikalini kuhusu mambo hayo mawili na ombi la bandari kavu *Bukwimba station*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote na Wizara yake. Mheshimiwa Waziri naomba kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* ni moja ya taasisi muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Yapo makampuni

ya simu ambayo baada ya agizo la Mheshimiwa Rais alipozindua *National Data Center* na kuyataka makampuni ya simu kujiunga ili kubaini kama makampuni hayo yanalipa *VAT* inayotakiwa; lakini hadi leo baadhi yao hayaja-*comply.* Naomba kujua kwa nini makampuni hayo yameshindwa kutekeleza agizo la Rais wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara na madaraja; mwaka 2017 Serikali ilitenga zaidi kilometa 200 za kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara ya Ilungu(Magu) Bukwimba – Ngudu – hadi Hungumalwa. Katika kitabu chake cha bajeti sijaona popote pesa zilizotengewa kwa ajili ya barabara hiyo. Naomba kujua ni kwa nini barabara hiyo haijatengewa pesa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Mto Simiyu (barabaraya Magu - Mara); daraja hilo ni muhimu sana. Ikumbukwe kuwa daraja hilo limecheza, hivi sasa kwenye daraja hilo magari hayaruhusiwi kupita nyakati za usiku kutokana na mvua. Lakini ukweli na watalam wako wanajua kuwa daraja hilo limechoka, ipo haja ya daraja hilo kujengewa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TTCL* huyu ni mtoto wetu lazima tumbebe kwa mbeleko ya Taifa. *TTCL* ni Shirika linalotoa huduma, lakini pia kupitia Mkongo wa Taifa tuutegemee kiuchumi na kiusalama, Serikali lazima tulilinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *DMI* na *NIT;* vyuoni hivi viwanda vya kuzalisha wataalam wa kwenye maji na barabarani, Serikali iviimarishe vyuo vyetu kwa kuzipa hela za kutosha kutokana na bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *ATCL,* nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa upendo mkubwa sana kwa Taifa. Rais Magufuli ni mzalendo *number one* kwa nchi yake, hasa katika kulifufua shirika. Ushauri wangu kwa Bodi ya Wakurugenzi katika kulisimamia vizuri shirika kwa kushirikiana na uongozi wote wa shirika. Hii ni katika kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Tuachanena

wanaobeza jitihada za shirika, tunalitaka shirika letu la *ATCL* lisiwasikilize wapinga kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hiyo hapo juu hasa nijikite katika masuala ya miundombinu ya barabara zote za Jimbo la Mtera zilizopo *TARURA*. Mwaka huu 2018 mvua zimeharibu sana barabara zote, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupata fungu la matengenezo ya uhakika wa barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atupatie majibu ya uhakika kuhusu ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka barabara kuu ya kwenda Iringa pale Mlowo barabarani mpaka *Mvumi Mission Hospital* kama ambavyo Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Mtera mwaka 2015. Naomba kujua ni lini barabara hiyo itajengwa? Ahsante.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Kuhusu barabara ya kutoka Mbande – Kongwa – Mpwapwa – Kibakwe hadi Chipogoro; barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa kujenga kwa kiwango cha lami. Hatua kadhaa zilianza kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuweka alama za "X". Kinachotusikitisha ni kuona haipo katika mpango wowote katika orodha ya barabara mbalimbali ulizozitaja katika hotuba yako. Aidha sijaona fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya shughuli yoyote ya maandalizi ya ujenzi. Hakika tumeshindwa kuelewa nini hatima yetu kwa majimbo ya Mpwapwa na Kibakwe, Mheshimiwa Waziri tunaomba msaada wako, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza Serikali, Mheshimiwa Waziri, viongozi na watendaji wote katika jitihada zote katika kuhakikisha sekta zote za Wizara hii

zinafanya kazi kwa maslahi ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango/ushauri kuhusu Shirika la Posta; Serikali iongeze fedha ili shirika liweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuweza kukabiliana na ushindani na kuongeza kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Serikali ione umuhimu wa kununua meli ya abiria kwa usafiri wa baharini kati ya Dar es Salam na Zanzibar kwa madhumuni ya kuwasaidia wananchi wanyonge ili waweze kumudu gharama za usafiri kwani usafiri wa kampuni binafsi au mtu binafsi bei zake ni za juu sana kwa mwananchi mnyonge na abiria wanahitaji huduma hiyo wanazidi kuongeza siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika letu la Simu *(TTCL);* nashauri zitafutwe fedha za ziada ili shirika liweze kupanua wigo zaidi wa kutoa huduma za kuwafikia wananchi katika maeneo yote ya nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBA* ikague nyumba zake zote na kuzifanyia matengenezo zile ambazo zinahitaji matengenezo ili nyumba hizo zisiendelee kuharibika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja, Hapa Kazi Tu, Mheshimiwa Waziri piga kazi.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja iliyoko mezani. Uamuzi wa Serikali wa kuachia *TBA* kujenga majengo yote ya Serikali na Serikali za Mitaa ni uamuzi usiokuwa na tija. Haiwezekani *TBA* ifanye *BOQ* halafu ijenge yenyewe kitendo hiki ni kinyume kabisa na utawala bora na ni kinyume na sera ya Serikali ya *PPP* katika ujenzi wa majengo ya Serikali au Serikali za Mitaa. TBA ingefanya kazi yake ya *manager* wa miradi ya ujenzi kwa niaba ya Serikali kuhakikisha *value formoney* na ubora wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBA* imezidiwa na miradi, wanashindwa kukamilisha miradi kwa muda na hata ubora

wake kama ilivyotokea kwa ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu. Ninashauri Serikali hili jambo litazamwe upya au kuhusisha sekta binafsi, sekta binafsi ndiyo *engine of growth* na ndivyo inavyotengeneza ajira kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchukuzi, Serikali ina mradi mkubwa wa reli ya *standard gauge.* Mradi huo utawaajiri wataalam waliobobea katika nyanja mbalimbali. Katika wasilisho la Waziri wa Fedha na Mipango katika eneo la rasilimali watu idadi ya wanafunzi watakaopelekwa katika mafunzo kwa ajili ya mradi huu haijafahamishwa kinaga ubaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali/Waziri mwenye dhamana ya uchukuzi awasiliane na Waziri wa Elimu ili kuhakikisha idadi inakuwa kubwa, ikionesha kwa namba ya wanafunzi watakaopelekwa vyuo vikuu pamoja na vyuo vya ufundi ili kutayarisha rasilimali watu ya kutosha kwa ajili ya reli ya *standard gauge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, Njombe kuna uwanja wa ndege ambao haujaendelezwa na upo karibu na makazi ya wananchi. Nahitaji majibu ya Serikali juu ya mipaka halisi ya uwanja wa ndege Njombe Mjini na nini hatua ya wananchi wenye makazi karibu na eneo la uwanja wa Njombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *upgrading of Sumbawanga – Namanyere–Mpanda Road, package 3*; *Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike Section 86.5 kilometres.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanikiwa kwa asilimia kubwa *package I & II* na sasa wananchi wanatumia barabara hizo, lakini *package III* bado haijatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 kiwango cha lami ambapo kilometa 35.5 kati ya kilometa 86.5 hazipo katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Naomba Waziri atuambie

wananchi wa Katavi ni lini fedha zitatengwa kwa ajili ya kipande hicho cha kilometa 35.5?

Mheshimiwa Naibu Spika, kupandishwa hadhi barabara ya *Katumba Complex II* (Msaginya – Mnyaki – Kanoge kilometa 21) Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo (Katavi). *TARURA* wameomba barabara hii ipande hadhi kuwa chini ya *TANROADS* kwa kuwa ni muhimu sana na ni kiunganishi cha barabara mbili zinazotoka nje ya Mkoa wa Katavi ambazo ni Mpanda – Ugala – Ulyankulu, Kaliua – Kahama kilometa 457 na Mpanda – Ipele – Tabora (kilometa 346).

Mheshimiwa Naibu Spika, reli Mpanda – Tabora, bado hali ni mbaya sana njia ya reli Mpanda – Tabora hususani kipande cha Kaliua – Mpanda, mpaka abiria walilala njiani siku mbili baada ya mvua kufanya uharibifu, ilikuwa tarehe 18/04/2018 waliondoka Tabora na walifika Mpanda tarehe 20/04/2018 saa 12 asubuhi. *TRL* inaombwa kuongeza ukarabati wa njia kwa kuwa ni tegemeo la wananchi na kusafirisha mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, inakabiliwa na changamoto kubwa ya mawasiliano katika kata za Ugala, Litapunguza, Kamage, Katumba, Uvaira, Nsimbo, Mtapenda, Kapalala, Machimboni, Itanka, Ibindi na Sitalike. Tunaomba sana Serikali kuboresha mawasiliano katika kata tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Soko la Hisa kwa Kampuni za Simu, Bunge lako lilipitisha sheria inayozilazimu kampuni zote za simu kujiunga na soko la hisa, lakini mpaka sasa Vodacom ndio pekee wameshajiunga. Je, ni lini kampuni nyingine zikiwemo *TTCL* watatekeleza matakwa ya sheria? Kwa kuwa bado kampuni zingine kutekeleza; je, sheria inasema vipi juu ya hatua za kuchukuliwa kwa kutotii sheria hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia ya matenki ya maji, mkataba wa mkandarasi Mpanda – Ipole – Tabora,

anatakiwa kufidia matenki mawili ambayo thamani yake zaidi ya milioni 250 lakini fidia iliyopo ni ndogo haizidi milioni 150; kwa hiyo tunaiomba Serikali iangalie upya fidia hiyo na ikiwezekana Halmashauri ya Nsimbo ipewe fedha moja kwa moja ili ijenge yenyewe miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *service levy V/s TCRA;* Kampuni za Simu zinaingiza mapato kutokana na minara hivyo kutokana na sheria za Serikali za Mitaa wanatakiwa kutoza *service levy* ya asilimia 6.3 ya mapato. Tunaomba *TCRA* wasimamie utaratibu mzuri ili kila Halmashauri inufaike na minara iliyopo katika eneo lao au Serikali ifanye *ring fence* ya *service levy* kutoka katika kampuni zote na pato hili kuwekwa Wizara ya Afya ili kusaidia kazi za kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia barabara ya Sitalike - Mpanda; bado kuna wananchi wanadai hawajalipwa na Serikali, tunaomba ifanye malipo haraka.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Pamoja na juhudi kubwa sana za Serikali ya Awamu ya Tano za kuifanya Tanzania kuwa Taifa la uchumi wa kati kupitia sera ya Tanzania ya viwanda, sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano inao mchango mkubwa katika mwelekeo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kujenga barabara za lami, madaraja makubwa, reli ya kisasa *standard gauge,* upanuzi wa bandari, ununuzi wa meli mpya katika maziwa yetu makuu pamoja na vivuko, ujenzi wa *flyovers* Jijini Dar es Salaam na mipango ya kuendeleza ujenzi kama huo Jijini Mwanza na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali kwa mpango wake wa kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi, hatua hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa kanda ya ziwa na nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki

na nchi za Afrika ya Kati kwani daraja hili litarahisisha usafirishaji wa watu na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe tunaipongeza Serikali kupigia *TANROADS* Mkoa wa Geita chini ya uongozi madhubuti wa Meneja wa *TANROADS* Mkoa Ndugu Haroun Senkunku na msaidizi wake na watumishi wote wa *TANROADS* Mkoa wa Geita kwa kazi nzuri ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kuuliza, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hatimaye kuanza kujenga kwa kiwango cha lami kwa barabara za Butengolimasa – Iparamasa – Mbogwe hadi Masambwe, barabara ya Katoro – Lulembela hadi Ushirombo na barabara ya Ushirombo hadi Bwehwa – Mbogwe ili kusaidia kukuza uchumi wa wananchi wa Wilaya yetu ya Mbogwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika Tanzania mpya ni hakika na siyo nadharia. Naipongeza kwa hakika Serikali kwa wazo la kushirikiana na Serikali ya Rwanda kujenga reli ya *standard gauge* kutoka Isaka – Kigali – Msongali. Reli hii itakuwa ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi baina ya nchi zetu mbili za Tanzania na Rwanda, naiombea mafanikio mipango yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa ndege na kulifufua shirika letu la ndege la *ATCL* kutaweza kuchangia katika kuitangaza nchi yetu kimataifa na kuleta tija katika sekta ya utalii kutokana na Taifa letu kuwa na vivutio vngi vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe pia Serikali itupie jicho ujenzi wa uwanja wa ndege wa mjini Geita uliopo eneo la Buhalahala, Geita ili kuiwezesha sekta ya usafiri wa anga kuchangia iwezekanavyo kwa wananchi wa Mkoa wa Geita na wale wa maeneo jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza ni hatua chanya katika kurahisisha ushirikiano wa kimataifa na kikanda kwa sekta ya utalii na ukuzaji wa uchumi kwa ujumla wake. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuendelea na hatua kama hizi kwa viwanja vyote vikubwa vya ndege vya *KIA*, *JNIA* Dar es Salaam, Songwe na viwanja vingine vya ndege nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe pia Serikali kuendelea na upanuzi wa bandari katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na kwa Mkoa wa Geita Bandari za Pores, Nungwe, Nkome, Chato, Nyamirembe na Bukondo. Naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wote wawili wa Wizara na uongozi mzima wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri ambayo imejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa sekta ya ujenzi (barabara), mawasiliano na usafiri wa maji unasimama vema. Niipongeze sana Serikali kwa kuweka kipaumbele barabara ya Handeni - Kibereshi - Kijungu - Kibaya - Mjaro - Olbolotiri - Singida kilometa 460. Kujenga kwa kiwango cha lami barabara hii ukiacha kwamba bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga bado barabara hii ni muhimu kwa shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa mikoa hii minne (Tanga, Manyara, Dodoma na Singida).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wananchi wa mikoa hii mimi naamini kabisa barabara hii itasaidia kufungua fursa nyingi za kiuchumi, niombe sasa Serikali ifanye jitihada kubwa kupata fedha za kutosha ili barabara yote iongezwe kilometa 460. Barabara hii ina faida kubwa hata kwa wafanyabiashara wa nchi jirani, mfano Burundi, Rwanda na Uganda. Bandari zikishakarabatiwa wafanyabiashara watanufaika kwa punguzo la gharama za usafiri kwa sababu barabara hii kwa kiasi kikubwa itakuwa fupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni ubora wa kazi za ukarabati, ujenzi

wa barabara zetu kwamba baadhi ya wakandarasi wanapopewa zabuni za barabara matengenezo ya barabara yapo chini ya kiwango. Naomba sana tena *TANROADS* wasimamie kwani Serikali inapoteza fedha nyingi kwa kazi zinafanyika chini ya kiwango. Kwa mfano ukarabati wa barabara ya Handeni – Kibarashi – Sange baadhi ya maeneo vifusi vilivyomwagwa vilikuwa ni vumbi badala ya kuweka vifusi vyenye mawe hasa katika maeneo ya Korosi. Hii imesababisha barabara hii kutopitika kwa takribani siku tano; mimi najiuliza kwa nini viwango vya kazi hivi kusimamia? Jambo hili litazamwe kwa jicho la karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu pia naomba uende kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*USCAF*) mfuko huu ni muhimu sana hususani kwenye maeneo yenye changamoto za mawasiliano kama katika jimbo langu la Kilindi. Nipongeze jitahada zilizofanywa na mfuko kwa kupitia maeneo yote yenye uhaba wa mawasiliano ya simu, nimeona orodha ya vijiji na kata ikiwemo eneo langu la Kilindi niombe maeneo yote yapatiwe mawasiliano ukizingatia mawasiliano ni ajira pia maeneo hayo ni Kata ya Sanyi, Kata ya Kilwa - Kijiji cha Kilwa, Kata ya Twande - Kijiji cha Iwande, Kata ya Tunguli, Kata ya Kwekivu, Kata ya Kilindi asilia Kijiji cha Misufini Kata ya Masagalu na vijiji vyake vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya lami ya kwa kilometa tano kwa kiwango cha lami, napongeza, jitihada za ujenzi zimeanza lakini kiasi kilichotengwa ni kidogo sana, ni *motor* zoo tu ndio zimeanza kujengwa. Niombe Wizara itenge fedha za kutosha kuhakikisha ahadi hii ya Rais wetu inatekelezwa naamini kabisa umuhimu wa kujengwa kilometa tano hizi zitasaidia kupandisha hadhi ya mji wetu wa makao ya Wilaya (Songe) na kubadilisha mwelekeo pia na mwisho barabara zote zinazosimamiwa na *TANROADS,* wakandarasi wahakikishe mitaro yote inayopitisha maji pembeni mwa barabara zetu inakarabatiwa na kusafishwa mara kwa mara ili kulinda barabara zetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kutoka Geita (Nyankungu) kwenda Kahama, barabara hii ambayo inapita Nyang'hwale kwenda Kahama ni kiungo kikubwa kwa Mkoa wa Geita na Shinyanga, na hii sasa inatumika sana kwa usafirishaji wa bidhaa mbalimbali zinazotumika mgodini. Tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami kama ahadi ya Mheshimiwa Rais ilivyokuwa mwaka 2015. Hivi sasa barabara hii ni mbovu sana kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uwanja wa Ndege Geita Mjini, Mheshimiwa Waziri kumekuwepo maneno mengi kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Chato. Sisi wananchi wa Geita hatuoni tatizo la ujenzi wa uwanja wa Chato. Tatizo tulilonalo ni umbali wa huduma hiyo kutoka Geita Mjini kwenda Chato, ndio utakuwa uwanja wa watu wa Geita Mjini; maana yake mtu atatakwa kusafiri kilometa 184 kutoka Geita kwenda Chato au kusafiri kilometa 120 kutoka Geita kwenda Mwanza Mjini na kwa sababu hiyo tatizo na uhitaji wa Uwanja wa Ndege Geita Mjini lipo pale pale. Ushauri wangu ni kwamba uwanja wa CCM uliopo hivi sasa ukarabatiwe na kuwa na uwezo wa kutumika kwa shughuli zote abiria wa Geita na CCM na kinachoweza kufanyika ni kutofautisha jengo la abiria peke yake hakuna sababu ya kuanza ujenzi wa eneo jipya.

Kuhusu barabara za Mjini Geita, Mheshimiwa Waziri tulipewa ahadi ya kilometa 10, ahadi ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli wakati wa kampeni yake mwaka 2015. Kwa kuwa muda uliobaki, sasa ni miaka miwili tu naiomba Serikali kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuwa hali ya barabara za Mji wa Geita ambao ni makao makuu ya Mkoa wa Geita ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubovu wa vivuko vya Kigongo Busisi, Mheshimiwa Waziri vivuko hivi vimechoka sana na vimekuwa vikisababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa kivuko, zipo nyakati feri inabaki moja tu magari na abiria wanakaa hapo zaidi ya masaa 10 kusubilia feri. Naiomba Serikali kuja na suluhisho lingine la mahali hapo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Itoni – Manda yenye urefu wa kilometa 211. Ujenzi wa kiwango cha zege kati ya Lusitu na Mawengi unasuasua sana. Naishauri Serikali kwamba barabara hii ipo ndani ya majimbo mawili au Wilaya mbili kwa maana ya Wilaya ya Njombe na Wilaya ya Ludewa na kazi imeanza ndani ya Wilaya ya Ludewa na kuruka kipande cha kilometa 52 kilichopo Wilaya ya Njombe ambacho ndicho kinaunga kwenye barabara kuu ya Makambako - Songea eneo la Itoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa pesa kidogo inayotenga kwa barabara hii, sasa iajiri mkandarasi mwingine aanzie Itoni ili kuweka imani kwa wananchi wa eneo la Jimbo la Njombe Mjini kwani ahadi ya lami kutoka Itoni ni ya muda mrefu sana.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera kwa timu nzima ya Wizara kwa kuendelea kuchapa kazi kwa ufanisi. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, wataalam na *supporting staff* wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara na madaraja, nashukuru Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuitengea fedha miradi ifuatayo katika Jimbo la Tunduru Kaskazini, Daraja la Fundimbanga, barabara ya Mkoa – Mjimwema – Ngapa – Tunduru - *Nachingwea Border.*Ninaomba utekelezaji wa miradi ifuatayo ambayo kimsingi ni ukamilishaji wa miradi ya barabara ya Nakapanga – Tunduru itengewe fedha ili ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya mchepuo *(bypass)* ya Mkapunda – Masonya, mzunguko wa barabara *(roundabout) – crossroad location.* Barabara hii ya Mjimwema – Ngapa – Tunduru/*Nachingwea Border* ni barabara ya mkoa na ni ya kiwango cha udongo *(earth road),* ni vema kuweka katika mpango kutenga fedha na kuijengea barabara hii kwa kuwa inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi. Pia kuna daraja la Mto Lumesule katika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wa ndege wa Tunduru, nafahamu kuwa vipaumbele kwa sasa vimewekwa katika viwanja vikubwa, viwanja vya Mikoa na vya kimkakati. Lakini ni ushauri wangu kwamba vigezo/ vipaumbele vijumuishe maeneo ya mpakani, maeneo yaliyoko mbali sana na viwanja vya ndege vinapotumika; kwa Tunduru kilometa 410 na kilometa 262 kutoka pande zote mbili, viwanja vya ndege vilivyokuwepo vikafungwa maeneo mapya yaliyofunguka na yenye *potentials* za kuchangia uchumi wa Taifa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uwanja wa Tunduru upewe kipaumbele.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali na Mawaziri wote. Tuna tatizo la barabara ya lami ambayo ipo katika Ilani ya Uchaguzi ya kutojengwa kwa kiwango cha lami kabla ya mwaka 2020 kama tulivyoahidi. Tunaomba kujengewa barabara hii Karatu – Mbulu – Haydom – Lalagu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano naomba minara ya simu katika Kata ya Endahagichan, Endomilay, Nqorati, Geterer, Endamasak, Eshkesh, Arri Tumat. Pia naomba mnara wa Maghang ufunguliwe na wa Yaeda - Ampa maana muda umepita sana. Naomba sana.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Mto wa Mbu hadi Serengeti – Mugumu, barabara hii ni muhimu kwa sababu pia imegundulika madini ya magadi pale Engaruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lini barabara hii itaanza kujengwa ikianzia Mto wa Mbu ili kurahisisha uanzishwaji wa Kiwanda cha Magadi Engaruka. Pia ni lini ahadi ya Rais ya kujenga kwa lami barabara ya Monduli kwenda Sokoine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itatupatia daraja la kudumu barabara ya Lokisale – Monduli?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kivuko cha MV Nyerere kimekuwa na matatizo ya mara kwa mara ya kuzimika katikati ya maji hali inayohatarisha maisha ya abiria, kwa mara ya mwisho nilipewa taarifa kuwa *engine* za kivuko hiki zingekamilika na kufungwa kabla ya mwezi Februari lakini sioni kinachoendelea. Ni lini *engine* za kivuko cha MV Nyerere zitafungwa na kuondoa kero ya usafiri kati ya Bugorola na Ukara?

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya usafiri kati ya Kisiwa cha Irugwa na Ukerewe ni ya hatari kutokana na ukweli kwamba inahitajika zaidi ya masaa manne kwa abiria kusafiri kati ya visiwa hivi viwili wakitumia mitumbwi jambo ambalo ni hatari. Ombi langu kwa Serikali itafakari na kusaidia upatikanaji wa usafiri wa boti/kivuko kati ya Irugwa kwenye wakazi zaidi ya 20,000 na Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo kwa watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL),* baada ya kampuni hii kudorora na meli nyingi kushindwa kufanya kazi, wafanyakazi wa kampuni hii hawajalipwa mishahara kwa miezi 23 jambo lisilo na afya. Serikali itumie vyombo vyake kubaini watumishi walio na matatizo waondolewe na wale waadilifu walipwe haki yao na hivyo kuongeza morali ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya nauli katika vivuko; utaratibu wa jumla kutoza kiwango fulani cha pesa kwa mizigo chini ya kilo 20 umekuwa na migogoro ya mara kwa mara kwa sababu wananchi wamekuwa wananyanyasika kwa kutozwa nauli kwa mizigo isiyostahili kama vile mabegi na vitu vingine vidogo vidogo ambavyo havistahili, hivyo, napendekeza malipo yoyote yaondolewe kwa mizigo ya chini ya kilo 20.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kala iliyoko mpakani kando kando mwa Ziwa Tanganyika ina vijiji vya

King'ombe, Mtambo, Kilambo, Mpasa, Kapumpali, Tundu na Kala. Vijiji vyote hivi havina mawasiliano ya simu licha ya kuwa na zaidi ya watu 2,000 na ikumbukwe kuwa hawana barabara ya kuaminika. Mheshimiwa Waziri Mbarawa nimekuja kwako siyo chini ya mara sita au saba, nimeandika barua mbili na nimechangia hapa Bungeni zaidi ya mara 10 sijasikilizwa, je, ni kwa nini hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi sijaelewa kwa sababu pia hujawahi kunipa sababu ya msingi ya suala hili kutokuwezekana kwa muda wa miaka saba nikiwa hapa Bungeni. Naomba Wizara inisaidie kwani sieleweki kwa wananchi hawa. Vilevile kuna Vijiji vya Kasapa, Kata ya Sintali na Vijiji vya Kisambara na Msamba – Kata ya Ninde.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Katongoro – Ninde; barabara ya Kitosi - Wampembe; barabara ya Nkana Kata zote zimefunga kutokana na mvua nyingi zinazonyesha huko Mkoani Rukwa na *TARURA* hawana fedha ya dharura. Naomba Serikali itoe fedha za dharura *TARURA* Nkasi vinginevyo wananchi hawapati huduma mbalimbali ikiwepo matibabu na bidhaa zingine za madukani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe barabara ya lami toka Chala kuendelea kuunga Paramwe barabara ya lami imezunguka Makao Makuu ya Wilaya na kuacha barabara ya zamani ya kwenda Mpanda ambapo Vijiji vya Londokazi, Miombo, Mashete Mtenga na Mwai vimebaki na barabara ya vumbi na vijiji vya uzalishaji mkubwa wanaomba waunganishwe kwa barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono nikipata majibu ya mtandao Kata ya Kala, Nkasi Kusini.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tunduru Kusini lipo pembezoni mwa mpaka katika Mto Ruvuma hivyo wananchi

wengi wa Tunduru wanaenda Msumbiji kupitia Mto Ruvuma, ninaomba kijengwe kivuko katika Mto Ruvuma sehemu ya Chamba au Makade ili wananchi waweze kutumia badala ya kutumia mitumbwi ambayo inahatarisha maisha ya wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za ulinzi, miaka ya 1970 mpaka 1980 kulikuwa na barabara ya ulinzi ilitoka Mtwara mpaka Mbamba bay, barabara hii ilikuwa inasaidia kufanya *patrol* kwa Wanajeshi wa JWTZ kwa ajili ya kulinda mipaka yetu. Barabara hii imekufa kabisa haionekani kabisa, barabara hii ilisaidia sana hasa wananchi wanaoishi kandokando ya Mto Ruvuma. Barabara hii ilitumika sana na askari wetu pamoja na wananchi kusafirisha mazao kwenda kwenye masoko. Sasa hivi wananchi wanazunguka sana kutoka kijiji kimoja kwenda kingine kwa kuwa barabara hii imekufa kabisa na imesababisha ongezeko la magendo sana kutokana na njia maalum inayounganisha vijiji vilivyo kando kando na Mto Ruvuma. Hivyo basi, ninaomba barabara ile ifufuliwe ili kuongeza ulinzi wa mipaka yetu kwa kuwa Watanzania wa vijiji hivyo wanaingiliana sana na wananchi wa Msumbiji na wamepata mahitaji yao ya kila siku kutoka Tanzania hasa Tunduru Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara ya Tunduru – Nalasi - Chamba na Nalasi – Mtwara Pachani; barabara hizi ni za vumbi na zina milima ambayo kila mwaka ukitengeneza kwa kifusi cha kawaida zinatumika miezi sita. Kwa hiyo, tunaomba barabara hizi zitengenezwe kwa kiwango cha changarawe hasa barabara ya Tunduru – Chamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano ya simu, tunaomba mitandao ya simu katika vijiji vya Misyaje, Nasomba, Lukala, Makande, Msinji, Semeni na Azimio upatikanaji wa mawasiliano umekuwa wa shida, hivyo tunaomba minara ya simu ijengwe katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli ya *Mtwara Corridor,* reli hii ni muhimu sana katika Kanda ya Kusini kwa

vile kuna makaa ya mawe na chuma kitasafirishwa katika reli hii pamoja na mazao ya korosho, kahawa, tumbaku, mahindi na maharage jambo ambalo litakuza bandari ya Mtwara na Bandari ya Mbamba bay. Hivyo naomba sana ujenzi huu kwa maana ya upembuzi yakinifu ufanyike kwa kina ili ujenzi uanze muda mfupi ujao kwa sababu barabara za Kusini zinaharibika haraka kwa sababu ya kupitisha malori makubwa ya makaa ya mawe, korosho na mahindi.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuikumbusha Serikali kwamba uwanja wa ndege Tanga unatakiwa kuboreshwa kama viwanja vingine kwa sababu uwanja huo utatumika sana baada ya bomba la mafuta toka Hoima hadi Tanga. Kwa hiyo, kutakuwa na wageni wengi watakaokuja Tanga kupitia usafiri wa ndege vikiwemo viwanda vingi vilivyopo na vinavyokusudiwa kujengwa pamoja na utalii uliopo Mkoani Tanga. Hivyo naiomba Serikali kuangalia uwanja huu kwa kutengea bajeti ya marorosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za lami Korogwe Mjini, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kilometa tano za lami ndani ya Mji huo. Niombe Serikali ahadi hii kama inawezekana ni kutoa kilometa 2.5 kila mwaka itakuwa imekamilika ahadi hiyo ndani ya miaka miwili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* wanafanya kazi nzuri lakini bajeti waliyopewa ni ndogo. Ni kwa nini wasigawane nusu kwa nusu na *TANROADS* ili kuwawezesha *TARURA* kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi ya barabara kwa uhakika. Vinginevyo ile shilingi 50 ya lita ya mafuta *(disease/petrol)* itolewe kwa *TARURA* ili kuwapa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mji wa Korogwe zinaharibika sana kwa mvua kutokana na Mji huu kuwa bondeni, ushauri wangu ni kwamba barabara

zinazojengwa kwa kiwango cha changarawe zijengewe mitaro au mifereji ili kusaidia kupunguza uharibifu. Kwa msingi huo tunaomba kupewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mitaro/ mifereji.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano pamoja na Naibu Mawaziri wake wawili, Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Elias Kwandikwa kwa juhudi zao za kuijenga nchi yetu katika sekta hii ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na bandari; bandari ndiyo chanzo kikubwa cha mapato katika nchi yetu lakini bado ujenzi wa Gati Namba 13 hadi 14 katika Bandari ya Dar es Salaam unazorota. Toka mwaka 2010 tumeanza na wimbo wa ujenzi wa Gati hii Namba 13 hadi 14 mpaka leo haujaanza, jambo hili linazorotesha uchumi wa nchi. Naishauri Serikali itenge pesa kwa ajili ya ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi za dhati kwa ununuzi wa ndege, tulikuwa hatuna ndege na ilikuwa ni aibu kubwa lakini leo nashukuru Serikali kwa ununuzi wa ndege. Naishauri Serikali kuwa na tahadhari ya kutosha katika kuhakikisha kuwa *ATCL* inajipanga kufanya kazi kwa faida. Kuna hujuma kubwa sana zinazofanywa na mawakala ambao wanatumiwa na mashirika binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lilikuwa likifanywa na wakaua shirika hili. Ninaomba Serikali ifungue ofisi za kuuzia tiketi na siyo kutegemea mawakala. Unapokwenda kukata tiketi unaambiwa ndege imejaa lakini ukienda kuangalia *airport* ndege ni tupu haijajaa, mawakala wanakuambia ukate tiketi ya ndege nyingine kumbe siyo kweli wanataka ukate tiketi mashirika mengine.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri wanazofanya. Natoa shukrani zangu za dhati ya moyo kutokana na miradi mingi ya Serikali iliyotekelezeka katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuzindulia miradi mbalimbali katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ujenzi wa barabara ya mwendokasi Mbagala sasa mradi ule uanze angalau tupate tumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa barabara ya Nzasa – Kilungule - Buza uangaliwe kwa moyo wa huruma kwani ni barabara muhimu ambayo itasaidia kuunganisha Wilaya ya Ilala na Temeke na Jet ambayo kama mtu anatoka Mbagala anaweza kufika mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Temeke Mwisho kwa jina *Mbagala Road* nayo sasa ijengwe kwa uimara zaidi kwa kuwa imekuwa inabomoka mara kwa mara. *TARURA* waongezewe nguvu kwa kupewa nyenzo za kufanyia kazi kama greda na vifaa vingine. *TANROADS* nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanazofanya wanajenga barabara nzuri sana kiasi kwamba tunataka barabara zote zichukuliwe na *TANROADS*, kwa hiyo tusiwapunguzie nguvu bali tuwaongezee nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wa ndege, naipongeza sana Serikali kwa kuwezesha ujenzi wa uwanja wa ndege mpya wa Dar es Salaam na kutuletea ndege tatu. Tunashukuru sana ukiangalia tulikotoka na tunakokwenda tumepiga hatua kubwa sana. Ombi langu tuboreshe huduma zetu ziende na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TBA* kwa kweli kuna haja ya kuboresha au kukarabati nyumba zetu na kama hakuna uwezekano tufanye utaratibu ambao mpangaji akifanya ukarabati kisha akatwe katika *rent*. Miundombinu ya nyumba, mifumo ya maji safi na maji taka imekufa kabisa

na hata mafundi wa *TBA* hawana vifaa vya kufanyia kazi. Nyumba za *TBA* ni nzuri na zimejengwa kwa uimara wa aina yake tatizo ni kukosa *service*. Tunaishi miaka kumi hakuna ukarabati wowote siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TPA* naipongeza Serikali kwa ujenzi wa mageti ndani ya Bandari yetu ya Dar es Salaam, nataka kujua Serikali ina mpango gani na Bandari ya Bweni? Fungu la *SSR* la kutoka bandari pamoja na kutuletea mashuka katika Hospitali yetu ya Temeke namshukuru na kuwapongeza sana kwa moyo wa huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu naomba *TPA* waangalie na shule zenye watoto walemavu na wenye mtindio wa ubongo ambazo ni Shule ya Mtoni – Maalum, Shule ya Sinza – Maalum na Uhuru Maalum. Shule hizi zina watoto ambao wana mahitaji; kuna wasioona, walemavu wa viungo na akili. Mamlaka yetu iangalie kundi hilo. Nawatakia kila la kheri *TPA* naona mizigo ni mingi na meli ni nyingi baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake thabiti, makini na uzalendo mkubwa. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalam na watendaji wa Wizara kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo nianze kwa kutoa mchango wangu na nianze na kuwasemea watu wangu wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na hasa kuhusu *TRC* kupitia *RAHCO*. Naipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa reli ya kisasa ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam

mpaka Morogoro na Morogoro mpaka Makutupora, Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maendeleo ya ujenzi huu wa reli kuna watu walioathirika kwa kupisha maeneo yao ili kujengwa kwa reli, lakini mpaka sasa watu hawa hawajalipwa fidia zao. Fidia hulipwa ndani ya miezi sita baada ya tathmini na hulipwa kabla ya eneo kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchelewa kulipwa fidia hii kumeleta athari kubwa kwa watu wetu kwa sababu wananchi walikuwa wanategemea maeneo hayo kwa shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, mifugo na pia ni makazi yao kwa baadhi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamebomolewa nyumba zao, mashamba yao, huduma za jamii kama zahanati, shule na kadhalika. Kwa mfano, watu wa Ngerengere na Mikese wamebomolewa nyumba zao bila kulipwa fidia na wengine kulipwa fidia ndogo isiyolingana na bei ya soko na hali halisi katika Kijiji cha *Mikese Station*, zahanati mpya inabomolewa na kutakiwa kulipwa shilingi milioni 70 ambayo ni ndogo kuliko gharama zilizotumika au kuhitajika kujenga upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali kulipa fidia kwa wakati na kiwango kinachostahili ili kuwainua wananchi kiuchumi au kuwalipa kwa kiwango kwa kuzingatia thamani halisi badala ya kuwarudisha nyuma zaidi kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuwalipa fidia watu hawa walioathirika.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi kubwa waliyoifanya chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli,

Rais wa Tanzania kwa jitihada za makusudi za kubadilisha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mambo machache yafuatayo nikianza na viwanja vya ndege, barabara za Mkoa wa Dar es Salaam na usafiri wa ndege za *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha vifaa vyote muhimu vinavyohitajika kwa ajili ya usalama wa anga na usalama wa ndege wakati inatua kwenye viwanja, kwa kuweka alama, taa ambazo rubani wa ndege anaweza kuziona wakati kunapokuwa na ukungu mkubwa kwenye viwanja vya ndege ili kuepusha athari kubwa (usalama kwanza).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na upungufu wa viwanja vya ndege ambavyo havikidhi viwango vitakavyowezesha ndege kubwa kuweza kutua katika viwanja hivyo kwa sababu mbalimbali kama kiwanja cha ndege cha Musoma, kiwanja cha ndege cha Mugumu – Serengeti (kwa ajili ya hifadhi), kiwanja cha ndege cha Iringa na kiwanja cha ndege cha Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuboresha viwanja hivi kutasaidia maeneo hayo kujiimarisha kiuchumi na kiusalama, kutokana na kiwanja cha Musoma na Mugumu ni eneo la kiutalii na ndiyo kuna Makumbusho ya Muasisi wa nchi yetu Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere. Hivyo, wageni wengi kutoka nchi jirani na watalii wengi kupitia Musoma kwenda *Serengeti National Park*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja cha Iringa ni muhimu sana kuboreshwa kutokana na uhitaji wa uharaka wa watumiaji pia ni kiwanja ambacho kiko karibu na kiwanja cha ndege cha Dodoma ambacho inapotokea dharura mfano ndege kupungukiwa na mafuta inaweza kutua kiwanja cha karibu cha Iringa na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za Mkoa wa Dar es Salaam; katika sekta ya barabara kumekuwa na changamoto nyingi katika barabara za mitaani, hali hii imesababisha adha na kero kubwa kwa wakazi wa Mkoa huo. Barabara ya Tabata kuelekea Segerea - Kinyerezi - Malamba Mawili - Msigani mpaka Mbezi kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaohamia, kwa sababu hiyo kumekuwa na changamoto ya foleni kubwa ya magari ambayo huchukua masaa mawili mpaka matatu hali hiyo husababisha watu kuamka mapema sana kuwahi foleni isiwakute muda wa saa 11.30 alfajiri ndiyo muda mzuri wa kuwahi kwenda mjini ili kuepuka adha hiyo. Tunaomba Serikali itafute utaratibu wa kuipanua barabara hiyo ili iweze kusaidia kutatua kero hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya barabara ya *Segerea Seminary* kuelekea Majumba Sita kupitia Kituo cha Polisi cha Stakishari Mheshimiwa Rais wa Tanzania aliahidi kuijenga kwa kiwango cha lami na daraja wakati akiwa kwenye mkutano wa kampeni mwaka 2015 katika viwanja vya Vingunguti. Naiomba Serikali itimize ahadi hiyo maana hali ya barabara hiyo ni mbaya sana, wananchi wanalalamika kwa kukosa barabara ya uhakika.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia Wizara hii muhimu katika nyanja mbalimbali za maendeleo, hususan katika uchumi, mawasiliano na usafiri wa anga, baharini, reli na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Pangani ni kongwe na ya kimkakati *(East Africa and Southern Roads Projects)*. Barabara hii kama itajengwa kwa kiwango cha lami itainua hali ya uchumi wa Mikoa na Majimbo ya Tanga, Muheza, Pangani, Bagamoyo na maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, mwaka jana barabara hii ilitengewa shilingi bilioni nne, naomba ziongezwe na barabara tuambiwe itaanza kujengwa lini? Barabara hii ni ya kihistoria na tayari ilishaahidiwa na Marais wanne waliopita akianzia Mheshimiwa Mwalimu Nyerere, Mheshimiwa Ally H. Mwinyi,

Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Tanga ni wa kizamani lakini tangu umeachiliwa na wakoloni haujafanyiwa ukarabati mkubwa wa maana. Nimezungumza katika bajeti mwaka 2016/2017, 2017/2018 na leo hii 2018/2019 nimeona shilingi bilioni 7.6; naomba fedha hizi zifanye kazi ya kubadili sura na hali ya uwanja, pia nataka nijue fedha hizi ni pamoja na fidia ya nyumba tatu zilizofanyiwa tathmini *(evaluation)* 2008 na nyumba 802 ambazo nazo zinatakiwa kubomolewa, zote hizi naomba wamiliki wake wafidiwe kuepuka mgogoro unaoweza kusababisha kesi mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali kufuatia miradi mikubwa ya bomba la mafuta toka Hoima - Uganda hadi Chongoleani - Tanga viwanda vya saruji vipya vya Kilimanjaro na Sinoma China chenye thamani ya shilingi trilioni saba. Naomba Tanga tujengewe uwanja wa ndege wa kisasa wa Kimataifa. Naomba pia huduma za bombadier kupitia *ATCL* zifike Tanga kwa kuwa Tanga kuna shughuli nyingi za kiuchumi, ukiwemo utalii, viwanda, uvuvi na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mipaka ya uwanja wa ndege wa Tanga iwekwe wazi na Waziri utaje vipimo vyake kwa kuwa kuna mgogoro ambao unasumbua wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirikia la Ndege *ATCL* pamoja na ununuzi wa ndege sita, lakini naiomba Serikali inunue ndege tano na fedha za ndege mbili zinunue *ambulance, helicopter* mbili ambazo zitasaidia kuokoa maisha ya wananchi wetu pindi zinapotokea ajali barabarani au katika vyombo vya usafiri. Ndege hizi zipatiwe *routes* za nje na ndani ili shirika lijiendeshe kwa faida na lisijiendeshe kwa hasara kama ilivyokuwa *Air Tanzania.* Shirika letu la ndege liajiri wataalamu na watumishi wenye weledi na ubunifu ili kuweza kufanya *competition* na mashirika mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya *standard gauge* katika bajeti ya mwaka 2017/2018 nililieleza Bunge na Serikali kuwa reli ya Tanganyika ilianza kujengwa mnamo mwaka 1905 ikianzia bandari ya Tanga hadi Kilimanjaro, Kigoma na hatimaye kufika Mwanza. Baada ya kuja *standard gauge* Tanga imeachwa, nashauri kama wasemavyo wanafalsafa kuwa mwiba unapoingilia hutokea hapo hapo, hivyo naomba *standard gauge* ifike Tanga ili uchumi wa Tanga nao uweze kukua kwa kasi kwani uchumi wa Tanga unategemea reli, barabara, bahari na anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Tanga ni miongoni mwa bandari kubwa nne za Tanzania (Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar na Mtwara) na kihistoria bandari ya Tanga ndiyo ya kwanza katika *East Africa*. Katika enzi za sayansi na teknolojia, bandari ni lango kuu la biashara, lakini bandari zetu zilizoko katika Bahari ya Hindi hazitumiki vizuri, ukilinganisha na bandari moja ya Mombasa nchini Kenya. Serikali yetu imeelekeza shughuli nyingi katika bandari ya Dar es Salaam na zingine za Tanga na Mtwara hazitumiki vizuri na kusababisha kujiendesha kihasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika bandari ya Tanga tarehe 28 Februari, 2018 nilialikwa katika kikao cha Bodi ya Bandari na wadau wa bandari, wafanyabiashara, wajasiriamali na kadhalika. Katika kikao hiki zilizungumziwa changamoto nyingi zikiwemo ukosefu wa zana mkononi, hakuna *cranes* za kubeba kontena za *40 fts*, magari ya kutosha, urasimu ni mkubwa, pamoja na udokozi katika bidhaa zinazoingizwa toka nje, kina cha bandari ni kifupi, meli haziwezi kukaa *longside* na kusababisha gharama kubwa katika ushushaji mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali bandari ya Tanga ipatiwe vifaa vya kisasa kama *cranes*, matishari, malori, *fire department*, waletwe watumishi wenye kujituma kuondoa urasimu, wazalendo/weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ianzishe *categories* za mizigo ambapo kila bandari ingepangiwa

utaratibu wa kupokea na kusafirisha mizigo kama ifuatavyo; Bandari ya Tanga ingepokea ama kusafirisha mizigo ya Arusha, Kilimanjaro, Simanjiro, Manyara, Musoma, Bukoba, nchi za nje, Uganda, Rwanda, Burundi na Congo DRC. Bandari ya Mtwara ingepokea ama kusafirisha mizigo ya Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Katavi, Rukwa, Sumbawanga, Kigoma na Tabora, nchi za nje mizigo ya Malawi, Zambia, Zimbabwe na Mozambique na Bandari ya Dar es Salaam ingepokea ama kusafirisha mizigo ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi za nje mamlaka ikiona ipo haja baadhi mizigo ya baadhi ya nchi zipitie Dar es Salaam lengo kuu liwe bandari zote zifanye kazi kwa kiwango kinachofanana na faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu ni kuwa *together we build our nation*.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kufika mahali hapa na kuchangia bajeti hii iliyopo mbele yetu. Bajeti hii inakwenda kutekeleza mipango, miradi mbalimbali ya kimaendeleo, vilevile inakwenda kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri yenye mrengo chanya wa kubadilisha sekta nzima ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imekuja na mipango mbalimbali ya kimaendeleo, mipango hiyo ni pamoja na miradi mikubwa ya ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa *(standard gauge)* yenye urefu wa kilometa 1,219 uendelezwaji wa barabara zikiwemo za juu *(flyover)* pamoja na kununua meli na vivuko, pia kulifufua shirika letu la ndege na kuliwezesha sasa kuanza kutoa huduma ndani na nje ya mipaka kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongeza kwa Serikali kwa kuendelea kuboresha mtandao wa barabara nchini, ujenzi

wa kilometa 776.45 za barabara kuu kwa kiwango cha lami umekamilika na kilometa 1,760 zikiendelea kujengwa. Vilevile barabara zenye urefu wa kilometa 17,054 zimekarabatiwa, ujenzi wa madaraja mbalimbali kukamilika na mengine kukarabatiwa, hizi ni hatua nzuri zilizofikiwa na Serikali katika kuhakikisha miradi hii inakwenda kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuja na mpango wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural and Urban Roads Agency-TARURA)* mpango huu ni mzuri kwani unakwenda kurahisisha huduma za usafirishaji na kuongeza kasi ya wananchi kujiletea maendeleo, lakini bado tuna changamoto mbalimbali ambazo naishauri Serikali kuzichukua kama fursa na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimboni kwangu na maeneo ambayo mradi wa barabara ya Bagamoyo – Mlandizi - Mzenga umepita hawajalipwa fidia mpaka leo na kukaa kwa muda mrefu bila kuwalipa fidia, hivyo kuwasababishia hasara kwani kiwango wanachotakiwa kulipwa kitakuwa ni kilekile ili miaka inavyozidi kusonga mbele gharama ya vitu inazidi kupanda juu.

Naiomba Serikali hasa katika bajeti hii kuwapa kipaumbele wananchi wangu niliowazungumzia hapo awali walipwe fidia zao na wao waendelee na shughuli zao za kimaendeleo, hata hivyo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha bajeti yake aje na majibu ya wananchi hawa ili waweze kusikia kauli ya Serikali juu ya lini sasa watalipwa fidia zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Soga kuna mradi mkubwa wa ujenzi wa reli, mradi ule umeleta ajira kwa wananchi wangu na wa maeneo mengine pia, lakini naleta ombi kwa Serikali tunahitaji barabara ya kiwango cha lami kutoka Kongowe - Soga ijengwe kwani kujengwa kwa barabara hiyo kutarahisisha shughuli za usafirishaji na kufikika kwa urahisi kwenda kwenye mradi husika na kuleta maendeleo kwa

wananchi. Vilevile barabara ya Bagamoyo - Makofia – Mlandizi - Mzenga zijengwe kwa kiwango cha lami ili kurahisisha shughuli za kibiashara kwani eneo hilo ni muhimu kiuwekezaji na pia naishauri Serikali kujenga bandari ya nchi kavu eneo hilo ili mizigo itakayoshushwa Bandari ya Bagamoyo iweze kuhifadhiwa mahali hapo na kuleta nafuu kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Kwala, Dutumi na Vigwaza barabara hiyo nayo tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami ili kurahisisha shughuli za kimaendeleo na kuinua uchumi wa maeneo husika. Kama nilivyosema hapo awali kuhusu hizo barabara zina umuhimu sana kwa maendeleo ya Jimbo langu na kwa nchi kwa ujumla na zikikamilika zitasaidia kuleta maendeleo kwa haraka na kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mawasiliano ya simu yanavyosaidia katika nyanja mbalimbali katika dunia ya leo, hata hapa nchini kwetu tumeona jinsi mawasiliano ya simu yanavyoleta tija kwa watu wetu na hata kutoa huduma mbalimbali za kifedha kwa kupitia mitandao hiyo ya simu. Hata hivyo, teknolojia hii imeleta pia maendeleo mbalimbali kwa wale watu wanaotumia kwa mrengo chanya. Pongezi ziende kwa Serikali kwani wameendelea kuboresha maeneo mbalimbali, kama kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, hatua hii ni nzuri na imesaidia sana pamoja na ujenzi wa kituo cha kuhifadhia *data*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo Jimboni kwangu wananchi hawana kabisa mawasiliano ya simu, kwa maana hakuna minara maeneo hayo ambayo ingewawezesha wananchi hawa kupata mawasiliano ya simu katika shughuli zao za kila siku, maeneo hayo ni Kata ya Boko - Mpigi, Mkalambati, Kata ya Doga - Kipangege, Misufini, Kata ya Kawawa - Kimara, Makazi Mapya, Makutupora, Msua, Mpelamumbi, Waya; Kata ya Mtongani-Madimia, Kisabi; Kata ya Kikongo- Ngeta, Mkino, Lupungo; Kata ya Ruvu - Kitomondo, Ruvu Station; Kata ya Dutumi -

Madege, Dutumi, Muembe Ngozi; Kata ya Gwata - Mguruka, Vinyenze, Ndwati, Kigoda; Kata ya Magindu - Lukenge, Masaki, Miyombo, Lukalasi, Magindu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua katika mpango wa Serikali kama ulivyoainishwa wa kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini. Je, maeneo hayo niliyoyaorodhesha hapo juu yatapatiwa mawasiliano katika mwaka huu wa fedha na kama si katika mwaka huu basi naomba kujua ni lini maeneo hayo yatapata mawasiliano na kuondokana na kero hiyo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika mradi wa ujenzi wa barabara ya njia sita kutoka Dar es Salaam na kuishia TAMCO ni mpango mzuri wa kimaendeleo, lakini nina ombi na ushauri kwa Serikali yangu sikivu, mradi huu usingeishia tu tamko bali mradi huu ungeendelea mpaka Chalinze na kufika Morogoro kwani uhitaji wa mradi huo kwa maeneo hayo upo na utasaidia sana kuleta maendeleo kwa haraka, kurahisisha shughuli za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM. Pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa utendaji kazi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa 81 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametujulisha kuwa mkataba wa Bandari ya Bagamoyo utasainiwa Juni, 2018. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hii. Sisi wa Bagamoyo tunahamu sana Waziri atuambie lini ujenzi utaanza? Pia atujulishe lini fidia zilizobaki takribani shilingi bilioni 12 zitalipwa? Pia lini wananchi 687 wanaopisha bandari ambapo wamethibitishwa kupunjwa fidia zao watalipwa? Kukamilisha malipo ya fidia yatasaidia kuliweka eneo la bandari kuwa huru ili likabidhiwe kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi mapya ya wananchi wa vijiji vya Pande na Mlingotini wanaopisha mradi wa bandari, wananchi hawa waliahidiwa na Serikali kupitia *EPZA* kuwa watapewa makazi mbadala (barua ya *EPZA* ya tarehe 20.01.2014 ambayo nimekabidhi meza ya Spika) Kijiji kizima cha Pande na sehemu ya kijiji cha Mlingotini vinahamishwa. Kaya zipatazo 460 (wakazi 1,670) zitaathirika. Wananchi hawa wanapoamuliwa kuondoka wanaenda kuishi wapi? Wengi fidia zao hazitowezesha kununua ardhi au kujenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itimize ahadi yake. Ahadi hii ni deni! Ikiwa Serikali itashindwa basi nashauri Serikali imuagize mwekezaji kulipia gharama za makazi mbadala kwa wananchi hawa *(resettlement).* Hizi ni taratibu za kawaida duniani kwa viwango vya utawala bora. Ni imani yangu mwekezaji atakubali kwa vile hata China na Oman wanawapa wananchi wao makazi mbadala kwa ujenzi wa miradi mikubwa.

Kuhusu ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Saadani – Pangani – Tanga katika ukurasa 129 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameahidi ujenzi wa barabara tajwa na kwamba kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ujenzi utaanza kwa kilometa 50 Tanga – Pangani. Naomba kumjulisha Mheshimiwa Waziri tuliopigania barabara hii ni pamoja na wananchi wa Bagamoyo na Mbunge wao! Naomba Waziri aweke wakandarasi wawili, mmoja aanze Tanga na mwingine aanze Bagamoyo kilometa 25 kila upande. Hii itaharakisha kazi na Tanga na Bagamoyo. Tulishafanya hivyo kwa miradi ya Manyoni – Tabora, Tunduma – Sumbawanga na kadhalika kipindi hicho mimi nikiwa Waziri. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ahadi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Bagamoyo mjini kilometa tano na atutengee fedha mwaka huu 2018/2019 kuendelea utekelezaji wa ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mbarawa pamoja na Naibu Mawaziri wake wawili, na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi zao nzuri tunazifuatilia na tunaziona. Napenda kuwatia moyo Mola awazidishie nguvu mna kazi kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, katika Mkoa wangu wa Kagera tuna madaraja ambayo ni mabovu naomba na sisi mtutizame, yatengenezwe yawe imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege, kiwanja ni kizuri sana kina viwango vya kutosha. Tatizo ni taa ndege haziwezi teremka usiku zinaishia Mwanza. Lakini tungekuwa na taa wasafiri wanaotoka Dar es Salaam, Arusha, Mwanza usiku wasilale Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu meli, sina shaka swali hili mnashughulikia. Naomba mkazane na ikibidi tuwe wa kwanza kutengenezewa meli wananchi wana shida sana muda umekwenda sana nawaomba sana sana tuwaonee huruma, mazao yetu yanaoza na kipato chetu tunategemea usafiri wa meli. Nawatakia kazi njema. Hapa Kazi Tu.

**MHE. JOEL M. MAKANYANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri sana mnayoifanya. Nawapongeza sana pia kwa bajeti yenu nzuri iliyowasilishwa Bungeni tarehe 23 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri sana kwamba mipango yote mliyoianisha ni mipango mizuri sana na kwamba kama ikifanikiwa kutekelezeka basi nchi hii tutashuhudia maendeleo kwa kasi kubwa. Kwa maana hii naiomba Serikali ijitahidi kupeleka fedha kwenye miradi iliyotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukurani zangu nyingi sana kwa kazi nzuri iliyofanyika katika kazi zifuatavyo:-

(i) Daraja kati ya Kijiji cha Chilonwa na Kijiji cha Nzali lilifukuliwa upande mmoja na sasa mwaka huu pamoja na mvua kuwa kubwa, lakini maji yalipita juu ya daraja kwa kimo cha futi moja tu badala ya mita moja karibia na futi tatu. Hongereni sana.

(ii) Kwa ujenzi wa madaraja mawili, moja dogo na moja kubwa pale kwenye Kijiji cha Membe, ahsante sana.

(iii) Ukarabati wa barabara yote kutoka Buigiri kwenda Chamwino Ikulu, kwenda Chilonwa, kwenda Membe, kwenda Dabalo, kwenda Itiso hadi Segala, Izava umeendelea kufanyika kwa ubora mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi mahsusi:-

(i) Daraja lililopo kati ya Kijiji cha Chilonwa na Kijiji cha Nzali ifukuliwe na upande wa pembeni ambapo lipo daraja lingine (madaraja haya yanafanya kazi sambamba). Hii itasaidia kuhakikisha maji hayapiti juu ya daraja kabisa.

(ii) Lipo daraja linaingia Dabalo linahitaji kutengenezwa/kujengwa ili eneo hilo liweze kupitika bila hofu wakati wa mvua.

(iii) Lipo daraja linalopokea maji kutoka daraja la hapo juu (namba 2) linalounganisha Kijiji cha Dabalo A na Dabalo B (Igamba) nalo naomba lipewe kipaumbele (daraja hili sasa lipo chini ya *TARURA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uyapokee maombi yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chilonwa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba sana tena sana Mheshimiwa Waziri, waichukue barabara ya Chikonji – Nangani kwenda Milola iingie kwenye barabara za *TANROADS*. Ni barabara kubwa na muhimu sana kwa uchumi wa wakazi wa Jimbo la Mchinga na Lindi Mjini. *TARURA* hawawezi kujenga barabara hii ina madaraja

mengi na makubwa hivyo kuachia *TARURA* si sawa hata kidogo.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuikumbusha Wizara hii kutenga pesa kwa ajili ya kumalizia barabara za *ring roads* ambazo ujenzi wake haujakamilika. Barabara ya *Davis Corner – Jet Lumo* inayounganisha Temeke na Jimbo la Segerea (Ilala), barabara hii haijatengewa pesa kwa mwaka wa tatu sasa. Hili sio jambo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara itenge fedha za kuimalizia barabara hii ili lengo la kupunguza kero ya foleni katika Jiji la Dar es Salaam itimie. Tafadhali naomba pesa kwa ajili ya barabara hii.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukumbushia ahadi za viongozi wakuu zifuatazo ambazo utekelezaji wake haujaanza Wilayani Misenyi, Jimbo la Nkenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya lami ya Katoma hadi Bukwali; barabara ya lami Kajai – Hospitali ya Magana (Hospitali Teule ya Wilaya); barabara ya lami ya Matukula hadi Minziro; barabara ya lami ya Kituo cha Afya Kabyaile hadi Gera; kilometa tatu za lami Makao Makuu ya Wilaya – Bunazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu Serikali ilisimamisha shughuli za maendeleo katika eneo la Kajunguti. Baada ya Serikali kufanya maamuzi ya kutojenga tena Uwanja wa Ndege – Kajunguti ni dhahiri wananchi walioacha kuendeleza maeneo yao ya Kajunguti watakuwa wamepata hasara kubwa. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa chochote wananchi kufidia hasara waliyoipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wizara nzima kwa kazi nzuri ya kusaidia kuweka miundombinu wezeshi ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Wilaya ya Karagwe barabara ya Nyakahanga – Nyakakika (kilometa 96) imekasimishwa *TANROADS* (2017/2018) na ilitengewa shilingi milioni 150. Fedha hizi ni kidogo mno ukilinganisha na ukorofi wa barabara. *Financial year* 2018/2019 imetengwa hiyo hiyo shilingi milioni 150, ninasikitika hii fedha haitaweza kutosha maeneo yote korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, barabara hii ni korofi sana naomba iongezewe fedha; ahadi ya kilometa tano za lami kwenda eneo korofi zaidi la Kajura Nkeito naomba itimizwe, eneo hili lipo barabara hii tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bugene – Benako ni *financial year* ya pili bajeti zinatenga hewa kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami, kwa nini? Je, wananchi wa hii barabara watalipwa lini fidia zao? *Detailed design* imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mugakorongo – Marongo kwa nini *detailed design* yake inachukua muda mrefu na wakati barabara hii ikiunganishwa na ile ya Bugene – Benako zinaunganisha Afrika Mashariki na kukamilika kwake kutachochea uchumi wa Kagera na nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara iongeze bajeti ya *TARURA* kwani hizi *feeder roads* za vijiji ndizo tunazitegemea kusafirisha mazao ya wakulima, wafugaji na wafanyabiashara wadogo kwenye kuzalisha uchumi wa kaya na nchi. *Ratio* ya mgao iwe angalau 40/60 *minimum. Ideally ration* iwe 45/55.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru sana Meneja wangu wa *TANROADS* Mkoa, *Engineer* Kasamwa kwa kazi nzuri ya kusimamia kazi za mkoa na kwa ushirikiano anaonipa. Ni matumaini yangu maombi yangu yatakubaliwa. Nawatakia majukumu mema. Ahsante.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kubwa ya dhati kwa kazi nzuri chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, bila kusahau kwa Waziri mwenye dhamana wa Wizara hii pamoja na Naibu Mawaziri kwa kushirikiana na wataalam, watumishi kwa ujumla wa timu hii imefanya kazi nzuri kwa nchi yetu na kwamba wametutendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na mawasiliano kwa mitandao kadhaa na yote yanatoa huduma ya kibenki, lakini mtandao wa Vodacom – Mpesa kumekuwa na wizi wa fedha, mteja akikosea namba akiwa ametuma fedha akitoa taarifa Vodacom jibu kuwa fedha hizo zimekwishatolewa na mhusika hana salio hivyo hesabu maumivu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni wizi kwani hawezi kufuatiliwa huyo mhusika anapokuwa na fedha hiyo basi irejeshwe kwa mteja aliyetoa taarifa, kuliko kumjibu hivyo au kwenda kuripoti polisi. Ni vema Wizara kuingilia kati kwani wakati mwingine ni pesa ya ada kwa wanafunzi vyuoni, kwa majibu hayo, hivyo mwanafunzi hatasoma chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mawasiliano ni muhimu kwani ni kiunganishi madhubuti kwa wananchi wetu hasa waliopo mipakani kuwa na mitandao yenye mitambo mikubwa kwa kuwa huwa wanaingiliana na mitandao ya nchi jirani hasa Zambia na Bujumbura. Mfano; Kata ya Kala, Kata ya Wampembe, kata ya Mambwenkoswe (Rukwa), mitandao inayumba. Tunaomba Wizara kuangalia mawasiliano kwa mikoa ya pembezoni, Bonde la Tanganyika na Bonde la Rukwa kuwa na mawasiliano kamili kuanzia milimani tuteremkapo bondeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi sana katika kuiunganisha nchi yetu, lakini wananchi wetu asilimia kubwa na wazalishaji wakuu hawana barabara (vijijini) na sasa na *TARURA* asilimia 30, hatutakuwa tumetenda haki kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda, hivyo ni bora wakati huu tukachukua maamuzi magumu ya kuwapa asilimia kubwa *TARURA.* Tuwaunganishe wazalishaji hawa tusonge mbele kwenye azma ya maendeleo ya nchi hii kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa msemaji wa kila mara katika Bunge hili kuhusu na barabara zinazoteremka kwenye mabonde ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa kwa sasa zimefikia mwisho wa kuendelea kuwa za changarawe/ udongo au kuweka viraka vya sementi na matengenezo ya maeneo korofi haya mara kwa mara kwa sasa basi. Tunaomba Serikali kuzingatia na kuzitengeneza kwa kiwango cha lami kama Milima ya Kitongo na Nyang'oro kuliko kuendelea kupanga bajeti kila mwaka kama 2018/2019 kwa kilometa 108.0 shilingi milioni 3,315.852 na kadhalika. Tuziangalie kwa huruma tupo pembezoni, tumechelewa kimaendeleo pamoja uzalishaji mkubwa wa chakula na biashara kwa ndani ya nchi na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau barabara ya Kibaoni (Katavi) hadi Kilyamatundu – Miangalua (Rukwa), ukifahamu Serikali inajenga daraja kubwa la Mamba (Rukwa/ Songwe) halafu barabara zake changarawe/udongo hali hii ngumu na haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali na Wizara kiutalaam wana haja ya kuinua Shirika la *TTCL* na kuweza kujiendesha, basi ni bora kuhakikisha kwa kuliwezesha kusambaa nchi nzima na vifurushi vyao kuwa rafiki kwa wananchi wetu, pamoja na simu zao kuwa na uwezo wa huduma zote za kimtandao kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi, na Serikali tusiendelee kuingiza

mitandao kutoka nje, naomba nguvu kubwa tuelekeze *TTCL* iweze kusimama na tujivunie shirika letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili. Mchango wangu unajielekeza kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu barabara, hili ni eneo muhimu sana kwa uchumi katika jimbo langu la Mufindi Kaskazini na Wilaya Mufindi. Barabara ya kutoka Mtiri – Ifwagi – Mdaburo – Ihamu – Isipii – Mpanga TAZARA mpaka Mlimba inaunganisha mikoa miwili ya Iringa na Morogoro (Wilaya za Mufindi na Kilombero) lakini shida yake imekuwa kubwa sana kwani haipitiki kabisa na *TARURA* haina uwezo wa kuunga barabara hii. Ikumbukwe Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi kuipandisha hadhi kuwa ya *TANROADS*. Mheshimiwa Waziri nimeshakuja kwako mara kadhaa lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuinusuru barabara hii yenye uchumi mkubwa wa chai, kahawa, pareto, msitu wa mbao, maharage, mahindi na utalii ambao ungeongeza pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Mheshimiwa Waziri atupe mkakati wa kukabiliana na barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kinyanambo A – Isalavani – Sadani – Madibira – Rujewa ambayo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi toka mwaka 2000 – 2005 - 2010 – 2015 – 2020, lakini hata kilometa moja tu haijajengwa. Ni vyema Mheshimiwa Waziri atuambie lini Serikali itaanza kutekeleza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka *J Corner* – Mtiri – Sawala – Mgololo kutokufungwa kwa kiwango cha lami, ni vyema sasa Serikali ikafunga barabara hii kwa kiwango cha lami ambako kuna uchumi mkubwa

wa viwanda kikiwemo kiwanda kikubwa kuliko vyote vya karatasi Afrika na Viwanda vya Chai zaidi ya vitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano, nimeongea mara nyingi na Mheshimiwa Waziri kuhusu maeneo ambayo hayana mawasiliano ikiwamo maeneo ambayo minara imefungwa lakini haifanyi kazi kama mnara wa Mapanda, Kata ya Mapanda, mnara wa Vodacom haufanyi kazi na mnara wa Ikwiha, Kata ya Ikwiha haufanyi kazi, kwa hiyo, hakuna mawasiliano. Katika Vijiji vya Uhafiwa, Mapanda, Ukami, Ihimbo na Chogo pia Ikurha, Uginza, Ilangamoto, Ihamu, Isipii na Mpanga Tazara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uchukuzi, naomba sana Mheshimiwa Waziri waweke kituo cha abiria kwenye Kata ya Mpanga TAZARA, Kijiji cha Mpanga TAZARA, reli ya TAZARA.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii nzuri iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri pia naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri sana katika kuendeleza ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Naishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara ya kutoka Njombe - Moronga kilometa 53 iliyoko jimboni kwangu, nimeona zimetengwa shilingi bilioni 12 ambayo imeweza kujengwa takribani kilometa 12 tu kwa mwaka 2018/2019, ninatarajia utaliangalia ili kasi ya ujenzi iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Njombe - Ramadhani - Iyaji kilometa 74 imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina toka mwaka 2013 yapata miaka mitano sasa kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami haijauza. Nimefuatilia hotuba hii sijaona mahali wala fedha kutengwa ili kuanza kazi ya ujenzi kulingana na upembuzi huo uliofanyika. Je, ni lini kazi ya ujenzi itaanza? Je, wananchi waliowekewa alama za “X” za kijani ni lini watalipwa fidia ili kuruhusu kazi za ujenzi kuanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Halali - Ilembule - Itulahumla nashukuru imetengewa fedha za matengenezo ya kawaida, lakini sijaona matengenezo ya Daraja la Halali ambalo limeathiriwa sana na mvua za mwaka huu. Naomba Serikali ifikirie kulijenga daraja jipya kwani ni jembamba sana na halijajengwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Wilaya yapo Igwichemya, mawasiliano ya simu yana kilometa mbili tu kwani ulienda zaidi ya kilometa tatu toka Igwachenya kwa mtandao ya Vodacom, Airtel, Tigo hakuna mawasiliano. Naomba Serikali irekebishe hali hii. Katika kuboresha viwanja vya ndege vya Milua, sijaona mpango wa kuboresha kiwanja cha ndege cha Njombe ili kiweze kuhudumia ndege kubwa. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 tuliahidiwa kuwa uwanja huu utaendelezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha hotuba hii niambie unasema nini kuihusu barabara ya Njombe (Ramadhani) Iyayi kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jitihada kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika kuliletea Taifa letu maendeleo ya kiuchmi. Miradi ya barabara ni muhimu sana katika kuleta maendeleo nchini. Kwa bahati mbaya sana katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 barabara muhimu kwenye Jimbo la Morogoro Kusini hazikupewa fedha za kutekelezea miundombinu hiyo muhimu. Barabara ya kutoka Bigwa - Kisaki tulishakubaliana kwenye bajeti ya miaka miwili ya nyuma kwamba barabara hiyo itapanuliwa na kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo ilikuwa igharamiwe ujenzi wake kwa kiwango cha lami na Marekani kwenye mpango wa *MCC II,* lakini kutokana na sababu za kisiasa Marekani ilisitisha utekelezaji wake. Serikali yetu ikathibitisha kwamba itachukua jukumu la kugharamia mradi huo muhimu kwa faida ya wananchi na kuahidi Bungeni kwamba ndani ya miaka mitano, Serikali itajenga barabara

hiyo ya Bigwa - Kisaki kwa kiwango cha lami. Inasikitisha kuona huu ni mwaka wa tatu wa miaka mitano Serikali bado haijaanza kutekeleza mradi huu. Kinachofanyika ni matengenezo tu, hili halikubaliki, fedha zilizotengwa kwenye bajeti ni matengenezo kwenye barabara ya udongo na changarawe, naiomba Serikali itekeleze ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo la Morogoro Kusini, tunashida sana na barabara za udongo na changarawe zinazowatesa wananchi hususani wakati wa mvua. Barabara ya kwenda Kongwa, barabara ya Mvua – Magogoni – Selembala, barabara ya Mtombozi – Lugeni – Nemele, barabara ya Kangazi – Mtombozi, barabara ya Konde - Mlono (kilometa 4.5), barabara ya Matombo shuleni – Tawa, Matombo – Uponda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Morogoro Kusini bado lina matatizo na mawasiliano ya simu. Haiwezekani katika karne hii, tunakuwa na wananchi kwenye vijiji vyetu vya Tanzania, haiwezekani kutumia simu zao kwa kukosa mtandao. Wengine inabidi wapande mitini ili kuzungumza na simu zao. Maeneo ya Kolero, Singisa, Bungu, Lugeni, Lusangalala, Uponda, Kasanga, Tandali na kadhalika wanahitaji huduma za simu hususani *TTCL,* Tigo, Airtel, Vodacom kilometa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali itende haki kwa kugawa maendeleo kwa wananchi wetu sawa kwa sawa. Jimbo la Morogoro Kusini tunahitaji barabara za lami, fedha zinapotea nyingi kufanya matengenezo kwenye barabara za udongo kila mwaka, hiyo si sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niombe na nichangie kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Naomba nichangie Wizara hii muhimu kwanza kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wote pamoja na wasaidizi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri kwanza kuiomba Serikali iondoe kodi kwenye mitambo ya kutengeneza barabara lakini pia utasaidia katika sekta ya maji kwenye mabwawa. Kodi itozwe kwenye kazi na siyo kwenye kuingiza mitambo pia kuondoa kodi kwenye miradi yenye maslahi ya kitaifa na ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia Wizara kupitia Serikali iangalie namna ya kuhakikisha suala la *NEMC* - utafiti wa mazingira katika suala la minara ya simu. Miradi mingi hukwama kwa ajili ya *Environmental Impact Assessment* (ripoti ya masuala ya mazingira). Serikali iangalie namna ya kuboresha mawasiliano hasa *data* ili twende na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze, ushauri wangu wa kuendelea kutumia taasisi za kwetu kama *TTCL* kwa shughuli za Serikali. Kazi yao sasa ni nzuri sana na tuendelee kuboresha kwa kuwekeza.

Naomba pia tuangalie namna ya kuboresha mapato kupitia mitandao hasa utumiaji wa simu za ndani na hasa fedha zinazopitishwa humo. *Sim Banking* leo hii hatupati mapato ya sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Wizara iwekeze kwenye viwanja vya ndege na bandari, zaidi huduma za kuhifadhi bidhaa ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuwa na *cold rooms.* Huduma za kuwekeza bidhaa hizo kwa hali ya hewa inayoweza kuratibiwa uwanja wa *KIA* inahitaji kwa haraka huduma hiyo kwa ajili ya kusafirisha maua na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Nashukuru na kupongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ilivyotekeleza Ilani ya Uchaguzi na utekelezaji wa maamuzi magumu na yenye tija ya Mheshimiwa Rais katika kuboresha

sekta ya uchukuzi kwa vitendo. Niwapongeze pia Waziri mwenye dhamana na Naibu Mawaziri wake kwa kazi kubwa na yenye tija kwa Taifa wanayoifanya kwa ushirikiano mkubwa na watendaji wao. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu katika miradi ya barabara, barabara ya Nyakato – Buswelu – Mhonze kilometa 18, kwa miaka mitatu mfululizo inawekwa kwenye bajeti lakini hadi sasa ni kilometa 1.2 tu imekamilika. Niombe walau kilometa 17 zilizobaki ziingie zote katika bajeti ya 2018/ 2019 ili tuondoe adha hiyo ukizingatia barabara hiyo inapita Makao ya Wilaya. Aidha, mkandarasi *JASCO* aliyepewa zabuni hiyo hana uwezo, ikiwezekana aondolewe. Katika bajeti imetegewa kilometa moja tu. Ninachelea kusema Awamu ya Tano itakwisha bila kukamilika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe ukamilishaji wa matengenezo ya kivuko cha Kayenze – Base ambacho kiliwekwa kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 na kinaonekana tena katika bajeti ya mwaka 2018/19. Naomba ukamilishaji wake ili kusaidia wananchi wa Kisiwa cha Base.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Barabara; matengenezo ya *Sabasaba - Busweru road*, tayari Halmashauri inaendelea kulipa fidia kwa wananchi. Niombe utekelezaji wake ukamilike kama ulivyopangwa ili kurahisisha mawasiliano na Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara za lami, mzunguko wa barabara za lami katika Manispaa ya Ilemela ni asilimia sita tu. Naomba ukamilishaji wa malengo yaliyowekwa ili hadhi ya Manispaa ilingane lingane na Manispaa zingine nchini.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi. Naomba kusema mkakati wa makundi uliochukuliwa na Wizara hii ya Ujenzi ili kuondo kero ya mafuriko katika jiji la Dar es Salaam. Nakushukuru kwa Wizara kuanza ujenzi wa barabara ya Kitunda, Kivule kilometa 3.2 kwa kiwango cha lami. Barabara hii huyu mkandarasi amegeuka kero kwa kwenda taratibu

sana tena wakati huu na mvua hali ni mbaya sana. Pamoja na kazi nzuri ya Meneja wa *TANROADS* naomba Wizara iingilie kati ili kuondoa kero ya barabara hii ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara kwa kuongeza kilometa tano za Kivule - Msongola ila naomba huyu mkandarasi asipate tena kazi kwa sababu ni mharibifu na anaichafua Serikali *(SAI* na *TANG Co.)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Pugu inahitaji mipango mikubwa ya kuipanua ili ikidhi kiwango na wakati kwa idadi ya watu waliopo. Barabara ya Chanika - Mbande ni kero kubwa hasa kwa daraja lilikatika na mashimo makubwa barabarani. Naomba Wizara iharakishe ujenzi wa barabara ya Pugu - Kinyerezi - Kifuru ili kupunguza mzunguko wa wananchi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kidogo katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mungu kwa mvua zinazoendelea katika nchi yetu pamoja na kuwa zimeleta madhara makubwa sana. Mfano, vifo kwa ndugu zetu na uharibifu mkubwa sana wa miundombinu ya barabara na madaraja. Ninapenda kujua Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha miundombinu hiyo niliyoitaja inatengenezwa ili kuondoa usumbufu mkubwa wanaoupata wananchi wetu kwa sasa uweze kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za *TBA* Dodoma, mimi ni mmoja kati ya wapangaji wa nyumba hizo ila nyumba hizo kwa sasa ziko kwenye hali mbaya, zinavuja, matengenezo hayafanyiki kabisa, tunafanya wenyewe, kibaya zaidi hali iliyopo sasa hivi mazingira yanayozunguka nyumba zetu ni mabaya sana, majani yamekuwa marefu sana yanahatarisha usalama wa maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kutokuzolewa kwa takataka kwenye maeneo yetu na hii kunaweza kuibua magonjwa ya kuambukiza mfano kipindupindu. Tunaomba sana usafi na matengenezo hayo niliyoonesha hapo juu yafanyiwe kazi ili kulinda afya za wapangaji wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kutoa mchango wangu huo, naamini niliyoyasema yatafanyiwa kazi kwa haraka hali ni mbaya, hasa nyumba zilizoko *Area D Site Two,* uchafu umezidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kuunga mkono hoja. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mafia ambayo kijiografia ni kisiwa ina tatizo kubwa la usafiri wa bahari kutoka na kuingia Mafia kupitia Bandari ya Nyamisati iliyopo Wilaya ya Kibiti. Tunaishukuru Serikali katika bajeti hii tumeona zimetengwa shilingi bilioni tatu kuanza ujenzi wa meli ya kisasa. Kwa kuwa mchakato wa kujenga meli hii utachukua muda wa miaka takribani miwili tunaiomba Serikali itupatie kivuko/meli ya muda wakati tunasubiri mchakato wa kujenga kivuko chetu ukiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tunaiomba Serikali iagize *SUMATRA* waje kuangalia upya katazo waliloliweka la kupakia abiria 50 tu kwa boti zinazofanya kazi sasa hivi ambazo uwezo wake wa kupakia abiria ni mkubwa sana mpaka kufikia abiria 200. Kwa hali ilivyo sasa wananchi wanalazimika kusubiri mpaka wiki nzima, jambo ambalo linaleta usumbufu hususani kwa wagonjwa na wenye dharura mbalimbali. Tunaiomba *SUMATRA* waje Mafia na kuliangalia suala hili kwa kushirikiana na wadau wa Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wa ndege wa Mafia ni muhimu sana katika kukuza utalii nchini, Wilaya ya Mafia inapokea watalii zaidi ya 10,000 kila mwaka na wote hao wanatumia uwanja huu wa ndege. Mafia imejaliwa vivutio vingi vya utalii ikiwemo maeneo ya *scuba diving, sports fishing,* fukwe nzuri na samaki wa ajabu aina ya potwe *(whaleshark)* ambaye anapatikana katika nchi chache duniani lakini hali ya uwanja wa ndege wa Mafia ni mbaya sana, hakuna jengo la abiria *(terminal building),* barabara ya kutua na kurukia *(runway)* ni fupi yenye urefu kiasi cha mita 800 hali ambayo hairuhusu ndege kubwa aina ya *Boeing* kutua na kusababisha kukosekana kwa safari za moja kwa moja kutoka nchi za ughaibuni kuja Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kilindoni mpaka Ras Mkumbi kilometa 55 ipo katika Ilani ya CCM 2010 – 2015 na ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Kikwete. Hali ya barabara hii ni mbaya sana na nyakati za masika inakatika na kuvunja mawasiliano baina ya Tarafa ya Kaskazini na Tarafa ya Kusini. Vilevile udongo unaotumika katika kufanya matengenezo ya kawaida *(periodical maintenance)* unapatikana kwenye vijiji viwili tu vya Bweni na Jimbo, udongo huo unakaribia kuisha na wahandisi wanasema umebaki udongo wa kutumika kwa miaka mitatu tu, baada ya hapo tutalazimika kutoa udongo kutoka Rufiji. Njia nyepesi ni barabara hii kuwekwa lami ili kuepusha gharama kubwa ya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, pamoja na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iondoe tozo, malipo kwa wananchi wa Kigamboni wanaotumia vyombo vya moto kupita katika Daraja la Kigamboni (Daraja

la Nyerere), ni ghali mno na kipato cha Watanzania na hali ya uchumi ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakandarasi wanaojenga barabara za lami chini ya kiwango wawajibike kuzikarabati zitakapoharibika kabla ya muda maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iondoe msongamano katika mizani iliyopo Vigwaza, Mikese na Morogoro. Kwa magari ya abiria (mabasi) yawe na eneo maalum la kupima uzito maana mabasi mara nyingi huenda kwa ratiba maalum, abiria wengine ni wagonjwa, watoto na mabasi hutumia muda mwingi katika mizani hiyo. Pia nashauri barabara zote zilizopo pembezoni mwa milima zijengewe *pavements* ili kuepuka mmomonyoko wa ardhi na ili zisiharibu miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya Dar es Salaam hadi Tanga ifufuliwe ili kuweza kusaidia mizigo mizito hususani malori kutumia reli ili kuepuka uharibifu wa barabara. Katika barabara kuu zijengwe kalvati ambazo zitakuwa na uwezo wa kuhimili wingi wa maji kipindi cha mvua za masika ili kuepuka maji kupita juu ya barabara na kuharibu miundumbinu. Mfano, barabara ya Dodoma - Morogoro eneo la Mbande hadi Kibaigwa ni eneo korofi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wa ndege wa Morogoro ambao upo maeneo ya Kihonda Bima, uwanja ule uboreshwe ili ndege ziweze kutua usiku na mchana na ukizingatia Morogoro kuna Mbuga za Wanyama za Mikumi na Selous ambazo ni vivutio vikubwa vya watalii, kwa kutumia uwanja huo tutaweza kuwavutia watalii wengi kuja Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe fedha kwa wakati ili kuwezesha Wizara kufanya kazi kwa muda uliopangwa kujenga miundombinu ya nchi yetu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *RCC* ya Mkoa wa Tanga na vikao vya Mfuko wa Barabara vya Mkoa *(Road Board)*kwa miaka miwili mfululizo tulikuwa tukipanga fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu *(feasibility study)* pamoja na *detailed design* barabara ya Lushoto hadi Mlalo kilometa 45. Hata hivyo, kwa mara zote ombi letu lilikuwa halipokelewi mara linapofika kwa Afisa Mtendaji wa Wakala wa Barabara wa Taifa *(TANROADS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi na ustawi wa maendeleo ya Mlalo. Ikumbukwe kwamba uchumi wa wananchi wa Mlalo unategemea sana kilimo cha mboga mboga na matunda. Matunda na mboga mboga ni bidhaa ambazo zinaoza kwa haraka sana. Hivyo basi, ili kujenga uchumi imara, tunahitaji barabara madhubuti ambazo zitafikisha mazao yetu sokoni kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara barabara zetu zimekuwa zikijifunga nyakati za mvua kutokana na *landslide* (maporomoko) hivyo kwa dhati kabisa tunaiomba Serikali yetu sikivu isikie kilio chetu tupate barabara ya kiwango cha lami. Eneo hili ni kilometa 45 tu kutoka Lushoto Mjini hadi Mlalo ambapo ndiyo kituo cha mwisho cha mabasi yaendayo maeneo tofauti ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Mlalo – Mng'aro kilometa 20, imepandishwa hadhi hivi karibuni miaka ya 2012 na Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Kikwete. Baadhi ya nyumba zilizopo pembezoni mwa barabara hiyo zimewekwa alama ya "X", tunapenda kujua tafsiri ya alama hizo kwa sababu wananchi wanashindwa kuelewa hatma ya nyumba zao na wanashindwa kuziendeleza. Hivyo, tunaomba Serikali itoe tafsiri ya alama hizo ili wananchi waweze kujipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mawasiliano ya simu za viganjani bado siyo rafiki sana, yapo maeneo ambayo yapo katika mabonde na yamefunikwa na vilele vya milima, mfano katika Kata ya Malindi hasa Kijiji cha Makose na kata ya Rangwi eneo la Longoi Mtaa wa Bustani na katika eneo lote la Mliifu Kata ya Manolo. Tunahitaji msaada huu kwa wananchi wa maeneo niliyoyataja ili kuongeza tija na ufanisi katika shughuli za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wa Jimbo la Mlalo hususani Makose, Longoi, Mliifu, Hambayo na Viti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya katika Wizara hii. Tumeona mambo mengi na makubwa yanayofanyika, ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege, ununuzi wa ndege, meli na kadhalika. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mbalimbali au Mikoa ambayo haijabahatika kupitiwa na reli, iwe ya zamani au reli iliyojengwa kwa *standard gauge.* Mikoa hiyo ambayo haipitiwi na reli ipewe kipaumbele kuhakikisha inatengeneza barabara za Mikoa kwa kupitika vizuri ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi (mfano Mkoa wa Rukwa). Barabara ya Kibaoni – Kilyamatundu – Kamsamba itengenezwe kwa kiwango cha lami kwani barabara hii ina umuhimu mkubwa sana kiuchumi kwa wananchi na kwa Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kalamba – Nzite – Ilemba ipanuliwe eneo la Mlimani kupunguza miinuko ya milima na kuweka zege eneo lote la Mlimani. Barabara ya Ntendo – Muze ijengwe kwa kwa kiwango cha lami. Eneo la Mlimani lipanuliwe, liwekewe kingo eneo la mlimani na mlima wote ujengwe kwa zege.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Miangalua– Chombe nayo ipanuliwe eneo la Mlimani iwekewe zege eneo

lote. Tunaomba ujenzi wa Daraja la Kilyamatundu – Kamsamba lijengwe haraka kama mkataba unavyojieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara iliyopo Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Moshi, Kata ya Old Moshi Mashariki kuanzia Kiboriloni – Kikarara – Tsudini mpaka Lango la Mlima Kilimanjaro, barabara hii ilikuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu, Dkt. Jakaya Kikwete na baadae kupewa ahadi na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Ni zaidi ya miaka 10 imekuwa ikitengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami lakini mpaka leo inafanyiwa upembuzi yakinifu. Je, zoezi hili linachukua muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile kwa umuhimu wake kwenye sekta ya utalii ambayo Wizara ya Maliasili inaifanya njia ya Old Moshi kwa ajili ya watu mashuhuri lakini cha kusikitisha barabara ile imeharibika sana, haipitiki kabisa. Kinachoonekana kule ni vibao vya *TANROADS* vinavyoashiria wataanza kutengeneza lakini hakuna kinachoendelea!

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahamia Dodoma rasmi lakini bado kuna Wizara pamoja baadhi ya barabara zipo *TARURA* sababu hapa ndiyo kioo cha nchi yetu ni lazima tuanze kuwa na mipango ya kuhakikisha barabara zote zinapitika kwa lami na kuwepo na njia za *ring roads* ili kuzuia msongamano, la sivyo, kile kichefuchefu cha foleni ya Dar es Salaam kitahamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege uliopo Moshi umesahaulika kabisa, kwa sasa uwanja ule wananchi wanautumia kwa ajili ya kilimo cha maharage. Uwanja ule upo *very strategic* kwa ajili ya kukuza utalii, unaweza kutumika kwa dharura, pia kutumika kwa ajili ya ndege ndogo kupeleka watalii *Serengeti National Park* baada ya kupanda mlima. Je, Serikali ina mikakati gani ya kukikarabati au kukifufua kiwanja cha ndege cha Moshi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu karakana iliyopo *Kilimanjaro International Airport,* karakana hii ipo pale *KIA* lakini haitumiki ipasavyo, ingeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kuongeza fedha za kigeni. Ndege kutoka nchi jirani zingeweza kuja pale na kufanya *service,* kupiga rangi na kadhalika, lakini Serikali haioneshi nia ya dhati ya kukarabati karakana ile. Je, ni lini Serikali itaanza ukarabati katika karakana ya *KIA* ili iweze kuchangia katika Pato la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TAMESA,* nia ya kujenga *TAMESA* kila Mkoa ilikuwa ni njia mojawapo ya kupunguza matumizi kwenye magari ya Serikali na magari yote ya Serikali yatengenezewe kule na kufanyiwa *service* kule, lakini karakana hizo vipuri vyake vimepitwa na wakati na magari yaliyopo sasa ni *automatic* na teknolojia mpya, badala yake *TAMESA* inatumika kuegesha magari ya Serikali yasiyofanya kazi kabisa na kwa sasa gari ya Serikali inapelekwa *TAMESA* halafu *TAMESA* wanawapa kibali kwenda kutengeneza au kufanya *service* kwenye *garages* za watu binafsi. Hii inasababisha Serikali kuwa na madeni makubwa sababu kule *private* malipo huwa zaidi ya hata mara mbili na sababu ni kwamba pia Serikali inachukua muda mrefu kuwalipa madai yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua Serikali ina mikakati au mipango gani ya kuhakikisha inaweka teknolojia ya kisasa katika karakana zote sababu miundombinu ipo ili magari ya Serikali sasa yaanze kutengenezewa *TAMESA* hatimaye kupunguza gharama kwa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba nyingi za *TBA* zipo katika hali mbaya sana, mfano hapa Dodoma, nyumba zilizokuwa chini ya *CDA* ni mbovu kupita kiasi na Serikali imewapangia wafanyakazi wanaohamia hapa kuishi kule. Naiomba Serikali itambue wafanyakazi hawa walitoka majumbani kwao, nyumba zenye hadhi leo hii *TBA* mnawapangia nyumba ambazo bado hamjazikarabati kabisa? Majengo mengi yamefubaa hakuna sababu ya kuyabomoa lakini wakarabati ili kuwepo na kumbukumbu

ya majengo hayo kwa vizazi vijavyo kujua Dodoma kabla ya Makao Makuu kuhamia Dodoma ilikuaje. Historia ni muhimu sana.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa, hongera sana kwa kazi kubwa na ya kutukuka unayoifanya wewe na timu yako ya Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote. Hakika mnatubeba wananchi, CCM wote chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba tu nikumbushie masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Lumecha – Kitanda – Londo – Kilosa kwa Mpepo hadi Lupiro kwa kiwango cha lami, barabara hiyo inaunganisha Mikoa ya Ruvuma na Morogoro kupitia Wilaya za Malinyi na Namtumbo ambao ni majirani wa asili wanaounganishwa kwa njia ya miguu tangu enzi za Wajerumani na Waingereza waliokuwa wakiitumia kusafirisha manamba kwa ajili ya kilimo cha mkonge katika Mikoa ya Pwani na Tanga. Tunaomba ujenzi uanze Lumecha kuelekea Londona - Lupiro ambapo kuna daraja linalotenganisha Wilaya na Mikoa hiyo miwili na hivyo kutekeleza Ilani ya CCM ya 2015/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukisubiri lami iliyoahidiwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tunaomba juhudi za kutoboa na kuchonga kipande cha barabara kuanzia Londo hadi Kilosa kwa Mpepo zingeharakishwa ili barabara hiyo inayounganisha Wilaya ya Namtumbo (Ruvuma) na Wilaya ya Malinyi (Morogoro) ianze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanadhani barabara hiyo imetoboka na hivyo inapitika, kumbe bado haijachongwa na kusababisha wanaotamani kuitumia na

kuanza kupita kwa gari ama pikipiki kudhurika kama ilivyotokea kwa Padri wa Hanga Monaskeri aliyetumia pikipiki ambayo ilikwama na hatimaye kutembea kwa miguu hadi kifo kilipomfika kwa sababu ya uchovu na njaa ya siku zaidi ya tatu. Nikuombe Waziri mpendwa, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, ushirikiane na Katibu Mkuu wako, *Engineer* Nyamhanga mtusaidie fedha za kukamilisha uchongaji wa kipande hicho cha barabara ili ianze kupitika. Mameneja wa *TANROADS* Mikoa ya Ruvuma na Morogoro wana dhamira ya dhati ya kuifanya kazi hiyo lakini wanakwamishwa na ukosefu wa fedha za kutosheleza ukamilifu wa kazi hiyo ya kuchonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nashukuru kwa kumlipa *advance payment* Mhandisi Mshauri wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtwarapachani – Likusanguse – Nalasi hadi Tunduru ili ijengwe kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa na Waheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Serikali hii ya Awamu ya Tano waliofanikiwa kupita katika barabara hiyo na kujionea wingi wa wakazi wanaotegemea barabara hiyo na fursa kubwa zilizopo katika maeneo hayo. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri uendelee kuwalipa *certificates* zao za kazi ili kazi hiyo ikamilike mwakani kama ilivyokubalika katika mkataba na ujenzi kuanza kwa wakati. Hivyo, naomba fedha za kutosha zitengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba ahadi ya kukipeleka Kivuko cha Ruhuhu kihamishiwe eneo la *custom* katika Kijiji cha Magazini, Wilaya ya Namtumbo ili safari za wakazi wa Namtumbo, Tarafa ya Sasawala na wakazi wa Tunduru Kusini, Nalasina Mbesa wapate kivuko salama cha kuwapeleka katika vijiji vya Wilaya ya Mabhagho nchini Msumbiji kwa shughuli za kijamii na kibiashara. Vilevile kwa wananchi wa Mabhagho kuja Mkoani Ruvuma kwa shughuli za kibiashara na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nikuombe uiwezeshe *TANROADS* Mkoa wa Ruvuma kifedha,

watekeleze miradi ya barabara zao ikiwa ni pamoja na barabara za Wilaya ya Namtumbo kama vile Namtumbo – Likuyu – Mkuju kunakojengwa Mgodi wa Madini ya Urani, Utwango – Namabengo – Mbimbi – Luegu, Mkonya – Mgombasi – Nangero – Naikesi na Mkongo Nakawale – Matimila – Mleke. Barabara hizo zipo maeneo ya kiuchumi ya Wilaya ya Namtumbo na zinahudumia wakazi wengi wa Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, *UCSAF* na *TCRA* wanatekeleza majukumu yao vizuri katika eneo langu na ninawaomba tu watekeleze ahadi zao kwa wananchi wa Namtumbo kupitia mimi Mbunge wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawasilisha.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lililo wazi kabisa kwamba kutokana na maendeleo ya kasi ya teknolojia ambayo yameathiri nyanja mbalimbali za maisha, ikiwemo sekta ya mawasiliano na uchukuzi, mtazamo na tafsiri katika sekta hizi umechukua wigo mpana sana. Kwa sasa ukizungumzia mawasiliano na uchukuzi unazungumzia ulinzi na usalama, unazungumzia haki na uwezo wa kupata taarifa na maarifa (elimu na ulinzi) kwa haraka, unazungumzia mwingiliano wa maisha ya kila siku ya binadamu katika nyanja zote zinazojulikana kuanzia uchumi, siasa, jamii na kila kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo, kupitia bajeti hii ya mwaka 2018/2019 ni vema Serikali ikalieleza Bunge ni kwa namna gani nchi yetu imejipanga katika sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika zama hizi za mapinduzi makubwa, tumejipanga vipi kuyatekeleza hayo kwa vitendo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia bajeti hii ya mwaka 2018/2019, sijaona mahali ambapo mipango na mikakati ya Serikali imeonesha kuwa Mkoa wa Mwanza unapaswa kuwa eneo la kimkakati katika nyanja za

mawasiliano na uchukuzi hasa kwa eneo la Maziwa Makuu na kipekee kwa Afrika Mashariki. Nilitarajia Serikali hii ingetumia kadri inavyowezekana kimkakati ili Mwanza iwe kitovu cha usafiri kwa maana ya anga, maji na nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetazamia katika nyakati hizi za ushindani mkubwa wa kibiashara na kiuchumi Serikali ingejikita katika kuimarisha na kuboresha miundombinu ya uchukuzi ili Mwanza kuwe kitovu cha usafiri kwa nchi za *EAC,* kwa maana ya kuunganika kwa njia ya barabara na nchi za Burundi, DRC, Uganda, Kenya, Rwanda na Sudani ya Kusini, na hii ni ahadi iliyowahi kutolewa na Rais Dkt. Magufuli mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwaambie wananchi wa Mkoa wa Mwanza ahadi hiyo imefikia wapi? Lakini wanataka kujua pia mikakati ya kuboresha na kurejesha reli yao, je, upo au ndiyo wasahau kabisa kama walishawahi kuwa na treni ambayo ndiyo usafiri rafiki kwa maendeleo ya kiuchumi duniani kote?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kumekuwepo na taarifa nyingi kuhusu dhamira ya kujengwa kwa daraja katika eneo la Kivuko cha Busisi – Kigongo. Ningependa kupata kauli ya Serikali suala hili limepewa uzito kiasi gani katika bajeti ya mwaka 2018/2019? Ili sasa isiwe tu maneno bali tuone utekelezaji, wananchi wa Mwanza hususani wanaotumia kivuko hiki kwa ajili ya kuingia na kutoka Jijini Mwanza kuelekea Sengerema, Buchosa au Mikoa ya jirani ya Geita, Kagera hadi nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda hadi DRC na kwingine wanataka kujua, je, ujenzi huu unaanza na kukamilika lini? Je, daraja litakalojengwa litakuwa la namna gani? Na sasa tuko katika hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mipango ya ujenzi wa meli, vivuko, kukarabati meli na vivuko vinavyofanya kazi katika maeneo mbalimbali ya Ziwa Victoria ikiwemo pamoja na baadhi ya maeneo ya visiwa 36 vilivyoko ziwani humo, nataka kusikia kutoka Serikalini, je, kwa mwaka huu unaoisha wamefanya ukaguzi wa vivuko

au meli ngapi ili kupima uimara wake na ufanisi wake au tunasubiri kufanya ukaguzi pale tunapopata majanga? Je, mipango ya ujenzi wa meli na vivuko na ukarabati wa meli na vivuko unahusiana na vivuko vingapi na katika maeneo yapi hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, katika vivuko hivyo Serikali ina mpango gani kukifanyia ukarabati mkubwa Kivuko cha Kome – Nyakalilo ambacho ni wazi kabisa kimeshaonesha dalili zote za kuchoka, kinaelemewa na abiria na mizigo hivyo kusababisha adha ya usafiri wa majini na usalama wa abiria na mali zao kutokuwa wa uhakika? Serikali inasubiri hadi maafa yatokee ndiyo iweze kukifanyia kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Kivuko cha Kome – Nyakalilo inavikabili vivuko vingi mathalani Kivuko cha Luchelele na mahali pengine, nasisitiza Serikali itoe takwimu ya jumla ya vivuko vinavyofanya kazi ndani ya Ziwa Victoria na viko katika hali gani kwa kila kimoja. Vivyo hivyo, takwimu za meli zinazofanya kazi Ziwa Victoria na hali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ulitoa ruzuku kwa makampuni ya simu ili kufikisha na kuboresha huduma za mawasiliano vijijini na kwenye maeneo yasiyokuwa na wa kibiashara, kwa Kanda ya Ziwa Mikoa iliyobahatika ni Mwanza na Mara. Ningependa kujua mpango huo umekuwa na mafanikio kiasi gani? Ruzuku hiyo ilitolewa kwa namna gani na kwa utaratibu upi na ilikuwa kiasi gani na makampuni yapi yaliyopewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza hivyo kwa sababu hali ya mawasiliano katika maeneo mengi ya vijijini bado siyo nzuri huku maeneo mengine yakiwa hayana mawasiliano kabisa, hasa maeneo ya visiwani ambayo yana vivutio vya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege, Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja iliyotolewa yako mengi ambayo yamesemwa. Lakini kwa ajili muda nitaomba nijikite katika maeneo mawili ambayo Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ambalo naomba nianze ni suala zima la *TARURA.* Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamechangia wengine wakiounga mkono *TARURA* uwanzishwaji walio wengi wameounga mkono uanzishwaji. Lakini ambalo limejirudia mara nyingi sana kwa kila Mbunge ambaye alipata fursa ya kuchangia kuhusiana na chombo hiki ni suala la mgawanyo asilimia 30 kwa 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitoa ufafanuzi wakati tunahitimisha hoja ya bajeti ya kwetu lakini kwa sababu chombo hiki kinaingiliana na *TANROADS* ndiyo maana na leo imekuwa likijirudia mawazo ambayo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge inaonesha jinsi ambavyo tuna kiu ya maendeleo kuhakikisha kwamba barabara zetu na hasa zile za vijijini zinapitika vipindi vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tunakiri, lakini pia si busara sana tukasema tunagawana umaskini kwa sababu mtandao wa barabara ambazo zinahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami ni nyingi na kila Mbunge ambaye amepata nafasi ya kusimama hapa aliomba barabara kiwango cha lami na hata kwako nimesikia upande wa kule wakati Mheshimiwa Frank Mwakibete anasema amesema na yeye anaomba barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kujenga barabara zetu kwa kiwango cha lami bado uhitaji ni mkubwa sana ni vizuri mkatupa fursa tukalichukua wazo jema kama hili ili tuje na namna ambayo itasaidia kuhakikisha

kwamba hatuendi kufifisha kazi nzuri ambayo imeanzishwa juu ya suala zima la kujenga barabara zetu kuziunganisha zile za Mikoa na zile za mipakani kwa kiwango cha lami eti tu kwa sababu tunataka kuongezea asilimia nyingi kwenda TARURA. Ni vizuri na tukaanza kufikiria sisi Wabunge kwa ujumla wetu namna mzuri ya kupata chanzo kingine ilikuwa ni kusema kwamba sasa tunaenda kubadilisha *formula* kutoka asilimia 30 na 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo imesemwa kwa urefu sana na ikawa inavuta hisia za Waheshimiwa Wabunge na hasa Wabunge wa kutoka Mkoa wa Morogoro na hoja hii iliibuliwa ikasemwa kwa uzuri sana na Mheshimiwa Devotha Minja. Sisi kama Serikali jambo hili tunalijua, lakini ni vuzri pia tukaelezana unaposema unajenga barabara kiwango cha lami tukubaliane hiyo barabara inajengwa kwa utaratibu upi na ni lami ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko aina nyingi za lami hasa katika mradi ambao umeendeshwa na unaendela tunategemea kwamba utakamilika ndani ya mwezi huu, Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa Mikoa ambayo kwa maana ya mji wa Morogoro ni mioungoni mwa miji ambayo imepata miradi huu mradi unaitwa *ULGSP* ambao unajengwa kwa jumla ya shilingi bilioni 12 ambao Waheshimiwa Wabunge hasa wa Morogoro walikuwa wanasema kwamba ni gharama sana kujenga barabara hii inafika mpaka bilioni tatu haijapata kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli haijapata kutokea, lakini hiyo barabara inajengwaje ndiyo suala ambalo lazima tuulizane. Barabara inapojengwa kuna hii inaitwa *surface dressing,* lakini ile ambayo tunajenga Morogoro inaitwa *asphalt concrete* ni miongoni mwa ujenzi wa barabara za lami ambazo zina gharama kubwa lakini ni vizuri pia tukaambizana ni kazi zipi ambazo zinafanyika. Barabara zile za Morogoro zinahusisha kilomita 4.6 na kazi ambazo zinafanyika naomba kwa ruhusa yako nizitaje. Kuna kutengeneza barabara ya Tubuyu - Nanenane Maelewano yenye urefu wa kilometa 4.6 na kazi zifuatazo zinafanyika:-

(i) Kutayarisha *road bed,* kuandaa matabaka ya barabara ambayo ni *G3, G7, G15* na *C1* kwa maana ya *cement stabilizer layer;* na

(ii) Kujenga njia za chini za ardhi kupitisha huduma kwa maana ya *service dacks.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa mashuhuda, inapotokea barabara imejengwa mtu anataka kupitisha mabomba anakwenda kuomba kibali eti aje aanze kukata barabara, sasa kwa barabara inayojengwa Morogoro jambo hilo halitatokea kwa sababu hiyo *service* imeshakuwa *provided*. Lakini kama hiyo haitoshi, kuna kuondoa tabaka la udongo pale Morogoro ilibidi kuondoa milimita 600 kwa sababu kuna ule udongo mweusi. Kwa ujumla naomba kwa ajili ya muda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hakuna senti tano ambayo imeliwa na Tume zimeundwa, TAKUKURU wameenda wamechunguza ukiitazama unaweza ukadhani kwamba pesa imeliwa lakini kwa sababu ni kitu ambacho ni *technical,* naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba ni thamani ya pesa imetumika Mheshimiwa Mbunge asiwe na shaka juu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu na nianze kwa kuunga mkono hoja. Niitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sbabau naongea kwa mara ya kwanza kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo yaliyojitokeza namshukuru sana Mungu kwa nafasi hii lakini nimshukuru kipekee Mheshimiwa Rais kunipa nafasi, kuniamini niweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe, nimshukuru Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge maalum niishukuru Kamati tumefanyakazi nayo, tumepokea ushauri wa Kamati na wameendelea kutuboresha katika utendaji wa kazi kwahiyo Mheshimiwa Kakoso pamoja na timu ya Kamati nzima nawashukuru sana.

Nitoe shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu mara zote tumepata ushauri wao, tumepata mijadala mbalimbali tukiwa ndani ya Bunge na nje ya Bunge kwa hiyo, Wabunge tunawashukuru ushauri wenu, maneno yenu kwa kiasi kikubwa yametusaidia kufanya shughuli zetu, lakini pia niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Ushetu muda mwingi kabla ya nafasi hii nimekuwa na muda mwingi wa kuwepo Jimboni, lakini sasa wananikosa na niishukuru pia familia yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwamba bajeti hii katika sekta ya ujenzi peke yake imechangiwa kwa kuzungumza hapa zaidi ya wachangiaji 95 na zaidi ya wachangiaji 50 wamechangia kwa maandishi. Niseme tu Katibu Mkuu na timu yake wanaendelea kukamilisha kabrasha la majibu kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mtayapata na mtaona namna Serikali kupitia Wizara hii inavyochukua hatua mbalimbali kuweza kutekeleza na saa nyingine kuona namna mambo ambayo yamefanyika kupitia pia michango ya kwenu kwa hiyo msiwe na wasiwasi mtapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii, niseme tu kwa ufupi sana nilitaka nitoe na ufafanuzi kidogo kwenye hali ya mtandao wa barabara nchini ili angalau tuwe na picha ya pamoja. Ukiisoma sheria yetu ya barabara hasa hasa ile *section* ya 12 inatoa mchanganuo wa aina za barabara. Sasa nilitaka nizungumze sambamba ili tuone pia jukumu lililopo kwenye Wizara, lakini jukumu pia ambalo lipo kwa upande wa wenzetu *TARURA* ili tuone tukifanya mchanganuo pale inaweza ikatupa picha kwamba michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge imezungumza juu ya namna *TARURA* iwezeshwe zaidi ni kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme tu kwamba kwa upande wa barabara kuu, tukizungumza barabara kuu tunazungumza juu ya barabara ambazo zinaunganisha Makao Makuu ya Mikoa lakini pia barabara ambazo zinaunganisha Makao Makuu ya Mikoa pamoja na majiji au inaunga nchi za nje ambapo kwa sasa tuna barabara zenye ukubwa wa zaidi ya kilometa 12,000 hivi. Lakini tukizungumza barabara zile za Mikoa tunazungumza juu ya barabara ambazo zinatoka kwenye Makao Makuu ya Mikoa zinaunga barabaa kuu.

Lakini barabara pia za Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa na hizi sasa kwa ukubwa tunazo kilometa yapata zaidi ya 23,000 sasa utaona kwa upande wa barabara kuu sehemu ambazo sasa zina kiwango cha lami ni zaidi ya kilometa 8,000 na zile ambazo ziko kwenye matengenezo na hata Waziri Mkuu akiwasilisha hapa, kilometa zaidi ya 1,700 ziko kwenye hatua mbalimbali. Sasa ukijaribu kupima utaona upande wa barabara kuu karibu sehemu kubwa tunaunganisha na Kamati imetoa ushauri tumeuzingatia na utaona Mikoa michache ambayo harakati zinaendelea katika hatua mbalimbali kuziunganisha ikiwemo maeneo ambayo yamebakia kama barabara kubwa ikitoka Mkiwa ukipita Itigi kwenda Mbeya, iko barabara kubwa ukitoka Morogoro sasa tunajenga Kidatu kwenda Ifakara lakini ukitoka Ifakara - Lupilo - Malinyi - Londo - Kilosa kwa Mpepo tunakwenda kutoka kule Namtumbo na hiyo barabara harakati zinaendelea vizuri. Kwa hiyo, ziko barabara zingine, barabara ya Mheshimiwa Chenge wakati akichangia jana alizungumza juu ya barabara ambayo itakuwa ikitoka Lalago kuja Sibiti na pale Sibiti tutakuwa na *route* mbili, moja itapita Eyasi kwenda Karatu, lakini nyingine itapita Mkalama itakwenda Haydom - Katesh - Mbulu Mjini itakwenda hadi Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii ni barabara muhimu sana kwa sababu itaunganisha Mikoa kwa maana ya Simiyu, kwa maana ya Shinyanga, Mwanza, Singida na baadae tutakuwa na vipande vichache ambavyo vitaunganisha ukitoka Singida Mjini kwenda Mkalama, lakini ukitoka Singida

Mjini kwenda Haydom. Kwa hiyo, unaona kwamba muunganiko wa barabara nchi nzima unakwenda vizuri na wale ndugu zangu wa Kigoma, maeneo ambayo yalikuwa yamebakia yako kwenye hatua nzuri kwa maana tutaiunganisha barabara kutoka Nyakanazi kuja Kibondo, unakuja Kidahwe mpaka Kigoma Mjini pamoja na matawi yanayounganisha nchi za jirani kwa maana sasa tunakwenda vizuri. Kwa hiyo, karibu maeneo mengi yanaunganishwa na hii ni itakuwa inatupa fursa kwenda kuunganisha barabara hizi ambazo tunaziita barabara za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa maana hizi barabara za Wilaya ni barabara ambazo zinaunganisha Tarafa, makao Makuu ya tarafa na tarafa zingine, inaunganisha pia makao makuu ya kata na tarafa, inaunganisha pia kutoka kwenye kata na kwenda vijijini lakini pia na barabara za mitaa. Kwa maana hiyo sasa utaona kazi ambayo inafanyika na *TARURA* sasa hivi ni kufanya tathmini ya hali halisi ya ukubwa na mtandao wa barabara zetu kote nchini na hili zoezi linafanyika vizuri, liko hatua za mwisho sasa wanaendelea kuhakiki, zitakuwa na *roughly* na takribani kilometa 108,000. Sasa baada ya kukamilisha hiyo itatuwezesha sasa katika kupanga rasilimali hii kwa ajili ya uboreshaji wa barabara ili sasa tuje kuwa na mgao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwahakikishie Wabunge na Bunge lako tukufu kazi kubwa inafanyika, ujio wa *TARURA* ni mkombozi kuhakikisha sasa uwiano wa barabara za kwetu unapata fedha vizuri na tunaendelea pia kuunganisha maeneo yaliyobakia ya nchi yetu pamoja na nchi za jirani. Ukiona hivi karibuni kuna mkataba umesainiwa pia ukitoka kule Mbinga kwenda Mbamba Bay, mkandarasi yuko *site,* lakini tunaunganisha na wenzetu upande wa Msumbiji naona Mheshimiwa *Chief Whip* wa kwetu hapa anazungumza, tutatoka Likuifusi tutakwenda Mkenda na tukitoka Mkenda tutarudi Tingi ili tuunganishe na barabara kubwa inayotoka kule Mbamba Bay lakini kule Mbamba Bay tutaunga na nchi za jirani pamoja na wenzetu wa Mbeya kwa maana ya ujenzi wa meli, lakini pia barabara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka pale Kitai ukienda Ruhuhu ziko kilometta 139 mwambao wa Ziwa Nyasa tunakwenda kuziboresha ili wananchi wa Ludewa waweze kwenda Kyela na kwenda Mbeya kwa wenzetu kule kwa maana muunganiko nilitaka nitoe mfano kwa maeneo machache muone namna Serikali inafanya juhudi ya kuunganisha Mikoa, lakini pia kutekeleza sera ambayo inataka tuanze kuunga Mikoa, tuunge na wenzetu wa nchi za nje ili tuweze kufungua fursa kwa sababu barabara pia itachangia katika maendeleo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme tu kwamba kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kimezungumza mambo mengi na niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tusome. Barabara zimeanishwa vizuri, saa nyingine ninataka niseme hivyo kwa sababu yako maeneo ambayo tumetaja kwa mfano, uboreshaji wa miundombinu katika Jiji la Dar es salaam na upande wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba wananchi wanahitaji wachangie katika uchumi wasikae muda mwingi barabarani ndiyo maana utaona nilikuwa nimejaribu kuonesha hapa maana yake nilishangaa juzi wakati Mheshimiwa Kubenea akichangia alisoma jedwali ila hakusoma kama Mheshimiwa Tambwe alizungumza hapa, alisoma jedwali akasema kuna barabara hewa nikaanza kushangaa nikitambua kwamba Mheshimiwa Kubenea ni mwandishi na nafikiri anahitaji kuwa makini zaidi ili saa nyingine ukizungumza jambo ulizungumze ukiwa na uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianda ukurasa wa 20 kama Mheshimiwa Tambwe alivyozungumza, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema wazi barabara ile ya Nzega - Puge - Tabora imetengewa fedha kwa ajili ya kumlipa mkandarasi, lakini yeye alisema kuna barabara hewa ambayo imekamilika na imetengewa fedha sasa hiyo siyo sahihi nilitaka niweke kumbukumbu sawa. Ni kwamba barabara zimeainishwa vizuri na mipango imeapangwa vizuri kwahiyo nilikuwa napenda Waheshimiwa Wabunge tukipitia tutaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nitoe mfano kwa upande huu wa barabara za Dar es Salaam, mtandao wa barabara ambao utakwenda kupunguza msongamano utakuwa na urefu wa kilometa 156 lakini ziko barabara ukitoka Tegeta tutakuwa tunakuja Mbezi sasa tunaendelea na usanifu, kutakuwa na barabara ambazo zitakuwa na njia sita. Lakini pia ukitoka Mbezi mwisho kwenda Pugu tunaendelea kufanya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka tu niseme kwa ufupi kwa sababu ya muda yako maelezo mazuri sana ukienda ukurasa wa 17 hadi ukurasa wa 21 tutaona namna tulivyojipanga ili kufanya mtandao wa barabara katika Jiji la Dar es salaam lakini pia upande wa Dodoma tumelitazama. Upande wa Dodoma tumejipanga kwa sababu ya uzoefu wa *conjection* katika Jiji la Dar es Salaam tumejipanga vizuri. Ziko barabara ambazo zimetajwa katika kitabu hiki utaona kuna barabara za mzunguko zina kilometa 104; lakini ziko pia barabara za ndani ambazo tutaziboresha ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Dodoma kwa ujumla waweze kupita na kufika katika maeneo yao na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona nitazama kwa sababu ya muda, sasa naomba nimalizie tu kwa kushukuru kwa nafasi hii lakini niwaombe Wabunge tu hata baada ya kikao tuweze kubadilishana mawazo hii nchi ni ya kwetu wote, kama kuna mawazo sisi kama Serikali tunayachukua kwa ajili ya kuyaboresha, muda wote tuzungumze, tubadilishane mawazo ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mwasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kunifanya niweze kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Lakini nichukue nafasi hii vilevile kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua niweze kumsaidia katika nafasi aliyonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa namshukuru Waziri wangu Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (Mbunge) kwa ushirikiano na muongozo anaonipatia mara kwa mara katika utendaji wa shughuli zangu. Nawashukuru vilevile watendaji, Dkt. Leonard Chamuriho - Katibu Mkuu wa Uchukuzi, *Engineer* Nyamuhanga - Katibu Mkuu wa Ujenzi na Dkt. Maria Sasabo - Katibu Mkuu wa Mawasiliano pamoja na *Engineer* Madete - Naibu Katibu Mkuu wa Mawasiliano kwa ushauri wanaonipatia katika kutenda majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Muhambwe ambao najua kabisa kwamba sasa hivi wanani-*miss,* lakini niwahakikishie kwamba niko nao katika majukumu yote ya Jimbo vilevile pamoja na kwamba siendi mara kwa mara. Naishukuru vilevile na familia yangu. *(Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, nitachangia kuhusu sekta ya mawasiliano pamoja na sekta ya uchukuzi kwa haraka haraka. Nimepata *concern* nyingi sana za Waheshimiwa Wabunge kuhusu masuala ya mawasiliano kwenye maeneo yao. Ni kweli kabisa kwamba takwimu za kiserikali zinaonesha kwamba nchi yetu tunawasiliana kwa asilimia 94, nitafafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema kwamba tunawasiliana kwa asilimia 94 ni kwamba karibu maeneo mengi sana ya nchi yetu yanapata mtandao wa mawasiliano

ya simu isipokuwa baadhi ya maeneo wanakuwa wako *selective* wanataka labda wapate na Vodacom, Tigo, Airtel pamoja na Halotel sasa Kiserikali hiyo hatuizuii ni kitu kizuri lakini sisi tunachosema kwamba eneo likipata huduma ya mawasiliano kama ni Halotel tunatia tiki kwamba hapo wanaweza wakawasiliana na kwa kweli katika hali ya kawaida kama kuna dharura yoyote wanaweza wakapata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unaitwa *UCSAF* ambao kazi yake kubwa unapeleka mawasiliano sehemu zile ambazo hakuna mvuto wa kibiashara. Tukumbuke siku za nyuma tulikuwa tunategemea sana hizi Kampuni za Simu kupeleka mawasiliano au minara sehemu ambazo wao wanaona kwamba zinafaa na zitawapatia faida katika majukumu yao ya kibiashara, lakini kutokana na hilo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kabisa kwamba tuunde Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ambao sehemu ambazo hazina mvuto wa kibiashara basi wale *UCSAF* wataweza kupeleka mawasiliano. Hii ndiyo kazi maalum kwa ajili ya kupeleka mawasiliano kwa Watanzania wote.

Kwa hiyo majuku yake makubwa kwanza ni kupeleka mawasiliano sehemu ambazo hakuna mvuto wa kibiashara na ambako hakuna kabisa mawasiliano na hilo jukumu limeendeelea kufanyika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tumegundua sehemu nyingi sana zimeshapelekewa minara hasa ya Halotel na hawa *UCSAF* wameingia mkataba na Halotel kwa ajili ya kupeleka mawasiliano sehemu hizo ambazo hakuna mvuto wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna maeneo ya mipakani, Wabunge wengi sana waliochangia hasa wanaokaa maeneo ya mipakani kama mimi wamezungumzia kwa kirefu sana kwamba kuna maeneo ambayo wakiingia mtandao unaosoma ni wa nchi jirani. Hilo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umeliona, lakini kwa kushirikiana na *TCRA* kuna mpango mkakati unafanywa kuhakikisha tunapeleka minara yenye nguvu lakini na

kuangalia masafa yanayozingatiwa ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata mawasiliano ya Tanzania na hao wengine wanaendelea kupata mawasiliano ambayo yanawahusu kwa nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile eneo la tatu ambalo linasumbua ni minara iliyopo sasa hivi kutokuwa na nguvu, ni kweli kabsia maeneo mengi ya nchi yetu baadhi hayajapata huduma za umeme na ndiyo maana kupitia mpango wa umeme wa vijijini Awamu ya Tatu *(REA III)* tuna uhakika kwamba matatizo yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kushirikiana na *TCRA* na *UCSAF* wameendelea kupeleka ujumbe kwa makampuni hayo ya simu yale ambayo yamepeleka *solar* waongeze nguvu ya hizo *solar energy* ili *at least* mawasiliano yaweze kupatikana masaa yote. Kwa sababu tumegundua kabisa ni kweli kwamba kama siku mvua imekuwa ikinyesha labda toka asubuhi mpaka mchana zile *solar* zinakuwa haziwezi ku-*charge* kwa sababu jua hakuna matokeo yake ikifika saa 12 jioni mawasiliano ya simu maeneo hayo yanakuwa hayapatikani.

Kwa hiyo, tumewashauri haya makampuni ya simu wamepele aidha, *generator* na hasa hasa wapeleke *generator* au waongeze nguvu ya zile *solar* kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tunaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo hayana mawasiliano yanapelekewa mawasiliano na hivi karibuni nimekuwa nikiongea na Wabunge na niliwaeleza waniletee tu maeneo ambayo wana uhakika kabisa hakuna mawasiliano ili kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote tuweze kuwapeleka minara waweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea kiasi kwa haraka haraka kuhusu *TCRA* na majukumu yake. Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameizungumzia sana

*TCRA* na ninashukuru sana kwa pongezi mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa kwa *TCRA,* kwa kweli tunazipokea na tunashukuru sana kwamba *TCRA* inaendelea kufanya kazi nzuri sana. Lakini niwakumbushe tu Wabunge kwamba pamoja na majukumu mbalimbali, *TCRA* vilevile inaendelea kuhakikisha tunadhibiti usalama wa mitandao yetu na tunasimamia masafa ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata faida kutojua na masafa ambayo ilipangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile, *TCRA* imeendelea kusimamia upatikanaji wa mapato stahiki ya Serikali kutokana na matumizi ya mawasiliano na hasa kwa kutumia ule mtambo wetu ambao tumeufunga wa *TTMS* ambapo kwa kupitia *TTMS* tunapata *telecommunication trafficking* yote ya ndani na ya nje kwamba mtu anapopiga simu kutoka nje na watu wanaopiga simu kutoka ndani tunaona wametumia dakika ngapi, wametumia shilingi ngapi kwa hiyo stahiki ya Serikali ni kiasi gani na stahii ya hayo makampuni y simu ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia hiyo nina uhakika kabisa *TCRA* wameendelea kuisaidia Seriakli na wananchi kwa ujumla lakini vievile wameendelea kuhakikisha kwamba wanapunguza matukio ya uhalifu kwenye mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kutokana na mtandao kukua sana tumekuwa na changamoto mbalimbali za matumizi mabaya mitandao yetu ambako hata viongozi wamekuwa wakitukanwa, sisi wenyewe Wabunge tumekuwa tukidhalilishwa hapa na pale, lakini kupitia *TCRA* wametengeneza muundo ambao tunaendelea kuwadhibiti hawa wahalifu wa mitandao na hasa wale ambao wanaleta lugha ambazo hazina maadili kwenye nchi yetu kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Jeshi la Polisi Kitengo cha *Cybercrime* kuhakikisha kwamba tunawadhibiti na matukio hayo kiasi fulani kwa kweli yamepungua na hata yanatokea mara nyingi tunao uwezo wa kuyafutailia na kuwakamata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kwa haraka haraka kuhusu *Data Centre,* tunacho kituo cha *Data Centre,* kuna baadhi ya Wabunge wameliongelea. Kituo hiki kinaendelea kutumika vizuri ambapo hadi sasa tunavyoongea taasisi za Serikali 41 tayari zinakitumia kituo hiki na taasisi 11 za binafsi na zenywe zinakitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kituo hiki ni kuhakiakisha kwamba matumizi yote yale yanayofanywa kwa *transaction*, wka mfano, unapohamisha pesa kutoka kampuni ya simu kwenda benki, benki kwenda kampuni ya simu au unapolipia *EWURA,* unapolipia *TANESCO* na mambo mbalimbali kuna tozo zile za Kiserikali ambazo zinatakiwa zirudi Serikalini. Kwa kutumia *Data Centre* ni rahisi sana kwa *TRA* kuweza kuona mapato hayo na kweza kuyadai kutoka kwenye taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu kwamba kituo kinafanya vizuri na ninatoa wito kwa Makapuni mbalimbali kuendelea kujiunga na *Data Centre* ili kujiridhisha na kuhakikishiwa kwamba wanapata pesa na *tender* nyingi kutoka Serikalini kwa sababu Serikali inahitaji kuona pesa inayoitoa ione matumizi yake lakini ipate stahiki kutokana na pesa inayoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kwa haraka haraka kuhusu sekta ya uchukuzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yetu, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Ninayo matangazo matatu na tangazo la kwanza linatoka kwa Mhesimiwa Shally Josepha Raymond ambaye ameandika wka niaba ya Katibu wa Jumuiya ya Thomas More (Bunge) anawatangazia kwamba leo siku ya Jumatano tarehe 25 Aprili, 2018 kutakuwa na ibada ya misa kwa wakristo wa madhehebu ya Kikatoliki mara baada ya kuahirisha Bunge saa 7:00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa Ghorofa ya Pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wengine wote wanaopenda kushiriki ibada hiyo mnakaribishwa.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Hamidu Bobali ambaye amesema yeye ni Katibu nadhani uongizi wa wapenzi wa Yanga Bungeni anawatangazia Waheshimiwa Wabunge naona mnashangilia kabla hamjasikia tangazo bado. Haya Katibu wa Wabunge anawatangazia wapenzi na mashabiki wa Yanga Bungeni kuwa Wabunge wafuatao wakutane bada ya kikao hiki cha Bunge na hii ni Kamati ya uongozi; Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Martha Mlata mnaombwa mkutane na Katibu kwa eneo ambalo ninyi mnalifahamu yeye anajua kwamba mtakutana mahali hapo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambaye anawatangazia kwamba leo kutakuwa na mkesha wa Muungano ambapo Papii Kocha na Baba yake na Bushoke watakuwa wanapiga muziki *Royal Village.* Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa huko na vimewekwa hapa viingilio; shilingi 30,000 *(VIP)* na shilingi 10,000 kawaida.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo yaliyotufikia mezani. Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, tuna mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ametembelea Bunge leo tarehe 25 Aprili 2018. Huyu ni Balozi wa Ufaransa nchini, Mheshimiwa Frédéric Clavier. Karibu sana Mheshimiwa Balozi, *bienvenue Udodoma. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia tena hapa leo kuendelea na kikao chetu hiki na mimi kupata fursa ya kuchangia au kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Spika wewe mwenyewe na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaoonesha katika kuliendesha Bunge letu. Nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa umakini wake kwa kusimamia shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nimshukuru sana au niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia hoja yangu niliyowasilisha hapa Bungeni kwa michango yao mizuri na yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingi zimetolewa na hii ni dalili ya dhati inayoonesha kwamba Waheshimiwa Wabunge wana maono makubwa kwenye kuendeleza Sekta hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili

sekta hizi ziweze kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, katika michango yao, imedhihirika wazi juu ya mahitaji makubwa ya miundombinu bora na ya kisasa kwenye huduma za usafiri wa anga, nchi kavu na majini ambazo ni muhimu sana kwa nchi yetu katika uchumi wa viwanda na uchumi wa kati ufikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imechangiwa na wachangiaji wengi ambapo wachangiaji 82 wamechangia kwa maandishi na 100 wamechangia kwa kuzungumza. Michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa mizuri sana na iliyosheheni mapendekezo, ushauri na busara namna bora ya kuendeleza sekta hizi za ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, siyo rahisi kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wote kwa kina na kutosheleza kwa muda huu mfupi nilionao ninaahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote majibu ya hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na Kamati ya Bunge ya Miundombinu umezingatiwa, hivyo napenda nitumie muda huu mfupi nilionao kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yangu itajikita kwenye sehemu tatu; kwanza, kwenye Sekta ya Anga, Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu halafu Sekta ya Usafiri wa Majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi kwenye kuchangia, Mheshimiwa Mlinga hapa amezungumzia kuhusu ujio wa ndege kubwa iliyokuja jana kwenye kiwanja cha Dar es Salaam, lakini yeye amezungumza Kibunge, mimi leo kwa sababu nasimamia sekta, nitazungumzia zaidi kiupande wa sekta ya anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kulikuwa na ndege ambayo ilikuwa inatoka Dubai kwenda Mauritius. Ni ndege

ya *Airbus 380 – 800,* ndege ambayo ilkuwa ni *Flight No. AK* 700 01E. Ndege hii baada ya kufika kwenye kisiwa cha Madagaska walipata taarifa kwamba hali ya hewa Mauritius ni mbaya. Kwa kawaida ukipata taarifa hiyo unakwenda kwenye uwanja wa ndege ulio karibu nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa marubani baada ya kupima viwanja vya ndege vyote vilivyopo karibu, ukiwa Madagascar kiwanja chake cha kwanza cha karibu inakuwa ni Madagascar wenyewe, cha pili pale ni Zimbabwe. Zimbabwe pale kuna Mozambique, vilevile kuna Namibia kuna *South Africa.* Baada ya kuangalia yote wakaamua waje watue kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege hii inachukua abiria 868, ni ndege kubwa duniani. Kwa jana ilikuwa na abiria 503. Ndege ile ilikuja Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam na ikatua vizuri na historia katika nchi yetu ama nchi nyingi za Afrika kutua *Airbus 380;* kwa niaba ya Serikali kwanza nawashukuru sana wafanyakazi wa kiwanja cha ndege cha *JNIA,* wafanyakazi wa *TCA* kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikuja bure, isipokuwa sasa ulimwengu unatambua kwamba viwanja vyetu vya ndege hasa vya kimataifa ina vigezo vya kisasa, vigezo bora na vigezo vya kimataifa. Vinginevyo kama ingekuwa hatuna vigezo hivyo, ndege ile isingekuja Dar es Salaam na wafanyakazi walifanya kazi kubwa kwa sababu kipindi cha saa saba mpaka saa 11 inakuwa ni *peak hours,* panajaa sana pale, lakini wafanyakazi wale walifanya vizuri, *immigration* ilifanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi hii nzuri, tuendelee kushirikiana ili tuhakikishe kwamba tunajenga sekta hizi kwa maslahi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye sekta moja kwa moja. Kama tunavyojua, mwaka 2017/2018 tulipata takribani abiria milioni 4,950 waliotumia usafiri wa anga. Usafiri wa anga ni muhimu sana kwanza kwenye sekta yenyewe ya anga, pili kwenye sekta ya biashara na tatu, sekta ya utalii. Sekta ya utalii kwenye usafiri wa anga ni muhimu sana. Ndege hizi zikija Tanzania zinachukua Watanzania, ama zinasafirisha Watanzania, lakini pia tunasafirisha watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii ni sekta ambayo inachangia sana kwenye pesa za kigeni na ni sekta ambayo inachangia sana ajira hapa Tanzania. Kwa vile ni dhamira ya Serikali na sekta yetu kuhakikisha kwamba tunatoa huduma kwenye usafiri wa anga, lakini wakati huo huo tunahakikisha kwamba sekta ya utalii tunaiboresha zaidi. Kwa kuangalia hivyo, kuna baadhi ya maeneo ya nchi yetu bado sekta ya utalii haijaendelea sana, kwa mfano, upande wa nyanda za juu, tuna mbuga nzuri za wanyama lakini watalii bado kule hawajawa wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kanda ya Magharibi kule, tuna *Game Reserve* nzuri sana. Kwa mfano tuna ile tunaita *BBK, Biharamulo Game Reserve,* tuna *Burigi Game Reserve,* tuna *Ibada Game Reserve* na nyinginezo, lakini bado watalii wengi wameshindwa kwenda kwa sababu kule hakuna viwanja vya ndege au barabara nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulijua hilo, sasa tumekuja na mpango mkakati ambapo kila kwenye maeneo haya ya uvutiaji wa utalii tutajenga kiwanja cha ndege, tutajenga barabara na ndiyo mmeona sasa mwaka huu tumepanga pesa kwa ajili ya kiwanja cha ndege cha Iringa pamoja na barabara yenyewe ya kutoka Iringa mpaka *Ruaha National Park,* tunaijenga kwa kiwango cha lami barabara yenye urefu wa kilometa 104. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tunajenga Kiwanja cha Geita ili kuhakikisha sasa tunatoa au tunakuza sekta ya utalii hasa kwenye Kanda ya Magharibi. Ili kuhakikisha

kwamba anga letu liko salama, Serikali kupitia *TCA* tumeamua kununua rada nne za kisasa kwa ajili ya ndege za abiria. Rada hizo zitagharimu takriban shilingi bilioni 67.3, rada hizo zitajengwa moja pale Dar es Salaam *JNIA;* ya pili, itajengwa Songwe; ya tatu, itajengwa *KIA;* na ya nne, itajengwa huko Mwanza. Hatukusimamia hapo tu kwa sababu kuna baadhi ya viwanja vya ndege sasa hivi ndege zimekuwa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar Kiwanja cha Abeid Amani Karume *traffic* imekuwa kubwa. Kwa kawaida ikishafikia hatua hiyo, tunaweka vifaa vya kisasa ambavyo tunaita *instrument landing system* kama alivyosema Mheshimiwa Zungu juzi, kwa vile Zanzibar tunajenga vifaa hivyo na tutatumia takribani shilingi bilioni 3.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia usalama wa anga yetu, tukiweka rada hizi tunazozizungumza, kwanza anga yetu kwa upande wa ndege za abiria itakuwa salama sana. Pili, kuna eneo kula ya Mashariki chini ya Pemba kule na Zanzibar, ndege zilizokuwa zinapita pale zilikuwa zinaangaliwa na anga ya Kenya. Sasa baada ya kuweka rada hizi, ndege zile tutakuwa tunaziangalia sisi wenyewe na kuziongoza sisi wenyewe na tutaweza kupata mapato yanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, kwenye viwanja vyetu huko kwenye madini na kwenye mbuga za wanyama, kuna *airport* ndogo ndogo nyingi. Sasa hivi hatuna uwezo wa kuziona, lakini baada ya kukamilika rada hizi nne, tutaweza kuona anga lote Tanzania na tutaweza kuangalia mali zetu inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kwa upande wa usalama wa anga, lakini unaweza kuwa na usalama wa anga huko mzuri lakini kama viwanja vyako haviko vizuri, hiyo siyo sahihi. Kwa kulijua hilo sasa, Serikali tumeamua kwanza kujenga jengo la abiria pale kwenye Uwanja wa Dar es Salaam, *JNIA,* jengo namba tatu ambalo lenyewe litakuwa

na uwezo wa kuchukua abiria milioni sita kwa mwaka. Jengo lenyewe litakuwa na uwezo wa kupaki ndege 21 kwa wakati mmoja, ndege aina ya *Airbus 320. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la abiria namba mbili tulililonalo sasa hivi lina uwezo wa kuchukua abiria milioni mbili tu na ndiyo ukienda Dar es Salaam kuanzia saa 7.00 mpaka saa 11.00, *peak hours* pale watu wamejaa; lakini mwisho wa mwaka huu, jengo la abiria namba tatu likikamilika, tunaamini tatizo hilo litaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mtwara tunataka kuifanya *hub* ya upande wa Kusini, tunapanua Uwanja wa Ndege wa Mtwara ambapo sasa ndege ya *Airbus 320* inaweza kutua. Gharama ya ujenzi huo itakuwa takribani shilingi bilioni 53.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazofanyika pale ni kutanua uwanja wa ndege na kuwa na urefu wa kilometa 2.8, kujenga jengo la kuegeshea ndege, kujenga vifaa vya kuongozea ndege, pia kujenga *parking* kwa ajili ya magari na barabara ya kuingilia kwenye kiwanja cha ndege. Hivi tunavyozungumza, mkandarasi wa kazi hiyo tumempata ambaye ni *Beijing Construction Engineering Group*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, nia ya Serikali kufanya kiwanja hiki kiwe kiwanja cha kimataifa sasa. Tunatanua Uwanja wa Ndege wa Mwanza na umefikia kilometa 3.5. Ndege kama iliyotua Dar es Salaam jana, ninaamini na Mwanza inaweza kutua yaani ndege ya *Airbus 380.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mwanza kazi zinazofanyika, tunajenga jengo la kuongozea ndege, tunajenga eneo la maegesho ya ndege, tunakarabati taa za kuongozea ndege na tunaongeza ndege kwa ajili ya ndege na kuengesha ndege za abiria, mwisho tutahakikisha kwamba tunajenga jengo la abiria. Kwa sababu huwezi kuwa na kiwanja cha ndege kizuri kama kile bila kuwa na jengo la abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea sasa hivi inagharimu takriban shilingi bilioni 85. Tuna kazi vile vile huko Sumbawanga, tunaongeza urefu wa Kiwanja cha Ndege Sumbawanga ambapo tunaongeza kiwe na urefu wa kilometa 1.75 ambapo gharama huko itatumia shilingi bilioni 55.6. Pale tunajenga jengo la abiria, tunajenga eneo la kugeuzia ndege au maegesho ya ndege. Pia tutajenga taa za kuongozea ndege na huko vilevile Mkandarasi tumeshampata. Kazi tunayofanya sasa hivi ni kulipa fidia kwa wananchi wale wanaostahili fidia kama sheria inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya kazi hiyo ya kujenga uwanja wa ndege Shinyanga ambao kazi inayofanyika ni kutanua uwanja wa ndege mpaka kufikia kilomita mbili na Mkandarasi yupo na pale tutajenga jengo la abiria. Vilevile gharama ya kiwanja hicho ni shilingi bilioni 49.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Songwe kazi inayoendelea sasa hivi ni kujenga jengo la abiria na gharama ni shilingi bilioni 11.5, lakini tunajua kilio cha muda mrefu cha watu wa huko Songwe ambao wanahitaji taa za kuongozea ndege, kwa vile sasa hivi tumempata mkandarasi ambaye atajenga taa ama ataweka taa kwenye kiwanja kile na taa hizo zitatumika kuongoza ndege saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi kama huo huko Musoma wa kuhakikisha na kiwanja cha Musoma sasa ndege yetu ya *Bombardier* inaweza kutua na Mkandarasi tayari tumeshampata, isipokuwa sasa hivi tuko kwenye mazungumzo na tunaamini kwamba hivi karibuni tutamaliza kuhakikisha kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kazi vilevile ya kujenga Kiwanja cha Ndege cha Iringa kama nilivyosema, kwa sababu nia ya Serikali sasa ni kuboresha utalii kwenye *Ruaha National Park* na tunajenga barabara kutoka Iringa mpaka huko kwenye *park* ambayo ina urefu wa kilometa 104. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uwanja wa ndege inandelea huko mkoa wa Geita na kama nilivyosema, nia kubwa ya Serikali ni kuhakiksha sasa tunaanzisha ule utalii kwenye Kanda ya Magharibi. Kama nilivyosema, kule kuna *game reserve* kubwa na utalii wa kule hasa sasa hivi ni utalii wa picha ambao ni utalii umechukua nguvu sasa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia viwanja vya ndege kwa ufupi, naomba nijikite kidogo kwenye Shirika la *Air Tanzania.* Nia ya Serikali kama nilivyosema huwezi ukawa na viwanja vya ndege, huwezi ukawa na anga lililokuwa salama kama huna shirika lako la ndege. Kwa kulijua hilo, Serikali imenunua ndege sita ambapo ndege tatu zimefika nchini na zinafanya kazi. Mwaka huu tunategemea vilevile ndege tatu ambazo zitawasili. Ndege ya kwanza ni *Boeing 787* yenye uwezo wa kuchukua abiria 262 ambapo ndege hii itakwenda masafa marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege nyingine mbili zenye uwezo wa kila moja kuchukua abiria 132 ni *Bombardier CSeries* 300 zitawasili ndege mbili hizi na tunaamini zitaanza kufanya kazi nzuri. Kwa kawaida huwezi kuwa na ndege moja ya masafa marefu na ikafanya kazi vizuri. Kwa vile kwenye bajeti hii tumeshapanga kununua ndege nyingine ya *Boeing 787* ili tuwe na ndege mbili. Kwa mfano, tukiamua tunaenda Guangzhou, ndege moja inatoka Guangzhou inakuja Dar es Salaam na nyingine zinapishana, inatoka Dar es Salaam inaenda Guangzhou. Hivyo ndivyo utaratibu unavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika letu la ndege limeanza kufanya kazi na linafanya kazi vizuri. Hivi tunavyozungumza, Shirika letu la Ndege linakwenda Dar es Salaam, hapa Dodoma na Wabunge wengi mnapanda ndege ya shirika letu la ndege, ni jambo zuri sana. Tabora, Kigoma, Mwanza, Bukoba, Kilimanjro, Zanzibar, Songwe na huko Hayahaya, Comoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tutaanza safari za kwenda Mpanda, Tanga, Entebe huko Uganda na

Bujumbura, Burundi. Kuanzia mwaka 2017 Shirikala la *Air Tanzania* Julai mpaka Machi, 2018 tumeweza kusafirisha abiria 150,518 ikilinganishwa na mwaka 2017 kwa kipindi kama hicho ambacho tulisafirisha abiria 104,207. Hili ni ongezeko la asilimia 46. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa na kuongezeka kwa mapato ghafi ambayo tumeongeza kutoka shilingi bilioni 34.4 mpaka shilingi bilioni 43.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja hapa Wabunge wengi walipiga kelele kwamba Shirika la *Air Tanzania* halina *business plan.* Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla *Air Tanzania* tunazo *business plan* ndiyo hizi hapa tunazotumia. Naomba mhakikishe kwamba tunakwenda kwa mipango na tunayo *business plan. Business plan* siyo msahafu, kila baada ya muda lazima ibadilishwe, kwa vile tutaendelea kuboresha *business plan* yetu hii kutokana na mahitaji ya soko na mahitaji ya Watanzania na wateja wetuwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja moja ilitokea juzi hapa; je, kwa nini *ATCL* isikodi ndege *(leasing)?* Kwa nini tunanunua ndege mpya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kununua ndege mpya ni rahisi kama ndege hizo zinakuwa zinatumika kwa muda mrefu. Kampuni nyingi za ndege kwa mfano *Kenya Airways, RwandAir, Ethiopia Airways, Emirates,* zote zinanunua ndege mpya. Wana-*lease* ndege ama wanakodi ndege tu kwa sababu maalum ya msingi. Kama imetokea *route* mpya wanataka kwenda, ndiyo wananunua ndege mpya, lakini kawaida, wana-*lease.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukinunua ndege mpya unapata faida kubwa kwa sababu *discount* ni kubwa. Hii inakupa faida kwenye uendeshaji wako wa ndege yako kwa sababu ndege mpya gharama zake za matengenezo ni ndogo ukilinganisha na ndege iliyozeeka. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge hili tulielewe.

Waheshimiwa Wabunge, nitatoa mfano mmoja, nita-*compare* ku-*lease* ndege na kununua ndege mpya na nitaangalia mfano kama nitakodi ndege ya *Bombardier Q400* na nitaangalia ndege mpya ita-*cost* kiasi gani? Kuna njia mbili za kukodi ndege. Aina ya kwanza tunaita *dry lease,* maana yake unakodi ndege bila marubani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njia ya pili tunaita *wet lease.* Ukichukua *wet Lease* maana yake unakodi ndege pamoja na marubani. Kitaalam, njia rahisi ya kukodi ndege ni *dry lease* ambapo unakodi ndege yako bila ya marubani, bila wahudumu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya wastani ya kukodi ndege kwa mwezi ni dola 200,000 mpaka 250,000 hiyo ya kwanza; ya pili, gharama ya matengenezo kwa mwezi, dola za Kimarekani 18,000. Kuna *withholding tax* ya *TRA,* ukikodi ndege unatakiwa ulipe dola 25,000 kwa mwezi. Jumla kwa mwezi mmoja unatakiwa angalau uwe na dola 300,000 ukikodi ndege. Kwa mwaka unatakiwa uwe na dola milioni tatu na nusu ukikodi ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua na bima unatakiwa uwe na dola milioni nne kwa mwaka mmoja. Sasa ndege za *Air Tanzania* kipindi chake cha kuishi *(life cycle)* ni miaka 35. Sasa kwa muda wa miaka 35 huo, ukiendelea kukodi ndege utatumia takriban dola milioni 140, lakini sisi tunanunua ndege moja ambayo *list price* yake ni kama dola milioni 35. *List price* nasema, ile *price* ambayo iko kwenye mtandao. Kwa vile kukodi ndege ni rahisi kuliko kununua; samahani kukodi ndege ni gharama kubwa kuliko kununua, ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tena, kukodi ndege ni gharama kubwa kuliko kununua kwa sababu gani? Narejea, kwa sababu ndege moja ya *Air Tanzania* ambayo tumenunua itaishi miaka 35. Ukikodi kwa muda huo utatumia dola za Kimarekani milioni 140, wakati ukinunua ndege mpya itakuwa gharama yako ni dola milioni 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa dola milioni 35 umenunua, dola milioni 140 umekodi, ipi faida? Mnataka Serikali iende wapi? Ikanunue au ikakodi? Waheshimiwa Wabunge, ninyi ndiyo mnawakilisha Watanzania, mnataka tukanunue au tukakodi ndege? Watanzania wametusikia na majibu wanayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitazungumzia *wet lease* kwa sababu bei yake ni mbaya zaidi. Nitazungumzia hiyo tu, nafikiri hiyo hapo imetosha, tuendelee mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida mashirika yanakodi ndege tu kama kuna matumizi ya muda mrefu kama nilivyosema. Kama leo imetokea *route* kwa mfano Dar es Salaam – Bombay na hatuna ndege, pale ndiyo unakodi ndege, lakini wakati huo huo unaagiza ndege yako. Ndivyo yanavyofanya mashirika ya ndege yote. Huwezi kwenda kukodi ndege kama unataka kutumia ndege muda mrefu. Kama nilivyosema Rwanda wana ndege nane, zote wamenunua. Sasa sisi tutafanya nini? Lazima tununue ndege na ndege kununua ni rahisi kuliko kukodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, niwaulize ninyi ni mashahidi, mmeshakuwa Bungeni huu ni mwaka wa saba sasa. Kila Mbunge akianza kuja Bungeni anafikiria kununua nyumba. Kwa nini hamfikirii kukodi nyumba kule mnakotoka? Kwa sababu kukodi nyumba ni bei ghai kuliko kununua. Ukizungumza kununua na kukodi huwezi ukalinganisha hata siku moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, hili jambo liko hivyo, Serikali tumefanya maamuzi sahihi ya kununua ndege na tutaendele akufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine wanasema kwa nini tunanunua ndege kutoka makampuni mbalimbali? Hali hii itasababisha kuwa na gharama nyingi za matengenezo. Tukinunua ndege, tunaangalia ndege ambayo italeta faida kwa Shirika la Ndege, italeta faida kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vigezo maalum vinatumika katika kununua ndege. Kigezo cha kwanza, unaangalia hiyo ndege yako inakwenda wapi? Yaani *runway,* kiwanja chako cha ndege kina urefu gani? Huwezi kwa mfano, leo unataka kwenda pengine Kiwanja cha Ndege cha Tabora ukasema upeleke *jet engine,* haiwezekani! Kile kiwanja kimetengenezwa kwa urefu wa kilometa 1.8, ni ndege ya *turbo propeller engine* ndiyo itakayokwenda tu, hiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha pili, unanunua ndege kutokana na hali ya hewa ya eneo lako. Hiyo ni muhimu sana na *temperature* ya kiwanja cha ndege, ndege yako inakokwenda. Eneo la tatu unaloliangalia ni mwinuko wa kiwanja cha ndege kule unakokwenda. Watu wengi tunakuwa na historia, tunapata simu au tunaambiwa kwamba *Fastjet* leo imekwenda Songwe na imeacha abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi hawajui kwa sababu gani inaacha abiria? Kiwanja cha Ndege cha Songwe kile wakati mwingine hali ya hewa inabadilika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Fastjet* haina uwezo wa kuchukua mzigo ule na abiria wale kwa wakati ule, ndiyo unakuta baadhi ya abiria wanaachwa na baadhi ya mizigo inaachwa. Ni kwa sababu kiwanja cha ndege kile wakati mwingine hasa mchana hivi hakiwezi kuchukua ndege ya *Fastjet* na mzigo wote. Kwa hiyo, ukichagua ndege yako lazima hiyo uiweke kwenye akili vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu unaangalia ndege yako, je, ndege hiyo inataka kwenda sekta gani? Kwa mfano, kama unataka kwenda Mumbai – India, inabidi utafute ndege ambayo itakupa faida kwa kwenda Mumbai. Huwezi kuchukua ndege ambayo ukienda Mumbai unapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunanunua ndege kutokana na kule tunakokwenda. Mfano mzuri, ni *Ethiopian Airlines today.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri leo *Ethiopian Airways,* ni shirika kubwa lakini wana *Airbus, Boeing* na *Bombardier.* Wana ndege zote hizi. Wakija Dar es Salaam wale wanaosafiri na Ethiopian *Airways,* usiku inakuja *Bombardier* hapa. Kwa sababu wanaona *need* ya kuja Dar es Salaam au mahitaji ya Dar es Salaam ni *Bombardier,* siyo ndege nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kununua ndege tu kama unavyonunua njugu za aina moja, hapana. Unanunua ndege kutokana na soko lako na mahitaji. Hiyo ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tuelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalofanya sisi Serikali au wanalofanya *Air Tanzania* ni jambo sahihi na hatukurupuki tu. Tunatumia utaalam wa kutosha na tunafanya maamuzi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mifano mizuri, *Kenya Airways* wana *Airbus, Boeing, Embria* halafu wana *Fokker 50,* kwa sababu huwezi kununua ndege za aina moja. Unanunua ndege kutokana na mahitaji na sekta kuhakikisha kwamba unapata faida. *Otherwise,* ukinunua ndege za aina moja, unataka *Airbus,* utafanya nini? Bukoba haiwezi kwenda *Airbus* kwa sababu *Airbus* hawana ndege ya *propeller.* Pemba, Tanga haiwezi kwenda *Airbus.* Tutawafanya nini Watanzania hawa sasa? Hatuendi hivyo bwana! Au Pemba naambiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja je, tumepata taarifa kuwa *ATCL* imeondolewa kwenye *IATA* kwa sababu ya madeni?

Waheshimiwa Wabunge, *ATCL* kweli iliondolewa kwenye *IATA* lakini siyo leo, ni mwaka 2008. Kazi tunayofanya sasa hivi Serikali ni kuirudisha *ATCL* kwenye *IATA* ambayo itawezesha kufanya *booking* popote pale duniani. Tunategemea kabla ya mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumeingia kwenye mfumo, kwa sababu Serikali imejipanga

na ninaamini Waheshimiwa Wabunge mtapitisha bajeti yetu tuhakikishe kwamba tunaingia kwenye mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kuna hoja nyingine inasema, Taarifa ya Ukaguzi wa *CAG* juu ya *ATCL* haijawasilishwa Bungeni ili ichambuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika jitihada zake za kufufua *ATCL* ilibaini kuwa hesabu za *ATCL* zilikuwa hazijakaguliwa toka mwaka 2007 mpaka 2015. Kazi tuliyoifanya Serikali ilimuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kufanya ukaguzi wa hesabu ya *ATCL* kuanzia mwaka 2007/2008 mpaka 2014/2015. Kazi hiyo imekamilika na ripoti imepelekwa kwenye Bodi ya *ATCL.* Kazi inayoendelea sasa hivi ni kufanya ukaguzi wa mwaka 2015/2016 na 2016/2017. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba *ATCL* inasimama. Lazima tuhakikishe kila senti tunayoingiza kwenye *ATCL* inatumika vizuri. Tukiweka shilingi tano tuhakikishe kwamba shilingi tano inatumika kwa maslahi ya *ATCL* na Watanzania. Kwa hiyo, naomba niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali tumejipanga na tutalisimamia jambo hili vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwenye sekta ya anga naomba niingie kidogo nizungumzie kwenye sekta ya usafiri wa nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano tunajenga reli ya kisasa ya kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es Salaam – Makutupora – Tabora – Isaka – Mwanza; Tabora – Kigoma; Tabora – Mpanda. Hiyo ndiyo *central line* ambayo ninaijua na Serikali tunaijua hiyo na tunaifanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, tumeanza Dar es Salaam – Morogoro kilometa 300; Morogoro - Makutupora kilometa 422. Tunajenga treni ambayo katika nchi zetu hizi za *East Africa* ndiyo treni ya kwanza kwa sababu treni hii itakuwa inatembea na umeme, itakuwa na uwezo wa kwenda *speed* ya kilometa 160 kwa saa. Maana yake nini?

Ni kwamba unatoka Dar es Salaam leo mpaka Dodoma kwa masaa yako mawili na nusu au matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zote za jirani, ukienda Kenya wanajenga treni yenye *speed* ya 120, ukienda Ethiopia 120; *speed* kama hii unaiona *South Africa* kwenye *Gautrain speed* 160 lakini wana kilometa 80 tu wao pale mjini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumejipanga na gharama ya ujenzi huu kutoka Dar es Salaam mpaka Makutupora ni shilingi trilioni 7.016. Pesa ipo na wakandarasi wanafanya kazi. Awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro itamalizika mwezi Novemba mwakani. Awamu ya Pili itamalizika mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na msukumo wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga reli ya kati na matawi yake yote kama nilivyosema. Tabora kwa upande wa Tabora – Kigoma tayari sasa hivi tunamalizia upembuzi yakinifu ambao unafanywa na kampuni ya *COY* kutoka Denmark. Tunahakikisha kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Hatuwezi kuanza ujenzi bila ya kuwa na *feasibility study. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa upande wa Tabora – Kigoma upembuzi wa kina, sehemu utakamilika mwezi Juni, 2018, miezi miwili inayokuja. Baada ya hapo ndiyo tutaanza kujipanga kuweza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Huwezi kuanza ujenzi kama huna *feasibility study.* Utajua shilingi ngapi? Si utakwenda kupigwa tu? Waheshimiwa Wabunge, tumejipanga na tutaifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna reli ya Dar es Salaam – Isaka – Rusumo – Kigali ambapo tunaanzia Isaka – Rusumo – Kigali kilometa 572. Reli hii imegawanyika sehemu mbili. Kuna Isaka – Rusumo ambapo Serikali ya Tanzania itajenga na Rusumo - Kigali Serikali ya Rwanda itajenga. Reli hii ina faida kubwa sana kwa sababu itahudumia mzigo wa Kigali

yenyewe, pia itahudumia mzigo wa Congo Kaskazini ambayo ni maeneo ya Goma na Bukavu.

Mhesimiwa Naibu Spika, kutoka Dar es Salaam leo mpaka Kigali ni masaa au ni kilometa 1,491. Kwa mwendo wa *standard gauge* au kwa kutumia *standard gauge* utatumia masaa 15, lakini mzigo ukitoka Mombasa, Malaba ambao unaenda Uganda mpaka Kigali ni kilometa 1,792 utatumia masaa 24 hasa ukiangalia reli ya Kenya ya mzigo ni kilometa 80 kwa saa. Sasa itakuwa jambo la kichekesho kwamba mtu wa Rwanda ambaye ana mzigo wake kutoka Dar es Salaam mpaka Kigali ambaye anaweza kutumia masaa kama 15 aende akapitie Mombasa ambako atatumia masaa 24, hiyo kwa biashara haiingii akilini hata siku moja. Mfanyabiashara yeyote anahakikisha kwamba anatumia njia fupi kusafirisha mzigo wake ambayo itampatia faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimesema tutapata mzigo wa Congo hasa kule sehemu ya Kaskazini? Ni kwa sababu kutoka Kigali mpaka Bukavu ni kilometa 225 na barabara iko nzuri sana unaenda masaa matatu umefika, kwa vile mzigo ukitoka Dar es Salaam mpaka Bukavu utatumia masaa 18. Mzigo huo huo ukitoka Mombasa mpaka Bukavu utatumia masaa 27 kwa reli ya Kenya. Mfanyabiashara wa Congo *especially* eneo la Kaskazini hataweza kutumia reli ya Kenya, atatumia reli ya Tanzania kwa sababu ndiyo njia rahisi. Hii hata huhitaji tochi wala huitaji *rocket science,* ni *simple, one plus one* inakupa mbili. Wala haina mjadala hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi Rwanda wanatumia Bandari ya Dar es Salaam na kuna zaidi ya tani milioni 1.1, asilimia 98 ya mzigo huu unapita barabarani, lakini unatumia bandari ya Dar es Salaam. Kule Bukavu Kongo kule kuna mzigo tani 772,000. Sasa ukichukua maeneo haya mawili, Rwanda na Kaskazini Kongo kuna takriban tani milioni mbili za mzigo ambazo zitapita Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, hii reli tunayoijenga itafika kwenye machimbo ya *Nickel* kule Kabanga ambapo kwenye machimbo yale kuna tani milioni 36.3, inahitaji reli hii inayotoka Dar es Salaam ikapita Isaka, Isaka ikaenda Rusumo, Rusumo - Kigali. Kabla hujafika Rusumo, unachepuka unakwenda Kabanga kwenye machimbo. Kwa hiyo, *plan* ya Serikali ni hiyo lakini wakati huo reli ya kati tunaijenga, hasa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, hii ya Kigoma nataka nayo niizungumze kidogo. Kutoka Kigoma tukijenga *standard gauge* mpaka Dar es Salaam, utatumia masaa kumi. Ni karibu Kigoma, lakini kutoka Kigoma mpaka Kalemie ni kilometa kama 120 kuvuka lile ziwa pale, lakini kwa meli ya mzigo utatumia masaa matano. Hii ni uzoevu kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka Pemba kwenda Zanzibar ni *distance* hii tu, lakini kwa meli ya mizigo unatumia masaa manne au matano, wale mashahidi si ndio; kwa meli ya mzigo siyo meli ya abiria. Ukienda ukishusha na kupakia mzigo wako utatumia kama masaa manane kupakia na kuteremsha mzigo. Halafu kutoka Kigoma au Kalemie unaenda Lubumbashi kwa sababu mzigo mkubwa pale uko kwenye Kasanga kule, sehemu ya kule Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Kigoma mpaka Lubumbashi ni kilometa 664 na bahati mbaya sana reli ya pale imekufa. Hii ya Tanzania ni nzuri kuliko ya pale, inaenda kilometa 25 kwa saa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mzigo ukipitia njia ya kule utachukua karibu masaa 41. Kule kuna tani milioni tatu sasa hivi ambapo Tanzania sisi tunapata tani 764,000. Mzigo mwingine unaenda Afrika Kusini, mzigo mwingine unaenda Durban, mwingine unaenda Namibia na mwingine unaenda Angola.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyosema, mahesabu siyo tatizo, tuko tayari kujenga reli ya kutoka Tabora mpaka

Kigoma. Tunalosubiri ni hiyo *feasibility study* ifanyike ili tujue mahesabu kiasi gani, tuanze kutafuta fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maoni kwamba Serikali tujenge reli kwa kutumia mfumo wa *PPP*. Ni kweli Serikali tunapenda sana mfumo wa *PPP*, ni mfumo mzuri, lakini katika historia ya ujenzi wa reli katika Afrika, hasa reli za *standard gauge* haijawahi kujengwa kwa kutumia mfumo wa *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wamechukua mkopo kutoka China; Ethiopia wamechukua mkopo kutoka China; Nigeria wanajenga *standard gauge,* wamechukua mkopo kutoka China; Morocco wamechukua mkopo na wao kutoka mabenki na Serikali. Kwenye miradi mikubwa kama hii, siyo rahisi kupata *PPP* kama watu wanavyofikiria. Serikali tuko tayari kushirikiana na mtu yeyote yule tuweze kufanya *PPP* lakini siyo rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee sekta ya bandari, usafiri wa nchi kavu. Bandari yetu inafanya kazi vizuri, mzigo umeongezeka. Kama nilivyosema, kutoka mwezi Julai, 2017 mpaka mwezi Machi, 2018 tumesafirisha takriban tani milioni 9.822 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la asilimia 14.6. Mizigo ya nchi za jirani mwaka huu tumesafirisha mizigo tani milioni 3.9 ikilinganishwa na tani milioni 3.1 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapato mwaka 2017 kuanzia mwezi Julai mpaka mwezi Desemba bandari wameweza kupata mapato ya shilingi bilioni 14.79 wakati matumizi yamekuwa shilingi bilioni 139, salio takriban shilingi bilioni 280. Kwa kipindi kama hicho mwaka uliopita kulikuwa na salio la shilingi bilioni 83 tu. Kwa vile bandari inafanya kazi vizuri na naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu tuendelee kui-*support* Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo miradi mingi sasa hivi tunatekeleza Bandari ya Dar es Salaam tukianzia pale

Dar es Salaam penyewe. Kwanza sasa hivi tunafanya ukarabati na kuongeza kina cha maji kutoka Gati Namba Moja mpaka Namba Saba. Vilevile tunajenga gati maalum sasa kwa ajili ya kupakilia na kupakulia magari ambapo kasi inaenda vizuri. Hivi karibuni tutaanza kutekeleza mradi mwingine kwa ajili ya kujenga eneo la kugeuzia meli na kuongeza gango la Bandari ya Dar es Salaam. Mradi unaoendelea hivi sasa unagharimu takriban shilingi za Kitanzania shilingi bilioni 377.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kazi tunaendelea nayo huko Mtwara, tunajenga gati jipya watu wa Mtwara wanajua. Gati hilo lina urefu wa mita 300 na tutatumia takriban shilingi bilioni 137 kwa kazi ile. Kasi inaenda vizuri na tunategemea kazi itamalizika vizuri. Tuna kazi huko Lindi tunajenga gati la Lindi na limefiki asilimia 70. Tuna kazi huko Kigoma tunajenga Bandari za Kigoma tatu; Kigoma wenyewe, Ujiji na Tiberizi, zote tunazijenga. Tumetenga pesa bajeti ya mwaka huu na kazi nzuri inaendelea. Tuna kazi hivyo hivyo huko Mwanza inaendelea kuboresha gati yetu ya Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usafiri wa majini, tunajenga meli mpya sasa huko Ziwa Tanganyika yenye uwezo wa kuchukua abiria 600 na tani za mzigo tani 400. Tunafanya kazi hiyo hiyo huko *Lake Victoria* ambapo tunajenga meli ya kuchukua abiria 1,200 na itachukua mzigo wa tani 200 na magari 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya kazi kama hiyo huko *Lake Nyasa*, tunajenga meli ya kuchukua abiria 200 halafu na tani 200 za mzigo. Vilevile tunafanya ukarabati wa MV. Liemba, MV. Victoria na Meli nyingine zote tunazifanyia ukarabati tuhakikishe kwamba sasa hivi zinafanya vizuri. *(Makofi)*

Mhshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuboresha usafiri wa majini tunataka kujenga kivuko kwa ajili ya ndugu zetu wa huko Nyamisati na Mafia. Tayari tumetenga kwenye bajeti hii shilingi bilioni tatu kwa kujenga *landing craft* mpya ambayo itatumika kwa watu wa Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo maelezo machache kuhusu usafiri wa majini. Naomba nizungumzie kidogo kuhusu usafiri wa nchi kavu. Tokea juzi kulikuwa na mazungumzo mengi hapa kuhusu *TARURA* na maoni ya Waheshimiwa Wabunge tumeyapokea, tunaheshimu na tutayafanyia kazi. Naomba nitoe maelezo kidogo na ninyi mpate picha ya Mfuko wa Barabara unafanya kazi vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Fedha za Barabara kwa kawaida unagharamia miradi ya barabara kuu na barabara za mikoa ambazo zinasimamiwa *TANROADS* halafu barabara za Wilaya ambazo zinasimamiwa na *TARURA.* Inatoa fedha kwenye *TARURA* na *TANROADS* huku asilimia nafikiri 70 huku 30. Vilevile kuna vigezo maalum vinatumika katika kutoa pesa. Kigezo cha kwanza tunachotumia, tunaangalia urefu wa mtandao wa barabara; kigezo cha pili, tunaangalia je, barabara hizo ni za lami, changarawe au udongo? Kigezo cha tatu tunachoangalia, tunatumia hali ya barabara yenyewe ikoje *(conditions)?* Kigezo cha nne, tunatumia wastani wa idadi ya magari na uzito wa magari yanayopita kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROARD* au mtandao wa barabara unaosimamiwa na *TANROAD* una jumla kilometa 36,257.97. Kati ya kilometa hizo, kilometa 9,264.57 ni za lami, kilometa 25,303.4 ni za changarawe na kilometa 1,690 ni za udongo. Mtandao wa barabara unaosimamiwa na *TARURA* una jumla ya kilomita 108,946.19. Kati ya kilometa hizo, kilomita 1,449.55 ndizo za lami ukilinganisha na *TANROADS* wenye kilometa 9,000 za mahitaji kwa kutengeneza au matengenezo ya barabara ya *TANROADS* ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* vilevile inahudumia kilometa 24,405 za changarawe pamoja na kilometa 85,091.24 za udongo. Kwa vile ukilinganisha tu mtandao *TANROADS* wanasimamia barabara kubwa sana za lami kuliko *TARURA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara za lami ni gharama zaidi kuliko matengenezo aina nyingine ya barabara. *TANROADS* yenye kilometa 9,264 za lami inahitaji fedha nyingi kuliko *TARURA* yenye urefu wa kilometa 1,449.55 za lami kwa sasa. Aidha, upana wa barabara zinazosimamiwa na *TANROADS* ni mita 8.5 mpaka mita 9.5. Upana wa barabara unaosimamiwa na *TARURA* ni mita 4.5 mpaka mita 6.0. Hii inafanya *TANROADS* ihitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya magari yanayotumia barabara kila siku, barabara kuu za mikoa idadi ya magari ni kati ya 300 mpaka 52,000. Ukichukua barabara ya *New Bagamoyo Road* ndiyo hayo. Wakati barabara za Wilaya nyingine ni kati ya magari matano mpaka 50 kwa siku. Kwa hiyo, wingi wa magari husababisha barabara kuharibika zaidi na kuhitaji zaidi fedha za matengenezo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzito wa magari yanayopita katika barabara zinazotumika na *TANROADS* ni tani 55 wakati barabara za Wilaya zote ni tani 10. Uzito wa magari husababisha barabara kuharibika haraka kwa vile barabara inayosimamiwa na *TANROADS* zinahitaji pesa nyingi. Tumetoa ushauri ambao tunasema, tumejaribu kuangalia ushauri wa kuongeza tozo la mafuta kuangalia kama tutapata pesa zaidi kwa ajili ya *TARURA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunasema tutafute vianzo vipya ikiwa ni pamoja na tozo ya maegesho ya magari mjini, ukaguzi wa magari, tozo ya magari mazito, tozo ya barabara na tozo ya matumizi ya barabara kulingana na uzito na umbali wa magari. Hivi ndiyo baadhi ya vyanzo vyote ambavyo tunapendekeza tuone jinsi gani tutaweza kuongeza pesa za *TANROADS* na pesa kwa ajili ya kukarabati barabara za *TARURA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema leo asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri, tunazo barabara nyingi tunazijenga kwa kiwango cha lami hivi sasa. Barabara tunazojenga kwa kiwango cha lami ambazo nyingi

zinaunganisha mikoa na mikoa kwa mfano sasa hivi tunajenga barabara kutoka Sumbawanga – Matai – Kasanga Port yenye urefu wa kilometa 112; tunajenga barabara ya Ushirombo - Lusahunga yenye urefu wa kilometa 110; barabara kutoka Kidatu - Ifakara yenye urefu wa kilometa 65; barabara kutoka Tabora - Sikonge yenye urefu kilometa 30; tunajenga barabara kutoka Usesula - Komanga yenye urefu wa kilometa 115.5; barabara kutoka Komanga mpaka Kasinde yenye urefu wa kilometa 112.8; barabara ya kutoka Kasinde - Mpanda kilometa 111.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunajenga barabara inayotoka Mara kwenda Arusha - Makutano - Sanzate kilometa 50; barabara kutoka Waso mpaka *Sare Junction* kilometa 50; barabara ambayo inatoka Mpanda mpaka kuelekea huko Kigoma ambayo tumeanzia kwanza Mpanda - Vikonge kilometa 35; barabara kutoka Kisole - Bulamba kilometa 50, barabara kutoka Maswa - Bariadi kilometa 49.5; barabara kutoka Kidahwe - Kasulu kilometa 63; barabara kutoka Nyakanazi - Kakonko kilometa 50; barabara kutoka Nduta – Kibondo - Kabingo inayojumuisha barabara ya kupita Kibondo Mjini kilometa 87.7 na tunajenga barabara ya Uvinza - Malagarasi yenye kilometa 51.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara vilevile itaanza maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara kutoka Tanga mpaka Pangani yenye urefu wa kilometa 50; huko Geita- *Bulyanhulu Junction* kilometa 58.3; barabara kutoka *Bulyanhulu Junction* mpaka Kahama kilometa 61.7; tunatayarisha ujenzi wa barabara kutoka Kazilambwa mpaka Chagu kilometa 42; tuna mpango wa kujenga barabara ya kutoka Ludewa – Kilosa kilometa 24; tuna mpango wa kujenga barabara kutoka Norangi – Itigi - Mkiwa kilometa 56.9; na tunajenga barabara kutoka Lusaunga - Lusaumo kilometa 91.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna mpango wa kujenga barabara ya Kibaoni - Stalike kilometa 71; tuna mpango wa kujenga barabara kutoka Vikonge - Mangunga mpaka Uvinza kilometa 159; tunafanya upanuzi wa barabara

ya kwenda Kiwanja cha Ndege Mwanza na tuna mpango wa kujenga barabara ya kutoka Nyangunge mpaka Simiyu - Mara - Boda yenye urefu wa kilometa 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingi siwezi kuitaja yote, lakini tuna kazi kubwa tunahakikisha kwamba mikoa yote ya Tanzania tunaifungua ili kuhakikisha Watanzania wanapata miundombinu hii ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyojua pia tunajenga huko Dar es Salaam *TAZARA flyover* ambayo tutatumia takribani shilingi bilioni 99. Tunajenga *Ubungo interchanges* ambayo tunatumia takriban shilingi bilioni 177; tunajenga daraja huko Momba, tunajenga daraja huko Magara, Sibiti, Lukuledi, Wami Juu, Simiyu, Sukuma mkoani Mwanza na daraja la Salenda Dar es Salaam; tunafanya *feasibility study* kwa ajili ya daraja la Mtera, Kigogo Busisi na Malagarasi Chini huko Kigoma.

Mheshimiwa naibu Spika, tuna miradi mingi sana ya barabara ambayo yote mnaweza kuiona kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mawasiliano muhimu sana kwa nchi yetu. Sekta ya mawasiliano ndiyo uchumi wa nchi yetu, ni maendeleo na ndiyo maisha ya Watanzania. Bila mawasiliano kwa kweli maisha kidogo yanaweza kuleta shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Desemba, 2017 tulikuwa na wateja wa simu takribani milioni 50; watumiaji wa *internet* takriban milioni 23. Watanzania ambao wanatuma pesa kwenye mitandao mbalimbali takribani kuna akaunti milioni 22. Pesa zilizotumwa kwenye mtandao mwaka 2017 ni takriban shilingi trilioni 104.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama nilivyosema, sekta ya mawasiliano ni muhimu sana na ni sekta ambayo inapeleka uchumi wetu kwenye hali ya juu. Kwa upande wa mawsiliano vijijini kama Naibu Waziri alivyosema

leo, kwa kipindi tulichopita tumejenga Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umepeleka mawasiliano kwenye Kata 551, vijijini 1,954.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWSILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeleka mawasiliano vijijini pamoja na makampuni yote takribani vijiji 5,751. Mwaka 2018/2019 utakuwa ni mwaka ambao utaleta maendeleo makubwa kwenye sekta ya mawasiliano. Naomba tu Watanzania waitumie miundombinu hii kwa maslahi ya maendeleo, wasiitumie mindombinu ya mawasiliano kwa kupeleka *message* za uchochezi, kupeleka picha chafu na kufanya ulaghai na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 68

### Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Kif. 1001 – *Admin. & HR Management*........Sh. 1,478,784,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ukurasa wa 412, hiki ndicho kifungu chenye mshahara wa Waziri. Kwa mujibu wa kanuni zetu nimeshaletewa hapa majina kutoka kwenye vyama, lakini majina yameletwa zaidi ya yale yanayohitajika hapa. Kwa hiyo, nitasoma jina lililoandikwa namba moja. Kwa sababu majina yamezidi, yameletwa mawili mawili, wakati ni ni jina moja tu linalohitajika.

Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sote tunafahamu kuwa sera na utaratibu wa mchakato wa kutengeneza bajeti ya Serikali unaanzia ngazi ya Serikali za Mitaa, kwa maana ya vijiji, kwenye kata, Wilaya, kwenye *Road Board* kwenda Serikalini na hatimaye hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana nami kwamba Waheshimiwa Wabunge nao ni Wajumbe muhimu katika kuwakilisha vikao vya Bodi ya Barabara, kuhakikisha hasa wanashiriki kikamilifu kuhakikisha barabara hasa zinazounganisha mkoa na mkoa zinafanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa iko baadhi ya mikoa ambayo utaratibu huu haukufuatwa na Wabunge hawakushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti imekuja katika Wizara hii, hususani za barabara, inaonekana bajeti hii baadhi ya mikoa Wabunge hawakushirikishwa ipasavyo na nilitaka kufahamu, je, bajeti hizi tunazopitisha hasa za barabara zitakuwa ni halali endapo Wabunge hawakushiriki kikamilifu kwenye baadhi ya mikoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikao ya maandalizi ya bajeti, kuna vile

vikao ambavyo viko kwa mujibu wa sheria ambavyo ni lazima vifanyike, lakini pia kuna vikao ambavyo ni vya kiushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kikao kama *RCC* ambacho kinazingatiwa ni pale ambapo kupitia kwenye Halmashauri zetu Madiwani wameshirikishwa, wakapitisha, inapokuja ngazi ya mkoa kinachofanywa ni *combination* ya yale yote ambayo yamefanywa kupitia kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote ambayo nayasema yalifanyika. Kwa hiyo, bajeti inapokuja hapa ni *combination* ya kwenye Halmashauri zetu. Ndiyo maana kwa mfano, hicho ambacho Mheshimiwa Mbunge anaongelea kwa Mkoa wake wa Morogoro, hatua zote zilifuatwa na vikao vyote vya ushauri vilifanyika isipokuwa ambacho alikosa nafasi ni kikao cha *RCC* ambacho kile ni kikao kwa ajili ya ushauri, lakini hakifanyi maamuzi ambayo yalishafanywa kwenye vikao vilivyotangulia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kutoa shilingi katika mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja, ulipaswa kuwa umesema mwanzo. Sasa hivi unaomba ufafanuzi wa ziada, shilingi huwezi kushika tena kwa mujibu wa taratibu zetu. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Waziri Mkoa wa Morogoro haukushiriki kikamilifu katika kuandaa bajeti hii, hatukukaa kikao chochote kuanzia ngazi zote anazozieleza. Kwa msikitiko makubwa, katika Kikao cha Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro aliidanganya Kamati kuwa *RCC* imekaa, *Road Board* imekaa, vitu ambavyo siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kujua, ni nini *commitment* ya Serikali kwa Wakuu wa Mikoa wa namna hii ambao hawafuati taratibu ambazo zinatakiwa kupaswa katika kuhakikisha kwamba wanatengeneza bajeti na badala yake wanaleta bajeti zao za mifukoni ambazo tumekuja kuzionea hapa Bungeni, ambapo vipaumbele vingine kwa sisi Wabunge havikuwa na nafasi katika baadhi ya barabara ambazo ni korofi za Mkoa wa Morogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha baadhi ya barabara ikiwemo ya Manispaa ya Morogoro ambayo fedha zake zimepigwa kisawasawa, tunataka kupata...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja, kwa maelezo uliyoyatoa sasa yameondoka kwenye ile hoja ya kuwa maswali ya hapa ni ya kisera. Kwa sababu hiyo na kwa sababu ulishaonesha tangu mwanzo kwamba huna mpango wa kushika shilingi, tutaendelea. Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi nilikuwa nataka ufafanuzi kwa Serikali. Wavamizi au wanaotumia ile *road reserve* ni watu wengi, lakini mara nyingi tumekuwa tukiona Serikali ikiwaondoa wananchi ambao wamejenga kwenye zile *road reserve,* lakini wakati huo huo ziko taasisi za Serikali ambazo na zenyewe zina miundombinu yake ndani ya *road reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano utakuta watu wa *TANESCO* wameweka miundombinu yao kwenye *road reserve,* watu wa *DAWASCO* wana miundombinu yao kwenye *road reserve,* watu wa *TTCL* wameweka miundombinu yao kwenye *road reserve,* lakini hawa huwa hawaondolewi *on time.* Matokeo yake tunapokwenda kwenye ujenzi, ujenzi unachelewa kuanza kwa sababu hawa wanakuwa bado hawajaondoa ile miundombinu yao kwenye maeneo ambayo barabara zinataka kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo ya Serikali, ni kwa namna gani wamejipanga safari hii kwamba

watakapokuwa wanasafisha zile *road reserve* na hizi taasisi nyingine za Serikali ambazo zina miundombinu yao pia wanaondoa wakati ule ule. Sasa kama sijaridhika na majibu ya Serikali ninakusudia kushika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sheria Namba 13 ya mwaka 2007 inaainisha bayana matumizi ya *road reserve* na imekuwa tu ni kawaida kwamba kumekuwa na matumizi mengine ambayo ndiyo yanasababisha hata tukasema kuna wavamizi. Kwa hiyo, hawa aliowataja Mheshimiwa Mbunge, *TANESCO* na *TTCL,* kwa mujibu wa ile sheria inawapasa kuomba leseni ya matumizi ya muda kwenye hizo *road reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Wizara tutaendelea kutoa mafunzo ili wananchi kwa ujumla waweze kuelewa kwamba matumizi ya *road reserve* ziko taratibu zake, zikifuatwa basi haiwezi kutuletea shida. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayoyazungumza hayo yanaeleweka, lakini kwenye utekelezaji hali haiko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwa mfano hapa mmeleta bajeti mnataka kujenga *Morogoro Road* kuipanua mpaka Chalinze, lakini mmeondoa nyumba zilizokuwa pembezoni, bomba la *DAWASCO* bado limepita pale na huwezi kuanza ujenzi bila kulitoa lile bomba. Itakuja hapa bajeti ya Wizara ya Maji, hutaona fedha yoyote kwa ajili ya kuondoa lile bomba. Maana yake mnachotaka kukijenga hakitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dar es Salaam tuna miradi ya *DMDP,* barabara ya kupita Chang'ombe Maduka

Mawili, tumeshindwa kuanza ujenzi kwa sababu *TTCL* hawataki kuondoa mitambo yao pale, zile *fibre optics* ambazo ziko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kwamba hawana bajeti ya kuondoa, nasi tayari tumeshampa mkandarasi aanze kujenga. Mkandarasi anashindwa kuanza kazi kwa sababu kuna mindombinu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mchicha na yenyewe iko ndani ya *DMDP.* Mkandarasi yuko *site,* hawa *TAZARA* hawataki kuhamisha taa, wamezijenga sehemu ambayo sisi tunataka tupitishe barabara. Wanataka sisi ama tuhamishe barabara tuipeleke sehemu nyingine, tukalipe fidia kwa wananchi, tuzikwepe taa mbili tu. Sasa haya ndani ya Serikali moja taasisi hii inakuwa na mpango huu, taasisi hii inapingana nayo, hatuwezi kwenda namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, kwa sababu naamini haya hayatokei tu Dar es Salaam, yanatokea na kwenu huko pia. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja ili tuweze kujadili tuilekeze Serikali cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa. Wachangiaji sasa Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI. Tuanze na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mtolea na lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba hivi vikwazo

vilivyopo ambavyo vinasababishwa na Wizara ya Ujenzi, viwe vinaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni mali ya wananchi wote. Kama ilivyo, ndiyo *business centre* ya wote na sisi wote tunaishi pale. Hizo barabara alizozisema Mheshimiwa Mtolea, kwa mfano, Barabara ya Mchicha, sisi wengine tumekuwa tukipita mara kwa mara pale. Tunaona kwamba ule ujenzi pale unashindwa kuendelea, tulikuwa hatuelewi, kumbe kikwazo ni hiki alichokisema Mheshimiwa Mtolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ilivyo Dar es Salaam inahitaji hizi *ring roads* ziwe za kutosha kuondoa msongamano wa magari barabarani, lakini pia lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba wananchi wanasafiri kwa haraka kwenda kwenye maeneo yao ya kazi.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aji-*commit, a*fanye *commitment* ya kutosha kuona kwamba hoja iliyokuwepo mezani, hivi vikwazo vilivyopo vya mataa na nini vinaondoka, badala ya miradi ya *DMDP* kuwa yenyewe inajigharamia, ninyi ondoeni kwa sababu hii yote ni Serikali na Serikali ni moja, inakuwaje mnakwamishana ninyi wenyewe kwa wenyewe? Kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa ni hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali na wewe una hoja yako ama unaunga mkono hoja ya mwenye hoja sasa? *(Kicheko)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nitangulize kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mtolea, kwa namna ambavyo Serikali moja na hususan kupitia Wizara ambayo leo inahitimisha hoja yake,

imekuwa ikifanya mambo kwa aina fulani ya *double standard.*

Mheshimiwa Mheshimiwa Mtolea amesema kwamba wananchi wanavunjiwa, lakini kuna taasisi za Serikali ambazo utaratibu unachelewa na kuchelewesha hata *tender* ambazo zimeshatangazwa. Sasa hii tofauti ambayo imekuwa ikitokea na ikifanywa ndani ya Serikali moja, imeonekana sana na hususan kwenye awamu hii. Mfano rahisi tu kuonesha ni namna gani kumekuwa na namna mbili kwenye Serikali moja, katika kuunga mkono hoja yake, watu wa Kimara wamevunjiwa nyumba zao Dar es Salaam na watu wa maeneo mengine kwenye nchi hii wamevunjiwa nyumba zao; Arusha tumevunjiwa nyumba zetu; lakini Rais alikwenda Mwanza, mahali ambapo wananchi wame-*encroach* kwenye *airport* akasema hao wasivunjiwe kwa sababu ndio walionipa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linaleta hisia mbaya kwa wananchi; suala hili linazuia miradi ya maendeleo kama alivyosema Mheshimiwa Mtolea; suala hili linafanya wananchi wanaanza kuhisi kwamba kwa namna moja ama nyingine wanakuwa *treated* kwa sababu ya maeneo walipo au ukanda wao, lakini vilevile ni tishio kwa demokrasia kwa sababu sehemu ambapo inaonekana Rais wa CCM hakupata kura, wananchi hao wanastahili kuvunjiwa, lakini maeneo kama Mwanza ambako anahisi alipata kura, anaona ni sahihi wananchi kutokuvunjiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile maeneo ambayo siko anakotokea Rais ama viongozi wengi wanaoonekana, yanaonekana kuwa *treated* tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mtolea kwamba, Serikali hebu iweke *commitment* basi kwamba, haita...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mtapewa nafasi ya ufafanuzi. Kwa hiyo, acha amalize ya kwake, utamjibu wakati huo. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa sababu, huyo ni Naibu Waziri, anayo fursa ya kutoa majibu upande wa Serikali, aniache Mbunge nimalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mtolea, Serikali iweke *commitment* kwamba haya mambo ambayo yamekuwa ya kubagua watu, haya mambo ambayo ni ya Serikali kuwa na *double standard* kwenye matendo yake kwamba, ni kutoka sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Umeshagongewa kengele Mheshimiwa. Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nipingane na kauli yake inayojaribu kuwachonganisha wananchi kwamba wananchi wa Mwanza walifikiriwa kwa sababu wao ndio peke yao walimpa kura Mheshimiwa Rais. Kwa sababu hata Chama cha CHADEMA kilipata kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kumekuwa na hali hiyo kwamba wananchi wakati mwingine wamekuwa wakijenga bila kufuata taratibu. Kuna baadhi ya huduma huwezi kuzifanyia kazi bila kuhakikisha kwamba vipimo sahihi vimewekwa pale. Kwa mfano, katika ujenzi wa *line* ya umeme kilovoti 11,000 ni lazima uwe na mita 1.5 kutoka kati, lakini vilevile kadiri ya umeme unavyokwenda juu, halikadhalika kwenye maji. Sasa kwenye mazingira kama hayo, Serikali inapotaka kufanya vitu vyake kwa viwango, lazima ifuate taratibu ambazo zinahusika kisheria, lakini vilevile kwa mujibu wa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, naomba tu kwamba huwezi kuendelea tena kujenga kwa kuharibu kama ambavyo unafikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuunge mkono na kama kuna taasisi inayohusika inahitaji kujenga, ina wajibu wa kuhakikisha kwamba inalipa hiyo fidia ili kuweza kutoa hiyo *way leave.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kupingana na Mheshimiwa Mtolea kwa sababu kwanza amekuwa *too general* na wakati *project* inategemea ni *project* ipi, inajengwa kwenda wapi na gharama zipi ambazo kwenye *project* zinakuwa *involved*. Kwa mfano, yeye ni shuhuda kuna mradi umefanyika kule Temeke, wananchi wa Temeke ambao walikuwa katika maeneo ambayo wako *supposed* kuwa *compensated* kabla hata hatujaanza ujenzi tunahakikisha kuwa wamekuwa *compensated* wameridhika ndiyo mradi unasonga mbele. Sasa uki-*generalize* ukasema kwamba kuna ambao wamekuwa hawatendewi haki tukumbushane. Mradi wa kwenda Morogoro hata majengo ya Serikali, *TANESCO* ni jengo la Serikali pale ilibidi libomolewe kwa sababu sheria ni msumeno.

Kwa hiyo, namuomba kwa heshima zote arudishe tu shilingi ya Mheshimiwa Waziri na kwa sababu anajua mipango mizuri ambayo inaenda kwake hana sababu ya kukwamisha shilingi airudishe ili tuweze kusonga mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angeline Mabula. Tusikilizane Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mabula endelea kwa sababu hawataki kusikiliza.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Naomba nitoe ufafanuzi kwa suala alililoliongea Mheshimiwa Joshua Nassari kuhusiana na Mheshimiwa Rais kuwa kuwa *double standard* kwamba kuna maeneo mengine anavunja na mengine anaachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa, alitoa maelekezo alisema nyumba zile zisivunjwe mpaka pale ambapo Wizara zinazohusika zitakapoweza kukaa. Kwa hiyo, kazi hiyo imekwishafanyika na Wizara zinazohusika ilikuwa ni Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara ya Uchukuzi. Kwa hiyo, hakuzuia kuvunja bali alisema taratibu zifuatwe na zizingatiwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tunasimamia sheria na sheria huwezi kubagua. Tulipokuwa tumevunja *Morogoro Road* tumevunjia nyumba za wananchi na pale tukaenda kuvunja jumba la *TANESCO* na Wizara ya Maji. Palepale kulikuwa na miundombinu mingi ya Serikali. Tulikuwa na *high tension cable* tunapojenga *Ubungo Interchange* kuna *high tension cable* ya umeme, tuna bomba kubwa la gesi, tuna bomba kubwa la maji na tuna nguzo za simu, tuna *fibre* ya simu vyote vile tumeondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Mbunge tunataka kukuhakikishia kama pahala amejenga *TTCL*, kama amejenga Vodacom, kama amejenga yeyote kama tunataka kujenga, tunasimamia sheria lazima waondoke. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja Mheshimiwa Abdallah.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninasikitika sana baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri wametoka kwenye hoja ya msingi wameenda kumjibu

Mheshimiwa Nassari. Hoja iliyokuwa mezani ni hoja yangu hii ya kuhamisha miundombinu ya taasisi za Serikali. Hoja hii nimeileta ni kukusaidia wewe Mheshimiwa Waziri kwa sababu miradi hii inakwama na inakwama kwa sababu hizo. Nimekupa mfano wa hizo barabara mbili, ile barabara ya Maduka Mawili - Chang'ombe majengo yalishalipwa fidia kweupe lakini *fibre optics* imepita chini ya ardhi, wa kuondoa ile miundombinu ni *TTCL* ambao ni wamiliki wa hiyo na hiyo sheria unayoisema ndiyo inataka wafanye hivyo, lakini wao wanasema hawana bajeti sasa wanafanyaje. Tukawaambia tuwasaidie, wanaleta bajeti ambayo ni ya kuyafanyia mabadiliko mfumo wao mzima, hatuna hela hizo, maana yake sasa mradi unasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo mkandarasi tulishaingia naye mkataba aanze kazi toka Januari, yeye anahesabu siku mradi haujaanza mwisho wa siku ule mradi utachukua muda mrefu, mkandarasi ataanza ku-*charge interest* na wewe haya mambo unayafahamu.Sasa nilitegemea uniunge mkono ili tukusaidie miradi hii uliyoiweka hapo ukatekeleze lakini na wewe hautaki. Sasa kama wewe hautaki na mimi nakuachia hivyo hivyo nakurudishia hiyo shilingi yako uende kwenye miradi ambayo hautoitekeleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea. Waheshimiwa Wabunge ili twende vizuri nitoe maelezo kidogo Mheshimiwa Mbunge anayetaka kushika shilingi anaposimama mara ya kwanza lazima aoneshe nia kama alivyosema Mheshimiwa Mtolea. Jambo la pili, anaposimama mara ya pili nikimwita hatoi tena maelezo aliyoyatoa mwanzo anapaswa aseme sijaridhika na maelezo aliyotoa Waziri nashika shilingi niungwe mkono ndiyo inavyokuwa. Kwa hiyo, tukifanya utaratibu huu maana yake Mbunge anachangia mara tatu na kanuni zetu haisemi hivyo. Mara ya pili Mbunge unasimama unasema sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, naomba niungwe mkono nashika shilingi. Kwa hiyo, Wabunge wanasimama wanakuunga mkono, unapewa tena nafasi ya maelezo marefu mwishoni. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu ulioko hapa kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ili twende vizuri uwiano wa humu ndani wachangiaji wa hoja wanakuwa sita. Wachangiaji wanne CCM, mchangiaji mmoja CHADEMA, mmoja CUF. Kwa hiyo, kama Waheshimiwa Wabunge tunataka kumwachia Mbunge ambaye hoja imetoka mahali ambapo tutanataka ndiyo yeye aseme wengine wote tusisimame maana sasa mimi nitachagua yeyote, kwa sababu ndiyo mamlaka niliyonayo ya kuchagua yeyote. Ili tusilalamikiane mkubaliane huko. Kama ni jambo la Ruaha muachieni Msigwa, kama ni jambo la Kilimanjaro mwachieni anayehusika ili tusilalamikiane.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Mimi kama Mheshimiwa Waziri hatoniridhisha nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyoko mbele yetu ni kwamba Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imesema *categorically* kwamba tunajenga reli ya *standard gauge* Dar es Salaam - Tabora; Tabora - Mwanza; Tabora - Kigoma; Kaliua - Mpanda - Kalemi; Uvinza-Msongati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona wanachoki-*implement* Serikali sasa ni mawazo yaliyobuniwa na *ADB* chini ya mtu anaitwa Kaberuka ambaye alitengeneza *plan* ya *northern route* kutoka Mombasa kwenda Kigali na kutoka Dar es Salaam - Isaka, Kigali ili kuifanya Kigali kuwa *the hub* ya kusafirisha mizigo. Naliona kosa hili linafanywa na Serikali yangu na mimi naomba kwa heshima kabisa, Waziri ame-*mislead* wakati anafanya jumuisho ndani ya Bunge hili. Amesema na ame-*qualify statement* yangu ya asubuhi kwamba tuna-*turn* Rwanda kuwa *the hub* ya nchi ya DRC na Burundi. Mizigo ya Bukavu na maeneo hayo ili iweze kusafirishwa kupitia Rwanda ni lazima mizigo ile ijengewe bandari kavu Rwanda. *And this is going to happen!* Nashindwa kuelewa kwa nini wataalam hawalioni, lakini inaeleweka kabisa *our cash cow* siyo Bukavu; *our cash cow*

ni *Eastern and Western part of Congo*, *our cash cow* ni maeneo ya Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika Waziri anasema haijafanyika *feasibility study* ya kutoka Tabora kwenda Kigoma. *Feasibility study* ya Isaka kwenda Rwanda imefanyika lini ni ile ya *ADB* iliyofanywa na Kaberuka ambaye ndiye *consultant* wa mradi. *This is unfair to our country*, *it is unfair to our party* ninashauri...

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari acha amalize mwenye hoja yake kama ambavyo nilimkatalia Waziri ni vilevile. Mheshimiwa Bashe endelea.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka niseme hatuna fedha ya kutoka Makutopora kwenda Tabora; tunaweka fedha ya Isaka kwenda Rwanda. Tutasafirisha kwa *SGR* mpaka Makutupora halafu tutabeba kwa *helicopter? How come!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizigo yote duniani kinacho-*determine* mizigo siyo *difference* ya *nine hours*, kinacho-*determine* ni *cost per unit* na *incentive* watakayopata lazima tufahamu tuta-*compete* na Bandari ya Mombasa kwa *zone* hii. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, *hundred bilioni* ya Isaka aiondoe airudishe kwa Makutupora na Morogoro, *this is where we need to put money,* tukamilishe *phase one* na *phase two* 2020, ninaomba kwa heshima kabisa *it is not health for our party it is not health for our country*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi au Naibu Waziri, nitoe maelezo kidogo tu ili tusiingie kwenye mambo ambayo yatatupa taabu kidiplomasia, watu wanatajwa majina humu ambao hawana fursa ya kuzungumza pia nchi zinatajwa kwa namna ambayo itatuweka vibaya.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge nawasihi sana, mjadala kuhusu Rwanda humu ndani saa hizi sitauruhusu. Kwa hiyo, kipande kitajwe kile ambacho tunacho sisi upande wetu wa nchi kwa sababu huko Rwanda hatuendi kujenga sisi. Hayo ndiyo maelekezo niliyowapa kwa sasa. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majumuisho yangu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa usizungumze na mimi, ukitaka kuzungumza na mimi omba ruhusa. Kila Mbunge akitaka kuzungumza na mimi nina masikio mangapi? Nasema hivi usizungumze na mimi kwa utaratibu huo kwa sababu kila mtu akizungumza na mimi hivyo tutajibizana mpaka saa ngapi tafadhali, tafadhali.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumza na wewe. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye majumuisho sasa hivi tunamalizia *feasibility study* ya kutoka Tabora - Kigoma hilo la kwanza. Pili, kama nilivyoongea tunaenda Rwanda halafu tutapata mzigo wa kule.

**MBUNGE FULANI:** Tutaharibu diplomasia, asitaje Rwanda huyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Lucy Magereli punguza sauti yako kidogo.

Mheshimiwa Waziri ukisema tunaenda Rwanda ndiyo

tunajenga Rwanda, maana maelezo uliyotoa ni kwamba tunaishia mahali kwa hiyo ishia pale tunakoishia sisi kwa sababu ndiyo bajeti yetu tunazungumzia hapo, kule kwingine wanaendelea wao wenyewe. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa sawa.

**MWENYEKITI:** Eeh.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Hussein Bashe kwamba biashara hakupenda kwamba nii-*qualify* kwa *distance* alivyosema yeye, lakini mimi nitai-*qualify* sasa kwa *value cost,* ukichukua kontena moja kutoka Dar es Salaam pengine naweza kutaja Kigali Mheshimiwa, mpaka Kigali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataja kilometa.

**MBUNGE FULANI:** Taja nchi jirani, taja nchi jirani.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisafirisha mzigo kutoka Dar es Salaam mpaka eneo ambalo lina kilomita 1,417

**MBUNGE FULANI:** Sema nchi jirani.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Dar es Salaam mpaka eneo ambalo lina kilometa 1,417 tunatumia dola 4,200 na tukisafirisha mzigo huo huo kutoka Mombasa mpaka eneo lenye urefu... *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane vizuri. Ukizungumza humu ndani ikiwa unamzungumzia mtu kwa jambo jema sisi wote ni watu wazima humu ndani

hakuna mtu ataona jambo hilo ni baya ama amezungumzwa na Bunge la Tanzania kwa namna fulani. Lakini ukizungumza kana kwamba huyo mtu atatakiwa aje ajieleze hapa hapana siyo sawa.

Kwa hiyo, tuelewane Waheshimiwa Wabunge vizuri. Namna Mheshimiwa Hussein Bashe alivyokuwa anazungumza ni kana kwamba hapa Mrwanda akikaa anatusikiliza yeye ataonaje na sisi tuko *East Africa*. Kwa hiyo, hapana lazima tutofautishe mambo haya na sisi lazima tufuate utaratibu uliopo. Hivyo vitu ni vitu tofauti na kwa hivyo tuvione hivyo. Huwezi kusema wewe mtu aliyezunguziwa vema atakuja alete malalamiko na yule aliyezungumziwa vibaya ataleta malalamiko hapana, si sawasawa. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima sipewi utaratibu mimi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajuaje kama nakupa wewe? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naomba ukae Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Halima Mdee wewe ni mwanasheria, mwanafunzi wangu mimi. Sasa kwa ajili ya wale ambao wanakuamini sana wakijua ni mwanasheria na sasa unaonesha kutokujua hizi kanuni ambazo umekaa sana humu Bungeni nitawasomea Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 5 (4) inasema hivi, muwe mnasikiliza ili muelewe nisirudie siku nyingine, mimi nilikuwa mwalimu, kwa hiyo, muwe mnasikiliza; "Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake..." *Shut up* Msigwa!

"...sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika." Kwa hiyo, mimi sipewi utaratibu hapa ndani, unaandika malalamiko yako kule ambako Kanuni hii imekuelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala hili lina sehemu mbili kama nilivyosema kwenye majumuisho yangu kwamba tunasubiri *feasibility study* kutoka kipande cha Kigoma au kutoka Tabora mpaka Kigoma kwa ajili ya ujenzi. Sasa hivi hatuwezi kusema tunajenga kwa kiasi gani kwa sababu hatuwezi kufanya hivyo mpaka tupate *feasibility study* ambayo itatupa mwelekeo kujua mradi huo uta-*cost* shilingi ngapi hili la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuhusu alivyosema Mheshimiwa Bashe kwamba nime-*mislead* kwa sababu nimetumia kilometa. Kutumia urefu wa kilomita ni sahihi kwa sababu ukitumia urefu wa kilometa ndiyo utakupa kujua kiasi gani umetumia lakini nabadilisha hiyo nakwenda sasa kutumia kwa kontena. Kuchukua kontena moja sasa hivi kutoka Dar es Salaam mpaka Kigali ama nchi jirani, *I don't care,* nikisema nchi jirani sawa tunatumia dola 4,200. Kontena hiyo kutoka Mombasa mpaka nchi jirani hivyo mnavyotaka niseme tunatumia dola 4,700 bado ni *expensive* kutumia njia ya kule kuliko njia ya huku.

Sasa vyovyote kwa mfanyabiashara ambaye ana akili timamu, mfanyabiashara ambaye anataka kutafuta faida hatoweza kupitia njia ile, naomba Mheshimiwa Hussein Bashe, wewe tunazungumza sana na hizi hesabu zipo na tunazungumza kwa hesabu kila dakika naamini tu tutakaa pamoja tutalizungumza jambo hili tutaelewana vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

nitaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tujadili kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ukishasema hivyo unaomba kuungwa mkono hutoi tena maelezo nadhani nimeshatoa maelekezo hapo.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungwa mkono na natoa hoja.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Wachangiaji Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa John Heche, Mheshimiwa Bashe wewe ukae ni mtoa hoja. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa George Simbachawene.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Gashaza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kwa uwiano ninayo tayari majina yote hapa kwa hiyo hakuna haja ya kuendelea kutaja huko. Tutaanza na Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hussein Bashe kwa misingi ifuatayo; ukitaka kufanya mradi wowote ule tangu unapoanza wazo *(idea/concept)* mpaka *formalization* lazima uwe na mpango wote, kwa lugha nyingine mpango mkakati wa *project* nzima. Hapa tunazungumzia Bandari ya Dar es Salaam na tunazungumzia reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tunawekeza fedha nyingi sana hasa na Bunge ndiyo linaloisimamia na kuishauri Serikali, ingekuwa ni vema kwenye mradi huu ili kuondoa utata wote unaojitokeza na sisi tuna washindani

wetu ambao ni Mombasa, Lamu na kwingineko, na *strategically* tuko vizuri. Serikali kwa hoja ya Mheshimiwa Bashe haioni tukafanya utaratibu wa maslahi ya humu ndani kwanza na hasa kwenye mizigo kwa sababu, *project* hii ni mizigo wala siyo abiria ndiyo *return* yenyewe itakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe hoja yake ni ya msingi badala ya kupeleka fedha kwenye kutengeneza *hub* (bandari kavu) kule Rwanda, tujihakikishe kwamba tunawekeza humu ndani kwanza kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam ambalo ndiyo langu kuu la uchumi katika nchi hii, reli ya kati hii iweze ikakamilika vizuri na tukawa na mawazo yanayofanana sote kwa sababu *project* hii tunakubaliana sote badala ya kufanya vipande vipande huku na huku. Kwa hiyo, niwaombe kabisa *idea* hii ni nzuri, wazo hili ni zuri, sote tunaliunga mkono lakini kwa maslahi mapana ya Tanzania kwanza, kabla ya maslahi mapana ya wengine. Kwa kuwa tuko kwenye *region* hii na tunajua tuna washindani wenzetu ndani ya *East Africa* sasa nyumbani kwanza tuhakikishe kwamba mradi mzima huu unawekwa wazi, unajulikana ili tukisimama tusimame kwa lugha za kitaalam, tusimame kwa lugha zinazofanana kwa maslahi mapana ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi namuunga mkono Mheshimiwa Bashe hoja yake kwa manufaa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa hesabu za darasa la pili mzigo unaokwenda Rwanda na Burundi ni asilimia 12 peke yake na mzigo unaokwenda Congo ni asilimia 36. Sasa kwa hesabu za kawaida tu za mtu ambaye anajua hata ukipiga wingi kwamba utatoa hata shilingi moja moja mwenye asilimia 36 atapata zaidi kuliko mwenye asilimia 12 na hizo ni nchi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa jamaa wamefanikiwa kutu-*manipulate,* wameleta watu wao wajanja hapa, wanataka kuhamisha uchumi wa nchi yetu wanapeleka kujenga nchi yao, na bahati mbaya suala hili inagharimu pesa nyingi sana za nchi hii. Kama ulimsikiliza jana Rais anasema amekwishatoa trilioni saba kwenye ujenzi wa *SGR*, tayari amekwishatoa alichosema. Hata ukija kwenye kitabu hiki ukurasa wa 170 pesa ambazo zimeombwa hapa ni trilioni 1.5 bado kuna mkanganyiko mkubwa kweli. Kipi sahihi alichosema Rais au tulichoandikiwa hapa? Haya ni maswali ambayo lazima tujiulize kwa sababu ina-*involve* pesa nyingi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bashe hili suala tulijadili vizuri kwa manufaa ya nchi hii na tusiende kunufaisha watu huko na inaleta *doubt* nyingi sana kwa nini tunakimbilia huko Rwanda ambako mzigo wake ni mdogo sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche hayo maneno ya mwisho ndiyo yaliyoleta taabu tangu mwanzo. Ndiyo hivyo Waheshimiwa lazima tuheshimu diplomasia ndiyo utaratibu huo.

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hussein Bashe kwa misingi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo Kamati ya Miundombinu, hili jambo kwenye Kamati tulilijadili sana na hoja ilikuwa hivi, reli hii ijengwe kwanza kipande cha Tabora - Kigoma. Waziri huyu na timu yake wakaja na hoja kwamba hapana kwa takwimu kwamba mzigo mkubwa uko Uganda. Kwa ku-*justify* reli ile itoke Tabora iende Mwanza, tukasema kwa takwimu hizi walikuwa na watu wa bandari tukasema hiyo ni kitu chema. Namba ya pili mzigo mwingine mkubwa uko DRC lakini uki-*combine* mzigo wa DRC na mzigo wa

Burundi unakuwa mkubwa kuliko mzigo ulioko Uganda. Sasa tukaogopa tusianze kugombana wenyewe kwa wenyewe tukasema *okay* sawa bwana, tuanze kipande cha kutoka Tabora twende Mwanza, halafu awamu inayofuata tutoke Tabora twende Kigoma. Sasa leo kinachonishangaza hizi bilioni 100 hata mimi nakubaliana na Mheshimiwa Hussein Bashe kwamba aah, kwa akili ya kawaida tuziweke basi Makutupora kwenda Tabora, kabla ya sekta ile ya kutoka Isaka kwenda nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine yale maeneo sisi wenyewe tumezaliwa maeneo ya Kigoma, tunaijua jiografia vizuri. *Cash cow* mtaji kwa *economics of geography* na *study* iliyofanywa na watu wa *TRC*, faida ya reli hii ni mzigo unaotoka DRC na viunga vyake kwa maana ya *South East*. Maana ukija Kalemi yake na Moba yake unachukua na mzigo wa Lubumbashi au upite Karema au unakuja bandari ya Kigoma ili reli hiyo iwe na faida, ndiyo hoja ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono mia kwa mia hizi bilioni 100 Waziri huna sababu ya msingi, kwa nini zianze kipande kile kwenda nchi jirani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Nsanzugwanko muda wako umekwisha. *Microphone* yako imezimwa Mheshimiwa, kwa hiyo muda wako umekwisha. Muda wako umekwisha. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia.

*(Hapa Mhe. Daniel Nsanzugwanko aliendelea kuongea wakati kipaza sauti kikiwa kimezimwa)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli hii ni kuondoa msongamano ulioko katika Bandari ya Dar es Salaam, kitu

ambacho Mheshimiwa Waziri anajua kwamba *feasibility study* ambayo alitakiwa afanye ni kuangalia huo mzigo tunaouondoa katika bandari ya Dar es Salaam, mzigo mkubwa unaenda nchi gani. Kwa hiyo, akishajua miongoni mwa hao majirani zetu mzigo mkubwa unaenda wapi basi kipaumbele chetu reli tupeleke kwa jirani ambaye anatupa mzigo mkubwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, aliyewasha *microphone* eneo lake aizime ndiyo maana Mbunge kule anashindwa kuwasha *microphone* inawaka kijani, yeyote ambaye *microphone* yake imewaka aizime tafadhali.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi naunga mkono hoja ya Serikali kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *historical context* ambayo ningependa ku-*share* na Bunge letu tukufu ambayo inafanya niunge mkono hoja ya Serikali. Mimi kabla ya kuwa Mbunge nilishiriki *feasibility study* ya *Kabanga Nickel* na moja ya sababu kubwa mradi wa *Kabanga Nickel* umeshindwa kufanyika yaani *investment* ni kwa sababu ya *infrastructure* ya reli haijafika kwenye *mining*. Kwa hiyo, bila hata reli kwenda kwenye nchi za jirani ukiangalia *mine deposit* ya *nickel* pale Ngara, Mkoa wa Kagera ni kubwa sana inaongoza Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya *deposit* ya *nickel* ambayo iko pale Kabanga ina-*justify* ile *volume* ya *nickel* kupeleka reli mpaka Ngara na ukishafika pale kwa sababu uwekezaji wa hii reli ni mkubwa sana, lazima yaani kuwe na *volume* ya kutosha ku-*justify investment*. Sasa ukishafika pale Kabanga na ile *volume* ya *nickel* ambayo iko pale na kwa vile nchi za jirani ziko *land locked* ina-*justify* kufikisha reli ili

kuweza kufanya hizi nchi ambazo ziko *land locked* ziweze kutumia bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, nadhani kwa sababu hii *historical context* ilikuwa haipo ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge hawajaunga mkono hoja, lakini kwa sababu nilizozitoa zina-*justify* kabisa kufanya uwekezaji na ku-*include* nchi ambazo ziko *land locked* ili tuweze ku-*mine* hii *nickel* kwa sababu ina *volume* za kutosha kwenye Bara la Afrika, lakini tukishafika pale tuweze kuchukua *custom revenue* kutoka kwa nchi ambazo ziko *land locked* za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono hoja ya Serikali na ninaomba Mheshimiwa Kaka yangu Hussein Bashe arudishe shilingi ya Waziri ili Serikali iendelee kujenga miundombinu kwa ajili ya kuinua uchumi wetu, lakini tutumie bandari yetu kukusanya *revenue* kubwa kutoka kwenye nchi ambazo ziko *land locked.* Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bashe kwa maslahi ya Taifa letu. Tunawapenda sana majirani zetu na hatuwasemi kwa ubaya, lakini Tanzania kwanza wengine baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Bashe tunaiunga mkono kwa sababu pamoja na kuwa hii reli inapeleka mizigo nje ya nchi lakini pia tuangalie itatumikaje kuchukua mazao kutoka kule inakopita kuja kuleta *centre* kwa maana ya Dar es Salaam na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii fedha iliyowekwa hapa bilioni moja inaweza kuanza mchakato reli kutoka hapa Dodoma kwenda Tabora kuelekea mpaka Kigoma kwa hiyo tukawa tume-*simplify*. Mimi naunga mkono kwamba fedha hii ianze mchakato kwenye barabara ambayo itapeleka mzigo mkubwa zaidi, lakini pia itasaidia kusafirisha mazao kutoka Kigoma kutoka Tabora kwenda Dar es Salaam na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia zote fedha hii ihame. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotufanya tupate shida hapa ni uzuri tulionao Tanganyika au Tanzania, kwamba *strategically* Mwenyezi Mungu ametuweka mahala pazuri na wenzetu wako *land locked,* lakini Tanzania ndiyo mababu wa diplomasia katika ukanda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza na kupanga mikakati yetu hatuwezi kumbagua yeyote yule, tunachoangalia ni namna gani yeye amekuja na anapenda kushirikiana na sisi kwa kuanza na jambo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa sana hoja ya Mheshimiwa Bashe na ninajua kwamba ilileta shida sana hata kwenye Kamati, lakini kama tu mipango ya kuijenga reli ya kutoka Tabora - Kigoma ipo, kwa sababu hata ingekuwaje hakuna uwezekano wa kuepuka kujenga reli ya kwenda Kigali, hakuna uwezekano. Hata kama ingejengwa hii na reli ya kwenda Kigali itajengwa kwa sababu na wao wanahitaji reli inayokwenda kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa nasema kwamba kwa maelezo ya Serikali yaliyotolewa na Waziri kwamba *feasibility study* ikikamilika na hii inajengwa, kuna haja gani ya kuhamisha fedha hiyo kuitoa wakati tayari sababu za kidiplomasia, sababu za kiuchumi na zenyewe ziko *valid* kwamba hata ingekuwaje na wao watahitaji tu hiyo reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema tu hayo na ninaomba sana uamuzi wa Serikali ambao una maudhui makubwa kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Spika wewe mwenyewe unapata shida kuvuruga diplomasia, ninaona uachwe kwa sababu tu Serikali imeji-*commit* kwamba *feasibility study* ikikamilika reli itajengwa kuelekea Kigoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna mambo mawili; kwanza tuzungumzie mzigo. Mzigo ndiyo una-*determine* hasa hiyo reli yenyewe itakuwa haina faida, hilo la kwanza, pili halafu tutakuja kuzungumzia hiyo bilioni 100 tunayoizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza mzigo tunaanzia mzigo wa Rwanda; mzigo wa Rwanda kuna tani milioni 1.1, halafu tukienda Congo imegawanyika sehemu mbili; mzigo unaokuja Tanzania unatoka sehemu mbili, unatoka kule Kaskazini ya Congo na sehemu za Kusini. Kaskazini ya Congo ambayo ni Bukavu na Goma pale kuna tani 750,000 ambao kwa ujumla hii inakupa tani milioni mbili. Ukienda upande mwingine Kusini, Lubumbashi ambayo yenyewe kuna tani milioni tatu, lakini tani milioni tatu zile zinagawiwa na nchi karibuni tano, kuna *South Africa Durban* pale wanachukua, kuna Namibia wanachukua, kuna Angola wanachukua, Mozambique, mzigo unaokuja Tanzania ambao unapitia Zambia ni tani 780,000 tu hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwa upande wa Tanzania kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge tuna *deposit* ya *nickel* ambayo kuna tani milioni 36.4; hii reli tunayoijenga kwanza tunajenga kwa sisi kuanzia Isaka mpaka Rusumo ndiyo pesa za Watanzania. Hatuendi kujenga kutoka Rusumo mpaka Kigali. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge kwa mzigo hasa kesi ile pale uko mzigo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bilioni 100, huwezi kujenga reli wakati wowote kwa bilioni 100. Bilioni 100 ni kama dola milioni 49 tumeweka pesa zile kwa ajili ya kulipa fidia na kwa ajili ya kufanya *feasibility study* kwa kipande cha kutoka Isaka mpaka Rusumo. Kwa msingi huo bado namuomba ndugu yangu Mheshimiwa Bashe hili jambo nafikiri tutaweza kulizungumza vizuri ili tuende nalo vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe mtoa hoja.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nieleweke kwa Mheshimiwa Waziri na Serikalini, hoja yangu ni kwa nia njema kwa maslahi ya nchi yetu, *that is number one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Mheshimiwa Waziri katoa takwimu kasema kusafirisha kontena moja ni dola 4,200 kutoka Dar es Salaam. Kutoka nchi ya jirani ya upande wa kule ni dola 4,700 lakini hajamalizia, Waziri angesema hizi ni *cost* za kusafirisha kwa barabara kwa malori siyo kwa treni, *that is number one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *number two*, *I agree* tuna *deposit* kubwa ya *nickel* Kabanga lakini lazima twende na taarifa za dunia. Migodi mikubwa ya *nickel* duniani imefungwa *because the price and value of nickel* imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba *at the end* ikifika mahali kama hatutoelewana Mheshimiwa Waziri nataka niingie kwenye kumbukumbu za Bunge kwamba hili jambo nimelisema, lakini kama tutaamua kuendelea nalo, mradi wa Isaka kwenda Rusumo ni kilometa 371 kwa kutumia *average cost per unit* tunazotumia kwa Morogoro – Dar es Salaam *we need over 1.5 billion dollar!* Kwa nini tunaenda *our 100 billion, why?* Kwa nini tusiweke sehemu ambayo tunakwenda ku-*rip* mapato, najiuliza tu, *because this* ni hela ya walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nasema Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri *with due respect* mwaka 2016/2017 tulitenga *900 billion shillings* kwa ajili ya *SGR,* mwaka 2017/2018 tulitenga kama *one trillion*, mwaka huu tumetenga 1.5, ukizijumlisha hizi ni 3.4/3.5; chukua hii 100 rudisha kwenye *phase one and two, please I beg you* Serikali, ninawaomba kwa jina la Mungu *this thing is not helping our country,* haitotusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *let's comment on* Rwanda nchi ya jirani uliyosema, Mheshimiwa Waziri na kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene kaongea vizuri, sina nia mbaya na majirani zetu, lakini *we should always remember the block* inaangalia kwanza *internal interest,* tuangalie *our internal interest. Our internal interest* ni sisi kuwa *super power* kwenye *transportation,* ndiyo maana tunapitisha *14 trilion shillings budget*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it's a business,* ninaomba *one minute...*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, sema unachotaka kuzungumza sasa yaani hiyo dakika huwezi kupewa muda umeisha kwa sababu pia tuna majina ya Waheshimiwa Wabunge wengine hapa.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuachie shilingi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimechangia kwa maandishi lakini pia nilivyokuwa nachangia huko nyuma siku zote nilikuwa naendelea kuishauri Serikali iendelee kufikiria na ninaomba safari hii na kama sitapata majibu ya uhakika nitaomba nitoe hoja ya kutoa shilingi na Wabunge wenzangu wachangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iendelee kuangalia namna itakavyoondoa kodi kwenye mitambo yote ambayo inahusiana na masuala ya ujenzi kwa mfano *grader, excavator, dozer* na *roller.* Kwa sababu leo tumeambiwa na nimeridhika na maelezo ya Serikali kwamba kuhamisha ile fedha ya *TARURA;* kugawanya ile pesa ya *TANROADS* kwenda *TARURA* barabara zetu za lami pia zitapata shida.

Kwa hiyo, fedha za *TARURA* inabidi tuitafutie fungu

jipya yaani iwe na mapato mengine ya ziada, barabara nyingi huko vijijini inachongwa kwa hii mitambo ambayo tunasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni makubwa yote na hasa haya ya nje ambayo yanafanya kazi Tanzania yanapata msamaha wa kodi lakini makampuni ya ndani ya wazawa hii mitambo inabidi walipie kodi, hawapati huo msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mitambo hiyo mingi iingizwe nchini bila kodi lakini wanapofanya kazi sasa, wanapokodisha ile mitambo kwenda kuchonga barabara na nini na itasaidia pia siyo kwenye masuala ya barabara tu hata kwenye masuala ya maji kuchimba malambo na nini, mitambo iwe mingi. Tuliona mfano mzuri kwenye matrekta yalipokuwa mengi, gharama zile za kulima zilishuka, lakini sasa wale wenye matrekta ndio wanatafuta wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepiga hesabu kwa mfano *grader, excavator, dozer* na *roller* ukikodisha leo ni shilingi milioni moja kwa siku, *average* unapata shilingi milioni tisa mpaka milioni 10 hiyo ni pamoja na kuweka mafuta na kulipa ma-*operator,* ambayo *average* kwa siku unaweza kuchonga kilometa tano kwa mitambo hiyo kwa *heavy grading* ambayo ni shilingi milioni 10 unaweza kupiga kilometa tano, milioni mbili kwa kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwa ajili ya *mobilization* kwa sababu mitambo haipo ya kutosha unakuta kwa mfano Manyara au Kanda nyingine ambazo hazina hiyo mitambo, gharama ya *mobilization* inakuwa ni shilingi milioni 10 mpaka 12 *one way*, kurudisha hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi kwenye barabara ya *TARURA* ambayo labda nimepewa milioni 10 huwezi kuchonga kwa kutumia hiyo mitambo kwa sababu hutakuwa na gharama ya *mobilization.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba na hii hoja leo ni mwaka wa nne napambana kwamba iondolewe lakini...

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa suala analozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni kuhusu kodi, anaomba kwamba iondolewe, suala la kodi linasimamiwa na Wizara ya Fedha, huko karibuni tutakuwa na *Finance Bill,* nafikiri hizi azilete wakati huo halafu tutaweza kulizungumza.

**MWNYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ingekuwa ni Wizara ya Fedha peke yake wanafanya maamuzi, mimi najua Serikali ni moja na bila Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na TAMISEMI, bila wao kuishauri Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha siyo mtaalam wa mambo ya barabara yeye anajua tu namna ya kupata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wao wangekubali hapa kwamba ni jambo muhimu na wataishauri Wizara ya Fedha ili tukifika kwenye *Finance Bill,* Wizara ya Fedha ikubali kwa sababu hawana utaalam kabisa kwenye masuala ya utengenezaji wa barabara na *costing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara waji-*commit* kwamba wao wataishauri Wizara ya Fedha ili ikifika kipindi hicho sisi tuiambie Wizara ya Fedha iondoe la sivyo miaka yote wao ikifika wakati wa Wizara ya Fedha Waziri atasema tunakubaliana na Wizara ya Fedha mapato...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni kama unatoa shilingi hii ni mara yako ya pili kusimama na nimetoka kutoa maelezo kwamba ukisimama mara ya pili kama hukuridhika na maelezo unatoa hoja yako unaungwa mkono. Sasa ukitoa maelezo marefu tena maana yake utakuwa umechangia mara tatu kwa sababu mwishoni tena wewe ni mtoa hoja.

Kwa hiyo, mara ya pili wewe unasema kama

umeridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri ama kama hukuridhika nayo. Mheshimiwa Waziri yeye ametoa maelezo yake kwamba hilo linahusiana na Wizara ya Fedha, wewe kama hukubaliani nalo hilo toa hoja yako watu wakuunge mkono, ndiyo taratibu zetu zilivyo, ama kama umeridhika na maelezo pia unaweza kutuambia.

**MHE. JITU V. SONI:** Basi, nitasubiri hiyo Wizara ya Fedha alivyosema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tuendelee na Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, kwanza nimpongeze kwa majibu mazuri sana na ya kina aliyoyatoa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi na katika mchango wangu wa maandishi niliiomba Serikali inisaidie, mwaka 2015/2016 tulianzisha Mfuko wa Reli na tukakubaliana kwamba kila mzigo unaopita bandarini tutoze kiasi cha asilimia 1.5. Sasa nataka niiulize pesa hizo mpaka sasa zimefika kiasi gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ambazo tunazo mpaka sasa hivi ni shilingi bilioni 273.899.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yake ni sahihi, lakini niombe sasa kwa sababu tunajenga hii *SGR* ningependa zaidi wakati tunamaliza kujenga hii *SGR* basi yale madeni *RAHCO* ambayo ni shilingi bilioni 20 kwa sababu pesa zipo, lakini kwa sababu Mfuko huu tuliuanzisha maalum kwa ajili ya kusimamia ukarabati wa reli, zile shilingi bilioni 20 kwa ajili ya reli ya Tanga mpaka Arusha na reli ya *TAZARA* pesa hizo basi ziende, ni ushauri. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, huo ulikuwa ni ushauri Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali katika ujenzi wa miradi ya maendeleo hasa huu ujenzi wa reli ya kisasa *(standard gauge)* na miradi mingine ya barabara. Miradi hii inapita katika maeneo mbalimbali ya watu na kama tunavyofahamu ardhi inamilikiwa na watu wa nne ambao ni kijiji, mtu binafsi, Serikali au hifadhi. Wakati miradi miradi hii pamoja na kwamba ni ya maendeleo, Serikali inatoa ardhi hiyo kwa ajili ya kupitisha miradi hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate majibu ya Serikali na kama sijaridhika nitashika mshahara wa Waziri kwa sababu tumepitisha mwaka jana hapa Sheria ya Fidia, tumesema kwamba ili ardhi ichukuliwe fidia inatakiwa ilipwe ndani ya miezi sita baada ya tathmini. Kuna miradi inatekelezwa sehemu mbalimbali kama ujenzi wa barabara na huu ujenzi wa reli kuanzia Dar es Salaam, Morogoro na Mikoa mingine watu nyumba zao zimebomolewa na ujenzi umeshaanza lakini mpaka leo fidia hazijalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali na watu hawa watalipwa lini kwa sababu watu hawa walikuwa wanategemea ardhi hiyo wengine kwa makazi kwenye nyumba zao zimebomelewa, lakini wengine walikuwa wanategemea kwenye ajira kwa ajili ya kilimo leo hii wameambiwa wasiendeleze kitu chochote na ardhi imechukuliwa inaendelezwa miradi ya maendeleo lakini fidia zao hawajalipwa. Nini kauli ya Serikali na watalipwa lini. Kama sitapata majibu ya kuridhisha nitashika mshahara wa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mbunge ni kweli kuna

baadhi ya maeneo tumechukua na tumechelewa kulipa hasa kwenye maeneo ya reli lakini sasa hivi tumeshaanza utaratibu wa kulipa. Wiki iliyopita tulitoa matangazo wale ambao wanastahili kulipwa wajitayarishe ili tuanze kuwalipa. Kwa hiyo, tunalisimamia hili na tutahakikisha wote ambao wako pale kisheria tutaweza kuwalipa kama sheria invyoelekeza. *(Makofi)*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri lakini tu niombe Serikali ndiyo wasimamizi wa sheria, wakati mwingine ni vizuri wenyewe wawe wa kwanza kufuata sheria kuliko mtu mwingine yeyote. Kama sheria Bunge hili tumetunga kwamba watu wanatakiwa kulipwa ndani ya miezi sita baada ya tathmini lakini pia kwamba mtu hawezi kuchukuliwa ardhi yake bila kulipwa ile fidia ili kwenda kujiendeleza zaidi. Sasa kama Serikali yenyewe ya kwanza kukiuka sheria haileti picha nzuri kwa watu wengine ambao tutatakiwa tufuate sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudisha hiyo shilingi lakini *message sent. (Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ..............Sh. 293,323,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ................. Sh. 325,214,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* .................. Sh. 126,699,000/=
Kif. 1005 – *Legal Services Unit* ................... Sh. 87,856,000/=
Kif. 1006 – *Government Comm. Unit* .........Sh. 250,325,000/=
Kif. 1007 – *Procurement Mgt. Unit* ............. Sh. 177,429,000/=
Kif. 1008 – *Mgt. Info. System* ......................Sh. 122,457,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Comm. Division* ...................... Sh. 648,227,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshmiwa Wabunge, tusipige meza

kipindi hiki kwa sababu sasa nitajua kwamba mtu ana hoja kumbe anapiga kwa kufurahi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Information, Comm & Tech*....... Sh. 346,109,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 62 – Uchukuzi**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Mgt*............... Sh. 3,945,575,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ............. Sh. 572,869,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ............... Sh. 2,178,919,000/=
Kif. 1004 – *Govt Comm. Unit*.................... Sh. 239,289,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit* ............. Sh. 429,245,000/=
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* ...................Sh. 303,396,000/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit* .................. Sh. 326,862,000/=
Kif.1008–*Information & Comm. Tech.Unit* ...Sh. 462,577,000/=
Kif. 2005 – *Transport Infrastructure Div*......... Sh. 1,412,647,000/=
Kif. 2006 – *Transport Service Division* ....... Sh. 75,799,443,278/=
Kif. 5002 – *Transport Safety and Environment Division*................ Sh. 621,856,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 98 - Ujenzi**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Mgt*.............. Sh. 11,790,085,066/=
Kif. 1002 – *Finance &Accounts* ................. Sh. 482,141,000/=
Kif. 1003 – *Policy & Planning Division* ......... Sh. 325,836,000/=
Kif. 1004 - *Govt Comm.Unit* ..................... Sh. 114,024,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt Unit*............. Sh. 166,388,000/=
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* .................. Sh. 156,356,000/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit* ................. Sh. 149,835,000/=
Kif. 1008 – *Info. & Comm. Tech. Unit*........... Sh. 157,839,000/=
Kif. 2002 – *Technical Services Division* ......Sh. 12,291,707,000/=

Kif. 2005 – *Roads Devt Division* ............ Sh. 16,785,949,000/=
Kif. 5002 – *Safety & Envi. Division* ................ Sh. 369,619,000/=
Kif. 6001 – *Airport Construction Unit* .......... Sh. 108,232,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIRADI YA MAENDELEO**

**KITABU CHA NNE**

**Fungu 98 – Ujenzi**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Div.*............ Sh. 250,000,000/=
Kif. 2002 – *Technical Services Div.*............ Sh. 30,450,000,000/=
Kif. 2005 – *Roads Devt. Division* ......... Sh. 1,573,893,269,000/=
Kif. 5002 – *Safety & Environment Div.*......... Sh. 2,500,000,000/=
Kif. 6001 – *Airport Construction Unit* .... Sh. 215,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 68 – Mawasiliano**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* ................ Sh. 350,000,000/=
Kif. 2001 – *Communication Division* ........ Sh. 4,650,000,000/=
Kif. 2002 – *Information, Comm. & Tech.*....Sh. 10,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 62 – Uchukuzi**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* .............. Sh. 6,000,000,000/=
Kif. 2005 – *Transport Infra. Div.*................Sh. 1,759,139,947,853/=
Kif. 2006 - *Transport Services Division* ......Sh. 535,600,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2018/2019 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pia Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuweza kuleta haya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ngazi ya Kamati, wale ambao wako kwenye Kamati hii ya Miundombinu, kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo wamewezesha kutushauri Wabunge wote na kuona namna ambavyo jambo hili linaweza kufanywa vizuri zaidi na mengine yale waliyokuwa wameyashauri kwenye ngazi ya Kamati Serikali imeshayachukua na imeyafanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na wale ambao wameshiriki mjadala kwa hapa Bungeni tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri, naamni ninyi kama wawakilishi wa wananchi mmeitendea haki Wizara hii.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Naibu Mawaziri hapo na Mheshimiwa Waziri, tunawatakia utendaji kazi mzuri ambao utahakikisha kwamba makadirio haya ambayo yamepitishwa leo naamini wakati mtakapokuwa mnatoa taarifa mwaka ujao tutakuwa na habari njema za utekelezaji mzuri wa makadirio ya mapato na matumizi. Niwatakie kila la heri pia watumishi wanaofanya kazi chini yenu ambao mnashirikiana nao, kwa maana ya wataalam na watendaji wote kwenye utekelezaji wa bajeti hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili hapa. Moja ni tangazo la wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao ni Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pia tunaye Ndugu Abdallah Mitawi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, karibu sana, tunaye pia Ndugu Issa Mlingoti ambaye ni Mratibu Mkuu Ofisi ya Uratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Dar es Salaam, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Hawana Ramadhani Juma na Ndugu Ramadhani Dau kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa William Ngeleja, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Anawatangazia kwamba michezo ambayo itakuwepo, kwanza mchezo utachezwa katika Uwanja wa Jamhuri na

mechi hizo za kirafiki ni kwa ajili ya mpira wa miguu na netiboli kati ya *Bunge Sports Club* na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EALA).* Mechi hizo zinatarajiwa kuchezwa jioni, tarehe 26 Aprili, 2018 baada ya kumalizika kwa sherehe za maadhimisho ya Muungano na zitatangazwa mubashara na Kituo cha Televisheni cha Azam. *(Makofi)*

Aidha, tarehe 28 Aprili, 2018 siku ya Jumamosi, kutakuwa na mechi za kirafiki za mpira wa miguu na *basketball* kati ya *Bunge Sports Club* na *NMB* katika Uwanja wa Jamhuri, mechi hizi pia zitarushwa mubashara na Kituo cha Televisheni cha Azam, baada ya mechi hiyo ya tarehe 28 Aprili, kutakuwa na mchapalo utakaofanyika katika Ukumbi wa Jengo jipya la *PSPF* hapa Dodoma. Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi mnaalikwa kushuhudia mechi hizo. Mheshimiwa Ngeleja hapa hajasema kama mchapalo ni wa watu wote au ni wa wachezaji, nadhani atafafanua wakati akitoa maelezo zaidi kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine; mnatangaziwa kwamba kesho kuanzia saa kumi na mbili na nusu asubuhi yatakuwepo mabasi kwa ajili ya kuwabeba Waheshimiwa Wabunge kutoka viwanja vya Bunge kuwapeleka Uwanja wa Jamhuri ili kuhudhuria maadhimisho ya Sikukuu ya Muungano. Kwa hiyo, kesho asubuhi yatakuwepo mabasi hapa kwa ajili ya kuwapeleka kwenye Sherehe za Muungano. Waheshimiwa Wabunge muda ni saa kumi na mbili na nusu, suala la chai hapa halijaandikwa.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi wakati wa mchango wa Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Saed Kubenea alisimama akitoa maelezo kwamba alikuwa ameshaambiwa afute kauli ambazo Mheshimiwa Munde alikuwa anataka kuzijibu na mimi nikasema kwa kuwa nilikuwa sijamsikia Mheshimiwa Munde akitoa hayo maelezo, nitaagiza Taarifa Rasmi za Bunge ili nizipitie.

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa za Bunge

nimekwishakuzipata, maelezo ya Mheshimiwa Kubenea sina haja ya kuyarejea, lakini kile nilichokuwa nimekisema ni kwamba nilikuwa sijamsikia Mheshimiwa Munde na kwa hiyo ningetaka kupitia hizi Taarifa ili nitoe hayo maelezo ambayo kikanuni yananitaka nitoe maelezo baada ya mtu kusimama na kuomba utaratibu, kwa sababu utaratibu maana yake kuna Kanuni inakuwa inavunjwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo yaliyopo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, maelezo aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Saed Kubenea kuhusu fedha kupelekwa eneo moja la Kanda ya Ziwa yalikuwa yamefutwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Munde sehemu ile ambayo alikuwa akimjibu Mheshimiwa Kubenea kuhusu kupeleka fedha Kanda ya Ziwa yataondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo ninapenda nilitolee ufafanuzi, lazima tuelewe tofauti ya mtu anapozungumzwa kwa jambo jema ndani ya Bunge na pia anapozungumzwa kwa jambo baya ndani ya Bunge. Kwa mfano, ukisema nchi fulani imefanya jambo fulani zuri ama unaipongeza nchi fulani kwa msaada iliyoleta ama unaipongeza nchi fulani kwa kuwapokea Watanzania waliokuwa wanapata shida sehemu ni tofauti na ukiwa unaishutumu nchi fulani kwa kuwaua labda Watanzania ama kwa kutokufanya jambo jema kwa nchi yetu. Haya ni mambo ambayo kidiplomasia, sisi wote ni viongozi hapa, tusingetaka kuliweka Bunge letu kwenye mazingira ambayo tunataka kuanza kujibizana hapa na pale. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, hizo tofauti kama hatuzijui vizuri basi tutafute namna ya kumuomba Mheshimiwa Spika ili tujue mipaka yetu.

Waheshimiwa Wabunge, huwezi kusimama hapa ukawa unaituhumu nchi kuwaua Watanzania, hapana! Lakini kama unaizungumzia nchi hiyo kwamba imefanya jambo jema kwa Tanzania ni sawasawa kwa sababu hili la pili linakuwa jema hata kwa hiyo nchi unayoisema lakini la kwanza linakuwa ni baya kwa nchi ile kwa hivyo linaleta shida kidiplomasia. Nadhani hilo litakuwa limeeleweka ili mtu

asije akajikuta kwamba anatoa maelezo siku nyingine kwamba sasa humu Bungeni watu hawaruhusiwi kutaja nchi, hapana. Ndiyo maana nchi hapa zimetajwa nyingi hata kwa mifano ya ndege, kwamba nchi fulani ndege inazo, nchi fulani imefanya hivi, lakini kwenye mambo mabaya humu Bungeni hiki ni chombo kikubwa sana kuwa kinajadili mambo ya nchi nyingine kwa ubaya, siyo jambo jema kidiplomasia.

Waheshimiwa Wabunge, nimelazimika kutoa ufafanuzi huo kwa sababu tutafika mahali Wabunge wataanza kukatazana kutoa maelezo ama kutaja jina la nchi ili mtu aseme kwamba mwongozo uliwahi kutolewa, mwongozo ni huo kwamba kama ambavyo unaweza kumsifia mtu akafurahi, vilevile mtu ukimsemea jambo baya pia atajisikia vibaya.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Ijumaa, Saa Tatu Asubuhi tarehe 27 Aprili, 2018.

*(Saa 1.33 Usiku, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 27 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*